

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 26 Mei, 2016**

*(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**DUA**

*Naibu Spika (Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

**NDG. NEEMA H. MSANGI-KATIBU MEZANI:** Hati za kuwasilisha mezani

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE - K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF - K.n.y MSEMaji MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**NAIBU SPIKA:** Katibu!

**NDG.NEEMA H. MSANGI-KATIBU MEZANI:** Maswali

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais, lakini kabla hatujaenda hapo swali namba 241 lina marekebisho kidogo Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko ameandikwa kama Mbunge wa Viti Maalum, swali hilo lirekebishwe palipoandikwa Viti Maalum huyu ni Mbunge wa Jimbo la Tarime Mjini. Kwa hiyo tunafanya hayo marekebisho halafu tunaendelea. Ofisi ya Rais TAMISEMI Mheshimiwa Moshi Seleman Kakoso Mbunge wa Mpanda Vijijini sasa aulize swali lake.

### **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 239

#### **Hospitali ya Mkoa Katavi**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO** aliuliza:-

Hospitali ya Wilaya ya Mpanda ndiyo pekee inayotoa huduma za Mkoa katika Mkoa wa Katavi, kwa kutumia bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda;

Je, ni lini Hospitali ya Mkoa itajengwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Suleiman Kakoso Mbunge wa Mpanda Vijijini kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za awali za ujenzi wa hospitali ya Mkoa wa Katavi zimeshaanza ambapo eneo la ekari 243 limepatikana. Katika bajeti ya mwaka 2014/2015, Mkoa ulipokea shilingi milioni 750, kati ya hizo shilingi milioni 468 zilitumika kulipa fidia kwa wananchi walioachia maeneo yao kupisha ujenzi wa hospitali. Hadi sasa Mkoa upo katika hatua za mwisho kusaini mkataba na kampuni ya *Y and P Consultant* ikiwa ni hatua muhimu ya kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka 2016/2017, Serikali imetenga shilingi bilioni 1.4 ili kuendelea na ujenzi wa hospitali ya Mkoa katika Mkoa mpya wa Katavi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Moshi Kakoso, swali la nyongeza!

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu ambayo Serikali imetoa ya hatua ya awali ya ujenzi wa hospitali ya Mkoa.

Swali langu la msingi nimeuliza kwa kuwa, hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda ndiyo iliyobeba uzito wa kuhudumia takribani wagonjwa zaidi ya laki tano wanaotumia bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda, ni lini Serikali itaharakisha mchakato wa ujenzi huo wa hospitali ya Mkoa ili kuepusha Halmashauri ya Mpanda inayotumia bajeti ya Halmashauri kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa wengi kinyume na utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuisaidia hospitali hii ili iweze kukidhi mahitaji kwa sasa?

Lakini swali la pili...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso hapo umeshauliza mawili, labda kama utataka Waziri achague moja wapo, endelea.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili naomba kuweka uzito, tunavyo vituo vya afya ambavyo kama vingemarishwa vingesaidia sana uzito wa hii hospitali ambayo imeelemewa. Serikali ina mpango gani wa kuviboresha vituo vya afya ambavyo vipo katika Mkoa wa Katavi, hususani vile vya Karema, Mwese na Mishamu, napenda kujua hayo. (Makofi)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ameuliza ni lini hospitali hii ya Mkoa itakamilika kwa sababu hospitali ya Mpanda ambayo ni ya Wilaya sasa ndiyo inayotumika kwa ajili ya kutoa huduma hizo za Kimkoa. Je, ni hatua gani za dharura ambazo Serikali inaweza kuzichukua kwamba tutajaribu kuona na kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda namna ambavyo tunaweza tukaiongezea uwezo wa dharura hiyo hospitali ya Wilaya ili kuweza kumudu majukumu ya Kimkoa. Hata hivyo, bado narudia kusema jibu la suluhu ya kudumu katika jambo hili ni kuhakikisha kwamba tunajenga hospitali hii na ndiyo maana Serikali inaendelea kutenga fedha kwaajili ya kujenga hospitali ya Mkoa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ameuliza je, kama kuna vituo vya afya ambavyo vinaweza vikasaidia kupunguza uzito huu wa wagonjwa katika hospitali hii ya Wilaya ambayo sasa inatumika kama hospitali ya Mkoa. Ni kweli Serikali tumejipanga na tutajaribu kuona kwa vipaumbele na kwa maeneo

aliyoyasema kama tunaweza tukaanza na vituo hivyo kutokana na bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Halmashauri ya Mpanda.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru. Mheshimiwa Waziri hospitali yetu ya Wilaya ya Siha haina wodi ya watoto wala ya wazazi na hii inasababisha msongamano mkubwa sana katika hospitali yetu ya Mkoa ya Mawenzi.

Je, ni lini fedha hizo zitatoka ili ujenzi huo uanze mara moja?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Naibu Spika, sikumsikia amesema hospitali ipi?

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Hospitali ya Wilaya ya Siha.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki nisiamini kwamba kweli hakuna wodi kwa ajili ya watoto na wazazi na kama kweli hakuna basi ni jambo ambalo linahitaji udharura wa hali yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango mingi ya vipaumbele katika sekta mbalimbali za huduma za jamii inapangwa kenye Halmashauri zetu. Kwa hivyo, tutajaribu kuona ni kwa namna gani wamepanga vipaumbele vyao na kwa sababu bajeti ya Wizara yangu imeshapitishwa na kwa maana ya Halmashauri zote nchini, basi tuweze kuona tunaweza tukaanza na hivi ambavyo ni muhimu zaidi katika sekta ya afya, kwa sababu kweli ni jambo gumu kidogo kuonekana kwamba hakuna wodi kwa ajili ya watoto na wazazi katika hospitali ambayo ina hadhi ya kuwa hospitali ya Wilaya. Kwa hiyo, nitalichukulia *very seriously* na kulishughulikia jambo hilo. (Makofi)

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Kituo cha afya cha Kirando kilianzishwa miaka 42 iliyopita wakati Kirando ikiwa ni Kijiji, leo kina wakazi mara 50 zaidi kutoka miaka 42, aliyekuwa Waziri wa Afya Mheshimiwa Dkt. Seif Rashid alifika pale Kirando na akaniahidi kwamba hiki kituo kweli kimezidiwa na ninafanya mpango wa kuwa hospitali kamili.

Lini Serikali yako itaipa hadhi kituo cha afya Kirando kuwa hospitali kamili kwa kuwa kimezidiwa na wagonjwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli inawezekana kabisa kwamba katika huduma za vituo mbalimbali vya afya kumekuwa na kuzidiwa kwa sababu ya umbali kutokana na maeneo yetu kati ya kituo kimoja hadi kingine. Lakini kwa

suala la kituo cha afya ya Kirando ambacho Mheshimiwa Mbunge anasema kwamba kimezidiwa na je ni lini au kuna mikakati gani ya kuimarisha ili kiweze kutoa huduma hiyo au kubadilishwa kuwa hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kikubwa hapa ni ushirikiano kati ya mamlaka ya Serikali za Mitaa ambapo Waheshimwia Wabunge ni Madiwani kule katika kupanga vipaumbele vyetu, ni vizuri mkawa mnaturahisishia kazi ya kupanga halafu mnajua kabisa kwamba hatua zile huwa ikitoka pale mnaenda kwenye Mkoa ambapo mnashauriana, katika Sekretarieti ya Mkoa kwenye kikao cha ushauri cha Mkoa pale ndipo ambao mnaweza mkaja na mapendekezo halafu Serikali Kuu tukaona tuanze na lipi katika eneo lenu.

Mheshimiwa Ally Keissy, nikuombe tu kwamba kama mtasema tukiimarisha hiki na kuwa hospitali, basi jambo hili lije kwa utaratibu wa kisheria kama ulivyoielezwa katika Sera ya Afya.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendea, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Mbunge Nzega Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 240

### **Utekelezaji wa Ahadi ya Mheshimiwa Rais**

**MHE. HUSSEIN M. BASHE** aliuliza:-

Wakati wa kampeni za uchaguzi Mheshimiwa Rais aliahidi ujenzi wa daraja la Nhobola na daraja la Butandula pamoja na barabara inayounganisha Kijiji hicho na Kijiji cha Mbogwe:-

Je, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa ahadi ya ujenzi wa madaraja hayo pamoja na barabara zake?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimwia Hussein Mohamed Bashe, Mbunge wa Jimbo la Nzega Mjini kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za awali za ujenzi wa daraja la Nhobola na Butandula zimeshafanyika kufuatia kukamilia kwa upembuzi yakinifu (*feasibility study*), usanifu wa awali (*preliminary design*) na usanifu wa kina yaani (*detailed design*) ili kujua gharama za ujenzi wa madaraja yote mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa usanifu huo daraja la Nhobola linatarajiwa kugharimu shilingi milioni 589.8 ambazo zitahusisha ujenzi wa barabara yenye kilomita 5.1 kuunganisha kati ya Mbogwe na Nhobola. Ujenzi wa daraja la Butandula utagharimu shilingi milioni 245.57 na utahusisha matengenezo ya sehemu zote korofi zenye urefu wa kilomita 16.2 katika vipande vya barabara ya Ijanija-Butandula, Butandula-Izegwa, Mwangoye na Butandula-Uchama. Kwa kuwa hatua hiyo imekamilika, Halmashauri itaweka katika mpango wa bajeti yake ili kupata fedha hizo na kuanza ujenzi wa madaraja hayo yote mawili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, swali la nyongeza!

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa msingi wa ahadi ya Mheshimiwa Rais ilikuwa ni kutazama uwezo wa Halmashauri, kwamba haina uwezo wa kujenga madaraja haya pamoja na barabara zake, thamani ya madaraja haya mawili ni zaidi ya milioni 800.

Je, Waziri yupo tayari kuthibitishia Bunge lako na wananchi wa Jimbo la Nzega kwamba miradi hii itapalekwa *TANROAD* kama ambavyo Rais aliahidi? (Makofi)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikubaliane na yeye kwamba kwa kulinganisha na bajeti zetu za Halmashauri, fedha hii tu peke yake inaweza ikawa ndiyo bajeti ya Halmashauri hiyo kwa mwaka mzima kwa barabara zote. Kwa hivyo ni kweli kama anavyosema Mbunge na ndiyo maana pengine Mheshimiwa Rais alisema madaraja haya yapelekwe *TANROADS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Serikali ni moja, na ahadi iliyotolewa fedha zinatoka zote Hazina, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa dhana ya *D by D* hata kama Halmashauri haina uwezo ama wa kitaalamu au wa kifedha, kazi ya Wizara yangu ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni *coordination* ambapo Wizara nyingine pia zozote zile zinaweza zikachangia ama rasilimali fedha au watu au ujuzi katika kuhakikisha kwamba Halmashauri zinafikia malengo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, hili Mheshimiwa Mbunge lisimpe shida, ndani ya Serikali tutaangalia kama linafaa kufanywa hivyo basi tunaweza tukashirikiana na Wizara ya Ujenzi kuona namna ya kutekeleza ahadi hii ya Mheshimiwa Rais.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri unafahamu kwamba gawio la Halmashauri za Mfuko wa Barabara ni ndogo sana zinazoenda kwenye Halmashauri zetu, tatizo la barabara siyo la Nzega tu lipo kwa nchi nzima baada ya mvua kunyesha sana mwaka huu barabara nyingi zimeharibika na madaraja. Napenda kufahamu Mheshimiwa Waziri kama upo tayari kuzungumza na Wizara ya Ujenzi ili gawio la Halmashauri ya fedha za Mfuko wa Barabara ziongezeke badala ya hivi sasa Halmashauri zimeshindwa kutengeneza barabara hizo zikiwemo za Babati Mjini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba gawio ambalo Halmashauri zinapata kama fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara zetu hazina uwezo wa kuhimili mambo ya dharura. Kwa maana hiyo, kweli ipo haja ya kutafuta nguvu ya ziada katika kuhakikisha kwamba kwa dharura za mvua hasa zilivyokuwa nyingi kwa mwaka huu, basi tunapata fedha ili tuweze kukarabati hizo barabara lakini pia kutokuathiri miradi yake ya kawaida iliyokuwa imepanga na Halmashauri katika maombi yao ya fedha za kibajeti. Kwa kufanya hivyo ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge Wizara ya Ujenzi mara nyingi imekuwa ikitengewa fedha kwa ajili ya dharura hiyo ambayo kusema kweli inaweza isitoshe, lakini pale kunapokuwa kuna dharura kubwa tunachukua hatua na wanatoa fedha na tunaweza kutengeneza barabara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kama dharura hiyo itakuwa ni kubwa kama ninavyoisema basi Serikali haitasita kufanya hivyo.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile fedha za Mfuko wa Barabara ni asilimia 30 kwa TAMISEMI na asilimia 70 kwa Serikali Kuu, hatuoni kutokana na mahitaji kama haya ya makorongo aliyoyasema Mheshimiwa Bashe, sasa wakati umefika wa kugawa fedha hizo asilimia 50 kwa 50 na Wilaya ya Hanang' ina makorongo makubwa kutokana na uharibifu wa mazingira lakini Halmashauri kama alivyosema Mheshimiwa Waziri haina uwezo kabisa wa kujenga makorongo hayo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, Mfuko wa Barabara unagawanywa kwa asilimia maana

mfuko ni mmoja, lakini Wizara ya Ujenzi inayoshughulikia barabara kwa maana TANROADS wanachukua asilimia 70 na Halmashauri zinachukua asilimia 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anajaribu kusema hapa kwamba, kwa sasa ni kama vile tunahitaji kuongezewa nguvu kwenye Mfuko wa Barabara katika upande wa barabara zinazosimamiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa takribani ni sawa kwa sawa na zile barabara za Kitaifa zinazounga Mikoa kwa Mikoa kwa sababu uharibifu mkubwa umetokea zaidi huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni la kisera na kwa hivyo siyo rahisi kulitolea jibu hapa, lakini sichelei kukubaliana na yeye kwamba kweli kwa sasa iko haja ya kuangalia kama tunaweza kubadilisha hizi namba hata angalau tukafika asilimia 40, sasa hili ni jambo la kisera siwezi kuliambia peke yangu hapa kusema ndiyo au hapana, Serikali tumesikia tuendeleo kulitafakari tuone kama kuna haja ya kufanya hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko Mbunge wa Tarime Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 241

**Madiwani na Wenyevitwa wa Mitaa/Vijiji kufanya kazi katika mazingira magumu**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza:-

Madiwani na Wenyevitwa wa Mitaa/Vijiji wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu sana, hali wakiwa ndiyo viungo wa shughuli za maendeleo katika jamii:

(a) Je, ni lini Serikali itaanza kuwalipa mshahara au posho Wenyevitwa wa Mitaa au Vijiji?

(b) Je, kwa nini Madiwani wasiwe na ofisi zao kama ambavyo Wabunge hupewa ofisi zao?

(c) Je, ni lini Ofisi za Wenyevitwa wa Mitaa au Vijiji zitajengwa ili kuepusha kuwa na ofisi majumbani kwako?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko unampa wakati mgumu Waziri hili swali ulilouliza lilikuwa ni la Tarime. Tuendeleo Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI. (Kicheko)



**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko Mbunge wa Tarime Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua wazi kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Madiwani na Wenyevitani wa Vijiji na Mitaa katika kusimamia shughuli za maendeleo nchini. Serikali imeweka utaratibu wa kuwalipa posho Viongozi hao kila mwezi ambapo kwa Madiwani posho hiyo imeongezeka kutoka 120,000 mwaka 2010/2011 hadi shilingi 350,000 mwaka 2015 kwa mwezi. Kwa upande wa Wenyevitani wa Vijiji na Mitaa posho hizo zinalipwa na Halmashauri kupitia asilimia 20 ya mapato ya ndani inayojumuisha ruzuku ya fidia ya vyanzo vilivyofutwa. Tunafahamu ziko changamoto kwa baadhi ya Halmashauri kutolipa posho hizo kutokana na makusanyo madogo. Mkakati uliowekwa na Serikali ni kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani kwa kubadili mifumo ya ukusanyaji pamoja na kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kujenga uwezo wa kulipa posho hizo.

(b) Serikali inatambua umuhimu wa Madiwani kuwa na ofisi kutokana na majukumu makubwa waliyonayo. Ofisi ya Diwani inatakiwa kuwemo ndani ya ofisi ya Kata, ambayo ndani yake inajumuisha ukumbi wa mikutano ya Kamati ya Maendeleo ya Kata, Ofisi ya Mtendaji wa Kata na Ofisi za Maafisa Wataalam ngazi ya Kata. Ujenzi wa ofisi hizo unafanyika kupitia bajeti za Halmashauri kwa kuzingiatia vipaumbele vinavyopitishwa na Mabaraza ya Madiwani.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa ofisi za Wenyevitani wa Vijiji na Mitaa unafanyika kupitia bajeti za kila Halmashauri. Hivyo kila Halmashauri inapaswa kuhakikisha inaweka kipaumbele na kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa ofisi hizo kwa awamu.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba, posho za Madiwani kwa maana ya vikao na posho za Wenyevitani wa Mitaa, Vitongoji na Vijiji zinalipwa na Halmashauri na kwa kuwa Serikali imekiri kabisa kwamba wanatambua kuna Halmashauri zingine hazina uwezo, makusanyo ya ndani ni madogo kama ilivyo Halmashauri ya Mji wa Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini sasa Serikali isione ni vema mathalani kwenye vikao vya Madiwani ambavyo tumeona vinatofautiana kati ya Halmashauri moja na nyingine, wengine wanalipwa 60,000, wengine 80,000 wengine 250,000 wengine 300,000, kwa nini wasi-standardize iwe kama

tunavyolipwa posho Wabunge kwa Tanzania nzima na iweze kutenga fedha, isitegemee mapato ya Halmashauri ili Madiwani wanavyokaa vikao vyao waweze kulipwa fedha ambazo ni *uniform* kwa Tanzania nzima, vilevile kwa Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili ni kuhusuiana na suala la Wenyeviti wa Mitaa na Vitongoji na Vijiji. Tumeshuhudia wananchi wakienda kupata huduma majumbani kwao. Serikali inajibu kwamba, inategemea mapato ya Halmashauri. Narudi pale pale tuna Halmashauri zingine mapato ni madogo sana na haiwezi kujenga Ofisi za Wenyeviti. Kwa mfano, kwangu Halmashauri ya Mji tuna Mitaa 81 Halmashauri ya Mji wa Tarime haiwezi ikajenga hizo ofisi. Kwa nini sasa Serikali isione umuhimu kuwapatia hawa Viongozi ofisi zao iwajengee, itenge fungu kutoka Serikalini ishuke chini kwenye Halmashauri zote nchini iweze kujengewa ofisi ili kuepuka adha ambayo inaweza kupelekea hata wengine kushawishika na kutoa na vitu vingine? (Makofi)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Wenyeviti wa Mitaa, Wenyeviti wa Vitongoji lakini pia Wenyeviti wa Vijiji wanafanya kazi nzuri sana na kila mmoja anajua. Lakini pia ndiyo ambao wanazisaidia sana hizi Halmashauri katika kutekeleza shughuli zake ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa hayo mapato yenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, itakuwa ni jambo la kusikitisha na linashangaza na tutachukua hatua kali sana kusema ukweli kwa Halmashauri zote ambazo hazitaheshimu *formular* ile ya asilimia 20 ya mapato ya ndani kuzipeleka kwa hawa watu muhimu sana wanaowasaidia katika kutekeleza miradi lakini pia kukusanya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itahakikisha inalisimamia jambo hili, lakini tusaaidiane Waheshimiwa Wabunge ninyi ndiyo Wajumbe wa Halmashauri zenu huko. Haya yanafanywa na watu ambao wako chini yenu kabisa kinidhamu, kwahiyo ni vizuri tukasikia huko mnachukuliana hatua kwa sababu mna hiyo mamlaka na sisi tukaja kusaidia pale tu ambapo huyu mtu amekuwa ni tatizo sugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vigumu pia kuweka *standard formula* na *standard formula* tulioiweka kama Serikali tumesema ni asilimia 20 ya mapato ya ndani, kwa sababu kwanza kabisa ili uweze ku-*establish* Halmashauri lazima vigezo kadhaa uweze kuvifikia ikiwa ni pamoja na hali ya uchumi wa eneo husika. Sasa tulipokuwa tunaomba Halmashauri, tunaomba tu ili tuweze kuzipata, lakini tunakuja kupata shida pale inapokuwa vigezo vile tulivyovisema

siyo halisi kwa sababu huko kiwango cha uwezo wa ndani ndiyo unao-determine uanzishwaji wa Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi naamini kwa Halmashauri zilizoanzishwa na kama kweli zilikidhi vigezo vilivyopo kwa mujibu wa sharia, basi haziwezi zikashindwa kabisa kuweza kuwalipa posho hawa watu muhimu sana katika ngazi ya Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa. Kwa sababu hawa watu kama nilivyosema ndiyo wanaosaidia kukusanya mapato hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili juu ya ofisi za Viongozi hawa muhimu ni kweli tungeweza kusema ni jambo zuri kwamba nchi nzima tukawa na utaratibu wa kujenga ofisi hizi zote, lakini kama mnavyofahamu bajeti yetu ni hiyo moja na kupanga ni kuchagua, ndiyo maana tumeziachia Halmashauri kwa dhana ya kupanga vipaumbele vyao, basi kama kipaumbele cha Halmashauri fulani ni ofisi hizi tunaweza tukaanza na hizo na sisi Serikali Kuu tutatenga kwenye bajeti yetu kwa kadiriri ya *sealing* ilivyopangwa kuhakikisha kwamba, tuna-facilitate au tuna-fund miradi ambayo imeibuliwa kutoka huko chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jukumu la Halmashauri kuhakikisha kwamba kutokana na makusanyo yao ya ndani ambayo hayana masharti kutoka Serikali Kuu, basi wanapanga kupunguza upungufu huo wa ofisi kila mara wanapopanga katika bajeti zao.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea Wizara ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Neema Wiliam Mgaya Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 242

### **Kutatua Mgogoro Kati ya Hifadhi ya Wananchi wa Wanging'ombe**

**MHE. NEEMA W. MGAYA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro wa ardhi kati ya hifadhi ya Mpanga na wananchi wa Wilaya ya Wanging'ombe?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa William Mgaya Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uhifadhi katika hifadhi ya Mpanga Kipengele ulianzishwa za Tangazo la Serikali (GN) Na. 483 la tarehe 25 Oktoba, 2002 ambapo eneo lililoidhinishwa lilitangwazwa kuwa pori la akiba kwa maslahi mapana ya Kitaifa. Uhifadhi wa eneo hili unahusisha utunzaji wa rasilimali zinazotoa fursa ya utalii, matumizi ya kiikolojia na vyanzo vya maji kupitia mito ya Mbarali, Mlomboji, Kimani na Ipera ambayo kwa pamoja huchangia maji ya mtoa Ruaha Mkuu, ambao ni muhimu kwa shughuli za kilimo ikiwemo umwagiliaji wa mashamba, mahitaji ya watu na uzalishaji wa umeme katika mabwawa ya Mtera na Kidatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Wilaya za Makete na Mbarali, poli la akiba Mpanga na Kipengere limepatikana na takribani Vijiji kumi vya Wilaya ya Wanging'ombe ambapo chanzo cha mgogoro ni wananchi wa Vijiji vinne ambavyo viko ndani ya mpaka wa hifadhi, na vingine vinne nje wa mpaka wa hifadhi kukataa kutambua mipaka iliyowekwa na Tangazo la Serikali na hivyo kugoma kuhama kupisha shughuli za uhifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za kutafuta suluhu ya mgogoro huu na eneo lote linalozunguka pori hili, Wizara yangu ilifanya vikao vya majadiliano na Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya ya Makete tarehe 20 mpaka 21, Novemba, 2014; Wanging'ombe tarehe 26 mpaka 27, Novemba 2014 na Wilaya Mbarali tarehe 26 mpaka 27, Februari, 2015 na hatimaye kufanyika kwa tathmini kutambua idadi ya wananchi na mali zao zisizohamishika na uthamini wa kiasi cha fedha kitakachohitajika kuwalipa fidia kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia uthamini uliofanyika mwaka 2007 na 2012 katika Wilaya ya Makete mwaka 2007, wananchi 325 wa Vijiji vya Ikovo, Usalimwani na Kigunga vya Wilaya ya Makete walilipwa fidia ya shilingi 190,067,151. Mwaka 2012 wananchi 161 wa Kijiji cha Ikovo walilalamikia kupunjwa, hivyo uthamini wa ardhi na gharama za kuhama ulifanyika tena ambapo walilipwa jumla ya shilingi 829,841,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika tathmini iliyofuata iliyofanyika na kukamilika mwaka 2015 Wilayani Mbarali, wananchi 308 katika Kitongoji cha Machimbo, Kijiji cha Mabadaga wanategemewa kulipwa jumla ya shilingi 717,650,000 katika mwaka wa fedha 2016/17. Tathmini na uthamini kwa Vijiji vya Wilaya ya Wanging'ombe imepangwa kufanyika kupitia bajeti ya mwaka wa fedha ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwaomba wananchi kuendelea kuwa watulivu, wavumilivu na kuepukana na shughuli ambazo zinaweza kuleta athari katika maeneo hayo muhimu kwa Taifa letu, kwani Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kutatua changamoto za migogoro ya mipaka kati ya hifadhi

na ya wananchi. Vilevile tunahimiza Mkoa, Halmashauri za Wilaya na Waheshimiwa Wabunge washirikiane na Wizara kuhamasisha elimu ya uhifadhi na pia kuwashawishi wananchi kukubali kuhama na kupisha uhifadhi mara baada ya taratibu kukamilika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mgaya swali la nyongeza!

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Nina swali moja tu la nyongeza, nataka kujua katika hifadhi ya Kitulo iliyokuwepo Makete kuna migogoro mikubwa sana pale kati ya hifadhi ya Kitulo na Vijiji vinavyozunguka hifadhi hiyo. Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba, matatizo ya mipaka kati ya wanavijiji wanaozunguka hifadhi ya Kitulo na hifadhi ya Kitulo ya Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Kitulo na migogoro ya ardhi inayotokana na wananchi wanaoishi katika Vijiji vinavyozunguka hifadhi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana wakati tukiwa tunatoa ufafanuzi wa hoja nzima ya migogoro ya ardhi katika maeneo ya hifadhi na yanayopakana nayo, tulitoa ufafanuzi kama ifuatavyo na ambao unahusisha pia hifadhi ya Kitulo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejipanga kwa ajili ya migogoro yote ya ardhi ikiwemo ile inayohusisha hifadhi. Kwa hiyo, kwa hifadhi ya Kitulo tunakwenda kuijumuisha hifadhi ya Kitulo kwenye orodha ya hifadhi zote ambazo zina migogoro kwenda kushughulikia migogoro hiyo kwa kuitazama inahusisha Wizara zipi kati ya zile Wizara sita zilizotajwa. Kwamba, tunakwenda kutazama migogoro hiyo chanzo chake ni nini, inahusu nini na suluhisho lake ni nini kwa kushirikisha Serikali katika Wizara zote zitakazohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema jana wakati tunapokwenda kupitia migogoro hiyo tunakwenda kuzingatia maslahi ya Taifa zaidi. *(Makofi)*

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2002 mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro ilifanya uhakiki wa mipaka yake na ndipo hapo ilipochukua maeneo ya wananchi katika Vijiji vya Endamaga na Lostete na tangu mwaka huo hadi wa leo kuna migogoro ambayo haiishi ni lini maeneo hayo ya wananchi sasa yatarudishwa kwao?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja ambalo napenda labda lieleweke vizuri hakuna mahali ambapo Serikali inatwaa ardhi bila kufuata utaratibu. Utaratibu wa Serikali kutwaa ardhi kwa ajili ya maslahi ya Taifa uko wazi, kwa upande wa hifadhi utaratibu huu ni shirikishi na unaanzia kwenye ngazi ya Vijiji vinavyohusika, Halmashauri zinazohusika,

vikao vya Mkoa mpaka kufikia vikao vya maamuzi vya Kitaifa ndipo ardhi itatwaliwa kwa ajili ya matumizi kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo pale ambapo kumetokea sababu yeyote ile ya kutokea kwa mgogoro labda kutoelewana au tafsiri tofauti ya sheria, tafsiri ya GN au matumizi yanayokiuka yale makubaliano ya awali. Hizo ni kasoro ambazo Serikali imekiri na ndiyo maana nimesema awali kwamba tunakwenda kupitia upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshajibu swali kama hili hapo nyuma na ninataka kusisitiza tena kwamba, tunakwenda kupitia mgogoro mmoja baada ya mwingine kuangalia ukweli wa mgogoro huo na ufumbuzi wake utapatikana kwa kushirikisha taasisi zote zitakazohusika ndani ya Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chegeni swali fupi!

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, katika ziara yake Mkoani Simiyu Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelekezo, kuna mgogoro mkubwa wa hifadhi na wananchi wa Wilaya za Busega, Wilaya ya Bariadi, Wilaya ya Itilima na Wilaya ya Meatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Waziri Mkuu alitoa maelekezo na maagizo kwamba, Mawaziri wanne wakutane mara moja, leo ni miezi mitatu imepita hakuna kinachoendelea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chegeni uliza swali!

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Je, Mheshimiwa Naibu Waziri lini sasa mtatii agizo la Waziri Mkuu la kukutana na kutatua migogoro hii?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali kupitia Waziri Mkuu akiwa Mkoani Simiyu alitoa maelekezo. Maelekezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri Mkuu akiwa Simiyu yamekwishaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tunayo taarifa iliyoandaliwa ya undani wa orodha ya migogoro yote inayohusika katika vijitabu ambavyo tayari vimeshagawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge wote, nia ya Serikali imekwishaelezwa mara kadhaa hapa kwamba umefika wakati sasa baada ya kukusanya taarifa za awali tunakwenda kukusanya Wizara zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mmoja anafahamu, Waheshimiwa Wabunge wanafahamu na wananchi wote kwa ujumla wanafahamu kwamba sasa tuna vikao muhimu vya bajeti ambavyo vinakamilika mwisho wa mwezi wa sita, mara tu baada vikao vya bajeti tunakwenda kutekeleza ahadi hiyo ya Serikali ya kwenda kupitia upya migogoro yote hiyo kwa kushirikisha Wizara zote zinazohusika, lakini baada ya kukamilisha jukumu hili lililoko mbele yetu la Bajeti ya Taifa. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Sixtus Raphael Mapunda, Mbunge wa Mbinga Mjini swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Janet Mbene

Na. 243

### **Kuwalinda Wakulima Wadogo wa Kahawa**

**MHE. JANET Z. MBENE (K.n.y MHE. SIXTUS R. MAPUNDA)** aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko kubwa la kampuni kubwa kuanzisha mashamba ya Kahawa katika maeneo ya Wilaya ya Mbinga na sehemu za Songea Vijijini jambo linalotishia uzalishaji na soko kwa Wakulima wadogowadogo wa Kahawa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalinda wakulima wadogo wasimezwe na wakulima wakubwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Sixtus Paphael Mapunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kumekuwepo na ongezeko la kuanzishwa kwa mashamba makubwa ya Kahawa katika maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na Wilaya za Mbinga na Songea Vijijini. Hali hii inachangiwa na sera na mazingira mazuri ya uwekezaji yaliyopo nchini. Aidha, uwepo na uanzishwaji wa mashamba makubwa nchini hautishii uzalishaji na soko la kahawa kwa Wakulima wadogo wa Kahawa bali una manufaa yafuatayo:-

(i) Uanzishwaji wa uwepo wa mashamba makubwa unawezesha wakulima wadogo walio karibu na mashamba hayo kujifunza teknolojia mbalimbali zinazotumiwa na mashamba hayo katika kuongeza tija na uzalishaji wa kahawa.



(ii) Baadhi ya mashamba makubwa yanaendesha miradi ya kuwasaidia wakulima wa kahawa walio karibu na mashamba hayo (*out growers schemes*) kwa kuwapa huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na huduma za ugani, ukoboaji na masoko ya Kahawa yao. Kwa mfano, shamba la AVIV lililopo Lipokela Halmashauri ya Wilaya ya Songea limekuwa likitoa huduma za ugani kwa wakulima wanaolizunguka. Aidha, mpaka sasa kiasi cha miche 550,000 imekwishagawanywa kwa wakulima tangu shamba hilo lianzishwe miaka minne iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na manufaa hayo, Serikali ilifanya marekebisho ya Kanuni zinazoongoza tasnia ya Kahawa ili kuwalinda wakulima wadogo wanaoingia makubaliano ya uzalishaji wa Kahawa na makampuni binafsi pamoja na mashamba makubwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janet Mbene, swali la nyongeza!

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Hizo huduma zinazosemekana kuwa zinatolewa kwa *out growers*, Je kuna mkakati maalum au inategemea na huruma ya huyo mwekezaji mkubwa?

Swali la pili linahusiana na soko; Kwa kuwa sasa hivi huu utaratibu wa minada ya Kahawa unaathiri kwa kiasi kikubwa mapato yanayopatikana kwa wakulima wadogo. Je, Serikali iko tayari kuruhusu wakulima wa kahawa na wao wenyewe kujitafutia masoko katika maeneo ambayo ni *nish* kwa ajili yao ili na wao waweze kupata mapato makubwa zaidi kwa ajili ya kahawa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Je, hii minada ni lazima iwe Kilimanjaro tu, hatuwezi kuwa na minada katika maeneo makubwa ambayo Kahawa inalimwa? Ahsante sana

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kuhusu huduma zinazotolewa na Wakulima wadogo kwenye *out grower schemes* hamna mkakati wowote maalum ambao umewekwa, isipokuwa uhamasishaji umekuwa ukifanywa ili mashamba hayo yaweze kutoa huduma mbalimbali ikiwepo kama nilivyosema kuwasaidia kupata teknolojia nzuri zaidi, kuwasaidia katika ukoboaji, kimsingi mashamba yale yanaangalia ni nini wanahitaji kwa ajili ya kuongeza tija katika uzalishaji wao na katika kupata masoko.



Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inachofanya ni kujaribu kuhamasisha na kuwashauri waweze kutoa huduma mbalimbali ambazo zitawasaidia wakulima wale wanaozunguka kuweza kupata tija katika uzalishaji

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masoko; Serikali kimsingi haikatazi wakulima kujitafutia masoko ilimradi wafuate taratibu ambazo zimewekwa ili kusiwepo na uholela pia vilevile ili wakulima wetu waweze kulindwa na mifumo ya kinyonyaji, kwa sababu ukiachia tu iende kiholela, wakulima wetu wanaweza wakaumia. Kwa hiyo kimsingi, masoko yanaweza kutafutwa na tayari kuna wakulima ambao wanauza Kahawa moja kwa moja nje lakini ilimradi taasisi zinazohusika na udhibiti zifanye kazi ili wakulima wasiweze kuonewa.

Pia, aliuliza kuhusu Je ni lazima soko la kahawa likafanyike tu Kilimanjaro. Kimsingi kuna aina tatu ya uuzaji wa kahawa. Kwa kutumia soko la Moshi, wakulima wanaweza wakauza moja kwa moja nje pia kuna utaratibu wa kutumia manunuzi ya wakati lakini kimsingi Serikali iko tayari kufikiria namna bora ya kuendesha soko la kahawa ikiwa ni pamoja na kuruhusu uanzishwaji wa masoko mengine kwa maeneo ambayo yana uzalishaji mkubwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Mmasi.

**MHE. ESTHER M. MMASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii nami niweze kuuliza swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Waziri, kupitia mpango wa AGOA ambao Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama sehemu ya ushiriki Nchi za SADC, tumepewa ridhaa ya kutumia soko la Marekani bila kuwepo na vikwazo vya kodi.

Je, Serikali inatupa *commitment* gani kuona vijana wahitimu wa Vyuo Vikuu wanaweza kutumia fursa hii ya mpango wa AGOA kuondokana na suala zima la tatizo la ajira? Ahsante. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa naibu Spika, ni kweli kwamba mpango wa AGOA unatoa fursa ya kuweza kuuza mazao yetu nje, na ni kweli vilevile kwamba ni fursa ambayo ikitumiwa vizuri inaweza ikawasaidia vijana wetu kujiajiri na kuondokana na adha iliyopo sasa ya ukosefu wa ajira. Kwa hiyo Wizara iko tayari kushirikiana na vijana wowote ambao wako tayari kujiingiza katika uuzaji wa kahawa ili kuitumia fursa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika bajeti yetu ya mwaka huu tumetenga baadhi ya fedha ili kuweza kuona namna ya kuwasaidia vijana waweze kuingia kwenye kilimo na tutaanza eneo la Rufiji, lakini tuko tayari kufikiria namna nyingine ya kuweza kuwasaidia vijana wengi waweze kuingia katika uzalishaji huo hasa katika eneo alilosema la kahawa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Nicodemas Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mjini sasa aulize swali lake.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba swali langu namba 244 kabla ya kujibiwa nifanye masahihisho madogo. Ni kituo cha Mbegu cha Bugaga siyo Bigoga. Baada ya masahihisho madogo hayo naomba sasa swali langu lijibiwe. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Marekebisho yako kwenye swali au kwenye jibu ulilopewa Mheshimiwa?

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Kwenye swali.

**NAIBU SPIKA:** Sawa, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Na. 244

### **Serikali Kuweka Katika Kilimo Mkoa wa Kigoma**

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO** aliuliza:-

Mkoa wa Kigoma ni kati ya Mikoa mitatu inayopata mvua nyingi katika nchi yetu kwa wastani na takribani milimita 1,300 kwa mwaka ikifuatiwa na Mkoa wa Katavi.

(a) Je, ni kwanini Serikali haifanyi jitihada ya kuwekeza katika kilimo ili kunufaika na uwepo mzuri wa hali ya hewa?

(b) Je, ni kwanini Mkoa wa Kigoma uliondolewa katika Mikoa na yenye uzalishaji mkubwa na kupata mgao mdogo wa pembejeo?

(c) Je, ni kwanini kituo cha Mbegu cha Bugaga kilichopo Wilaya ya Kasulu kimetokelezwa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mjini lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa kwa siku za nyuma Mikoa ya pembezoni ukiwepo Mkoa wa Kigoma imekuwa na changamoto nyingi za kimaendeleo kutokana na kukosekana kwa miundombinu muhimu kwa maendeleo. Serikali imefanya jitihada kubwa kuwezesha uwekezaji katika Mikoa hii ikiwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa miundombinu muhimu kama barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa katika Mkoa wa Kigoma, zinaendelea tafiti mbalimbali za kilimo kwa kushirikiana na wadau wengine kama vile kampuni ya Kigoma Sugar kwa zao la Miwa, na *Belgium Technical Cooperation* kwa zao la chai kabla ya kuanza kuhamasisha sekta binafsi kwa uzalishaji mkubwa. Aidha, Mkoa wa Kigoma uko katika mpango wa *BRN* katika kilimo cha miwa (*Sugarcane Cluster*) ambapo katika mpango huo, mashamba makubwa mawili yameshatambuliwa na wawekezaji kama vile Kigoma Sugar wameshaonyesha nia ya kuzalisha sukari kwa kushirikiana na wakulima wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kigoma umepewa kipaumbele kwa upande wa ruzuku ya pembejeo ambapo ni kati ya Mikoa mitano iliyopewa ruzuku kubwa ya pembejeo kwa msimu wa 2015/2016 kati ya Mikoa 24 Nchini. Hii ni kutokana na umuhimu wake katika uzalishaji mkubwa wa chakula hasa mahindi hapa Nchini. Idadi ya kaya zilizopata ruzuku ya pembejeo za kilimo katika Mkoa wa Kigoma imeongezeka kutoka kaya 60,239 msimu wa 2013/2014 na kufikia kaya 74,000 msimu wa 2015/2016. Aidha, mgao mdogo wa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa wakulima kila Mkoa ikilinganishwa na mahitaji hutokana na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, shamba la kuzalisha mbegu la Bugaga lenye ukubwa wa hekta 336.906 limekaa muda mrefu bila kuzalisha mbegu kutokana na ufinyu wa fedha. Wizara imeweka mkakati wa kulifufua shamba hilo katika msimu wa 2016/2017 ili liweze kuzalisha mbegu kwa wingi kwa ajili ya wakulima wa Kanda ya Magharibi ikiwemo Wilaya ya Kasulu. Aidha, Serikali inahimiza makampuni na vikundi mbalimbali Mkoani Kigoma kushirikiana na ASA katika shughuli za uzalishaji mbegu za mazao mbalimbali ili kuchangia maendeleo ya kilimo katika Mkoa wa Kigoma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nsanzugwanko swali la nyongeza!

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu yaliyotolewa. Naomba tuweke rekodi vizuri. Hakuna ujenzi wa miundombinu uliokamilika katika Mkoa wa Kigoma hilo la kwanza, Pili, Kampuni ya Kigoma Sugar haifanyi utafiti wa miwa wala BTC hawafanyi utafiti wa chai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa ruhusa yako naomba swali langu kipengele (a) litafutiwe majibu muafaka kwa sababu hayo siyo majibu yake. Kwa sababu shamba la chai limeachwa limekuwa poro kwa muda mrefu na hakuna utafiti kama huo. Swali la kipengele cha (b) limejibiwa sawasawa. Swali (c)....

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nsanzugwanko kuna nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa hiyo umechagua kusahihisha jibu au utauliza swali la nyongeza? Kwa sababu kama una malalamiko kuhusu jibu umeshayaleta na Kiti kimepokea kitatoa uamuzi. Kama ni hayo tu tumalize au kama unauliza swali la nyongeza uliza swali, suala la kulalamikia jibu tumeshalipata.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, shamba la Bugaga ambalo Mheshimiwa Waziri anajibu kwamba halikuendelezwa kwa sababu ya ufinyu wa fedha ni kwamba shamba hili hata mwaka huu wa fedha halina fedha. Kwa hiyo ni vizuri tu Wizara waturudishie shamba letu kama wameshindwa kuliendeleza shamba hili la Bugaga tunaomba waturudishie shamba letu ili tulitumie kadri tutakapoona inafaa, kwa sababu inaonekana Serikali haina nia hata kidogo ya kufufu shamba hili la Mbegu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ya swali la Mheshimiwa Nsanzugwanko. Tunaposemea Serikali tunapanga kulifufua shamba hilo hatumaanishi tu kwamba tunategemea bajeti ya Serikali, hata mashamba mengine ambayo tunasemea tunategemea kuyafufua, tumeweka *arrangement* za tofauti. Kwa mfano, tulisema kwenye shamba la Kitulo tunawategemea ndugu zetu wa Banki ya Kilimo, wiki mbili zijazo wataenda kutembelea shamba hilo waweze kuangalia miundombinu iliyopo na mahitaji ili waweze kuwakopesha *nuclear farm* pale waweze kuliendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kwenye lile shamba la Bugaga, tunategemea kutumia sekta binafsi kama ambavyo tumetumia kwenye lile shamba ambalo liko kule Mbozi na tunategemea pia kutumia ule utaratibu tuliosema kwa wale vijana ambao watakuwa tayari kushiriki kwenye shughuli hizi

za kilimo waweze kushiriki kwa *arrangement* hizo tofauti za kuitumia sekta binafsi na baadae kuuza mbegu zile kwenye taasisi yetu ya mbegu ya Taifa ili iweze kuuza kwa wakulima.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Nsanzugwanko, uridhie tu kwamba tumeshaanza utaratibu wa kuweza kulifufua na kulifanyia kazi na hiyo itaenda sambamba na utaratibu wa kuwarejesha vijana kwenye shughuli za kilimo, sawa na kuwafanikisha vijana kuyafikia masoko kama swali lile lililoulizwa na Mheshimiwa Esther Mmasi ambalo linatupatia masoko mengine ambayo vijana wanaweza wakafikia wakafanya kazi hiyo. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge baada ya Bunge kuwa limeisha, natarajia kuzungukia kwenye shamba hilo na yeye atakuwepo na tutakuwa pia na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mbegu ikiwa ni mikakati ya kwenda kwenye utekelezaji wa jambo hili ambalo tunalisema.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea. Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali, sasa aulize swali lake.

Na. 245

### **Kuanza Kutumika kwa Gati la Kilindoni - Mafia**

**MHE. RIZIKI SHAHARI MNGWALI** aliuliza:-

Serikali ilijenga Gati kubwa la Kilindoni katika Wilaya ya Mafia kwa mabilioni ya fedha ili kuwezesha meli kubwa kutia nanga na hivyo kutatua tatizo sugu la usafiri wa majini Wilaya ya Mafia, licha ya Gati hilo kukamilika na kuzinduliwa na Rais aliyepita Mheshimiwa Jakaya Kikwete tangu mwaka 2013, bado Gati hilo halijaanza kutumika jambo ambalo limesababisha wananchi kuendelea kupata adha kubwa ya usafiri kwa kutumia bahari.

Je, Serikali itaelekeza meli kubwa na boti zenye viwango na bima kuanza kuwahudumia wananchi wa Mafia kwa kutumia Gati la Kilindoni?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu makuu ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ni pamoja na kujenga miundombinu ya kibandari na kuendesha shughuli za Bandari. Katika utekelezaji wa majukumu yake, Mamlaka ilikamilisha Ujenzi wa Gati la Kilindoni-Mafia lililofunguliwa rasmi tarehe 2/10/2013

na aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Ujenzi wa Gati hili uligharimu kiasi cha shilingi bilioni 27. Aidha, katika kuboresha matumizi ya Gati hili, mamlaka ilikamilisha kazi zifuatazo:-

- (i) *Landing barge* kwa ajili ya kuegesha majahazi,
- (ii) *Shed* kwa ajili ya mizigo, na
- (iii) Uzio kwa ajili ya usalama wa waendao kwa miguu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoieleza awali, Gati hili lilikamilika na liko tayari kwa ajili ya matumizi. Hata hivyo, pamoja na utayari huo kama tunavyofahamu, wadau wakubwa wanaoendesha shughuli za usafiri wa majini katika mwambao wa bahari ni sekta binafsi. Kwa kutambua hilo, Wizara yangu itaendelea kuwashawishi na kuwashauri wadau hao wawekeze katika usafiri wa kwenda Mafia kwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa na Bunge ambazo zinasimamiwa na SUMATRA.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara ya usafiri wa majini ni kama ilivyo biashara nyingine yoyote. Hivyo, milango iko wazi kwa makampuni yanayotoa huduma hii, pia kuwekeza katika Mwambao wa Mafia. Hata hivyo, tunamuomba Mheshimiwa Mbunge aendeleo vilevile kuwashawishi wananchi kwa ujumla kujitokeza na kuwekeza katika Mji wa Mafia ili ukue kibiashara zaidi ya ulivyo sasa ili kuwavutia watu na watoa huduma kushawishika na kuwekeza katika Mwambao wa Mafia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shahari swali la nyongeza

**MHE. RIZIKI SHAHARI MNGWALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nina maswali mawili ya nyongeza na ukiniruhusu nina ombi pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuondoa huduma za usafiri wa majini kwa wananchi wa Mafia kwa upande wa Serikali, lakini bado Serikali hiyo ikatoa huduma kwa Mashirika yake ya Umma kwenye sehemu nyingine za Maziwa Makuu. Serikali haioni kama inawabagua watu hawa wa Mafia?

Swali la pili; Waziri atakubaliana nami kwamba, kwa sababu katika swali langu la msingi niliulizia pia viwango vya boti. Huo utaratibu ambao wameruhusu SUMATRA wauendeshe ndiyo huo wa kutuwekea boti ambazo hazina viwango na pia hazina bima. Je, Serikali haioni kuna ulazima sasa wa kuwa na mipango ya muda mfupi, kuwa na usafiri wa kuaminika wa majini kwa Watu wa Mafia wakati wakiendelea kushawishi hao wawekezaji binafsi kuja kutoa huduma hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nina ombi na hili ni kwa jumla siyo kwa Waziri wa Wizara hii tu, bali kwa Mawaziri wote kwamba tafadhalini sana, peaneni *dose ya know your country*, kwa sababu majibu mnayotoa ni *standard* namuomba Waziri husika aje Mafia aone kama hilo Gati analozungumzia lina viwango hivyo anavyovieleza hapa. Ahsante(Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana kwa karibu sana na Mbunge wa Jimbo la Mafia, Mheshimiwa Mbaraka Dau. Wameondoa tofauti ya Vyama, wameungana, wanawatumikia watu wa Mafia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbaraka Dau muda wote amekuwa akisisitiza kuhusu gati la Nyamisati ili kuweza kuunganisha kati ya Kilindoni na Nyamisati ili uwezekano wa kuongeza uvutiaji wa wawekezaji wa kutoa huduma katika eneo hilo. Nawashukuru sana kwa kuungana na mimi nawahakikishia Muungano huo tutahakikisha unazaa matunda haraka iwezekanavyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ubaguzi kwa kutoa huduma kwenye Maziwa Makuu, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba uamuzi huu wa kuondoa shirika ambalo lilikuwa linatoa huduma za meli baharini upande wa Bahari ya Hindi ulifanyika ndani ya Bunge hili na kama mnaona kuna ulazima wa kurudia tena ili tulianzishe Shirika la Kutoa Huduma kwenye Bahari ya Hindi tutafanya uamuzi humu ndani, baada ya Serikali kulitafakari suala hilo kwa kina na kuangalia faida na hasara zake. Suala la ubaguzi halipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu SUMATRA kutoa vibali kwa boti ambazo hazina *standard*, nimemsikia na naomba kumhakikishia nitalishughulikia hilo kuona ukweli wake, undani wake na sababu zake ili tuweze kurekebisha huduma zinazostahili na boti zinazostahili kutoa huduma pale Mafia ziweze kufanya kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shahari nadhani ombi lako atakujibu Mheshimiwa Waziri baadaye baada ya kujiridhisha kama anaweza kuja huko.

Mheshimiwa Ally Saleh, swali fupi tafadhali.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.



Kwa kuwa, katika jibu lake la msingi Mheshimiwa Waziri amesema sababu moja kubwa ya uwekezaji au kuvutia uwekezaji ni kukua kwa biashara, na kwa kuwa Mikoa ya Kusini, Ruvuma, Lindi, Mtwara ina karibu Watanzania milioni 5, na kwa sababu kwa Mikoa hii haijapata huduma ya uhakika ya usafiri wa meli kwa zaidi ya miaka 10 hivi sasa.

Je, Serikali haioni kuna haja sasa ya kuipa kipaumbele cha juu kabisa Mikoa hii kushawishi wawekezaji kuwekeza?(Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumhakikishia tumelisikia hilo tukalifanyie kazi, tutakuja na majibu pale Serikali itakapoona njia ya muafaka kulifanyia kuhusu wasafiri hao wa maeneo ya Kusini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Elias John Kwandikwa Mbunge wa Ushetu sasa aulize swali lake.

Na. 246

### **Mawasiliano ya Simu-Ushetu**

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA** aliuliza:-

Kata za Uyogo, Igwamanoni, Ushetu na Chena katika Jimbo la Ushetu hazina mawasiliano ya simu za mkononi ya uhakika. Je, ni lini maeneo hayo yatapatiwa mawasiliano ya simu za mkononi yenye uhakika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Elias John Kwandikwa, Mbunge wa Ushetu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa naibu Spika, vijiji vya Manungu na Uyogo katika Kata ya Uyogo pamoja na vijiji vya Iramba, Luhaga, Mwamanyili kutoka katika Kata ya Igwamanoni na vijiji vya Mwazimba na Nundu kutoka katika Kata ya Chela vimekwishapata huduma ya mawasiliano kupitia utelekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi wa Kampuni ya simu ya *Vietel*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vya Jomu na Buchambaga vya Kata ya Chela, vijiji vya Mhuga na Ibambala, Kata ya Ushetu na Kipangu na



Igwamanoni Kata ya Igwamanoni vipo katika utekelezaji wa awamu ya pili na awamu ya tatu ya miradi ya kampuni ya simu ya Vietel ulioanza Novemba 2015 na kutarajiwa kukamilika Novemba 2017.

Aidha, kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote, vijiji vya Kata ya Ushetu, vijiji vya Bugoshi na Kalama kutoka katika Kata ya Uyogo na vijiji vya Chela, Mhandu kutoka katika Kata ya Chela, vitaingizwa katika awamu zijazo za mradi kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kwandikwa swali la nyongeza.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu lakini nashukuru pia Serikali kwa msukumo wa kuimarisha mawasiliano. Nina swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, iko minara ambayo imeshindikana kuihudumia muda wote kutokana na tatizo la barabara, katika Kata za Ulowa, Ushetu, Ubagwe, Bulumbwa, Ulewe, Nyankende wameshindwa kupeleka mafuta wakati wa mvua. Je, Serikali iko tayari kututengenezea madaraja ya katika maeneo ya Kasheshe na Karo ili mawasiliano yaweze kuimarika na huduma zingine kuendelea?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba barabara ni wajibu wetu vilevile pamoja na mawasiliano. Ninachoomba ni kumhakikishia matatizo ya barabara na hasa madaraja hayo mawili, daraja ya Karo na daraja la Kasheshe yatafanyiwa kazi haraka iwezekanavyo na kwa nafasi hii namtaka Meneja wa TANROADS Mkoa wa Shinyanga afuatilie madaraja hayo mawili ili wajibu wetu kama Wizara wakutoa huduma ya mawasiliano pamoja na barabara uweze kutekelezwa kikamilifu katika eneo hilo la Ushetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Ulega, swali fupi.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Kwa kuwa, tatizo hili la Ushetu la mawasilinao lipo pia katika Jimbo langu la Mkuranga katika vijiji kama vile vijiji vya Mkuruwiri, Nyanduturu, Kibesa, Msolwa, Kibewa na kwingineko. Je, Serikali ina mipango gani ya kuhakikisha kwamba wananchi hawa wa vijiji nilivyovitaja na vinginevyo viweze kupata mawasiliano

ya simu na wao waweze kuwasiliana na ndugu zao na shughuli zao zingine za kijamii na kiuchumi. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, chukuzi na Mawasiliano!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikiliza, nimepokea maombi yake. Tutayafanyia kazi na tutawasiliana naye mara nitakapopata taarifa kamili kuhusu maeneo haya aliyoyaelezea. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Tauhida Cassian Galos, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Faida Bakar.

Na. 247

### **Kuwekea Uzio Vituo vya Polisi-Zanzibar**

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR (K.n.y MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOSS NYIMBO)** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka uzio kwenye vituo vikubwa vya Polisi vilivyopo Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tauhida Cassian Galloss, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inao mpango wa kujenga uzio katika Vituo na Makambi yote ya Polisi Tanzania. Aidha, Jeshi la Polisi kwa kutumia rasilimali zilizopo eneo husika, limekuwa likijenga uzio wa muda au wa kudumu katika maeneo mbalimbali na litaendelea kujenga uzio katika vituo zaidi hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Zanzibar, Serikali imeanza kujenga uzio kwa baadhi ya maeneo ya Kambi ya Ziwani Zanzibar, mathalani eneo la Chuo Ujenzi umeanza kwa kutumia fedha zilizotokana na mapato ya ndani. Aidha, kwa upande wa mbele ujenzi unafanyika sambamba na kujenga maduka ambayo yatasaidia kuendesha shughuli za Polisi na kujiingizia mapato.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Faida swali la nyongeza!

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza:-

Kwa kuwa, Naibu Waziri amekiri kwamba wameshaanza kujenga uzio katika kituo cha Ziwhani pale Zanzibar, tunashukuru sana Serikali. Naomba kumuuliza sasa, Zanzibar ina vituo vingi sana ikiwemo na vituo vya Pemba, je, ni lini Seriali itajenga uzio katika vituo vya kule Pemba?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amejibu kwamba itajenga uzio katika maeneo mbalimbali ya Tanzania, ninavyoelewa kwamba bila ya bajeti uzio hizo hazitoweza kujengwa na hatujaona katika bajeti yake kukiwemo ni makisio hayo. Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba katika mwaka ujao wa 2017/18 iweze kuweka bajeti ya kuwajengea uzio katika vituo mbalimbali na makambi ya Polisi. Ahsante. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza kwamba ni lini vituo vitajengewa uzio. Kama ambavyo nimekuwa nikizungumza kila siku kwamba ujenzi wa uzio, ukarabati wa vituo na kadhalika inategemeana na uwezo wa kifedha. Hata hivyo, kwa kuwa malengo ya kujenga vituo ambavyo kwa mujibu wa PGO namba 287 inaonesha kwamba maeneo ambayo vituo vinavyohitaji kujengewa uzio ni vituo class (a) na (b), lakini kwa mujibu wa PGO namba 314 vilevile inaonesha dhamira ya ujenzi wa uzio ni kuhakikisha usalama unaimaridhwa katika maeneo husika.

Hata hivyo kwa kukidhi ile PGO 314 ni kwamba unaimarisha ulinzi katika maeneo hayo katika kipindi hiki ambako bado bajeti haijaweza kukidhi kujenga vituo vyote. Kwa hiyo, kimsingi ni kwamba tunaweza kutekeleza hili jambo la kuimarisha usalama katika vituo vyetu kwa kuimarisha ulinzi. Kwa kuanzia wakati huo huo tunatafuta fedha za kuweza kujenga uzio.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili ni kwamba anajaribu kupendekeza bajeti ya mwaka ujao wa fedha tuweze kuwa na bajeti ya kutosha kwa ajili ya kujenga uzio. Mimi naamini kabisa chini ya utaratibu ambao Serikali hii ya Awamu ya Tano tunakwenda nao ya kuhakikisha kwamba tunaongeza kukusanya mapato katika nchi hii, basi imani yangu ni kwamba kadri ya miaka inavyokwenda mbele tunaweza kupata bajeti ya kutosha na Wizara ya Mambo ya Ndani kuweza kukabiliana na changamoto mbalimbali ikiwemo ujenzi wa uzio katika vituo vyetu vya Polisi.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea! Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Cecilia Daniel Parezzo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 248

**Mfumo wa Kielektroniki wa Taarifa za Mfuko  
wa Taifa wa Bima ya Afya.**

**MHE. CECILIA D. PAREZZO** aliuliza:-

Serikali kupitia mfumo wa Bima ya Taifa ilitoa tenda kwa kampuni moja binafsi kwa ajili ya kufunga mfumo wa kielektroniki wa kutunza kumbukumbu za wagonjwa na taarifa za Bima:-

(a) Je, ni fedha kiasi gani ilitumika kwa hospitali hizo kufunga mfumo huo?

(b) Je, ni kwa kiasi gani Serikali ilizingatia thamani halisi ya fedha (*value for money*) ukilinganisha na mahitaji makubwa katika sekta ya afya kama madawa, vifaatiba na watumishi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwaniaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Parezzo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Zabuni hii ilitangazwa Kimataifa ambapo kampuni za ndani na za nje ziliruhusiwa kushiriki. Na jumla ya kampuni 17 ziliwasilisha zabuni zao. Baada ya mchakato wa uhakiki, kampuni ya *Maxcom Africa Limited* ya hapa nchini ikishirikiana na kampuni ya *Sevenhills E-Health PVT LTD* ya nchini India zilishinda zabuni hii. Thamani ya zabuni hiyo ni shilingi 5,887,079,539 ikijumuisha kodi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini zabuni hii ilizingatia thamani halisi ya fedha kutokana na uzoefu ambao Wizara yangu imeupata kwa kuimarisha mfumo ya habari na mawasiliano, ambao ni pamoja na vituo kuongeza mapato ambayo yamepelekea kuongezeka kwa ari na tija katika vituo vyetu. Vile vile, zabuni imewezesha upatikanaji wa taarifa na takwimu za uhakika kuhusu huduma za afya nchini. Taarifa hizi zinasaidia katika mipango mbalimbali na utoaji taarifa mbalimbali kwa wadau wa sekta ya afya pamoja na tafiti mbalimbali zinazohusu sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani ya Wizara yangu kuwa, kwa kuwa na mifumo madhubuti ya kielektroniki katika taasisi hii, tutaweza kuongeza tija katika utoaji huduma za afya kwa wananchi wetu hasa tunapoelekea kuwa na Bima ya Afya ya lazima kwa kila mwananchi. Aidha, kwa kupitia zabuni hii sasa Taasisi yetu ya *NHIF* (Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya) imeweza kupata mfumo halisi (*source code*) inayoumiliki na kuwezesha mfumo huu kuwekwa katika vituo vingine nchini katika siku za usoni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso swali la nyongeza!

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo huu umegharimu shilingi bilioni tano kwa hospitali ya Bombo, Tanga, Mwananyamala na kitengo cha *MOI*. Je, Serikali ilifanya utafiti wa gharama halisi za mfumo hii kutoka kwenye taasisi zingine ambazo zimefunga mfumo huu kwa gharama nafuu sana mfano hospitali ya Haydom imefunga kwa gharama ya shilingi milioni 150, Hospitali ya Seliani imefunga kwa gharama ya shilingi milioni 120. Je, mlifanya utafiti?

Swali la pili; kuna tafiti zimefanyika katika kufunga mfumo huu kwenye hospitali za Wilaya inagharimu kati ya shilingi milioni 28 mpaka 35 na hospitali za Rufaa inagharimu kati ya shilingi milioni 75 mpaka milioni 200. Nataka kupata taarifa ya Serikali, hapa hakuna harufu ya ufasadi kwa Hospitali 5 kufunga mfumo kwa shilingi bilioni 5 na hapo hapo, Hospitali ya Bombo ya Tanga ilishakuwa *funded* na Wajerumani kufunga mfumo huu lakini kupitia *NHIF* tena wamepewa fedha katika hii bilioni 5.

Je, mko tayari kufanya utafiti? Kufanya *Special audit*? Kuleta taarifa hapa na wahusika wawajibishwe? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya!

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze kwa maswali yake ya nyongeza. Pili nimpe taarifa tu kwamba kuna tofauti ya mfumo inayofungwa kwenye hospitali za Wilaya na mfumo huu ambao umefungwa kwa ufadhili wa mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

Katika hospitali za Wilaya, tunafunga *Electronic Payment Systems* tu! Hatufungi *Comprehensive, Health Management Information System*, ambayo yenyewe inaunganisha hadi na taarifa za Bima ya Afya na taarifa za Vizazi na Vifo lakini pia taarifa za *claims – Online Claims System* ambayo inawafanya

hospitali husika waweze ku-submit maombi ya madai yao ya Bima ya Afya kwa Bima ya Afya kwa njia ya mtandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo mifumo tunayofunga ni tofauti sana kati ya hii inayofungwa kwenye Hospitali za Wilaya, Hospitali za Mikoa na huu mfumo mahsusi ambao umefungwa katika hizi hospitali 5 kwa majaribio na taasisi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), labda nimwambie tu kwamba kwa kufanya huu utaratibu wa kufunga mifumo ya kielektroniki, Serikali imeweza kufanya mapinduzi makubwa katika makusanyo ya fedha zinazopatikana kwa kutoa huduma za afya kwa wananchi nchini. Mimi hapa ninayezungumza nimekuwa *pioneer* wa wazo hili ndani ya Serikali, hivyo ninafahamu mifumo hii na ninaelewa tunachokifanya ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie kwamba mfumo uliofungwa kwa ufadhili huu wa NHIF umekuja pamoja na *source codes*, kitaalam ndiyo mfumo halisi, ndiyo ile *Architecture* halisi ya mfumo huo. Kwa hiyo, kazi iliyobaki sasa ni kwa taasisi ya NHIF kuchukua hizi *source codes* na kuwekeza kwenye *switch* zile za mtandao kuwekeza kwenye *computer*, kwa ajili ya kutanua mfumo huu kwenye hospitali nyingine mbalimbali. Kwa hivyo, kwa kuwa, tuna *source codes* zetu wenyewe sasa tuna uwezo wa kufunga mfumo huo kwa gharama ya chini zaidi kwenye hospitali nyingine zote nchini na huko ndiko tunakoelekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza hapa, mwezi wa sita taasisi ya Bill & Melinda Gates imeamua kumtuma mke wa Bill Gates, Melinda Gate, kwa ajili ya kuja kuzungumza na Naibu Waziri wa Wizara hii, tayari kuwekeza kwa kiasi kikubwa kwenye mifumo ya taarifa za afya nchini. Haya ni mafanikio ambayo yanakuja kutokana na *initiative* tuliyoifanya ndani ya Serikali ya kuwekeza kwenye mifumo ya *ki-electronic*.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali, ninayo matangazo machache. Tunaanza na Matangazo ya Wageni:-

Waheshimiwa Wabunge, wageni ambao wako sehemu ya Spika, kundi la kwanza ni wageni wa Profesa Joyce Ndalichako, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ambao ni Ndugu Maimuna K. Tarishi, Katibu Mkuu wa Wizara wa Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, karibu sana. Waheshimiwa Wabunge huyu ni mama wa Mheshimiwa Mbunge Zainab Katimba kwa hiyo, karibu sana mama. Mgeni mwingine ni Profesa Simon Msanjila, Naibu Katibu Mkuu Sayansi. Tunaye pia, Dkt. Leonard Akwilapo, Naibu Katibu Mkuu Elimu, Profesa Eustellah Bhalallusesa, Kamishna wa Elimu, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri ni pamoja na Wenyeviti wa Bodi wa Mashirika yaliyo chini ya Wizara, hawa wasimame wote kwa pamoja,

karibuni sana. Tunao pia Makamishna, Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na Maafisa wengine wote kutoka Wizara hii na Taasisi zilizo chini ya Wizara, nao pia wasimame kwa pamoja, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia, ipo familia ya Mheshimiwa Waziri ikiongozwa na Profesa Bakari Mwinyiwiwa, Mume wa Waziri, karibu sana shemeji yetu na Baba yetu. Tunao pia ndugu Dajos Alimosa mtoto wa Waziri. Tunaye pia, Fortunata Majaliwa, mtoto wa Waziri. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge, kundi la kwanza ni Wageni 33 ambao ni Wageni wa Mheshimiwa Mohamed Abood ambao ni Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro. Karibuni sana. *(Makofi)*

Kundi lingine ni Wageni sita wa Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, ambao ni Madiwani wawili na wageni wengine kutoka Chato Mkoa wa Geita wakiongozwa na Mheshimiwa George Magezi - Diwani, Mheshimiwa Joseph Magomamoto – Diwani, hao ndiyo wageni wa Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni 23 wa Mheshimiwa Esther Michael Mmasi ambao ni Marais na Viongozi Waandamizi Serikali za Wanafunzi Vyuho Vikuu vya Mkoa wa Dar-es-Salaam wakiongozwa na Ndugu Leon Erasmo ambaye ni Rais Serikali ya Wanafunzi Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam. Pia Ndugu Ignathio Mkumbo, Spika wa Bunge la Wanafunzi Chuo Kikuu Ardhi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia, tunao Wageni wawili wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni wapigakura wake kutoka Jimboni, Ndugu Imani Mwaipaja na Ndugu Aisha Abdallah. Karibuni sana. Tunao pia, Wageni wawili wa Mheshimiwa Juma Nkamia ambao ni wapigakura wake, Ndugu Justice Lawrance na Ndugu Rahel Magoda, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia, wageni 11 wa Mheshimiwa Dotto Biteko amabo ni Madiwani kutoka Bukombe na Chato wakiongozwa na Mheshimiwa Leokadia Kasase ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Bukombe. Karibuni sana. Tunao pia, Wageni sita wa Mheshimiwa Angelina Malembeka ambao ni Madiwani na Makada wa CCM kutoka Jimbo la Nungwi Zanzibar na Ukonga wakiongozwa na Ndugu Edwin Adam ambaye ni Kaka yake na Mheshimiwa Aziz Mwalile, Diwani Kata ya Msongola, Ilala. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia, wageni sita wa Mheshimiwa Kanyasu Costantine ambao ni Wafugaji na wavuvi kutoka Kanda ya Ziwa. Karibuni sana. Wageni wanne wa



Mheshimiwa Susan Lyimo ambao ni Maafisa kutoka Haki Elimu na TENMET. Karibuni sana. Tunao pia, wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo Bungeni na hawa ni Wanafunzi 10 wa Shahada ya Pili, (Uzamili) kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibuni sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo Wageni waliotufikia siku ya leo. Matangazo mengine ni:

Tangazo la Kikao cha Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo, Mwenyekiti anawatangazia kwamba, leosaa 7:30 mchana mtakutana katika Ukumbi wa Msekwa D, Mwenyekiti anawasihi msiahe kuhudhiria.

Tangazo lingine, Waheshimiwa Wabunge, mnatangaziwa kuwa kesho Ijumaa, tarehe 27 mwezi wa 5, saa 7.30 mchana kutakuwa na warsha ya Wabunge wote kuhusu magonjwa yasiyoambukiza itakayofanyika katika Ukumbi wa Msekwa. Aidha, siku ya Jumamosi tarehe 28 mwezi wa 5 kuanzia saa 4.00 Asubuhi kutakuwa na zoezi la upimaji wa hiyari wa afya litakalofanyika kwenye Zahanati ya Bunge. Waheshimiwa Wabunge, huduma hii itakuwa ni bure na Wabunge wote mnakaribishwa na kusesitizwa mkaangalie afya zenu. (Makofi)

Tangazo lingine; Katibu wa Kamati ya Wabunge Wanawake wa CCM, Mheshimiwa Subira Mgalu, anawatangazia Wabunge wote Wanawake wa CCM kwamba leo tarehe 26 mwezi wa 5 kutakuwa na Kikao cha Wabunge wote wanawake katika Ukumbi wa Msekwa, Saa 7.00 Mchana mara baada ya kuahirisha Bunge. Wabunge wote wa CCM wanawake wanasisitizwa kuhudhuria.

Waheshimiwa Wabunge, juzi uliombwa Mwongozo na Mheshimiwa Esther Matiko, sijui kama bado yupo humu ndani, lakini kwa sababu nimeutaja acha niusome, lakini muktadha wa maombi haya alikuwa anaeleza kuhusu posho ya Askari Magereza, kwamba, wamecheleweshewa posho yao sana kwa hivyo, aliomba Mwongozo wa Kiti kwa namna ambayo ilikuwa ni swali.

Nitanukuu; "Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetaka kupata Mwongozo wako Mheshimiwa Mwenyekiti ni kwa nini Serikali, na nilishamwambia Waziri wa Mambo ya Ndani, Naibu, takribani wiki sasa! Ni kwa nini hawaoni umuhimu wa kuweza kuhakikisha wanawapa posho ambayo ni haki yao tarehe 14 mpaka tarehe 16 Askari Magereza?"

Waheshimiwa Wabunge kwa sababu, Mwongozo huu uliombwa kwa namna ya swali, Mwenyekiti alimuagiza Mheshimiwa Waziri ama Mheshimiwa Naibu Waziri aweze kuleta majibu hayo. Kwa hiyo, kwa nafasi hii nampa muda



Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, aweze kulitolea maelezo suala hilo na huo ndiyo utakuwa Mwongozo wetu, halafu tutaendelea.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia fursa hii ya kuweza kutoa ufafanuzi kuhusiana na Mwongozo ambao ulitolewa na Mheshimiwa Esther Matiko, juu ya ucheleweshaji wa posho za Askari Magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuweza kutoa maelezo hayo nilikuwa naomba nitoe utangulizi ufuatayo; kwanza ni kweli Mheshimiwa Esther Matiko aliniambia hili jambo na binafsi nilimjulisha kwa maandishi kwamba, tukutane kwa ajili ya kumpatia majibu muda kadhaa uliopita. Nilishangaa kumuona amekuja kuleta hapa kwenye Mwongozo. Hata hivyo kwa kuwa, amelileta hapa kuomba Mwongozo kwenye Bunge hili rasmi na mimi nitachukua fursa hii kumfafanulia kupitia Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jingine ambalo nataka nilizungumze kabla ya kutoa hii taarifa fupi ni kwamba, ieleweke wazi kwamba, kutokulipwa kwa posho hizi za Askari Magereza ni za mwezi mmoja tu, huu mwezi ambao tunao sasa hivi. Kwa hiyo, *ration allowance* ilishalipwa kwa miezi yote, isipokuwa mwezi huu tulionao sisi. Niliona hili vilevile niliweke sawa kabla ya kusoma taarifa yangu ili Waheshimiwa Wabunge na Wananchi waweze kufahamu isionekane kwamba, labda Serikali haikulipa, haiwajali! usahihi ni kwamba, ni mwezi huu ndiyo posho hii haijalipwa! Mwezi wa Aprili kwenda nyuma ililipwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jingine, hii ni posho gani? Posho hii kama nilivyozungumza ni *Ration Allowance*, ni Posho ya Chakula, ambapo katika changamoto iliyosababisha ucheleweshaji wa kulipwa posho hii.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba, Askari walikuwa wakulipwa shilingi 180,000 kama *Ration Allowance*, Novemba mwaka jana ndipo ambapo ikaongezwa kutoka shilingi 180,000 mpaka shilingi 300,000. Tukumbuke kwamba, wakati hali hiyo inafanyika tayari bajeti ya mwaka jana ilikuwa imeshapita hivyo, kulikuwa kunahitajika utaratibu wa kufanya *reallocation* ili waweze kulipwa na ndiyo jambo hilo lilisababisha posho hii ikachelewa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine muhimu ambalo nataka niliweke wazi kabla sijasoma hii ripoti kwa ufupi ni kwamba, hivi ninavyozungumza posho hiyo imeshalipwa ya mwezi huu ambao imechelewa. Natarajia wakati wowote kuanzia sasa wanaweza wakaona zimeingia katika akaunti zao. Kwa hiyo, ni

utaratibu tu wa zile *transaction* za masuala ya kifedha yanavyokwenda, lakini kimsingi ni kwamba posho hii tayari imeshalipwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya maelezo hayo mafupi naomba sasa nisome kwa ufupi hii taarifa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tatizo la Askari Magereza kuchelewa kulipwa posho lilijitokeza zaidi katika mwezi huu wa Mei mwaka huu. Itakumbukwa kwamba, mwezi Oktoba, 2015 Serikali iliongeza Posho ya Chakula kwa Askari wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani kutoka shilingi 180,000 hadi kufikia shilingi 300,000 kwa kila Askari. Ilipofika mwezi Februari, 2016 Jeshi la Magereza liliomba Hazina kufanyike uhamisho wa fedha za ndani (*Internal Reallocation*) ili zipatikane fedha za kuweza kuwalipa Askari wake posho za chakula kwa mwezi wa Machi na April mwaka 2016. Uhamisho wa fedha hizo wa ndani ulifanyika na Askari wakalipwa posho ya chakula ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Aprili, 2016 Jeshi la Magereza pia liliomba uhamisho wa fedha za nje ya bajeti ya Jeshi la Magereza kwa ajili ya kulipa Askari wake posho hiyo kwa mwezi wa Mei, 2016 na Juni. Taratibu za kuwalipa posho hizo za chakula Askari wa Magereza kwa mwezi wa Mei, 2016 zimeshakamilishwa na Hazina na zitakuwa zimelipwa ama kukamilika kulipwa wakati wowote wiki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa ulipaji wa posho mbalimbali kwa Maafisa na Askari wa Jeshi la Magereza na Vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, huzingatia maelekezo yanayotolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hapa nazungumzia posho nyingine ambazo Mheshimiwa Mbunge pia alizigusia, kwa mfano posho ya pango pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa maelekezo ya Serikali, Posho ya Pango la Nyumba kwa Askari Magereza hulipwa kupitia orodha ya malipo ya mishahara kwa kutumia mfumo shirikishi wa taarifa za kiutumishi na mishahara ambao unaitwa (*HCMIS Lawson*). Kamishna Mkuu wa Magereza huweka taarifa za Askari wake wasioishi katika nyumba za Jeshi kwenye mfumo huu na kuidhinishwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Mpaka sasahivi wapo Maafisa Askari 3,241 ambao tayari wanalipwa posho hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kuwasilisha. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni ambao walisahaulika kwenye orodha niliyoletewa, hawa ni Viongozi wa Umoja wa Wamiliki wa Shule

Binafsi Nchini, chama chao kinaitwa TAMONGSCO wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu. Mzava ambaye yuko pale juu, pia tunaye Katibu ambaye ni Ndugu Nkonya. Karibuni sana Waheshimiwa Wageni wetu. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu!

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, naomba ukae! Mheshimiwa Sugu, Mwongozo!

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako kwa Kanuni Namba 68(7), naomba niokoe muda!

Mheshimiwa Naibu Spika, nilizungumza ndani ya Bunge hili mapema kwamba, suala la kutokuonesha Bunge *live* ni hatari kwa usalama wa nchi, sasa suala hili limeshaanza kujitokeza kwa sababu, wananchi wameanza ku-*get loose* na kukosa uvumilivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi, *weekend* iliyopita kwenye tamasha la muziki huko Mwanza wananchi wamekosa uvumilivu wamemzomea Waziri wa Habari ambaye wanaamini kwamba, ndiye aliyezuia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Serikali kuzomewa ni Serikali imezomewa. Hiki ni kitu kibaya kwa usalama wa nchi ni kibaya sana na siku atazomewa Waziri Mkuu halafu atakuja atazomewa Rais kwa sababu ni dalili mbaya. (Makofi)

Mimi naomba nisisitize tena, kama Waziri Kivuli, na unipe Mwongozo wako suala hili ni chanzo kimojawapo cha kuvuruga amani ya nchi. Kwa nini, sasa Bunge lako Tukufu lisiiamuru Serikali, liielekeze kwamba, mara moja kwa niaba ya wananchi, tuielekeze Serikali irudishe Bunge *live* kwenye *TBC* mara moja ili kuleta utulivu wa Nchi? (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru kwamba, Mwongozo wangu umepatiwa majibu, lakini nimeomba Mwongozo kwako kwa mambo ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyazungumza. Jambo la kwanza, ni kweli nilimpatia taarifa kama wiki hivi na akaniandikia kwamba, tuzungumze! Hatukuweza kuzungumza!

Jambo la pili ambalo nimesimama posho ya mwezi wa nne, kitu ambacho Naibu Waziri ameongea uwongo mbele ya Bunge lako Tukufu! Askari Magereza walilipwa kuanzia tarehe 5 mwezi wa 5 na ile ni posho ya chakula ambayo inatakiwa ilipwe tarehe 14 mpaka tarehe 16.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine amezungumzia kuhusu posho ya pango kuingizwa kwenye mishahara ya hawa Askari Magereza. Posho ile ya Pango ilizuiliwa ni miaka mitatu sasa hivi kwamba wanaifanyia marekebisho na hawajaanza kuwalipa.

Kwa hiyo, ninaomba Mwongozo wako pale ambapo Waziri anajaribu kulipotosha Bunge na Umma kwa kuongea uwongo kuhusu hizi Posho za Askari Magereza kitu ambacho ni *serious* sana. Hadi leo, amesema wengine wameshapata, atambue hii ya sasa hivi ni *process*, kama ameanza kuifanyia kazi naweza nika-*accommodate* hiyo maana mpaka leo hawajapata, lakini ya mwezi uliopita kusema imelipwa mwezi huo huo wakati wamelipa mwezi wa tano huu! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mwongozo wa Spika!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina, nimesimama!

Waheshimiwa Wabunge, nadhani siku zote huwa tunakumbushwa matumizi ya Kanuni ya 68(7). Mimi nichukue fursa hii kuwakumbusha tena Waheshimiwa Wabunge kwamba, hii Kanuni inazungumzia unaweza kuomba Mwongozo kwenye mambo gani.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 68(7) inasema hivi, "Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadaye kadiri atakavyoona inafaa."

Waheshimiwa Wabunge, kuna mambo mambo matatu, la kwanza, jambo liwe limetokea Bungeni. La pili liwe limetokea Bungeni mapema maana yake siku hiyo.

**WABUNGE FULANI:** Aaah.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, la tatu ni kwamba jambo hilo unakuwa unauliza swali, je, linaruhusiwa au haliruhusiwi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, naomba tuzingatie hayo tunapoomba mwongozo wa Kiti kwenye jambo lolote. Kama kuna jambo limetokea nje ya haya, tutumie Kanuni zingine fursa hiyo ipo. Kwa hiyo, tutumie fursa mahsusi, mwongozo unaombwa kwa jambo lilotokea Bungeni, mapema na kuuliza kama linaruhusiwa au haliruhusiwi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nianze na mwongozo wa kwanza wa Mheshimiwa Joseph Mbilinyi kuhusu suala lililotokea Mwanza kwenye Tamasha la Muziki na kwa mujibu wa maelezo aliyotoa juzi. Kwanza, limetokea nje ya Bunge...

**WABUNGE FULANI:** Aaah.

**NAIBU SPIKA:** Halijatokea mapema hapa na siyo kwamba linaruhusiwa ama halirusiwi humu ndani. Kwa hiyo, huu mwongozo wa Mheshimiwa Joseph Mbilinyi nimeshautolea maelezo. Halijatokea Bungeni, wala mapema wala siyo swali la kuuliza kama linaruhusiwa au haliruhusiwi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mwongozo wa pili ulioombwa ni wa Mheshimiwa Esther Matiko na kwamba Mheshimiwa Waziri amesema uongo. Mheshimiwa Matiko masikitiko ni kwamba alipoanza Mheshimiwa Waziri umemkuta akisoma, alianza kwa kutoa maelezo kwanza, hajatoa maelezo kwamba fedha hizo zililipwa Aprili, hicho hajasema. Alipokuwa anatoa maelezo ya mwanzo Waheshimiwa Wabunge nadhani wote mmemsikia.

Waheshimiwa Wabunge, lakini niseme hivi, kwa majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri ikiwa Mheshimiwa Esther hayo aliyoyasoma anaona hayako sawasawa basi atatuletea yeye ushahidi alionao, tutalinganisha na yale aliyosema Mheshimiwa Waziri halafu tutayatolea mwongozo wakati huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Amina Molel ulikuwa unaomba mwongozo, naomba nitishe miongozo kwa sasa nitakupa nafasi baadaye, Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:** Hoja za Serikali kwamba Bunge likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

## HOJA ZA SERIKALI

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 – Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi**

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nape, nitakupa nafasi baadaye kama nilivyomuahidi Mheshimiwa Amina Molel. Tunaendelea na Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi.

### **HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI MHESHIMIWA PROF. JOYCE LAZARO NDALICHAKO (MB.) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2016/17 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI**

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara kwa Mwaka 2015/2016 na Mpango wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2016/2017. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi Teknolojia na Ufundi kwa mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyenzi Mungu ambaye ameniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kuwasilisha bajeti hii. Aidha, napenda kutoa pole kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu kwa kufiwa na mama yake mpenzi, Mheshimiwa Injini Stella Manyanya, namuombea Mwenyenzi Mungu amtie nguvu katika kipindi hiki kigumu na aipumzishe roho ya marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kabisa na kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa imani kubwa aliyoonesha kwangu kwa kuniteua kuwa Mbunge na Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi. Ninataambua ukubwa na dhamana aliyonipa na changamoto zilizopo katika sekta hii. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais na wananchi wote kwa ujumla kuwa nitafanya kazi hii kwa uadilifu na umahiri wa hali ya juu ili kuweza kuhakikisha kwamba tunakidhi matarajio ya Tanzania katika sekta hii ya elimu ambayo ndiyo uti wa mgongo wa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Tano. Aidha, nampongeza kwa uongozi wake wenye kuzingatia uwajibikaji na utendaji kazi wenye tija na kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwatumikia Watanzania kwa moyo wa dhati kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kuandika historia muhimu ya kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais mwanamke katika nchi yetu tangu tulipopata Uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Job Ndugai, Spika wa Bunge na kwako wewe Naibu Spika, Dkt. Tulia Ackon pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge hili la Kumi na Moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha pili na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi kwa kuwa Makamu wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Peter Serukamba kwa ushauri na maelekezo yenye lengo la kuleta ufanisi katika utendaji wa sekta ya elimu, sayansi, teknolojia na ufundi. Aidha, namshukuru Waziri Kivuli wa Wizara hii Mheshimiwa Susan Lyimo kwa ushirikiano wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nielezee vipaumbele katika sekta ya elimu kwa mwaka 2016/2017. Vipaumbele vyetu vitakuwa kwanza kuinua ubora wa elimu na mafunzo katika ngazi zote za elimu kwa maana ya kwamba kuanzia elimu ya awali hadi elimu ya juu; kuimarisha mifumo na usimamizi wa ithibati na uthibiti wa ubora wa elimu na mafunzo; kuongeza upatikanaji wa fursa za elimu na mafunzo; na kuimarisha tafiti na matumizi ya sayansi, teknolojia na ufundi kwa lengo la kuongeza chachu ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nipitie utelezaji wa bajeti katika mwaka 2015/2016. Katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu ilikusudia kukusanya jumla ya Sh.286,074,571,684.47 na hadi kufikia tarehe 30 Aprili makusanyo ya madhuhuli yalikuwa ni jumla ya Sh.199,422,233,349.12 ambayo ni sawa na asilimia 69.7 ya makadirio.



Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, bajeti ya Wizara yangu ilikuwa ni Sh.1,094,195,824,888.49 na hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2016 fedha ambazo zilikuwa zimepokelewa zilikuwa ni Sh.789,460,338,331.61 ambayo ni sawa na asilimia 72.15 ya bajeti ya Wizara. Aidha, fedha zilizokuwa zimetumika hadi kufikia tarehe 30 Aprili zilikuwa ni Sh.694,148,943,065.89 ambayo ni sawa na asilimia 87.9 ya fedha zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niwapitishe katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2015/2016 na mpango wa bajeti kwa mwaka 2016/2017. Mwaka 2015/2016, Wizara ililenga kusimamia utekelezaji wa shughuli ambazo zimeainishwa katika katika aya ya 15, ukurasa wa 10 wa kitabu cha hotuba yangu. Shughuli hizi ambazo zimeainishwa nitazifafanua, kwanza ilikuwa ni utungaji na utekelezaji wa Sera ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara yangu imekamilisha maandalizi ya mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 na kuhuisha mitaala ya elimu msingi. Aidha, vitabu vya kiada vya darasa la kwanza vinavyoendana na mtaala uliohuishwa vinasambazwa katika mikoa na halmashauri zote nchini. Katika kutekeleza azma ya Serikali ya kutoa elimu msingi bila malipo, Wizara yangu ilitoa Waraka wa Elimu Na.6 ambao umeweka bayana majukumu ya wadau wote muhimu katika utekelezaji wa sera hiyo. Naomba nitaje majukumu kwa wazazi ambayo ni:-

- (i) Kununua sare za shule na michezo, vifaa vya kujifunzia, chakula kwa wanafunzi wa kutwa na kugharamia matibabu;
- (ii) Kulipia nauli ya kwenda shule na kurudi kwa wanafunzi wa kutwa; na
- (iii) Kulipia nauli za wanafunzi wakati wa likizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kutoa wito kwa wazazi, walezi na jamii yote kwa ujumla kuunga mkono juhudi za Serikali za kuhakikisha kuwa watoto wote wanapata elimu ambayo ni haki yao ya kikatiba. Nawasihi sana wazazi kuwawezesha watoto wao kupata mahitaji ya shule na kujenga utamaduni wa kukagua madaftari ya watoto wao ili waweze kujiridhisha kama watoto wanafundishwa inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia nafasi hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali hutoa fedha ya chakula kwa wanafunzi ambao wako shule za sekondari za bweni tu. Kwa hiyo, napenda kutumia nafasi hii kuwafahamisha kwamba kwa shule za kutwa ambazo wananchi wamejenga hosteli na miundombinu ambayo inakidhi shule hizo kuwa shule za bweni, naomba sana na nitumie nafasi hii kuelekeza Maafisa wa Elimu nchini kote



wazitambue na kuwasilisha maombi kwenye Wizara yangu ya kubadilisha hadhi ya shule hizo ili ziweze kuwa shule za bweni. Maombi yakiwasilishwa, Wizara yangu itafanya ukaguzi na kama vigezo vimezingatiwa basi shule hizo zitapandishwa hadhi zitakuwa shule za bweni. Kwa kufanya hivyo, ina maana kwamba Serikali itapeleka fedha za chakula kwa wanafunzi kwa sababu Waraka unaelekeza kwamba fedha ya chakula inapelekwa tu kwenye shule za bweni na sio vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017, Wizara yangu itaendelea na utekelezaji wa Sera ya Elimu iliyotoka mwaka 2014 pamoja na mkakati wake. Wizara itafanya mapitio ya sera, sheria kanuni na taratibu za Wizara pamoja na taasisi zilizo chini ya Wizara yangu kwa lengo la kuimarisha na kuangalia maeneo ambayo yanahitaji marekebisho ili kuweza kuleta ufanisi katika utekelezaji Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014. Aidha, Wizara yangu itakamilisha taratibu za uundwaji wa Bodi ya Kitaalam ya Walimu na itaendelea kuimarisha mpango wa matumizi ya TEHAMA katika ufundishwaji na Ufundishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017, Wizara yangu itaimarisha na kuongeza kasi ya ukuaji wa sayansi, teknolojia na ubunifu ili kufanikisha azma ya Wizara hii. Wizara itafanya mapitio ya sera ikiwa ni pamoja na Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia; Sheria iliyoanzisha Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia yaani *COSTECH*; na Sheria iliyoanzisha Tume ya Nguvu za Atomiki ili kuangalia namna ya kuweza kuleta ufanisi katika maeneo ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie suala la upatikanaji wa fursa za elimu na mafunzo, nitaanza kuzungumzia elimu maalum. Kwa kuzingatia kwamba elimu ni haki ya kila Mtanzania, Wizara yangu imeendelea kupanua fursa za elimu na mafunzo kwa kuimarisha elimu kwa wanafunzi wenye hitaji maalum. Katika mwaka 2015/2016 pamoja na shughuli nyingine ambazo Wizara yangu ilifanya lakini vilevile ilitoa mafunzo ya ufundishaji wa sayansi na hisabati kwa wanafunzi wasioona.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017, Wizara yangu imedhamiria kwa dhati kabisa kuimarisha elimu maalum. Wizara yangu itahakikisha kuwa vifaa muhimu kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum ikiwemo mashine za nukta nundu, fimbo nyeupe, viti vya magurudumu na visaidizi vya kusikia vinapatikana kwa watoto wenye mahitaji maalum. Aidha, Wizara itawezesha upatikanaji wa vifaa vya maabara na vifaa vya kufundishia kwa wanafunzi hao wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nizungumzie suala la kuinua ubora wa elimu na mafunzo nchini kwetu. Wizara yangu inatambua kuwa

uthibiti wa ubora wa shule ni jambo muhimu sana katika kuimarisha ubora wa elimu na mafunzo yanayotolewa katika shule za msingi na sekondari. Hadi kufikia Aprili 2016, jumla ya shule 7,882 zilikuwa zimekaguliwa. Aidha, walimu 292 waliteuliwa kuwa Wathibiti Ubora wa Shule kwa lengo la kuimarisha ukaguzi wa shule. Katika mwaka 2015/2016, Wizara ilifungua Ofisi za Uthibiti wa Ubora wa Shule na kupeleka Wathibiti wa Ubora wa Shule katika Halmashauri mbalimbali ambazo zimeorodheshwa katika kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuthibiti ubora wa shule kwa mwaka 2016/2017, Wizara yangu imepanga kufanya mambo yafuatayo:-

- (i) Kukamilisha ujenzi wa ofisi za uthibiti wa ubora wa shule katika wilaya sita ambazo zimetajwa katika kitabu;
- (ii) Kufuatilia ufundishaji katika elimu ya awali na stadi za Kusoma, Kuandika, Kuhesabu kwa wanafunzi wa darasa la kwanza na la pili;
- (iii) Kuandaa kiunzi cha uthibiti wa ubora wa shule na kuhuisha mwongozo wa uthibiti bora wa shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu katika mwaka 2015/2016 iliendelea kusimamia ubora wa elimu ya ufundi kupitia Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi. Katika mwaka 2016/2017, Wizara itaendelea kukagua vyuo vya ufundi na kufanya tathmini ya ubora wa mafunzo yanayotolewa kama ilivyoainishwa katika aya ya 36, ukurasa wa 21 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeendelea kusimamia ubora wa elimu ya juu na kupita Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania katika mwaka 2015/2016 vyuo vikuu 15 vilikaguliwa kwa lengo la kusimamia ubora. Katika ukaguzi huo ilibainika kwamba Chuo cha St. Joseph *campus* za Songea na Arusha hazikuwa zimekidhi vigezo vya ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Vyuo Vikuu kwa kutumia mamlaka iliyopewa kisheria ilifuta usajili wa *college* za Songea na *campus* ya Arusha za Chuo cha St. Joseph na jumla ya wanafunzi 3,585 waliokuwepo walihamishiwa kwenye vyuo vingine. Hata hivyo, imekuwepo changamoto katika kupokelewa kwa wanafunzi hao kutokana na mapungufu katika elimu ukilinganisha na mwaka wa masomo ambayo walikuwepo. Ili kuhakikisha kwamba wanafunzi hawa wanapata maarifa stahiki baadhi ya vyuo ambavyo wanafunzi hawa wamehamishiwa wameamua ama kuwarudisha mwaka mmoja nyuma ama kuwarudisha *term* moja nyuma au kuwapa mafunzo maalum ili kuweza kuziba lile pengo la ujuzi na maarifa ambalo wameona hawa wanafunzi wanalo ukilinganisha na muda waliokuwa wamekaa vyuoni. Hali hiyo inathibitisha kuwa elimu iliyokuwa inatolewa katika Chuo cha St. Joseph haikuwa inakidhi viwango

vinavyotakiwa na hali hii ndiyo iliyosababisha kuwepo kwa migogoro ya wanafunzi ya mara kwa mara katika chuo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie kuhusu wanafunzi wa kidato cha nne wa chuo hicho cha St. Joseph waliokuwa wanachukua digrii ya miaka mitano ambao wamefukuzwa au wameondolewa chuoni. Kama utakumbuka suala hili liliwasilishwa pia katika Bunge lako Tukufu, siku ya tarehe 17 Mei na Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga. Kwa mujibu wa Kanuni ya 28(11) aliwasilisha Maelezo Binafsi na akiitaka Serikali itoe ufafanuzi kuhusu hatua hiyo. Naomba nitumie fursa hii kutoa ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza Chuo cha St. Joseph kilikuwa na changamoto na katika zoezi la kuwahamisha wanafunzi wa chuo hicho *campus* ya Arusha ilibainika kuwa walikuwepo wanafunzi ambao walidahiliwa kujiunga na digrii ya ualimu kwa masomo ya sayansi wakati hawakuwa na sifa stahiki. Wanafunzi hao walikuwa wamemaliza kidato cha nne wakiwa na ufaulu hafifu ambapo mwanafunzi wa kidato cha nne aliyepata D katika masomo manne tu alikuwa anadahiliwa kujiunga katika chuo kikuu hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kusikitisha zaidi ni kuwa katika kudahili wanafunzi hao ambao walikuwa wanachukua digrii ya ualimu wa sayansi, masomo ya msingi ambayo wanafunzi hao waliyasoma hayakuzingatiwa kabisa. Kwa mfano, wapo wanafunzi waliokuwa wamechukua mkondo wa biashara yaani masomo ya *commerce* na *book-keeping* lakini walidahiliwa katika kusoma digrii ya ualimu wa sayansi. Aidha, wapo wanafunzi ambao hawakuwa wamechukua kabisa masomo ya sayansi, kwa mujibu wa Wizara yangu tunaposema sayansi tunamaanisha fizikia na kemia (*physics and chemistry*), hiyo ndiyo maana ya sayansi. Masomo ya *biology* na hisabati au *biology* na *mathematics* hayo ni masomo ya lazima kwa kila mwanafunzi. Hivyo basi, anayechukua masomo ya sayansi hawezi kuhesabika kwa kigezo cha kuchukua *biology* na *mathematics* kwa sababu hayo ni masomo ya lazima kwa kila mtu. Hata yule anayechukua sanaa, ni lazima asome *biology* na *mathematics*. Kwa hiyo, mapungufu ambayo yamejitokeza ndiyo hiyo pamoja na kwamba mtu ambaye hajachukua masomo ya sayansi wa kidato cha nne lakini alidahiliwa kwenda kusoma digrii ya ualimu wa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile wapo wanafunzi ambao walikuwa wamechukua masomo ya sayansi lakini walikuwa wamefeli katika masomo hayo na bado wakawa wamedahiliwa kwenda kuchukua masomo ya digrii ya sayansi. Kutokana na Tume ya Vyuo Vikuu kubaini udhaifu wa sifa za wanafunzi hao imefuta udahili wa wanafunzi hao. Niseme kwamba Tume ilipokuwa inatangaza mara ya kwanza kufuta udahili wa wanafunzi hao walikuwa wapo wanafunzi 424 lakini hata hivyo zoezi la uhakiki limeendelea na wanafunzi ambao wamebainika wamefikia 489.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hili suala nilielezee vizuri. Naposema wanafunzi 489 hawana sifa, sina maana kwamba hawana sifa za kuchukua digrii. Hawa wanafunzi wamepimwa kwa vigezo vya kuangalia sifa za kuchukua mafunzo ya cheti cha ualimu. Kwa maana hiyo hawa wanafunzi ambao walikuwa wanafanya mafunzo ya digrii ya ualimu kimsingi hawa 489 hawana hata sifa ya kuchukua mafunzo ya cheti cha ualimu. Wanafunzi wengine waliobaki tunaosema wana sifa si kwamba wana sifa ya kusoma digrii lakini wana sifa ya kusoma cheti cha ualimu na Wizara haina pingamizi kama mafunzo yao yataishia katika ngazi ya cheti cha ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimeona niliweke vizuri hili kwamba siyo kwamba hawana sifa za kuchukua digrii, hawa hawajafikisha hata sifa za kuchukua cheti cha ualimu ambayo ndiyo ngazi ya chini kabisa ya sifa za ualimu. Wakati wanafunzi hawa wanadahiliwa mara ya kwanza mwaka 2013/2014 sifa ya chini kabisa ya kujiunga na cheti cha ualimu ilikuwa ni *point* 27. Kwa hiyo, hawa wengine walikuwa na *point* 31, *division four*, kwa hiyo hata kwenye cheti cha ualimu walikuwa hawastahili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na dosari hiyo ambayo Wizara yangu imesikitika sana, Serikali imechukua hatua ya kuivunja Kamisheni ya Tume ya Vyuo Vikuu na kuwasimamisha kazi watendaji wanne ili kupisha uchunguzi ambao unaendelea kufanyika sasa hivi. Kwa kweli tunataka uchunguzi wa kina kwa sababu haiwezekani elimu ikafanywa ndiyo shamba la bibi au kitu gani sijui yaani watu ambao hawana sifa tunawapeleka wakachukue ualimu halafu atamfundisha mtoto wa nani? Kwa hiyo, uchunguzi wa kina lazima ufanyike na wote watakaobainika kuhusika na jambo hili hatua kali za kinidhamu na za kisheria zitachukuliwa dhidi yao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nizungumzie uboreshaji wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Mazingira ya kufundishia na kujifunzia yana mchango mkubwa katika kuinua ubora wa elimu nchini na nafikiri nilimjibu jana Mheshimiwa Mariam kwenye swali lake. Hivyo basi, katika mwaka 2015/2016 Wizara iliandaa mpango wa ukarabati wa shule kongwe hapa nchini. Napenda kuliharifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu imedhamiria kwa dhati kabisa kuboresha elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia tunaanza na shule 33 kongwe ambazo tumeziorodhesha kwenye hotuba na shule kongwe nchini kwa maana ya zile shule tulizozioea Ihungo, Tabora Girls ambayo ndiyo shule yangu niliyosoma, Tosamaganga, Nangwa, Kibiti na nyinginezo ambazo zimeahinishwa kwenye kitabu changu, Wizara yangu inataka zisimame na ziwe na heshima ile ziliyokuwa wakati wetu ambayo imeniwezesha mimi leo hii kusimama hapa kama Waziri wa Elimu kutokana na elimu bora ambayo nimeipata. Hivyo basi, kama sisi tuliweza kupata elimu iliyo bora katika shule zetu za kawaida kwa nini

hawa watoto wetu wa sasa wasiipate? Naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu zile shule zitarudi katika hadhi yake, zitatoa elimu bora, zitakuwa na mazingira mazuri na Watanzania watanufaika kama ambavyo sisi tumenufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka leo hii niseme kwamba ni kutokana na malezi mazuri sana na mafunzo mazuri sana niliyopata kwa walimu wangu ndiyo yaliyoniwezesha kufika hatua hii na kamwe sitasahau walivyonilea. Kwa kuwaenzi basi, lazima na mimi nihakikishe kile kidogo au kile kizuri walichonipatia na wenzangu niwarithishe. Hiyo ndiyo itakuwa shukrani na heshima kwa Walimu ambao wameniwezesha nisimame mbele yenu. Nawashukuru sana Walimu wangu kwa elimu lakini pia na kwa malezi mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017, Wizara kupitia mamlaka ya elimu pia itaendelea kufanya ukarabati wa shule kongwe tutaongeza saba. Kwa hiyo, hizi 33 hamtazona kwenye vitabu vya mafungu kwa sababu tumeangalia katika mafungu yetu. Sasa hivi tunavyoongea, timu ya wataalam kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi imeshaenda katika hizi shule kufanya *conditional survey* yaani kuangalia hali halisi ya miundombinu na kuweza kubainisha mahitaji. Kwa hiyo, tutaongeza pia nyumba za Walimu 30 ambazo zitakuwa na uwezo wa kuchukua Walimu 180.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu itaendelea pia kuboresha mazingira ya kujifunzia katika elimu ya juu. Utaratibu au mipango itakayofanyika imeainishwa katika aya ya 53 - 55 ya kitabu cha hotuba yangu ambayo inapatikana katika ukurasa wa 29 hadi 32.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kuwa ujenzi wa hospitali ya kufundishia ya *campus* mpya ya Mloganzila ya Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili yaani MUHAS iliyojengwa kwa ushirikiano wa Serikali yetu pamoja na Serikali ya Korea ya Kusini inatarajia kukamilika mwezi Juni 2019. Waheshimiwa Wabunge wakiangalia nyuma ya vitabu vyao, huo ndiyo mwonekano wa hiyo hospitali ya kufundishia ambayo itakuwa na uwezo wa kulaza wagonjwa 571 kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba tunaposema hospitali ya kufundishia maana yake nini? Hii *campus* kwa sababu iko chini ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Afya na Sayansi cha Muhimbili...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** *(Aliongea bila kipaza sauti)*

**MBUNGE FULANI:** Endelea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee, muache Waziri amalize, kwa sababu sasa anashindwa ku-concentrate kusoma kwa sababu wewe unaongea na inabidi asikilize, Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA ELIMU, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa natoa tu ufafanuzi kwamba hospitali ya kufundishia maana yake ni sehemu ambayo wale wanafunzi katika chuo watakuwa wanaenda kupata experience au kupata uzoefu wa jinsi ya kuwahudumia wagonjwa. Katika mwaka 2016/2017, Wizara yangu pia, itaanza ujenzi wa Kituo Mahiri cha Magonjwa ya Moyo na Mishipa ya Damu, cha Afrika Mashariki katika eneo hilo la Mloganzila. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la huduma za maktaba. Huduma za maktaba zinachangia katika utoaji wa elimu bora na katika mwaka 2015/2016, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za maktaba na kusambaza vitabu vya rejea 68,000 kwa masomo yote katika maktaba za mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017, Wizara kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba, itaendeleza miundombinu ya Chuo cha Ukutubi na uhifadhi wa nyaraka kilichoko Bagamoyo na kujenga maktaba ya chuo. Aidha, itakarabati majengo ya maktaba za Mikoa ya Tabora, Tanga na Rukwa na kuanza na matayarisho ya ujenzi wa maktaba za Mikoa ya Singida na Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ina jukumu la kufanya tafiti na kutoa huduma kwa jamii. Baadhi ya tafiti zenye matokeo makubwa kwa jamii zilizofanyika 2015/2016 zimeainishwa katika aya ya 63, ukurasa wa 36 - 38 wa kitabu cha hotuba. Katika mwaka 2016/2017, Wizara itaendelea kufanya tafiti na tafiti ambazo zimepangwa zimeainishwa katika aya ya 65, ukurasa wa 39 - 40 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu. Wizara yangu inatambua umuhimu wa sayansi na teknolojia na ubunifu pamoja na matumizi yake katika kuleta maendeleo ya nchi yetu. Wizara imekamilisha uandaaji wa Mpango wa Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia na mkakati wa utekelezaji. Katika mwaka 2016/2017, Wizara yangu imepanga kuanzisha maabara na kupanua vituo vya sayansi, teknolojia na ubunifu. Aidha, Wizara itashirikiana na Ofisi za Halmashauri za Miji na Wilaya ili kubaini wagunduzi na wabunifu kwa lengo la kuendeleza vipaji vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kuelezea utekelezaji wa masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika taasisi zinazosimamia sekta hiyo. Naomba nianze na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH). Katika mwaka 2015/2016, Tume ya Sayansi imeratibu mtandao wa kuunganisha vyuo



vikuu na taasisi za utafiti na imeweza kuunganisha taasisi 28. Vilevile imesimamia Kituo cha Kuendeleza Ubunifu yaani BUNI *Innovation Hub*. Kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Tume imeanzisha Atamizi ya TEHAMA iliyoko katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume na Atamizi ya Usalifu wa Mazao ya Kilimo iliyopo katika Kituo cha Utafiti cha Kilimo Kizimbani Zanzibar. Mwaka 2016/2017, Wizara yangu kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia itaendelea kugharamia tafiti zenye lengo la kutatua matatizo ya wananchi. Pia itagharimia uanzishwaji wa atamizi katika vyuo vya elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam yaani *DIT*. Taasisi hii imeendelea kutoa mafunzo ya teknolojia kwa lengo la kuongeza ujuzi katika fani mbalimbali. Aidha, iliendelea kuboresha mtandao wa mawasiliano wa tiba ambao unaitwa *Telemedicine* unaunganisha hospitali saba za taifa. Hospitali husika zimeahinishwa katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie Tume ya Nguvu za Atomiki. Katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki imeendelea na jukumu lake la kudhibiti mionzi katika migodi na vituo vya huduma kwa kufanya mambo yafuatayo:-

(i) Kukagua migodi na kuhakikisha kuwa viwango vya mionzi vinavyotumika kwenye sehemu za kazi na vyakula vinadhibitiwa; na

(ii) Imesajili vyanzo vya mionzi na vituo vinavyomiliki vyanzo vya mionzi na kupima mionzi itokanayo na minara ya simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017, Wizara yangu itaendelea na mikakati ya kuhakikisha kuwa wananchi na viumbe hai hawaathiriki na mionzi hatarishi hasa kwenye sehemu zao za kazi. Hivyo, ukaguzi wa migodi mitano mikubwa utafanyika na vituo 120 vyenye vyanzo vya mionzi vitakaguliwa. Matokeo ya ukaguzi yatasaidia katika kuandaa taratibu yaani *standard operating procedures* za kufanya kazi katika maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kutoa maelezo kuhusu baadhi ya taasisi na wakala zilizo chini ya Wizara yangu. Kutokana na muda sitaweza kuzitungumzia taasisi zote lakini zimeorodheshwa katika kitabu changu na naomba nianze na Tume ya Taifa ya Vyuo Vikuu. Tume ya Taifa ya Vyuo Vikuu kwa mwaka 2015/2016, ilifanya mapitio ya miongozo ya udhibiti wa ubora wa elimu ya juu nchini na katika mwaka 2016/2017, Tume itaendelea kuratibu na kusimamia udahili wa wanafunzi, kuboresha mfumo wa ukusanyaji taarifa kutoka kwa vyuo vikuu, vyuo vya elimu ya juu na kutathimini programu za masomo katika vyuo vikuu nchini.



Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie kuhusu suala la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. kwa mwaka 2015/2016, Wizara yangu kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu iliendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaodahiliwa kusomea masomo ya vipaumbele ikiwemo udaktari, uwalimu wa sayansi, hisabati pamoja na fani adimu kama vile uhandisi wa gesi pamoja na uhandisi wa umwagiliaji. Aidha, Serikali imeendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wa masomo mengine kwa kuzingatia viwango vya uhitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inatambua changamoto zilizopo katika utoaji mikopo na katika mwaka 2016/2017, Wizara imeboresha mwongozo wa utoaji mikopo ili tuweze kutoa kipaumbele zaidi katika uhitaji. Uhitaji utakuwa ndiyo kipaumbele zaidi kuliko utaratibu ambao ulikuwa unatumika, tulikuwa tunaangalia zile fani ambazo ni za kipaumbele. Kwa hiyo, kipaumbele kitawekwa kwa waombaji ambao ni wenye uhitaji mkubwa na waombaji waliodahiliwa kwenye fani za vipaumbele vya kitaifa yaani watapatiwa mikopo lakini kwa kuzingatia uhitaji wao. Kwa sababu mtu anaweza akawa anasoma fani ambayo ni kipaumbele cha Taifa lakini mzazi wake ana uwezo mkubwa. Kwa hiyo, tutawapa kipaumbele katika kuwapa mikopo lakini utoaji huo wa mikopo utazingatia upimaji wa uwezo yaani *Means Testing*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu urejeshwaji wa mikopo ya elimu ya juu. Urejeshwaji wa mikopo bado upo katika kiwango kisichoridhisha na changamoto zilizopo ni pamoja na kutokuwepo kwa mikakati thabiti ya ufuatiliaji wa wakopaji na udhaifu wa Sheria ya Bodi ya Mikopo ambapo makato ya marejesho ya mikopo kutoka kwenye mishahara siyo ya lazima yaani *statutory deductions*. Aidha, bado kuna muitikio mdogo wa wanufaika kujitokeza na kuanza kurejesha mikopo pamoja na waajiri kutokupeleka wanufaika waweze kurejesha mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na changamoto hiyo na kuongeza kasi ya marejesho ya mikopo, katika mwaka 2016/2017, Wizara yangu itafanya mapitio ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ili kuimarisha urejeshwaji na itaendelea kuimarisha mifumo ya urejeshwaji wa mikopo. Naomba nichukue nafasi hii kuwakumbusha wanufaika wote wa mikopo ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hata Waheshimiwa Wabunge humu ndani wengine baadhi yenu ni wanufaika wa mikopo, naomba kwa heshima kabisa, niwakumbushe wale ambao hamjarejesha mikopo yenu tafadhali kwa heshima na taadhima tuirejeshe ili Watanzania wengine wenye uhitaji waweze kunufaika ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge. Nawasihi wale wote wenye uwezo wa kurejesha mikopo kwa mkupuo mmoja wafanye hivyo ili kupunguza utegemezi wa Bodi ya Mikopo kwa Serikali. Ikifanyika hivyo, fedha za Serikali

zinazotengwa kwa ajili ya Bodi ya Mikopo zitatumika katika kuboresha maeneo mengine ya sekta ya elimu ambayo pia yana uhitaji muhimu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa wananchi wote waliojitokeza na kulipa mikopo yao kwa mkupuo mmoja baada ya Bodi ya Mikopo kuwapa siku 60 ambazo ziliisha lakini Bodi imeongeza siku 30. Naamini kwamba watu watajitokeza zaidi na baada ya hapo majina ya ambao watakuwa hawajalipa yatawekwa kwenye magazeti ili kuongeza kasi ya urejeshaji. Kwa hiyo, naomba sana Waheshimiwa Wabunge kama mna mikopo, mimi ni mwenzenu nisingependa majina yenu yakae kwenye magazeti, kwa heshima kubwa naomba turejeshe mikopo kama tunayo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu Taasisi ya Elimu Tanzania. Katika mwaka 2015/2016, Taasisi ya Elimu imeboresha mitaala ya elimu msingi na imeandaa mihtasari. Aidha, Taasisi ya Elimu imekusanya maoni ya wadau kuhusu mahitaji ya utekelezaji wa mtaala wa elimu ya sekondari. Taasisi pia imesimamia uchapaji wa vitabu vya kiada kwa darasa la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, naomba kutoa taarifa kwa Bunge lako Tukufu kwamba kwa bahati mbaya mzabuni mmoja aliyekuwa amepewa kutoa kitabu cha Najifunza Kusoma *Part One* na *Part Two*, kitabu alichokichapa kimekuwa hakina ubora. Naomba niseme kwamba makosa yaliyobainika si makosa ya kiudhui bali ni makosa ya uchapaji. Makosa hayo ni mfano mambo ya rangi haijatokea vizuri na kadhalika. Hivyo basi, kwa kuwa mzabuni alipatikana kwa utaratibu wa kutumia Sheria ya Manunuzi na kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Manunuzi, mzabuni aliyekuwa amepewa kazi hiyo ametakiwa kurekebisha dosari zake kwa gharama zake mwenyewe. Kwa hiyo, anachapa vitabu vingine kwa gharama zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017, Taasisi imelenga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- (i) Kutayarisha kitabu cha kiada cha elimu msingi na sekondari vinavyozingatia mtaala ulioboreshwa; na
- (ii) Kuboresha mtaala wa elimu ya msingi na sekondari na mitaala ya elimu ya ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Mitihani la Tanzania. Ili kusimamia upimaji na utoaji wa tuzo, Serikali kupitia Baraza la Mitihani la Tanzania liliendesha mitihani ya upimaji endelevu yaani *formative assessment* kwa watahiniwa wa darasa la nne na kidato cha pili. Aidha, Baraza la Mitihani

limeendesha mitihani ya kumaliza elimu ya msingi, kidato cha nne pamoja na mitihani wa maarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017, Baraza la Mitihani la Tanzania litaboresha mfumo wake wa ukusanyaji na uchakataji wa takwimu na kuweka mfumo wa kumtambua mwanafunzi. Aidha, litaimarisha vitendea kazi kwa kusimika mashine ambao zitaweza kufunga bahasha bila kuhitaji usaidizi wa binadamu yaani *automatic wrapping and parking machines*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi yaani VETA. Shughuli za Mamlaka hiyo zimeorodheshwa katika ukurasa wa 57-59 na katika aya ya 91.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie Mamlaka ya Elimu ambayo shughuli zake pia zinapatikana katika kitabu. Katika mwaka 2016/2017, itaendelea na jukumu lake za kuboresha miundombinu na kutatua changamoto za uhaba wa walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya miradi yameorodheshwa katika aya ya 108 – 134, ukurasa wa 64 - 82 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani. Napenda kutambua mchango mkubwa sana unaotolewa na viongozi wenzangu katika Wizara katika kufanikisha majukumu yangu. Kwa namna ya pekee, namshukuru sana Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, Naibu Waziri kwa ushirikiano wake mkubwa anaonipatia, namshukuru Bi. Maimuna Kibenga Tarishi, Makatibu Wakuu, Kamishna wa Elimu na watendaji wote wa Wizara yangu kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia. Nawashukuru pia viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi, Chama cha Walimu, Wamiliki wa Shule Binafsi, wanataaluma na wadau wote wa elimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru pia familia yangu ikiongozwa na mume wangu mpenzi, Profesa Bakari Mwinyiwiwa kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua pia mchango wa wadau wa maendeleo ya elimu na kwa sababu ya muda sitaweza kuwataja lakini wameorodheshwa katika kitabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo yote, sasa kwa unyenyekevu mkubwa kabisa, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh.1,396,929,798,625.00 ili kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizo mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:-

(i) Sh.499,272,251,000.00 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo Sh.386,904,995,000.00 ni kwa ajili ya mishahara na Sh.112,367,256,000.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

(ii) Fedha za miradi ya maendeleo ni Sh.897,657,547,625.00 na katika fedha hizo Sh.620,693,856,575.00 ni fedha za ndani na Sh.276,963,691,050.00 ni fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kutoa shukrani za dhati kabisa kwako wewe binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI MHESHIMIWA  
PROF. JOYCE LAZARO NDALICHAKO (MB.) AKIWASILISHA BUNGENI  
MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2016/17  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika,** kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara kwa mwaka 2015/16 na Mpango wa Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2016/17. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa mwaka wa fedha 2016/17.

**2. Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa na kwa heshima kubwa napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa imani kubwa aliyoonesha kwangu kwa kuiteua kuwa Mbunge na Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi. Ninatambua ukubwa wa dhamana aliyonipa na changamoto zilizopo katika Sekta hii. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais na wananchi wote kwa ujumla kuwa nitafanya kazi hii kwa

uadilifu na umahiri wa hali ya juu, ili kuhakikisha kuwa tunakidhi matarajio ya Watanzania katika sekta hii ya elimu ambayo ndiyo uti wa mgongo wa maendeleo ya taifa letu.

**3. Mheshimiwa Spika,** naomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Tano. Aidha nampongeza kwa uongozi wake wenye kuzingatia uwajibikaji na utendaji wenye tija kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwatumikia kwa moyo wa dhati wananchi wote.

**4. Mheshimiwa Spika,** Napenda pia kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kuandika historia muhimu sana ya kuwa Makamu wa kwanza mwanamke tangu nchi yetu ilipopata uhuru. Vilevile, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, kwa kuteuliwa na Rais na baadaye kuthibitishwa na Bunge lako kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Job Ndugai (Mb) na Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb) kwa kuchaguliwa kuwa Spika na Naibu Spika wa Bunge hili la 11 pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge.

**5. Mheshimiwa Spika,** napenda pia kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha Pili na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi kuwa Makamu wa Pili wa Rais.

**6. Mheshimiwa Spika,** ninapenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Peter Serukamba, kwa ushauri mzuri waliotupatia wakati wa maandalizi ya Bajeti hii. Wizara yangu imezingatia na itaendelea kuzingatia ushauri na maelekezo ya Kamati kwa lengo la kuleta ufanisi katika utendaji wa Sekta ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia. Aidha, napenda kumshukuru Waziri kivuli wa Wizara hii, Mheshimiwa Susan Lyimo, kwa ushirikiano wake.

**7. Mheshimiwa Spika,** Hotuba yangu imegawanyika katika sehemu kuu Saba: Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi; Sehemu ya Pili ni Dira, Dhima na Majukumu ya Wizara; Sehemu ya Tatu ni Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2016/17; Sehemu ya Nne ni Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2015/16; Sehemu ya Tano ni Mapitio ya Utekelezaji kwa mwaka 2015/16 na Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2016/17; Sehemu ya Sita ni Shukrani; na sehemu ya Saba ni Maombi ya Fedha.

## **2.0 DIRA, DHIMA NA MAJUKUMU YA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI**

### **DIRA NA DHIMA YA WIZARA**

**8. Mheshimiwa Spika,** Dira ya Wizara ni kuwa na Mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa, stadi, umahiri, uwezo na mitazamo chanya ili kuweza kuchangia katika kuleta maendeleo ya Taifa. Aidha, Dhima ya Wizara ni kuinua ubora wa elimu na mafunzo na kuweka mifumo na taratibu zitakazoweza kupata idadi kubwa ya Watanzania walioelimika na wanaopenda kujielimisha zaidi ili waweze kuchangia katika kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa letu.

### **MAJUKUMU YA WIZARA**

**9. Mheshimiwa Spika,** Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi ni kama ifuatavyo:

(i) kutunga na kutekeleza Sera za Elimu, Utafiti, Huduma za Maktaba, Sayansi, Teknolojia, Ubunifu na Uendelezaji wa Mafunzo ya Ufundi;

(ii) kuendeleza Elimumsingi kwa Kutoa Ithibati ya Mafunzo ya Ualimu na Maendeleo ya Kitaalamu ya Walimu;

(iii) kubainisha Vipaji na Kuviendeleza;

(iv) kusimamia Uendelezaji wa Mafunzo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi;

(v) kusimamia Mfumo wa Tuzo wa Taifa;

(vi) kuainisha Mahitaji ya Nchi katika Ujuzi na Kuuendeleza;

(vii) kuweka Viwango vya Taaluma ya Ualimu;

(viii) kusimamia Ithibati na Uthibiti wa Shule;

(ix) kusimamia Huduma za Machapisho ya Kielimu;

(x) kutegemeza/kuimarisha utumiaji wa Sayansi, Uhandisi, Teknolojia na Hisabati;

(xi) kuendeleza Wataalamu wa ndani katika Sayansi, Teknolojia na Ubunifu;

- (xii) kuratibu utafiti katika Sayansi na Teknolojia;
- (xiii) uendelezaji wa Rasilimaliwatu na Uongezaji Tija ya Watumishi walio chini ya Wizara; na
- (xiv) kuratibu Shughuli za Idara, Mashirika, Wakala, Programu na Miradi iliyo chini ya Wizara.

### **3.0 VIPAUMBELE VYA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI**

**10. Mheshimiwa Spika**, Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025) imelenga kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Katika juhudi za kufikia lengo hili, Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi ina jukumu la kuandaa wataalamu wenye ujuzi na maarifa watakaotoa mchango wenye tija kwa maendeleo ya nchi yetu. Wizara yangu inatambua kuwa utekelezaji wa azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuwa na uchumi wa viwanda inategemea kwa kiasi kikubwa ufanisi katika Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Ubora wa rasilimali watu ni jambo la msingi sana katika kuhakikisha kuwa tija na ufanisi vinakuwepo katika Sekta zote muhimu ili kuchochea kasi ya ukuaji uchumi na hatimaye kuiwezesha nchi yetu kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

**11. Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia mwelekeo huo, katika mwaka 2016/17, vipaumbele vya Sekta ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi ni kama ifuatavyo:

- (i) kuinua ubora wa elimu na mafunzo katika ngazi zote za elimu na mafunzo nchini;
- (ii) kuimarisha mifumo na usimamizi wa Ithibati na Uthibiti wa Ubora wa Elimu na mafunzo;
- (iii) kuongeza upatikanaji na ushiriki katika fursa za elimu na mafunzo; na
- (iv) kuimarisha tafiti na matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa lengo la kuongeza chachu ya maendeleo.

### **4.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2015/16**

**12. Mheshimiwa Spika**, naomba nianze kutoa tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/16 kuanzia tarehe 1 Julai, 2015 hadi tarehe 30 Aprili, 2016.



### **Ukusanyaji wa Maduhuli Kwa Mwaka 2015/16**

**13. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16, Wizara ilikusudia kukusanya jumla ya **Shilingi 286,074,571,684.47** ambapo Shilingi **9,268,457,100.00** zilitarajiwa kukusanywa na Idara wakati Shilingi **276,806,114,584.47** zilitakiwa kukusanywa na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Makusanyo ya maduhuli hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2016 yalikuwa ni jumla ya **Shilingi 199,422,233,349.12** ambayo ni sawa na **asilimia 69.7** ya makadirio. Kati ya fedha hizo, Shilingi **5,723,343,678.36** zilikusanywa na Idara na **Shilingi 193,698,889,670.76** zilikusanywa na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

### **Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka 2015/16**

**14. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2015/16 bajeti ya Wizara ilikuwa ni **Shilingi 1,094,195,824,888.49** (Matumizi ya kawaida **Shilingi 511,525,227,000.00** na Matumizi ya maendeleo **Shilingi 582,670,597,888.49**). Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2016 fedha ambazo zimekwishatolewa na Hazina zilikuwa **Shilingi 789,460,338,381.61** (Matumizi ya kawaida **Shilingi 351,284,829,898.00** na Matumizi ya Maendeleo **Shilingi 438,175,508,483.61**) sawa na **asilimia 72.15** ya bajeti ya Wizara. Aidha, fedha zilizotumika hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2016 zilikuwa ni **Shilingi 694,148,943,065.89** (Matumizi ya kawaida **Shilingi 313,796,049,657.61** na Matumizi ya maendeleo **Shilingi 380,352,893,408.28**) sawa na **asilimia 87.9** ya fedha zilizotolewa.

### **5.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA MWAKA 2015/16 NA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2016/17**

**15. Mheshimiwa Spika**, mwaka 2015/16, Wizara ililenga kusimamia utekelezaji wa mambo makuu yafuatayo:

- (i) utungaji na utekelezaji wa Sera za Elimu;
- (ii) upatikanaji wa fursa za elimu na mafunzo;
- (iii) ithibati ya Shule;
- (iv) uthibiti ubora wa elimu;
- (v) mafunzo ya Ualimu, hususan wa Sayansi, Hesabu, Ufundi (ikiwemo ufundi sanifu maabara), Lugha na KKK;
- (vi) uratibu wa shughuli za Taasisi na Wakala; na
- (vii) usimamizi wa utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali.

## 5.1 UTUNGAJI NA UTEKELEZAJI WA SERA YA ELIMU

**16. Mheshimiwa Spika**, mojawapo kati ya majukumu ya msingi ya Wizara yangu ni kubuni na kutunga Sera mbalimbali za kusimamia Elimu, Mafunzo ya Ufundi, Sayansi, Teknolojia, Ubunifu, Huduma za Maktaba na Utafiti.

### **Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo (2014)**

**17. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, yafuatayo yalifanyika:

(i) kutafsiri Sera ya Elimu na Mafunzo (2014) kwa lugha ya Kiingereza na kukamilisha maandalizi ya Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Elimu;

(ii) kufanya uchambuzi wa mahitaji ya mabadiliko ya sheria ili kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo (2014);

(iii) kuhuisha mitaala ya elimu ya awali, elimu ya msingi na elimu ya sekondari. Aidha, vitabu vya kiada vya Darasa la Kwanza vinavyoendana na Mtaala uliohuishwa vinasambazwa kwenye Mikoa na Halmashauri zote nchini; na

(iv) ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

### **Utekelezaji wa Elimumsingi bila Malipo**

**18. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza azma ya Serikali ya kutoa Elimumsingi bila Malipo, Wizara yangu ilitoa Waraka wa Elimu Namba 6 wa mwaka 2015 kwa lengo la kutoa mwongozo wa namna ya kutekeleza Elimumsingi bila malipo. Waraka wa Elimu Na. 6 umeweka bayana majukumu ya wadau wote muhimu katika utoaji wa Elimumsingi bila Malipo ambapo imeainishwa kuwa wazazi wanatakiwa kufanya yafuatayo:

(i) kununua sare za shule na michezo, vifaa vya kujifunzia, chakula kwa wanafunzi wa kutwa na kugharamia matibabu kwa watoto wao.

(ii) kulipia nauli ya kwenda shule na kurudi kwa wanafunzi wa kutwa.

(iii) kulipa nauli za wanafunzi wakati wa likizo; kununua vifaa kwa ajili ya malazi shuleni na vifaa vya kujifunzia.

**19. Mheshimiwa Spika**, natoa wito kwa wazazi na walezi kuunga mkono juhudi za Serikali za kuhakikisha kuwa watoto wote wanapata elimu. Ni

muhimu wazazi mkawawezesha watoto wenu kupata mahitaji ya shule na muhimu zaidi mjenge utamaduni wa kukagua madaftari ya watoto wenu ili kujiridhisha kama wanafundishwa shuleni.

**20. Mheshimiwa Spika,** serikali hutoa fedha ya chakula kwa wanafunzi wa bweni tu. Hivyo, kama kuna shule za sekondari ambazo zimesajiliwa kama shule za kutwa lakini wamejenga Hosteli na miundombinu inayokidhi vigezo vya kuwa shule za bweni, Maafisa Elimu wazitambue na wawasilishe maombi kwenye Wizara yangu ya kuomba kuzibadilisha hadhi. Endapo zitakuwa zimekidhi vigezo muhimu zitabadilishwa na kuwa shule za bweni. Kwa kufanya hivyo, wanafunzi wataweza kutengewa fedha ya chakula kama ilivyoainishwa kwenye Waraka wa Elimu Na. 6 wa mwaka 2015.

#### **Mpango wa Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo (2014) kwa mwaka 2016/17**

**21. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Wizara yangu itaendelea na utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo (2014) na Mkakati wake. Wizara itafanya mabadiliko ya Sheria ya Elimu na kupitia Sheria, Kanuni na Taratibu za taasisi zilizo chini ya Wizara, hususan Baraza la Mitihani, Taasisi ya Elimu Tanzania, Taasisi za Ithibati na Uthibiti, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na Mamlaka ya Elimu Tanzania kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo (2014) kwa ufanisi. Aidha, Wizara itakamilisha taratibu za uundwaji wa Bodi ya Kitaalamu ya Walimu.

**22. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Wizara yangu itaendelea kuimarisha Mpango wa matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji. Vilevile, Wizara itatoa mwongozo wa kuwatambua na kuwaendeleza wanafunzi wenye vipaji, vipawa na mahitaji maalumu na wenye kasi kubwa ya kujifunza masomo ya Sayansi na Hisabati ili kuweza kuwaendeleza katika fani mbalimbali za teknolojia.

#### **Sera ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu**

**23. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Wizara yangu imedhamiria kuimarisha na kuongeza kasi ya ukuaji wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa kukamilisha mapitio ya Sera zifuatazo:

(i) Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1996 na kutunga sera mpya ya Taifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu;

(ii) Sheria Na. 7 ya mwaka 1986 iliyoanzisha Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) na kutunga sheria mpya ya Maendeleo ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu; na

(iii) Sheria Na. 7 ya mwaka 2003 iliyoanzisha Tume ya Nguvu za Atomiki (Tanzania Atomic Energy Commission - TAEC).

## 5.2 UPATIKANAJI WA FURSA ZA ELIMU NA MAFUNZO

### Udahili wa wanafunzi vyuoni

**24. Mheshimiwa Spika**, Serikali ina lengo la kuendelea kuongeza fursa za Elimu na Mafunzo ili kuandaa rasilimali watu itakayochangia maendeleo ya taifa. Kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Wizara iliendelea kuratibu udahili wa wanafunzi ambapo kwa mwaka 2015 wanafunzi 189,687 walidahiliwa katika vyuo mbalimbali vya ufundi. Aidha, kwa kupitia Baraza la Elimu ya Ufundi wanafunzi 75,186 walidahiliwa kwenye vyuo mbalimbali kupitia mfumo wa pamoja wa udahili.

**25. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kupitia Tume ya Vyuo Vikuu imeendelea kuratibu udahili wa wanafunzi wanaojiunga na Elimu ya Juu kupitia Mfumo wa Udahili wa Pamoja (Central Admission System) wa kudahili wanafunzi wa Digrii ya kwanza. Katika mwaka 2015/16 wanafunzi 65,064 wa Digrii ya kwanza walidahiliwa wakiwemo wanawake 22,225 sawa na asilimia 34.2 na kufanya jumla ya wanafunzi wote wa elimu ya juu kufikia 210,000. Wanafunzi hao walidahiliwa katika vyuo vikuu na vyuo vikuu vishiriki 49 na Taasisi zisizo vyuo vikuu 21 (kama ilivyo kwenye kiambatisho Na. 1).

### Elimu Maalum

**26. Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia kwamba elimu ni haki ya msingi ya kila Mtanzania, Wizara yangu imeendelea kupanua fursa za elimu na mafunzo kwa kuimarisha elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Katika mwaka 2015/16, Wizara yangu iliendesha mafunzo kwa walimu 142 kuhusu ufundishaji wa Sayansi na Hisabati kwa wanafunzi wasioona. Aidha, kupitia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania wanafunzi 45 viziwi na wasioona walipewa mafunzo ya kutumia TEHAMA katika kurahisisha kujifunza ili waweze pia kupata maarifa na taarifa mbalimbali zilizoko kwenye mtandao.

**27. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17 Wizara yangu itafanya yafuatayo:

(i) kununua vifaa mbalimbali vya wanafunzi wenye mahitaji maalum. Vifaa hivyo ni pamoja na mashine za nukta nundu, fimbo nyeupe, viti vya magurudumu, visaidizi vya kusikia, na vifaa vya vituo maalum vya msaada wa kitabibu;

(ii) kukarabati na kufanya matengenezo ya vifaa vya wanafunzi walemavu; na

(iii) kuwezesha upatikanaji wa vifaa vya maabara na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum wa shule za msingi na Sekondari.

### **5.3 KUINUA UBORA WA ELIMU NA MAFUNZO**

**28. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inatambua kwamba elimu bora ina nafasi ya pekee katika kufanikisha ujenzi wa msingi wa uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegemea. Ili kukidhi azma hii, Wizara yangu imeimarisha na kuboresha mfumo wa ithibati na uthibiti wa shule na vyuo, mafunzo ya ualimu, mazingira ya kufundishia na kujifunzia pamoja na huduma za maktaba.

#### **Ithibati ya Shule za Msingi na Sekondari**

**29. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kusimamia ithibati ya shule kwa lengo la kuzipatia shule idhini ya kufundisha masomo husika, kuthibitisha Wamiliki na Mameneja wa Shule na kutoa vibali vya ujenzi wa shule zisizo za Serikali. Hadi kufikia Aprili, 2016 shughuli zifuatazo zilifanyika:

(i) shule 174 zikiwemo shule za awali 4, msingi 115 na sekondari 55 zilisajiliwa;

(ii) kutoa vibali kwa Wamiliki 151 na Mameneja 154 wa shule na vibali vya ujenzi wa shule 201 zisizo za Serikali;

(iii) kufuta vibali vya ujenzi kwa shule 37 kwa kuwa vilikuwa vimeombwa zaidi ya miaka kumi iliyopita, na hapakuwa na jitihada za kuendelea na ujenzi na kuanza taratibu za kusajili shule hizo; na

(iv) Wamiliki na Mameneja wa shule 13 walifutiwa uthibitisho kutokana na shule zao kubadili umiliki.

**30. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2016/17, Wizara yangu itafanya yafuatayo katika ithibati ya shule;

(i) kuhuisha na kuandaa Mwongozo wa Usajili wa Shule za Serikali na zisizo za Serikali kulingana na mahitaji ya sasa;

(ii) kusajili shule za Awali, Msingi na Sekondari kwa kutilia mkazo uanzishwaji wa shule zenye mwelekeo wa Sayansi, Kilimo, Teknolojia na Ufundi; na

(iii) kusajili vituo vinavyotoa Elimu Nje ya Mfumo Rasmi na Elimu Huria.

### **Uthibiti wa Ubora wa Shule za Msingi na Sekondari**

**31. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inatambua kwamba, uthibiti ubora wa shule ni jambo muhimu sana katika kuimarisha ubora wa elimu na mafunzo yanayotolewa katika shule za msingi na sekondari. Hadi kufikia Aprili, 2016, shule 7,882 kati ya 17,242 ambayo ni sawa na asilimia 46 ya shule zilizolengwa zilifanyiwa ukaguzi. Aidha, walimu 292 waliteuliwa kuwa Wathibiti Ubora wa Shule na kupangwa katika ofisi za Kanda na Wilaya kwa lengo la kuimarisha ukaguzi wa shule.

**32. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inafuatilia kwa karibu na kuhakikisha kwamba watoto wote wanafundishwa vema na wanaweza kumudu stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK) kuanzia hatua za mwanzo. Katika kutimiza azma hii Wathibiti Uborawa Shule wapatao 1,435 wamepatiwa mafunzo ya stadi za kufundisha KKK ili waweze kufuatilia utekelezaji wake katika shule za msingi na kutoa msaada kwa walimu wanapofundisha. Vilevile, Wizara ilifungua ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule na kupeleka Wathibiti Ubora wa Shule katika Halmashauri za Wanging'ombe, Makambako, Kaliua, Nyasa, Geita (Mji), Njombe (Mji), Nyangh'wale, Ikungi, Kalambo, Mbogwe, Buligwe, Gairo, Chemba, Majinga, Momba, Bumbuli, Handeni (M), na Mkarama. Ofisi hizi zimesaidia walimu na wadau wa elimu kupata huduma za Wathibiti Ubora wa Shule kwa karibu zaidi.

**33. Mheshimiwa Spika,** katika uthibiti ubora wa shule kwa mwaka 2016/17, Wizara imepanga kufanya yafuatayo:

(i) kufuatilia ubora wa utoaji elimu katika shule 10,818 na kutoa ushauri kwa lengo la kuboresha ufundishaji;

(ii) kutoa ushauri wa kitaalamu na kitaaluma kwa wadau wa elimu;

(iii) kukamilisha ujenzi wa ofisi za uthibiti ubora katika Wilaya za Hai, Masasi, Mtwara Mjini, Namtumbo, Urambo na Sumbawanga Mjini;

(iv) kufuatilia ufundishaji katika elimu ya awali na stadi za KKK kwa wanafunzi wa Darasa la I na II;

(v) kuandaa kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule (Basic Education Quality Assurance Framework) na kutekeleza mapendekezo ya uimarishaji wa mfumo wa ukaguzi;

(vi) kuhuisha mwongozo wa Wathibiti Ubora, kuchapa na kusambaza kwa Wathibiti Ubora wote; na

(vii) kununua na kugawa pikipiki kwa Waratibu Elimu Kata wa Mikoa 18 na kuchangia mafuta kwa ajili ya magari na pikipiki zilionunuliwa chini ya Mpango wa LANES.

### **Ithibati na Uthibiti wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi**

**34. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2015/16, Wizara yangu iliendelea kusimamia ubora wa Elimu ya Ufundi nchini kwa kupitia Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi. Baraza lilivifanyia tathmini na kuvisajili vyuo 70, kutoa ithibati kwa Vyuo 23 vya Ufundi; na kuhakiki jumla ya Wakufunzi 807 ili kubaini uhalali wao wa kufundisha katika ngazi husika. Aidha, Baraza limetambua Idara 35 na kuzipatia ithibati ya kuendesha programu za mafunzo.

**35. Mheshimiwa Spika**, ili kuimarisha elimu ya ufundi nchini, Baraza liliendesha mafunzo ya kuhakiki ubora wa mafunzo vyuoni kwa wafanyakazi 30 wa Baraza na kwa wakufunzi 22 wa vyuo pamoja na kukagua jumla ya vyuo 35 ili kutathmini ubora wa utoaji wa mafunzo. Aidha, Baraza liliidhinisha mitaala 93 inayozingatia umahiri ikiwemo 42 ya ngazi ya Cheti, 34 ya Diploma, 16 ya Digrii na 1 Digrii ya uzamili. Baraza pia limetoa mafunzo ya jinsi ya kutumia mitaala inayozingatia umahiri kwa wakufunzi 417 wa vyuo.

**36. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara yangu kupitia Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi itaendelea kukagua na kusajili vyuo vya ufundi kulingana na maombi na mahitaji ya nchi. Baraza pia litaendelea kusajili wakufunzi ili kuhakiki sifa zao pamoja na kukagua na kutoa ithibati kwa vyuo vya ufundi na kutambua idara zenye uwezo wa kuendesha programu mbalimbali za ufundi.

**37. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara yangu pia kupitia Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi litafanya shughuli zifuatazo:

(i) tathmini ya ubora wa mafunzo katika vyuo 60 na kuboresha miongozo na taratibu za usajili na utoaji ithibati kwa vyuo vya ufundi.

(ii) litadahili wanafunzi 90,000 katika ngazi ya Cheti, Diploma na Digrii kupitia mfumo wa pamoja wa udahili.

(iii) litajengea uwezo vyuo 60 katika kujihakiki na kusimamia ubora wa mafunzo vyuoni, kupima na kuhakiki ubora wa mitaala ya vyuo vya ufundi katika ngazi zote,



(iv) litatengeneza mfumo wa kielektroniki wa kupokea na kuhakiki mitaala, kufanya tafiti zenye lengo la kuboresha utoaji wa mafunzo ya elimu ya ufundi,

(v) kuratibu mafunzo ya kutumia mitaala inayozingatia umahiri kwa walimu 400,

(vi) kuandaa moduli za mafunzo kwa walimu kuhusu kuandaa, kupitia, kufundisha na kupima mitaala ya elimu ya ufundi.

### **Uthibiti Ubora wa Vyuo vya Elimu ya Juu**

**38. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu imeendelea kusimamia ubora wa elimu ya juu kupitia Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania. Katika mwaka 2015/16, Tume ya Vyuo Vikuu ilikagua na kutathmini vyuo vikuu 15 nchini kwa lengo la kusimamia ubora. Katika ukaguzi huo, ilibainika kuwa Chuo Kikuu cha Mt. Yosefu Kampasi ya Songea (Koleji za Kilimo, Teknolojia na TEHAMA) na Kampasi ya Arusha hazikukidhi viwango vya ubora stahiki. Changamoto zilizobainika ni pamoja na vyuo kutokuwa na wahadhiri wenye sifa stahiki na mitaala kutoandaliwa ipasavyo. Mazingira ya kufundishia na kujifunzia kutokidhi vigezo hususan ukosefu wa mafunzo kwa vitendo kutokana na kutokuwepo kwa maabara.

### **Kufutwa kwa Ithibati kwa Chuo cha Mt Yosef**

**39. Mheshimiwa Spika,** Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania kwa kutumia mamlaka yake kisheria ilifuta usajili wa Koleji za Songea na Kampasi ya Arusha. Kutokana na hatua hiyo, jumla ya wanafunzi 3,585 waliokuwa kwenye vyuo hivyo walihamishiwa kwenye Vyuo vingine. Hata hivyo, imekuwepo changamoto katika kupokelewa kwa wanafunzi hao kwani vyuo vilivyowapokea vimeona hawakuwa wamesoma kwa kiwango cha kutosha ukilinganisha na mwaka wa masomo waliokuwepo. Ili kuhakikisha wanapata maarifa stahiki kwa miaka waliyopo, baadhi ya vyuo vimewarudisha mwaka wakati vingine vimelazimika kuwapa mafunzo ya ziada kukabiliana na mapungufu kitaaluma waliyoyabaini.

**40. Mheshimiwa Spika,** Hali hiyo inathibitisha kuwa elimu iliyokuwa ikitolewa katika Chuo cha Mt Yosef haikuwa inakidhi viwango hali iliyosababisha kuwepo kwa migogoro ya wanafunzi ya mara kwa mara katika chuo hicho. Napenda kuchukua nafasi hii kuviagiza vyuo vyote vya elimu kuhakikisha vinaendeshwa kwa kufuata Sheria. Kanuni na Taratibu. Wizara yangu haitasita kuchukua hatua kali dhidi ya chuo kitakachokwenda kinyume na taratibu.

## **Wanafunzi wa Kidato cha 4 waliokuwa wanachukua Digrii Katika chuo cha Mt. Yosef**

**41. Mheshimiwa Spika**, naomba sasa nizungumzie suala la wanafunzi 424 wa Mt Yosef walioondolewa chuoni. Suala hili liliwasilishwa katika Bunge lako tukufu siku ya tarehe 17/05/2015 na Mh Cosato David Chumi (Mbunge wa Mafinga). Kwa mujibu wa Kanuni 28(11) aliwasilisha maelezo binafsi akitaka Serikali kutoa ufafanuzi kuhusu hatua hiyo. Nitatoa ufafanuzi wa kina ili sababu za uamuzi huo ziweze kueleweka ipasavyo.

**42. Mheshimiwa Spika**, katika zoezi la kuwahamisha wanafunzi wa Mt. Yosef kampasi ya Arusha, ilibainika kuwa walikuwepo wanafunzi ambao walidahiliwa kujiunga na Digrii ya Ualimu kwa masomo ya Sayansi wakati hawakuwa na sifa stahiki. Wanafunzi hao walikuwa wamemaliza Kidato cha Nne wakiwa na ufaulu hafifu ambapo mwanafunzi aliyepata 'D' nne sawa na Divishen IV ya pointi 31 alipewa fursa ya kudahiliwa kwenye Digrii ya Ualimu wa Sayansi.

**43. Mheshimiwa Spika**, jambo la kusikitisha zaidi ni kuwa katika kudahili wanafunzi hao kwenye Digrii ya Sayansi, masomo ya msingi aliyoyasoma mwanafunzi hayakuzingatiwa. Kwa mfano, wapo waliochukua mkondo wa Biashara yaani masomo ya Book-keeping na Commerce lakini walidahiliwa kusoma Sayansi. Aidha, wapo ambao hawakuchukua kabisa mkondo wa Sayansi yaani masomo ya Sayansi lakini walidahiliwa. Vilevile, wapo wanafunzi waliofeli masomo ya Sayansi Kidato cha Nne lakini wakadahiliwa kuchukua Digrii ya Sayansi ya Ualimu kama inavyooneshwa katika mifano ifuatayo:

<b>S/N</b>	<b>INDEX</b>	<b>UFAULU KWA MASOMO</b>
1	S2123/0043/2011	CIV-D,HIS-F,GEO-D,KIS-F,ENG-D,PHY-D,CHE-F,BIO-D,MAT-F
2	S0194/0027/2012	CIV-C,HIS-D,GEO-D,BIB-D,KIS-D,ENG-D,BIO-D,MAT-F,COM-D,BOO-F
3	S0348/0068/2005	CIV-D,HIS-F,GEO-D,KIS-F,ENG-D,PHY-F,CHE-D,BIO-D,AGR-F,MAT-F
4	S0353/0091/2009	CIV-D,HIS-D,GEO-F,KIS-D,ENG-F,PHY-F,CHE-D,BIO-D,AGR-C,MAT-F
5	S2295/0019/2012	CIV-D,HIS-C,GEO-D,KIS-D,ENG-D,BIO-C,COM-D,MAT-F

**44. Mheshimiwa Spika**, kutokana na wanafunzi kuwa na sifa za aina hiyo ambazo hazitoshelezi hata kujiunga na mafunzo ya Cheti cha Ualimu, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Vyuo Vikuu, imefuta udahili wao wa Digrii ya Ualimu wa Sayansi. Serikali imesikitishwa sana na na kitendo hicho cha kudahili wanafunzi hao kujiunga na Digrii ya Ualimu wa Sayansi wakati hawana sifa stahiki. Katika mwaka 2013/14 walipodahiliwa kwa ufaulu wa Kidato cha 4 kwa kiwango cha angalau 'D' nne, sifa za kujiunga na Cheti cha Ualimu zilikuwa ziko juu zaidi. Aidha, wanafunzi hao walipewa mikopo licha ya kutokuwa na sifa stahiki.

**45. Mheshimiwa Spika**, kutokana na hali hiyo, Serikali imeunda Kamati ya kuchunguza mchakato mzima wa uanzishwaji wa programu hiyo na sababu za wanafunzi wasio na sifa kudahiliwa. Hatua kali zitachukuliwa dhidi ya wote watakaobainika kuhusika na suala hilo.

### **Mafunzo ya Ualimu**

**46. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inatambua umuhimu wa kuwa na walimu wenye sifa, maarifa na weledi katika kuinua viwango na ubora wa elimu. Katika mwaka 2015/16 Wizara yangu iliendelea na juhudi za kuongeza walimu, hususani walimu wa Sayansi na Hisabati ili kukabiliana na upungufu wa walimu wapatao 22,000 uliopo sasa. Walimu tarajali 5,690 walidahiliwa kwa ngazi ya Diploma ya Ualimu wa masomo ya Hisabati na Sayansi katika Chuo Kikuu cha Dodoma na vyuo vya ualimu vya Kleruu, Monduli na Korogwe. Aidha, Wizara imeendelea kufilia mkazo sifa za kudahili wanafunzi katika programu za Ualimu, ambapo ufaulu wa chini ni Daraja la Tatu katika mtihamu wa kuhitimu Kidato cha Nne na Kidato cha Sita.

**47. Mheshimiwa Spika**, ili kuimarisha uwezo wa kitaaluma wa wakufunzi wa Sayansi na Hisabati katika vyuo vya ualimu, Wizara yangu kupitia ufadhili wa China Trust Fund na UNESCO – Tanzania imetoa mafunzo ya TEHAMA kwa wakufunzi 20 na kuweka miundombinu ya TEHAMA kwa vyuo vya Monduli na Tabora. Miundombinu hii imeimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Sayansi na Hisabati.

**48. Mheshimiwa Spika** kwa kutambua kwamba wanafunzi wanaojiunga na elimu ya sekondari wanahitaji mafunzo kabilishi ya lugha ya kiingereza, Wizara yangu imetoa mafunzo kwa walimu 2,485 wa shule za sekondari kwa lengo la kuwawezesha walimu hao kumudu kuwasaidia wanafunzi wa Kidato cha Kwanza. Aidha, vitabu 26,000 vya wawezeshaji na walimu vimeandaliwa na kusambazwa kwenye wilaya 37 na mikoa 5 ya majaribio.

**49. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17 Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo tarajali (Pre- service) ya walimu wa elimu ya awali pamoja na wale wa masomo ya Ufundi kwa shule za sekondari za ufundi na mafunzo ya Ufundi Sanifu wa Maabara kwa ajili ya maabara za shule za Sekondari. Aidha, Wizara yangu itaendelea kuendesha mafunzo kazini kwa Walimu wa Elimu Maalumu, Elimu ya Ufundi na kwa masomo yote ya Elimumsingi.

## Uboreshaji wa Mazingira ya Kufundishia na Kujifunzia

### Elimumsingi na Sekondari

**50. Mheshimiwa Spika,** Mazingira ya kufundishia na kujifunzia yana mchango mkubwa katika kuinua ubora wa elimu katika ngazi zote. Katika mwaka 2015/16, Wizara imeandaa mpango wa ukarabati wa shule kongwe za sekondari nchini ambapo katika Awamu ya Kwanza shule 33 zitakarabatiwa. Shule hizi ni Ihungo, Ilboru, Kilakala, Mwenge, Msalato, Mzumbe, Nganza, Pugu, Same, Tabora Boys na Tabora Girls. Shule nyingine ni Azania, Jangwani, Kantalamba, Mpwapwa, Tosamaganga, Malangali, Milambo, Nangwa, Kibiti, Minaki, Ifakara, Songea Boys, Ndanda, Kigoma, Kibaha na Shule za Ufundi za Bwiru Boys, Ifunda, Iyunga, Moshi, Mtwara, Musoma na Tanga.

**51. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu kwa kushirikiana na wabia wa maendeleo na OR-TAMISEMI imewezesha shule 250 za msingi na sekondari katika wilaya 25 kuunganishwa kwenye mtandao wa "internet" na kupatiwa kompyuta mpakato, Projector na kompyuta endeshi (Server) kwa ajili ya matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

**52. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Elimu itaendelea na uimarishaji wa miundombinu ya Shule na Vyuo vya Ualimu, ikiwemo ukarabati wa shule za sekondari 7 kongwe pamoja na ujenzi wa nyumba 30 za walimu zenye uwezo wa kuchukua walimu **180**, katika maeneo yasiyofikiwa kwa urahisi. Wizara pia itajenga vyumba 25 vya madarasa na matundu 200 ya vyoo katika shule zenye uhitaji mkubwa.

### Elimu ya Juu

**53. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inatambua umuhimu wa mchango wa elimu ya juu katika juhudi za kufikisha nchi yetu katika uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Kwa kuzingatia hilo, Wizara yangu imekuwa ikiongeza majengo na kukarabati miundombinu ya Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa lengo la kuinua ubora na kuongeza fursa kwa wanafunzi wengi zaidi kujiunga na Elimu ya Juu. Katika mwaka 2015/16 baadhi ya shughuli zilizofanyika katika taasisi za elimu ya juu ni pamoja na:

(i) Kukamilisha ujenzi wa maabara kwa ajili ya Kitivo cha Sayansi-Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo unaogharimiwa na Mradi wa *Enhancing Pro-poor Innovation in Natural Resources and Agricultural Value-chain* (EPINAV). Mradi huu umekamilika kwa asilimia 75. Aidha, Chuo kimekarabati maktaba na maabara na kupeleka maji Kampasi ya Solomon Mahlangu; na

(ii) kukarabati vituo vya Mikoa ya Temeke, Mbeya, Bungo na Kinondoni vinavyosimamiwa na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

**54. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Wizara yangu itaendelea kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunzia kwa kufanya yafuatayo:

(i) kukiwezesha Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kukarabati miundombinu katika mikoa ya Ruvuma, Rukwa, Kilimanjaro, Singida, Mara na Pwani;

(ii) kukarabati hosteli za wanafunzi, kumbi za mihadhara, Kituo cha Polisi, nyumba za wahadhiri pamoja na miundombinu ya majitaka katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;

(iii) kukarabati hosteli za wanafunzi Kampasi kuu na ujenzi wa majengo ya madarasa na ofisi za kampasi ya Mbeya ya Chuo Kikuu cha Mzumbe;

(iv) kujenga maabara katika Chuo Kikuu cha Ardhi ambayo itakuwa na matumizi mbalimbali (Mult- purpose Laboratory) pamoja na kukarabati hosteli za wanafunzi;

(v) kukarabati kumbi za mihadhara, maabara na hosteli za wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo;

(vi) kukarabati majengo na miundombinu mingine katika Kampasi Kuu ya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi na Kampasi ya Kizumbi;

(vii) kukamilisha ujenzi wa jengo la Utawala na kuanza ujenzi wa Maabara za Sayansi ili kuongeza fursa kwa wanafunzi zaidi kudahiliwa katika mafunzo ya Sayansi katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam;

viii) kujenga madarasa na Hosteli kwa Chuo cha "Earth Sciences" pamoja na Chuo cha "Natural and Mathematical Sciences" katika Chuo Kikuu cha Dodoma;

(ix) kukamilisha jengo la Mihadhara la Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa na kukarabati miundombinu ya Chuo hicho;

(x) kujenga na kuweka samani katika jengo la Maktaba ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya ili kuendana na ongezeko la udahili;

(xi) kukamilisha ujezi wa jengo la ghorofa kumi katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam na kuweka umeme na samani katika Kampasi Kuu na kukarabati

miundombinu ya majitaka kwa Kampasi ya Mwanza ambayo itaanza kutoa mafunzo katika ngazi ya cheti katika fani ya utunzaji na usindikaji wa ngozi kuanzia hatua ya mnyama akiwa hai, akichinjwa hadi kufikia hatua ya uchunaji na usindikaji wa ngozi; na

(xii) kuendeleza ujenzi wa Hosteli katika Kampasi ya Kivukoni ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere na kununua samani kwa ajili ya Kampasi ya Bububu, Zanzibar.

**55. Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea na mpango wa uanzishwaji wa Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Julius K. Nyerere. Utaratibu wa ujenzi wa Kampasi kuu ya Butiama utaanza mwaka wa 2016/17. Kuhusu kutumia majengo ya Shule ya Sekondari Oswald Mang'ombe, Wizara imefanya mazungumzo na wamiliki kukamilisha uhamishaji wa miliki ya majengo kisheria. Aidha, tunawashukuru wamiliki pamoja na Mheshimiwa Nimrod Mkono kwa mchango wao katika kukuza elimu nchini.

### **Kampasi Mpya ya Mloganzila**

**56. Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa taarifa kuwa ujenzi wa hospitali ya kufundishia ya Kampasi mpya ya Mloganzila ya Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili (MUHAS) iliyojengwa kwa ushirikiano wa Serikali yetu na Serikali ya Korea Kusini inatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2016. Hospitali hii itakuwa na uwezo wa kubeba wagonjwa 571 wa kulazwa kwa wakati mmoja.

**57. Mheshimiwa Spika**, pamoja na juhudi za Serikali kukamilisha Awamu ya Kwanza ya ujenzi wa hospitali hii, bado kuna changamoto ya majengo mengine ya chuo kama madarasa, maabara, maktaba, majengo ya utawala, mabweni ya wanafunzi, nyumba za wafanyakazi n.k. Majengo haya ni muhimu ili Kampasi hii ya Chuo ikamilike na hivyo Chuo kiweze kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 3,000 wa sasa na kufikia wanafunzi 15,000 kitakapokamilisha Awamu ya Pili. Katika mwaka 2016/17 Wizara inalenga kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza awamu ya pili ya ujenzi ambapo tayari andiko la kutafuta fedha kutoka kwa wafadhili na wawekezaji limeandaliwa.

### **Ujenzi wa Kituo Mahiri cha Magonjwa ya Moyo – Mloganzila**

**58. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17 Wizara yangu itaanza ujenzi wa Kituo Mahiri cha Magonjwa ya Moyo na Mishipa ya Damu cha Afrika Mashariki katika eneo la Mloganzila.

## Huduma za Maktaba

**59. Mheshimiwa Spika**, huduma bora za Maktaba zinachangia katika utoaji wa Elimu bora katika nchi yoyote ile. Wizara yangu kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba ina jukumu la kuanzisha, kusimamia, kuongoza, kuimarisha, kutunza na kuendeleza Maktaba za Umma. Uendelezaji wa huduma za Maktaba, unaanzia ngazi ya Kijiji, Wilaya hadi Mkoa pamoja na kutoa mafunzo na kuendesha mitihani ya Taaluma ya Ukutubi. Katika mwaka 2015/16 Wizara kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba imefanya yafuatayo:

(i) imeendelea kuimarisha huduma za Maktaba kwa kusambaza vitabu vya rejea 68,000 kwa masomo yote katika maktaba za mikoa.

(ii) imetoa ushauri wa kitaalamu kuhusu uanzishaji na uendeshaji wa Maktaba katika shule 28 (17 za msingi na 11 za sekondari), vyuo 5 na Halmashauri za Wilaya 4 ambazo ni Mkinga, Longido, Kongwa na Ushirombo.

**60. Mheshimiwa Spika**, ili kukabiliana na upungufu wa wataalam wa Maktaba katika asasi na taasisi za elimu nchini, Wizara kupitia Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka (SLADS) Bagamoyo, imeratibu utoaji wa mafunzo kwa wanafunzi 1,363; wakiwemo Cheti 390; Diploma 773 na kozi ya miezi mitatu “*Elementary Library Course*” 200. Wanafunzi hawa watakapohitimu wataongeza idadi ya wataalam wa Maktaba katika maeneo yaliyo na uhitaji mkubwa wa wakitubi, ikiwa ni pamoja na Shule, Vyuo vya Ualimu na Maktaba za Umma. Aidha, ukarabati mdogo umefanyika katika Maktaba za mkoa wa Mtwara na Tanga.

**61. Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kutoa wito kwa Halmashauri zote nchini pamoja na wadau kuona umuhimu wa kuanzisha maktaba na kuhamasisha wananchi kujenga utamaduni wa kusoma vitabu, vijarida na machapisho mbalimbali. Wizara yangu iko tayari kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu uanzishwaji na uendeshaji wa maktaba.

**62. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba itafanya yafuatayo:

(i) itaimarisha na kuinua ubora wa huduma za maktaba katika mikoa 21 kwa kuongeza machapisho/vitabu 40,000 ya watu wazima na watoto ili kuongeza ari ya usomaji katika jamii;

(ii) itatoa ushauri wa kitaalamu juu ya uanzishaji na uendeshaji wa Maktaba za Shule, Vyuo, Taasisi na Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya nchini;



(iii) itatoa mafunzo ya Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka kwa walengwa 700 wa Cheti, 700 wa Diploma na 500 wa mafunzo ya muda mfupi kwa ajili ya wafanyakazi wa Maktaba;

(iv) itaendeleza miundombinu ya Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka (SLADS), Bagamoyo kwa kujenga maktaba ya chuo pamoja na kukarabati majengo ya maktaba za Tabora, Tanga na Rukwa; na

(v) itaanza matayarisho ya ujenzi wa majengo ya maktaba za mikoa ya Singida na Shinyanga ili kutoa fursa kwa wananchi wa mikoa hiyo kupata machapisho na huduma nyingine za maktaba za umma.

#### **5.4 TAFITI NA HUDUMA KWA JAMII**

##### **Utekelezaji wa Tafiti na Huduma 2015/16**

**63. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu ina jukumu la kufanya tafiti na kutoa huduma kwa jamii kupitia Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara yangu kupitia Vyuo Vikuu imefanya tafiti mbalimbali zenye matokeo makubwa kwa jamii kama ifuatavyo:

##### **Chuo Kikuu cha Sokoine**

(i) udhibiti wa magonjwa ya mifugo yaletwayo na kupe, mbung'o na minyoo kwa wafugaji wa asili, ambapo wafugaji hao sasa wamefanikiwa kuongeza kipato kutokana na kupungua kwa magonjwa ya mifugo yao;

(ii) kutumia Panya Buku kutatua matatizo ya jamii ikiwa ni pamoja na kutambua wagonjwa ya kifua kikuu kwa kasi kubwa na kwa usahihi zaidi ya darubini. Aidha, utafiti umegundua kuwa wanyama hao wanafundishika na wanao uwezo wa kutumika kutegua mabomu katika jamii zilizokumbwa na vita. Panya hao wameweza kutegua mabomu katika nchi za Cambodia, Msumbiji, Jamhuri ya Lao, Vietnam na Thailand, ambapo nchi hizo sasa zimetangaza kwamba hazina tena tishio la mabomu baada ya kuwatumia panya hao; na

(iii) uzalishaji wa mbegu bora za maharage zenye kustahimili magonjwa na ukame, kuzaa vizuri na kuiva kwa muda mfupi. Matokeo ya utafiti huu yamesambazwa kwa wakulima ambapo wanatumia mbegu bora za maharage (SUA 90, ROJO, Mshindi na Pesa) na wameweza kuongeza uzalishaji na kipato chao.

### **Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili**

(i) utafiti wa majaribio ya chanjo ya VVU awamu ya II, uliohusisha nchi za Tanzania na Msumbiji (Tanzania Mozambique Vaccine – TaMoVac II). Chanjo hii ilijaribiwa na kuthibitishwa kuwa salama na ina uwezo wa kufanya mwili utengeneze viashiria vya kinga. Pia majaribio hayo yamewezesha wanasayansi kubaini dozi sahihi ya chanjo na namna ya kutoa ili iweze kufanya kazi katika kiwango kinachotakiwa;

(ii) matibabu ya ugonjwa wa Malaria na kuboresha mfumo wa matibabu ya ugonjwa kwa lengo la kupunguza athari zitokanazo na Malaria hasa kwa akina mama wajawazito na watoto; na

(iii) ugonjwa wa Selimundu ambapo utafiti huo umebaini mbinu bora zaidi za kuhudumia wenye tatizo hilo.

### **Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

Tafiti zifuatazo zilifanyika:

(i) ufuatiliaji wa mienendo ya Tembo kwa kutumia teknolojia ya GPS (Global Positioning System) inayoonesha mahali tembo alipo kwa wakati wote. Matokeo ya utafiti huu yanasaidia kukabiliana na tatizo la ujangili wa tembo. Utafiti huu umewezesha ulinzi wa tembo kufanyika kwa ufanisi mkubwa zaidi;

(ii) utafiti kuhusu kilimo cha uyoga pori kwa matumizi ya chakula na biashara, ambao umewezesha wakulima wapatao 4,000 kulima aina tano za uyoga na hivyo kuongeza uzalishaji wa zao hili na kujiongezea kipato; na

(iii) ufugaji wa samaki wa maji baridi aina ya Tilapia katika maji chumvi ambao umewasaidia wakulima wa Rufiji kuweza kufuga aina hii ya samaki katika maeneo yao na hivyo kuongeza kipato cha kaya.

**64. Mheshimiwa Spika,** Napenda kuchukua fursa hii kuwajulisha wananchi na wadau mbalimbali wanaweza kusoma na kuona matokeo ya tafiti hizo kwenye tovuti za vyuo husika.

### **Malengo ya Tafiti na Huduma 2016/17**

**65. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu kupitia vyuo vikuu itaendelea kufanya tafiti na kutoa ushauri kwa jamii kwa kutumia fedha za Serikali na wadau wa maendeleo. Katika mwaka 2016/17 baadhi ya tafiti zitakazofanyika zitakuwa kama ifuatavyo:

(i) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kitaendelea kusimamia miradi 12 ya utafiti inayofadhiliwa na Sida kuhusu rasilimali maji (water resources); sayansi za bahari na rasilimali zake; usalama wa chakula (Food Security); mabadiliko ya tabianchi; utalii; biashara ya rasilimali za kilimo; kujenga uwezo katika Hisabati, na Sayansi za Molekali Biolojia (Molecular Biosciences) na “Nishati Joto”;

(ii) Chuo Kikuu cha Ardhi, kitafanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu matumizi bora ya ardhi, ujenzi, usanifu majengo na usimamizi wa mazingira;

(iii) Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, kitafanya tafitina kutoa ushauri wa kitaalam na kuchapa makala kwa lengo la kusambaza elimu inayokidhi mahitaji ya sasa ya jamii ili kupunguza umaskini;

(iv) Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili, itaendelea na tafiti za: afya ya akina mama na watoto, majaribio ya chanjo dhidi ya maambukizi ya VVU, uchunguzi wa kifua kikuu (TB); malaria; magonjwa makuu ya tropiki yasiyopewa kipaumbele (Neglected Tropical Diseases) na magonjwa yasiyoambukiza (magonjwa ya moyo, kisukari, selimundi n.k); na

(v) Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Taasisi ya Afrika ya Nelson Mandela ya Sayansi na Teknolojia (NM-AIST) vitafanya tafiti nne ambazo zinaviandaa kuwa vituo mahiri vya utafiti na taaluma katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini. Tafiti hizo ni SUA (*Innovative Rodent Management and Biosensor Technology Development*; na *Infectious Disease Surveillance*) na NM-AIST (Miundombinu ya Maji na Nishati Endelevu; na ya pili ni kuhusu Maendeleo na Elimu Endelevu ya Kilimo).

## 5.5 SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UBUNIFU

**66. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inatambua umuhimu wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu pamoja na matumizi yake katika kuleta maendeleo ya nchi. Wizara imefanya yafuatayo katika mwaka 2015/16:

(i) imekamilisha uandaaji wa Mpango wa Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia na mkakati wa utekelezaji ambao uliandaliwa kupitia mpango wa Matokeo Makubwa Sasa.

(ii) imesimamia majadiliano ya Mkataba wa Ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Zambia katika masuala ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu na kufanya Mikutano ya kuhamasisha umuhimu wa kuwa na dawati la sayansi, teknolojia na ubunifu kwa wadau.

(iii) iliendesha Kambikazi ya Maabara ambapo matokeo yake yamekuwa msingi wa kuandaa programu za utekelezaji wa mpango wa maendeleo ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu.

(iv) katika kuongeza idadi ya wanafunzi wa kike wanaojiunga na masomo ya Sayansi, Wizara yangu pia iliendesha mafunzo maalumu ya kuongeza uwezo wa kitaaluma wa wanafunzi wa kike 305 ambao hatimaye walijiunga na kozi katika Vyuo vya Elimu ya Juu na Ufundi vitano (5) vya Tanzania Bara na Zanzibar.

**67. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Wizara yangu imepanga kuanzisha maabara na kupanua vituo vya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu pamoja na kufadhili miradi mipya na inayoendelea na utafiti katika maeneo ya TEHAMA, Kilimo, Afya, Viwanda na Maliasili. Aidha, Wizara itashirikiana na ofisi za Halmashauri ili kubaini wagunduzi na wabunifu ili kuboresha vipaji vyao. Vilevile, kituo cha kuendeleza ubunifu na ujasiriamali katika fani ya TEHAMA kitajengwa kwenye Taasisi ya Afrika ya Nelson Mandela ya Sayansi na Teknolojia pamoja na kuanzisha Kituo mahiri cha "Agricultural Biotechnology" katika Chuo Kikuu cha Sokoine.

#### **Taasisi zinazohusika na Sayansi Teknolojia na Ubunifu**

**68. Mheshimiwa Spika,** naomba sasa nitumie fursa hii kueleza utekelezaji wa masuala ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu yaliyofanywa na Taasisi zetu za Sayansi na Teknolojia:

#### **Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)**

**69. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu kwa mwaka 2015/16 kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia, imefanya yafuatayo:

(i) imeratibu mtandao wa kuunganisha Vyuo Vikuu na Taasisi za Utafiti na Maendeleo ambapo taasisi **28** zimeunganishwa.

(ii) imeendelea kuhawilisha teknolojia mbalimbali nchini ambazo zimewezesha ujenzi wa maabara ndogo yenye uwezo wa kutoa machapisho mbalimbali kwa njia ya kidijitali kwa kutumia teknolojia ya 3D "*printers*" ambazo zimetengenezwa hapa nchini kutokana na mabaki ya vifaa vingine vya kielektroniki. Ubunifu huu umefanyika katika Atamizi ya *BUNI* ambayo inasimamiwa na Tume.

(iii) imesimamia Kituo cha kuendeleza ubunifu (*BUNI Innovation Hub*) ambacho kimekuwa kikiendesha mpango maalum wa kuandaa waatamizi

watarajiwa (*pre-incubation program*) kwa wanafunzi wa vyuo vikuu kupitia mafunzo kwa vitendo (*field practical and Internship program*).

(iv) kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeimarisha Atamizi ya TEHAMA (*ICT Incubator*) iliyopo katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume, na Atamizi ya Usarifu wa Mazao ya Kilimo (*Agribusiness Incubator*) iliyopo katika Kituo cha utafiti wa Kilimo cha Kizimbani, Zanzibar. Atamizi ya Usarifu wa mazao ya kilimo inalenga kuongeza mnyororo wa thamani katika kubiasharisha mazao mbalimbali ya kilimo na mifugo.

(v) Imetoa huduma za maktaba mtandao (e-library) na;

(vi) kutoa taarifa za utafiti kupitia tovuti ya utafiti (*Research web*).

**70. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17 Wizara yangu kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia itafanya yafuatayo:

(i) kuendelea kugharimia tafiti zenye kulenga kutatua matatizo ya wananchi;

(ii) kuanzisha mfumo wa kitaifa wa kufadhili tafiti za masomo baada ya Digrii ya uzamivu (*post doctoral research*);

(iii) kuanzisha mfumo wa kufuatilia viwango, ubora na maadili ya utafiti katika taasisi za utafiti na maendeleo;

(iv) kuhamasisha uanzishwaji wa atamizi katika vyuo vya elimu ya juu; na

(v) kujenga maabara ya kutunza maarifa na machapisho.

#### **Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam - (DIT)**

**71. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya teknolojia kwa wanafunzi na wafanyakazi wa viwandani ili waweze kujiongezea ujuzi mpya katika taaluma mbalimbali. Katika mwaka 2015/16 Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam, ilidahili wanafunzi wapya 1,386 ambapo 654 walikuwa ni Diploma ya Uhandisi, 648 Digrii ya Kwanza ya Uhandisi na 84 Digrii ya Uzamili ya Uhandisi na kufanya Taasisi kuwa na jumla ya wanafunzi 4,187 Wanawake 541 na wanaume 3,646. Aidha, Taasisi ilianzisha kozi mpya za Diploma ya Biotechnology, Digrii ya Uhandisi katika Mafuta na Gesi, Digrii ya Uzamili ya Matumizi ya Teknolojia ya Ukokotoaji katika fani za Sayansi na Uhandisi na kupata ithibati kutoka NACTE.

**72. Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafunzo yaliyotajwa, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam imejenga na kuendelea kuukarabati mtandao wa mawasiliano wa tiba mtandao (Telemedicine) unaunganisha hospitali 7 za Taifa Muhimbili, Rufaa Mbeya, Amana, Temeke, Mwananyamala, Tumbi Kibaha na Bagamoyo.

**73. Mheshimiwa Spika:** katika mwaka wa fedha 2016/17, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam itatekeleza mambo yafuatayo:

(i) kuanzisha kozi mpya ya Diploma ya Uhandisi Ujenzi na Barabara (Civil and Highway Engineering);

(ii) kufundisha kozi mpya ya Digrii ya Uzamili katika Nishati Endelevu (MEng. Sustainable Energy);

(iii) kuendesha mafunzo ya awali (pre-entry) ili kupata wanafunzi wa kike 65 wasio na vigezo vya kutosha kudahiliwa katika kozi zinazoendeshwa na Taasisi;

(iv) kuendelea kuhudumia mradi wa matibabu mtandao (Telemedicine) kwa kushirikiana na Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto; na

(v) kuanza kufundisha kozi za Diploma za bidhaa za ngozi (Leather goods) na Sayansi na Teknolojia ya Maabara (Science and Laboratory Technology) na kuendelea na utoaji wa kozi fupi na za kitaalam katika Teknolojia ya ngozi na bidhaa zake katika Kampasi ya Mwanza.

### **Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya**

**74. Mheshimiwa Spika,** Chuo hiki kina majukumu ya kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu na kitaaluma. Katika mwaka 2015/16, *Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya* kilitekeleza yafuatayo:

(i) kudahili wanafunzi 3,682 ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 82 kutoka kwa wanafunzi 3,600 waliodahiliwa mwaka 2014/15 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 2;

(ii) kuajiri wafanyakazi katika fani mbalimbali (wafanyakazi 43 wameajiriwa kuanzia mwezi Julai 2015 mpaka Januari 2016);

**75. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17 Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kitaendelea kuongeza udahili wa wanafunzi kuhamasisha wanafunzi wa kike katika shule za sekondari kusoma masomo ya sayansi ili hatimaye waweze kujiunga na vyuo vya ufundi.

### **Tume ya Nguvu za Atomiki**

**76. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16 Wizara yangu kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki imeendelea na jukumu lake la kudhibiti mionzi katika migodi na vituo vya huduma kwa kufanya yafuatayo: kukagua migodi 3 na vituo 72 kati ya vituo 100 sawa na asilimia 72 na kuhakikisha kuwa viwango vya mionzi vinavyotumika kwenye sehemu za kazi na vyakula vinadhibitiwa. Hili lilifanywa kwa kupima viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 840 kutoka katika vituo 300 vya uzalishaji pamoja na kupima mionzi kwenye vyakula na mbolea kwa sampuli zipatazo 6,633.

**77. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa vyanzo vya mionzi vinadhibitiwa na haviathiri mazingira na afya za viumbe hai, Wizara kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki imesajili vyanzo vya mionzi vipatavyo 1045 na vituo vinavyomiliki vyanzo vya mionzi vipatavyo 1032. Kati ya vyanzo hivyo, 387 vina viasili vya mionzi (*radioactive materials*). Aidha, Tume pia kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeweza kupima mionzi itokayo katika minara ya simu katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Arusha, Mwanza, Mbeya, Lindi na Mtwara. Vituo vipatavyo 294 vimepimwa na matokeo ya vipimo yameonesha viwango vya mionzi viko chini ya viwango vya usalama vya kimataifa.

**78. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara yangu itaendelea na mikakati ya kuhakikisha kuwa wananchi na viumbe hai hawaathiriwi na mionzi hatarishi hasa kwenye sehemu za kazi kwa kufanya ukaguzi wa migodi 5 mikubwa inayofanya kazi ili kubaini hali ya usalama inayoendelea katika migodi hiyo. Aidha, vituo 120 vyenye vyanzo vya mionzi vitakaguliwa ili kubaini hali ya usalama kwa wafanyakazi 1,700 na umma kwa ujumla. Ukaguzi huu utasaidia kuandaa taratibu (*standard operating procedures*) za kufanya kazi katika maabara.

**79. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki kwa mwaka 2016/17, itaendelea na udhibiti wa mionzi hatarishi kwa kusajili vituo vyenye vyanzo vya mionzi vipatavyo 1045 pamoja na kupokea na kutathimini maombi 450 ya leseni mbalimbali ili kuona kama yanakidhi matakwa ya Sheria na Kanuni za Usalama na Kinga ya Mionzi ya mwaka 2004. Aidha, Tume itakusanya mabaki ya mionzi katika vituo vyote na kuyahifadhi katika maabara maalum na kutafuta mabaki ya mionzi katika viwanda vinavyokusanya vyuma chakavu. Vile vile, Tume itaimarisha mfumo wa kielektroniki katika kutoa vibali,



na kuwa na vifaa vya kupimia mionzi katika vituo 2, ambavyo ni Namanga na bandari ya Dar es salaam pamoja na kuanzisha vituo vya kanda ya kusini katika mkoa ya Ruvuma na Mbeya.

## **5.6 URATIBU WA TAASISI NA WAKALA**

**80. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu ina Taasisi na Wakala za elimu, Sayansi na Teknolojia inazosisimamia. Naomba sasa kutoa maelezo kuhusu Taasisi na Wakala hizo:

### **Tume ya Taifa ya Vyuo Vikuu Tanzania**

**81. Mheshimiwa Spika**, Tume ya Vyuo Vikuu pia imefanya mapitio ya miongozo mbalimbali ya uthibiti ubora ili kuthibiti na kusimamia ithibati ya elimu ya juu nchini. Miongozo hiyo inajumuisha ya uhakiki ubora wa programu za masomo ya elimu ya juu na utoaji wa mafunzo katika ngazi ya Digrii za juu (postgraduate training). Miongozo hii imewezesha vyuo vya elimu ya juu kutoa elimu yenye viwango vinavyokidhi ubora kitaifa na kimataifa na mahitaji ya soko la ajira na jamii ya sasa na ya baadae.

**82. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara kupitia Tume ya Vyuo Vikuu imepanga kufanya yafuatayo:

(i) kusimamia ubora wa elimu ya Vyuo Vikuu vyote nchini kwa kufanya ukaguzi na tathmini za mara kwa mara vyuoni na pia mipango ya kuanzisha/kuhuisha Vyuo Vikuu 20 ili kusimamia ubora wa elimu itolewayo na Vyuo Vikuu nchini;

(ii) kuendelea kuratibu na kusimamia udahili wa wanafunzi wapatao 65,000 watakaojiunga na Vyuo Vikuu kupitia mfumo wa udahili wa pamoja (CAS), ili kufikia lengo la kuwa na wanafunzi wapatao 300,000 kwenye Taasisi za Elimu ya Juu nchini ifikapo mwaka 2017;

(iii) kuboresha mfumo wa ukusanyaji taarifa mbalimbali toka vyuo vya elimu ya juu nchini ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wakati zitakazosaidia katika kufikia maamuzi sahihi ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya elimu ya juu nchini;

(iv) kutathimini programu 200 za masomo katika Vyuo Vikuu nchini;

(v) kuendelea kuratibu na kuandaa Maonesho ya kumi na moja ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ili kuelimisha umma kuhusu malengo, maendeleo na mchango wa Taasisi za Elimu ya Juu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini;

(vi) Kuendelea kuratibu mafunzo ya wanataaluma kutoka vyuo vikuu nchini wanaoendelea na masomo ya Uzamivu nchini Ujerumani (DAAD) kwa lengo la kukabiliana na changamoto za upungufu wa wanataaluma wenye sifa stahiki katika vyuo vikuu nchini; na

(vii) Kuanza ujenzi wa ofisi za kudumu za Tume katika kiwanja cha Uporoto, Dar es Salaam.

### **Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM)**

**83. Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu una majukumu ya kuandaa na kuendesha mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika uongozi na uendeshaji wa elimu; kufanya utafiti, kuandaa na kusambaza makala na vitabu pamojana kutoa ushauri wa kitaalamu katika mambo yanayohusu uongozi na uendeshaji wa elimu. Katika mwaka 2015/16, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu, umefanya yafuatayo:

(i) umetoa mafunzo ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu kwa ngazi ya Cheti kwa Walimu Wakuu 881 ambao wanaendelea na mafunzo katika Mikoa ya Mbeya, Njombe na Iringa; na ngazi ya Diploma ya Uongozi wa Elimu (DEMA) kwa walimu 815;

(ii) umetoa mafunzo ya Diploma ya Ukaguzi wa Shule kwa Wathibiti Ubora wa Shule 332 wa mwaka wa kwanza na 118 wa mwaka wa pili;

(iii) umekamilisha uanzishaji wa Kampasi ya Mbeya ambapo wanachuo 70 wameanza mafunzo ya Diploma ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu (Diploma in Education Management and Administration);

(iv) umeendesha mafunzo ya Muda Mfupi ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Walimu Wakuu 10,870 na Waratibu Elimu Kata 2,480, juu ya Uongozi wa Shule na Usimamizi wa Ufundishaji wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK);

(v) Maafisa Elimu Sekondari kutoka Halmashauri 179 wamepata mafunzo ya Uongozi wa Elimu na Udhibiti wa Majanga katika Elimu;

(vi) umefanya utafiti wa kubaini mahitaji ya mafunzo kwa walimu na wadau wengine kuhusu Uthibiti wa Ubora wa Elimu ili kuweza kuanzisha Digrii ya Menejimenti na Uthibiti wa Elimu (Bachelor in Education Management and Quality Assurance);

(vii) umetoa huduma ya Ushauri wa Kitaalamu juu ya Uongozi na Menejimenti ya Elimu kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, UNICEF, Rufiji Social Development Initiative, Equip(T) na SHIPO; na

(viii) umeandaa makala mbalimbali kwa wadau wake ambazo ni pamoja na Moduli ya Uongozi na Uthibiti wa Majanga kwa Maafisa Elimu Sekondari na Moduli ya Uongozi wa Shule na Usimamizi wa Ufundishaji KKK kwa Waratibu Elimu Kata na Walimu Wakuu.

### **Uratibu wa Shughuli za UNESCO nchini**

**84. Mheshimiwa Spika,** Tume ya UNESCO ina majukumu ya kuratibu na kutekeleza programu za UNESCO nchini. Tume hii inatekeleza programu katika nyanja za Elimu, Sayansi Asilia, Sayansi Jamii, Utamaduni, Mawasiliano na Habari. Katika mwaka 2015/16, Tume ya Taifa ya UNESCO, ilifanya mapitio ya Toleo la 12 la Jarida la UNESCO Tanzania na kusambaza nakala 600 kwa wadau wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kutoa taarifa kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Tume hiyo. Aidha, Tume imefanikiwa kuunganisha shule 10 za sekondari na chuo kimoja cha ualimu nchini kwenye mtandao wa shule nyingine duniani ili ziweze kubadilishana uzoefu wa kielimu kupitia mtandao wa shule wa *UNESCO Associated Schools Project Network (ASP- Net)*.

**85. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2016/17 Wizara yangu kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO itatekeleza yafuatayo:

(i) kutathmini miradi yote ya kielimu itakayopata ufadhili wa UNESCO makao makuu na ile itakayopata ufadhili kutoka kwa wafadhili wengine kupitia UNESCO;

(ii) kuendelea kutangaza na kuratibu 'fellowships' na 'sponsorship' zitakazoletwa nchini kwa lengo la kukuza weledi na uzoefu wa wafanyakazi wa kada mbalimbali;

(iii) kuendelea na jitihada za kuunganisha Serikali ya Tanzania na UNESCO kupitia Wizara; na

(iv) kuendesha semina wezeshi zitakazojenga uwezo wa wadau katika kushiriki shughuli mbalimbali ikiwepo kuwa mstari wa mbele katika kutimiza malengo ya maendeleo ya dunia na maendeleo endelevu ifikapo 2030.

### **Taasisi ya Elimu Tanzania**

**86. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inatambua umuhimu wa kuandaa mitaala bora ili elimu itolewayo iwe na viwango vinavyokubalika

kitaifa na kimataifa. Wizara imekuwa ikitekeleza jukumu hili kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania. Aidha, Taasisi hii inalo jukumu la kutoa miongozo kuhusu vifaa vya kufundishia na kujifunzia, kutoa mafunzo kwa walimu kazini na kufanya utafiti na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mitaala katika ngazi za elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu.

**87. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2015/16, Taasisi ya Elimu Tanzania imetekeleza yafuatayo:

(i) imeboresha Mtaala wa Elimu ya Awali na Elimu ya Msingi Darasa la III hadi VII ili uendane na dhana ya elimumsingi na kuandaa Mihtasari na Miongozo ya Elimu ya Awali na Elimumsingi Darasa III – VI kwa masomo ya Kiswahili, English, Hisabati, Stadi za Kazi, Sayansi na Teknologia, Maarifa ya Jamii, Uraia na Maadili na Lugha ya Kifaransa;

(ii) imekusanya maoni ya wadau kuhusu mahitaji ya utekelezaji wa mtaala wa elimu ya sekondari Kidato cha 1-4 uliofanyika katika mikoa 26 ya Tanzania Bara ambapo Wilaya 52 na taasisi mbalimbali zilifikwa;

(iii) imeandika na kusimamia uchapaji wa nakala 6,862,800 za vitabu 6 vya kiada kwa Darasa la Kwanza. Wizara imeweza kubaini kasoro za kiuchapaji kwenye nakala 2,807,600. Mchapaji amewajibishwa kurudia kazi hiyo kwa gharama zake;

(iv) imefanya tathmini ya vitabu vya ziada vilivyoandikwa na wachapishaji mbalimbali vitakavyotumika shuleni katika ngazi mbalimbali za elimumsingi, sekondari na vyo vya ualimu ambapo jumla ya vitabu 146 vimefanywa tathmini kwa ajili ya kupewa ithibati; na

(v) imeandaa Mwongozo wa Walimu Washauri wa Vituo Shikizi (Satelite Schools) kwa ajili ya maandalizi ya shule za awali katika maeneo ambayo ni magumu kufikika.

**88. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Taasisi ya Elimu Tanzania imelenga kutekeleza yafuatayo:

(i) kutayarisha vitabu vya kiada vya Elimumsingi na sekondari vinavyozingatia mtaala ulioboreshwa;

(ii) kuhuisha na kuboresha mtaala wa elimu ya Msingi na Sekondari Kidato cha 1-4;

(iii) kuhuisha na kuboresha mtaala wa sekondari Kidato cha 5-6;

(iv) kuhuisha na kuboresha mtaala wa elimu ya ufundi; na

(v) kufanya tafiti za kielimu kuhusu mitaala inayotumika katika vyuo vya mafunzo ya elimu ya ualimu kwa lengo la kubaini ulinganifu wake na mitaala ya elimumsingi na sekondari.

### **Baraza la Mitihani la Tanzania**

**89. Mheshimiwa Spika**, ili kusimamia upimaji na Utoaji Tuzo, Serikali kupitia Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), liliendesha mitihani ya upimaji endelevu kwa watahiniwa 1,037,305 wa Darasa la Nne; na Kidato cha Pili watahiniwa 396,770; mitihani ya kumaliza Elimu ya Msingi kwa watahiniwa 763,606; na Kidato cha Nne watahiniwa 448,373 pamoja na upimaji wa Maarifa (QT) kwa watahiniwa 19,547.

**90. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17 Baraza la Mitihani la Tanzania litaboresha mfumo wake wa ukusanyaji na uchakataji takwimu pamoja na kuweka mfumo wa kumtambua mwanafunzi kwa namba maalumu ili kuweza kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi kuanzia anapoandikishwa mpaka anapomaliza mzunguko wa masomo. Baraza pia litaendelea kuimarisha utendaji wake kwa kusimika mashine mbili za kufunga bahasha zenye karatasi za mitihani (*Auto Poly Wrapping and Packing machines*) ili kuondokana na hatari na gharama za ufungaji wa mitihani kwa kutumia mikono na kuimarisha usalama wa Mitihani kwa kupunguza idadi ya watu wanaoshiriki katika maandalizi ya mitihani.

### **Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA)**

**91. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ina majukumu ya kuratibu, kudhibiti, kugharimia, kutoa na kukuza mafunzo ya ufundi stadi nchini. Katika mwaka 2015/16, *Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi*, ilifanya yafuatayo:

(i) ilikamilisha taratibu za uandaaji wa Michoro ya ujenzi wa chuo cha Wilaya ya Karagwe pamoja na kuandaa Hadidu za Rejea (TOR) na ombi kwa ajili ya pendekezo (RFP) na kuwapatia washauri elekezi kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vya Wilaya za Chunya, Korogwe, Kilindi na Ukerewe.

(ii) iliendelea na ukarabati wa miundombinu ya vyuo vya ufundi stadi vya mikoa ya Tanga, Mwanza, Moshi, Kihonda (Morogoro) pamoja na chuo cha walimu wa ufundi stadi cha Morogoro.

(iii) imenunua mitambo na zana za kisasa za kufundishia na kujifunzia na zimeanza kutumika katika vyuo vya ufundi stadi vinne vya; Moshi- fani ya uchoraji majengo; Tanga- Vifaa vya fani ya Umeme wa majumbani na

viwandani; Mwanza-fani ya TEHAMA na umeme; na Makete-vifaa vya fani ya ufundi magari.

(iv) ilitoa mafunzo kwa wanafunzi 400 waliopata mafunzo nje ya mfumo rasmi wa elimu na mafunzo (informal apprentices) katika Mikoa ya Mbeya na Dar es Salaam pamoja na kuwapatia mafunzo walimu wa ufundi 567 katika ngazi ya Cheti na Walimu 27 katika ngazi ya Diploma.

(v) ilitoa mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi 389 (wanaume 253 na wanawake 136) wanaofanya kazi katika Sekta Rasmi kwa makampuni 17 kupitia mpango unaojulikana kama "Skills Enhancement Programme".

(vi) ilitoa mafunzo katika vikundi mbalimbali vya sekta isiyo rasmi kwa washiriki wapatao 878 (Wanaume 344 wanawake 534) katika kutekeleza mpango wa mamlaka wa kuboresha na kuimarisha ufanisi wa utendaji kazi katika Seka isiyo rasmi.

**92. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa mafunzo ya ufundi stadi yanatolewa katika kiwango cha ubora unaotakiwa na soko la ajira, tayari mamlaka imeimarisha eneo la ukaguzi kwa kuwajengea uwezo wakaguzi wapatao 66 (22 toka viwandani na 44 toka vyuoni) kwa mwaka huu wa fedha.

**93. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17

Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi itatekeleza yafuatayo:

(i) kuendelea na ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Mkoa wa Njombe na kuwapata Wakandarasi na kuanza ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya mikoa ya Geita, Simiyu na Rukwa;

(ii) kuanza ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Wilaya za Namtumbo, Chunya, Kilindi na Ukerewe;

(iii) kukamilisha ukarabati wa miundombinu ya Vyuo vya Ufundi Stadi vya Tanga, Mwanza, Moshi, Kihonda na Chuo cha Mafunzo ya Ualimu wa Ufundi cha Morogoro;

(iv) kuanza ukarabati wa vyuo vya Wilaya ya Karagwe na Korogwe;

(v) kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo vya Ufundi stadi vya Iringa; Arusha Oljoro; Morogoro–Kihonda, Mkoa wa Mbeya; Mkoa wa Mwanza; na Chuo cha Ufundi stadi Singida pamoja na Chuo cha Walimu wa Ufundi Stadi cha Morogoro; na

(vi) Kuendelea kufanya tathmini na utahini kwa mafundi stadi wa nje ya mfumo rasmi wa mafunzo (informal apprentices) kwa kuongeza idadi ya fani na kuwajengea walimu wa ufundi stadi uwezo katika eneo hili.

**94. Mheshimiwa Spika**, pamoja na shughuli hizo Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi itatekeleza yafuatayo:

(i) maandalizi ya awali kwa ajili ya kujenga vyuo vipya vya wilaya katika wilaya ya Chato na Nyasa;

(ii) ujenzi wa bweni la wasichana katika chuo cha VETA Makete;

(iii) ujenzi wa bweni la wasichana katika chuo cha VETA Mbeya;

(iv) kukamilisha ujenzi wa chuo cha ufundi stadi katika Halmashauri ya wilaya ya Busokelo na maandalizi ya kuanza mafunzo katika chuo hicho ifikapo 2017;

(v) ukarabati wa Chuo cha Ufundi Stadi cha katika Halmashauri ya wilaya ya Ruangwa; na

(vi) kuviwezesha vyuo viwili vya maendeleo ya Wananchi (Folk Development Colleges) vya Kibondo na Kasulu pamoja na Chuo kimoja cha Ufundi Stadi cha Nkowe ili kuimarisha mafunzo ya ufundi stadi.

#### **Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi**

**95. Mheshimiwa Spika**, kufuatia kuhamishiwa kwenye Wizara yangu Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDC), Wizara imedhamiria kuvitumia Vyuo hivyo ili kuimarisha utoaji wa Mafunzo ya Ufundi stadi kwa maendeleo ya wananchi. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara yangu imepanga kubainisha hali halisi ya miundombinu katika vyuo vyote vya FDC, na kuainisha Vyuo ambavyo vitaweza kutumika kutoa mafunzo ya Ufundi Stadi katika hali yake ya sasa kwa kuzingatia mahitaji ya jamii husika.

**96. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara yangu kwa kutumia fedha zilizokuwa zimetengwa chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto itaanza ukarabati wa vyuo vya Ilula, Newala na Kilosa. Aidha, itajenga vyoo katika vyuo vya Buhangija, Bariadi na Kisarawe. Vilevile itaunganisha umeme katika vyuo vya Mwanhala, Malya, Rubondo, Ulembwe, Munguri na Msingi. Wizara pia itashughulikia upatikanaji wa hatimiliki wa vyuo vya Kilwa Masoko, Chisalu, Kisarawe, Chilala, Arnautoglu, Musoma, Mwanva, Ikwiriri, Msingi na Ifakara.



## **Mamlaka ya Elimu Tanzania**

**97. Mheshimiwa Spika**, katika kugharimia Elimumsingi hapa nchini, Serikali kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania inayosimamia mfuko wa Elimu nchini, imeweza kukusanya jumla ya Shilingi 33,647,048,003.00/= ambapo vyanzo vyake ni Tozo ya Elimu (Education Levy) kiasi cha Shilingi 30,486,481,326.00 na mapato ya ndani ni Shilingi 3,160,566,677.00.

**98. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Mamlaka ya Elimu Tanzania iliwezesha utekelezaji wa yafuatayo:

(i) Kuwajengea uwezo walimu na wanafunzi wa Hisabati, Biologia, Kingereza na Kiswahili ambapo walimu 15,000 na wanafunzi 6,000 walinufaika;

(ii) ilijenga mabweni 11 katika shule za Muyenzi (Ngara), Moyowasi (Kibondo), Mkongo (Rufiji), Endasak (Hanang), Shelui (Iramba), Kishamapanda (Busega), Kilumba (Nyasa), Mbuga (Mpwapwa), Kisiwani (Same), Kibaigwa (Kongwa), na Ufana (Babati); na

(iii) Imegharimia uchapishaji wa vitabu 558,720 vya jinsi ya kujibu maswali ya mitihani ya Kidato cha Pili na cha Nne na Miongozo 75,360 katika kufanikisha mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN). Vitabu hivi vimewezesha walimu na wanafunzi kutambua mada ngumu na kutoa miongozo kwa walimu na watahiniwa kuhusu namna ya kujibu maswali ya mitihani hiyo.

**99. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Mamlaka ya Elimu Tanzania itatekeleza yafuatayo:

(i) ukarabati wa majengo ya Shule kongwe 7 za Sekondari pamoja na kuzipatia vifaa vya maabara;

(ii) kuliwezesha Baraza la Mitihani kununua mitambo ya uchapishaji na ufungaji mitihani ili kuboresha na kufanikisha shughuli za uandaaji na utoaji wa mitihani; na

(iii) kutoa motisha kwa wanafunzi 10 watakaofanya vizuri na shule za msingi na sekondari 3000 zitakazofanya vizuri. Aidha, katika kupunguza changamoto za nyumba za walimu, Wizara itajenga nyumba za walimu 50 zitakazowezesha walimu 300 kupata makazi katika maeneo yasiyofikika kirahisi.

## **Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

**100. Mheshimiwa Spika**, Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ni nyenzo kubwa katika kuongeza wataalam katika ngazi ya elimu ya juu nchini. Wizara

kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, ilitoa Mikopo kwa wanafunzi wanaodahiliwa kusomea masomo ya kipaumbele kama vile Udaktari na Ualimu wa Sayansi na Hisabati. Mikopo hiyo pia imekua ikitolewa kwa wanafunzi wanaosomea fani adimu kama vile Uhandisi wa mafuta na gesi pamoja na Uhandisi umwagiliaji. Aidha, Serikali imeendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaosoma masomo mengine kwa kuzingatia viwango vya uhitaji.

**101. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16 hadi kufikia Machi 2016, jumla ya wanafunzi 124,243 walikuwa wamepatiwa mikopo ya kiasi cha Shilingi 467,425,257,529.00. Idadi hii ilijumuisha wanafunzi 54,072 wa mwaka wa kwanza na 70,171 wanaoendelea na masomo. Aidha, Bodi pia ilitoa Mikopo kwa wanafunzi 7,996 wa Diploma ya Ualimu wa Hisabati na Sayansi na pamoja na wanafunzi 270 wa mafunzo ya sheria. Aidha, wanafunzi 685 wanaosomea nje ya nchi kwa makubaliano ya ushirikiano baina ya Tanzania na nchi rafiki (Algeria, Ujerumani, Cuba, Misri, Msumbiji, China na Urusi) hukopeshwa fedha za kujikimu.

**102. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, wanafunzi 1,957 wanaosomea udaktari wa binadamu wamepatiwa ruzuku kwa kiasi cha Shilingi 5,514,656,888.00. Idadi hii inahusisha wanafunzi wanaoendelea na wanafunzi wapya kwenye fani hii ya udaktari wa binadamu.

### **Mwongozo wa Utoaji Mikopo**

**103. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, imeboresha mwongozo wa utoaji mikopo kwa ajili ya mwaka 2016/17. Mwongozo huo unalenga kuondoa au kupunguza malalamiko kutoka kwa wanafunzi wasiopata mikopo kwa kuwapa kipaumbele waombaji wenye uhitaji mkubwa. Aidha, waombaji waliodahiliwa kwenye fani za vipaumbele vya kitaifa na masomo mengine watapatiwa mikopo kwa kuzingatia matokeo ya upimaji uwezo (Means Testing).

**104. Mheshimiwa Spika**, ili kuhakikisha kuwa wadau wa Bodi ya Mikopo wanapata taarifa sahihi na kupunguza malalamiko, katika mwaka 2016/17 Wizara yangu itaendelea kuendesha kampeni ya elimu kwa umma, ili kuelimisha wadau juu ya huduma zitolewazo na Bodi hiyo.

### **Urejeshwaji Mikopo**

**105. Mheshimiwa Spika**, kiwango cha urejeshwaji mikopo bado kipo katika kiwango kisichoridhisha. Changamoto zilizopo ni pamoja na kutokuwepo kwa mikakati thabiti ya ufuatiliaji wa wakopaji, udhaifu katika Sheria ya Bodi ya Mikopo ambapo, makato ya marejesho ya mikopo kutoka kwenye mshahara si ya lazima (*statutory deductions*). Aidha bado kuna mwitikio mdogo kutoka kwa

wanufaika kujitokeza kuanza kurejesha mikopo yao pamoja na waajiri kutokutimiza majukumu yao ya kuwasilisha taarifa za wanufaika wa Mikopo.

**106. Mheshimiwa Spika**, ili kukabiliana na changamoto na kuongeza kasi ya marejesho ya mikopo katika mwaka 2016/17, Wizara yangu kupitia Bodi ya Mikopo imeweka mikakati ya kuongeza ukusanyaji na kasi ya marejesho ya mikopo kwa kushirikiana kwa karibu na mamlaka nyingine za Serikali kwenye kukusanya marejesho; na kuendelea kutoa elimu stahiki kwa wadau kuhusu urejeshwaji wa mikopo hii. Aidha Sheria ya Bodi ya Mikopo inafanyiwa marekebisho ili kuongeza kiwango cha urejeshwaji.

**107. Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua nafasi hii kuwakumbusha wanufaika wote wa mikopo kufanya marejesho ili watanzania wengine wenye uhitaji waweze kunufaika. Nawasihi wale wenye uwezo walipe kwa mkupuo mmoja ili kupunguza utegemezi wa Bodi ya Mikopo kwa Serikali. Kwa kufanya hivyo, fedha zinazotengwa kwenye Bodi ya Mikopo zingeweza kutumika kuimarisha sekta ya elimu katika maeneo mengine muhimu. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wale wote waliojitokeza kulipa mikopo yao kwa mkupuo mmoja.

## **5.7 USIMAMIZI WA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI**

**108. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16, Wizara yangu imeendelea kusimamia utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali zinazotekelezwa katika ngazi zote za Elimu na Mafunzo.

### **Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu II (MMES II)**

**109. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES II) kwa ushirikiano na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tangu mwaka 2010 hadi sasa. Mradi huu umelenga kuboresha miundombinu ya shule za sekondari 1,200; kuhakikisha kuwepo kwa walimu wa kutosha na kuboresha ufundishaji hususani katika masomo ya Hisabati, Sayansi na Lugha. Malengo mengine ni kusimamia matumizi sahihi ya rasilimali fedha kwenye shule kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na kujenga uwezo wa Wakala na Taasisi za Elimu ili kutekeleza mikakati ya kielimu iliyopo na ile ijayo.

**110. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI imeimarisha mfumo wa takwimu kwa ajili ya kukusanya, kuchakata na kuhifadhi takwimu. Aidha, mfumo na zana zilizokuwa zinatumiwa katika ukusanyaji takwimu zimefanyiwa mapitio na kuboreshwa ili kukidhi mahitaji ya takwimu za elimu.

**111. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16, Wizara imetekeleza yafuatayo:

(i) imetoa mafunzo kwa walimu 3,419 wa shule za sekondari wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Lugha; na

(ii) imefanya mapitio ya mwongozo wa mafunzo na moduli za ufundishaji na ujifunzaji kwa walimu wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Lugha yenye lengo la kuhakikisha kuwa elimu bora yenye viwango vya kimataifa inatolewa kwa wanafunzi wa Kitanzania.

**112. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara inalenga kutekeleza yafuatayo:

(i) kutoa mafunzo kwa walimu 7,000 wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Lugha pamoja na kununua vifaa vya TEHAMA vya kufundishia na kujifunzia kwa Vituo 50 vya TEHAMA vilivyopo kwenye Shule za Sekondari;

(ii) kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miundombinu ya shule za sekondari 408 itakayojengwa kupitia Halmashauri mbalimbali nchini;

(iii) kufanya tathmini ya MMES II na kuandaa Andiko la Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu ya Tatu (MMES III);

(iv) kukagua matumizi ya fedha za MMES II kwenye Wizara na Halmashauri;

(v) kugharimia uchapaji wa vitabu vya Sayansi na Hisabati; na Kiongozi cha Mwalimu kwa wanafunzi wasioona na wenye uono hafifu;

(vi) kuhakiki uchakataji na uboreshaji wa mfumo wa ukusanyaji takwimu za elimu na kutegemeza matumizi ya takwimu; na

(vii) kuwezesha na kutegemeza shughuli za MMES II zinazohusiana na mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN).

**Mradi wa Kusaidia Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (Literacy and Numeracy Education Support (LANES))**

**113. Mheshimiwa Spika**, katika juhudi za kuhakikisha kwamba watoto wanaojiunga na elimu ya msingi wanamudu vema stadi za Kusoma Kuandika na Kuhesabu, Wizara yangu inaendelea na uratibu wa utekelezaji wa Programu wa Kukuza Stadi za KKK.

**114. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa fedha 2015/16, Wizara imetekeleza yafuatayo:

(i) imegharimia mapitio ya Mitaala ya Elimu ya Awali na Msingi kwa lengo la kwenda sambamba na dhana ya Elimumsingi;

(ii) imegharimia mafunzo kuhusu mabadiliko ya ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za KKK kwa Wathibiti Ubora wa Shule 1,500. Aidha, magari 38 yamenunuliwa na kugawiwa katika Wilaya ambazo hazikuwa na magari na hivyo kuwawezesha Wathibiti Ubora wa Shule kuzifikia shule nyingi zaidi na kwa urahisi; na

(iii) imegharimia mafunzo ya menejimenti na uongozi wa shule kwa Waratibu Elimu Kata 2,480 na Walimu wakuu wa Shule za Msingi 10,870. Kupitia mafunzo haya Walimu Wakuu wa shule za msingi sasa wataweza kuandaa na kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Shule kwa ufanisi zaidi (*Whole School Development Plan*).

**115. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa fedha 2016/17, Wizara yangu kupitia programu hii itatekeleza yafuatayo:

(i) itaimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK kwa kutoa mafunzo kabilishi kwa walimu 22,955 wa Darasa la III & IV kuhusiana na mtaala uliohuishwa;

(ii) itakamilisha mpango wa kuimarisha miundombinu ya matumizi ya mfumo wa kielektroniki kwenye Halmashauri zote nchini. Mfumo huu utasaidia upatikanaji wa takwimu za ngazi ya shule moja kwa moja kwenye mtandao na hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa gharama za ukusanyaji wa takwimu kwenye mifumo isiyo ya kisasa;

(iii) itagharimia usimikaji mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji taarifa za wanafunzi chini ya Baraza la Mitihani Tanzania ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa hizo wakati wa Mitihani. Utaratibu huu utaisaidia Serikali kupunguza matumizi makubwa ya fedha za ukusanyaji taarifa chini ya mfumo wa TSM9;

(iv) itawezesha kamati za shule kupata mafunzo ya kuandaa mipango ya maendeleo ya shule kwa lengo la kuziwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu ili kuharakisha maendeleo ya shule;

(v) itahamasisha jamii kushiriki kwenye utekelezaji wa mpango wa LANES kupitia vyombo vya habari na utoaji taarifa kwa umma, machapisho, matamasha na vikundi vya watoto (childrens 3Rs Clubs);

(vi) kutoa nafasi za masomo na tafiti ili kuongeza ufahamu wa masuala ya elimu ya awali;

(vii) kuajiri mtaalamu elekezi kuandaa na kutekeleza katika ngazi ya majaribio maudhui ya kieletroniki ya KKK ili yatumike kuongeza ari ya kujifunza kwa watoto;

(viii) kufanya tathmini ya Sekta ya Elimu na kutumia mapendekezo yake kutengeneza Mpango wa Maendeleo wa Elimu wa miaka mitano 2016/17 hadi 2020/21;

(ix) kufuatilia na kutathmini mipango ya Sekta ya Elimu; na

(x) kuimarisha usimamizi, utekelezaji na ufuatiliaji wa mipango ya LANES kwa kutoa mafunzo ya matumizi bora ya rasilimali fedha kwa Watendaji na Wakurugenzi pamoja na kununua vifaa vya uendeshaji kwa Idara, Taasisi na vitengo vinavyotekeleza LANES.

### **Mradi wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni “School Water, Sanitation and Hygiene (SWASH)”**

**116. Mheshimiwa Spika**, lengo la Mradi wa Huduma ya Maji, Afya na Usafi wa Mazingira ni kuboresha miundombinu ya vyoo bora, upatikanaji wa maji safi na salama pamoja na utoaji wa elimu ya afya na kutunza mazingira ya shule. Katika mwaka 2015/16, miundombinu ya vyoo vya shule za msingi 1,087 iliboreshwa; shule 2,531 ziliunda vikundi vya usafi ambavyo hutoa elimu ya afya shuleni; na kuweka vifaa vya kunawia mikono shuleni. Aidha, timu za usafi wa mazingira za mikoa 10 (Dar es Salaam, Morogoro, Ruvuma, Njombe, Iringa, Tanga, Kilimanjaro, Pwani, Dodoma na Mtwara) ya Tanzania Bara zilipatiwa elimu elekezi kuhusu utumiaji wa Mwongozo wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira shuleni.

**117. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, mradi wa SWASH umelenga kufikia jumla ya shule 4,200 (za msingi 3,500 na 700 za sekondari). Aidha, Serikali itashirikisha wadau mbalimbali wa elimu ili kupata rasilimali fedha ili kutatua tatizo la ukosefu wa vyoo bora shuleni.

**118. Mheshimiwa Spika**, mradi huu pia umelenga kutekeleza yafuatayo:

(i) kufanya ufuatiliaji na tathmini ya ujenzi wa vyoo bora kwenye shule zilizopatiwa fedha za mradi, kujenga uwezo wa utekelezaji na upanuzi wa mradi kwa waratibu wa mradi ngazi ya Mkoa na Halmashauri na kuwezesha kuandaa mfumo wa ukusanyaji takwimu za taarifa za upatikanaji maji, vyoo bora na vifaa vya unawaji mikono;

(ii) kukusanya takwimu za vyoo, maji na elimu ya usafi wa mazingira shuleni ili kupanga mipango ya muda mfupi na mrefu ya kuboresha miundombinu ya vyoo na mifumo ya maji katika mikoa 14; na

(iii) kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa huduma ya maji, afya na usafi wa mazingira, kuchapa miongozo, kugharimia ununuzi wa vitendea kazi na kuendesha harambee kwa ajili ya ujenzi wa vyoo na miundombinu ya maji safi na taka.

### **Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (Mpango wa Ugharimiaji - Lipa Kulingana na Matokeo (Programme for Results – P4R)**

**119. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutekeleza programu mpya ya kufadhili sekta ya elimu inayoitwa “Lipa Kulingana na Matokeo” (P4R) kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo ambao ni Benki ya Dunia, DfID na Sida. Programu hii inalenga kujenga uwezo wa Serikali wa kutekeleza vipaumbele vyake ilivyojiwekea. Programu ilianza kutekelezwa mwaka 2014/15 ambapo mpaka sasa jumla ya Shilingi bilioni 90 zimepatikana kutokana na Serikali kutekeleza vipaumbele vyake kwa ufanisi. Aidha, kupitia programu hii, Wizara imelenga kuhakikisha madai yote ya walimu yasiyo ya mishahara yanalipwa. Kupitia programu hii, hadi kufikia mwezi Aprili, 2016 jumla ya walimu 63,409 wa shule za msingi na sekondari wameshalipwa madai yao yanayofikia Shilingi bilioni 22.24.

**120. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Wizara yangu itatumia fedha zitakazopatikana kupitia programu hii kusaidia kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kufanya ukarabati mkubwa kwa shule kongwe za sekondari nchini. Kwa hivi sasa uchambuzi wa mahitaji ya ukarabati (conditional survey) wa shule 22 za awamu ya kwanza unafanyika na ukarabati unategemewa kuanza mwezi Agosti, 2016.

**121. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17 Serikali imejipanga kuhakikisha kuwa shule zetu za sekondari zina vifaa vya maabara na vitabu vya kutosha ambapo tayari Wizara yangu imetangaza zabuni ya ununuzi wa vifaa hivyo vya maabara na uchapaji wa vitabu hivyo, ambavyo vitasambazwa nchini kote. Maabara zote zilizojengwa na Halmashauri kwa kushirikiana na wananchi zitapatiwa vifaa vya maabara. Ununuzi wa vifaa vya maabara utafanyika kwa awamu tatu ambapo awamu ya mwisho inategemewa kukamilika mwaka wa fedha 2018/19. Nia ya Serikali katika mpango huu ni kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa inakidhi viwango na wanafunzi wanapatiwa zana zote muhimu katika kujifunza.



**122. Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kuzihamasisha Halmashauri ambazo hazijakamilisha maabara zikamilishe ili ziweze kunufaika na mpango huu wa Wizara yangu wa kutoa vifaa vya maabara.

**Mradi wa Kutegemeza Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Ualimu**

**123. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inatekeleza mradi wa kutegemeza Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Ualimu unaolenga kuongeza udahili, usawa na ubora katika maeneo hayo. Hii inahusisha pia kujenga uwezo wa wakufunzi na walimu wa sekondari na vyuo vya Ualimu katika masomo ya Sayansi na Hisabati. Katika mwaka wa fedha 2015/16 mradi umefadhili walimu 5 wa Chuo cha Ufundi Arusha, watatu katika ngazi ya Digrii ya uzamili na wawili katika ngazi ya uzamivu. Aidha, wanataaluma 162 wa vyuo vya ufundi vilivyosajiliwa na NACTE wamejengewa uwezo katika kuendeleza mitaala, kufundisha na kutathmini mafunzo yanayozingatia umahiri ili kuinua ubora wa Elimu na Mafunzo yatolewayo katika Vyuo vya Ufundi.

**124. Mheshimiwa Spika,** mradi huu umewezesha ununuzi wa kompyuta 400 kwa ajili ya vyuo 40 vya ufundi. Aidha, katika mwaka 2016/17 mradi unalenga kukarabati vyuo sita vya ualimu wa Sayansi vya Dakawa, Tabora, Kleruu, Butimba, Mpwapwa na Marangu ambapo kwa mwaka 2015/2016 uchambuzi wa awali wa mahitaji ya ukarabati umefanyika. Vilevile, mradi utagharimia ukarabati wa Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi cha Morogoro na kununua vifaa vya maabara kwa ajili ya mafunzo ya ufundi kwenye fani za gesi na mafuta kwa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi cha Mkoa wa Mtwara.

**125. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2016/17, mradi huu utawezesha ununuzi wa vifaa mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vya Ufundi Stadi vya Mkoa ya Mtwara, Njombe, Geita, Simiyu na Rukwa ili kuinua ubora wa Elimu na Mafunzo yatolewayo katika Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Aidha, mradi pia utaanza ujenzi na ukarabati wa majengo ya hosteli na madarasa katika Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro.

**Mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Vyuo vya Ualimu vya Ndala, Shinyanga, Kitangali na Mpuguso (Upgrading of Teachers' Colleges)**

**126. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Wizara yangu itatekeleza Mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Vyuo vya Ualimu vya Shinyanga, Mpuguso, Ndala na Kitangali ambao unalenga kuinua ubora wa elimu ya msingi na sekondari. Lengo la mradi huu ni kuboresha mazingira ya kusomea kwa walimu waliopo, kusaidia kuvutia walimu wapya na kuhakikisha kuwa

walimu wanafunzi wana motisha ya kupata ujuzi ili waweze kutoa elimu bora kwa wanafunzi wao mara watakapohitimu. Idadi ya watakaohitimu baada ya kukamilika kwa ukarabati wa vyuo hivi vinne inatarajiwa kufikia wanachuo 3,300 kwa mwaka.

### **Mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu (STHEP)**

**127. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha miundombinu na ufundishaji wa Elimu ya Juu, Wizara imetekeleza Mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa Awamu ya Pili, kuanzia mwezi Septemba 2014 hadi Januari 2016. Mradi huu umepata ufadhili wa Benki ya Dunia. Vyuo na Taasisi za Elimu ya Juu zilizonufaika katika mradi huu ni;

- (i) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam,
- (ii) Chuo Kikuu cha Ardhi,
- (iii) Chuo Kikuu Huria cha Tanzania,
- (iv) Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo,
- (v) Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar,
- (vi) Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu cha Dar es Salaam,
- (vii) Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa,
- (viii) Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam,
- (ix) Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu,
- (x) Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi; na
- (xi) Tume ya Vyuo Vikuu.

**128. Mheshimiwa Spika**, malengo ya mradi huu yalikuwa ni kujenga uwezo wa wanataaluma na watumishi wa Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu kwa kudhamini mafunzo katika ngazi ya uzamili na uzamivu, kujenga miundombinu mipya ya vyuo vikuu na kufanya ukarabati wa majengo katika Taasisi. Mradi pia ulisaidia ununuzi wa vifaa na samani za kufundishia na kujifunzia kulingana na vipaumbele vya Taasisi husika.

**129. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Aprili, 2016 mradi umegharimia masomo ya wanataaluma 188 wa ngazi ya uzamivu (asilimia 30 ni wanawake); na wanataaluma 208 wa ngazi ya uzamili (asilimia 28 ni wanawake). Zaidi ya asilimia 60 ya wanufaika wamehitimu mafunzo yao na wanaendelea na kazi katika Taasisi zao na waliobaki wako katika hatua za mwisho za kuhitimisha mafunzo yao.

**130. Mheshimiwa Spika**, mradi pia umejenga majengo mapya 25 ya kufundishia na kujifunzia, na pia umefanyia ukarabati majengo yaliyokuwepo katika vyuo vikuu 7. Ujenzi na Ukarabati huo umeviongezea vyuo vikuu uwezo wa kuchukua wanafunzi wa elimu ya juu 47,622 zaidi ikilinganishwa na kabla ya mradi. Aidha, wakutubi, wataalamu wa maabara na watumishi wengine 1,794

katika taasisi za ARU, DUCE, DIT, OUT, MUCE, SUA, na UDSM walipata mafunzo ya muda mfupi ya kuwaongezea ujuzi katika maeneo yao. Vile vile wananchi 2,194 wanaozunguka vyuo wamenufaika na miundombinu ya kitafiti iliyojengwa kama vile mitambo ya kusafisha maji taka iliyojengwa Chuo Kikuu cha Ardhi, Dar es Salaam.

**131. Mheshimiwa Spika**, mradi pia umewezesha ununuzi wa vifaa vya maabara 5,634 vinavyotumiwa na wanafunzi 16,600 wa elimu ya juu. Kwa upande wa TEHAMA vifaa 1,831 vilivyonunuliwa vimeweza kusaidia wanafunzi takriban 5,400 katika fani mbalimbali za elimu ya juu. Aidha, vitabu 6,121 vilisambazwa kwenye Taasisi na vilipunguza tatizo la upungufu wa vitabu kwa kiasi kikubwa. Hatua hizi zimechochea ongezeko na ubora wa wanafunzi wanaohitimu katika fani ya Sayansi na Teknolojia kutoka wahitimu 3,353 kwa mwaka 2007 hadi kufikia wanafunzi zaidi ya 8,294 mwaka 2015.

**132. Mheshimiwa Spika**, mradi pia umewezesha ujenzi wa mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya udahili wa wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini. Mfumo huu umewezesha waombaji kuchagua programu katika vyuo mbalimbali kwa ufanisi kupitia mtandao na simu za mkononi. Aidha, mfumo huu umesaidia kuondoa tatizo la wanafunzi kudahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja pamoja na kubaini wanaotumia matokeo ya kughushi kwa kuwa mfumo huu umeunganishwa na Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA). Mfumo huu umepunguza kwa kiasi kikubwa gharama za maombi ya udahili katika vyuo vya elimu ya juu kwa kuwa mwombaji anaomba na kulipia mara moja tu.

#### **Mradi wa Elimu na Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi (Education and Skills for Productive Jobs Program– ESPJ)**

**133. Mheshimiwa Spika**, baada ya kukamilisha mradi wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, Wizara imeandaa mradi mpya utakaoanza mwaka 2016/17 kwa ajili ya kukuza stadi za kazi na ujuzi. Mradi huu umeandaliwa ili kuwezesha utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza na kupanua stadi za kazi na ujuzi. Mkakati huu uliandaliwa na Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi Vijana na Ajira, na Walemavu. Mradi utajikita katika kuongeza fursa za upatikanaji wa stadi za kazi na kuongeza ujuzi katika sekta sita za kipaumbele za kukuza uchumi ambazo ni kilimo na kilimo uchumi, utalii, uchukuzi, ujenzi, nishati na madini; na TEHAMA. Uchaguzi wa sekta hizi umezingatia mahitaji makubwa ya waajiri katika sekta hizo, mchango wa sekta katika uchumi, upungufu mkubwa wa wataalamu, uwezo wa kuongeza ajira; na mahusiano kati ya sekta hizi na nyingine.

**134. Mheshimiwa Spika**, lengo kuu la mradi wa ESPJ ni kuimarisha na kupanua upatikanaji na ukuzaji wa ubora wa stadi za kazi na ujuzi katika ngazi za ufundi na ufundi stadi, elimu ya juu na sekta isiyo rasmi kwenye maeneo

lengwa. Aidha, mradi unalenga kuimarisha mfumo wa kitaasisi wa kusimamia, kuratibu na kugharimia uendelezaji stadi za kazi katika ngazi ya kitaifa na kisekta kwa kushirikiana na sekta binafsi. Jumla ya wanafunzi watakaopata mafunzo katika mradi inatarajiwa kuwa zaidi ya 47,000 kwa miaka mitano. Mradi huu wa miaka mitano kuanzia mwaka 2016/17 unagharimiwa na Serikali kupitia mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 120 kutoka Benki ya Dunia.

## 6.0 SHUKRANI

**135. Mheshimiwa Spika**, napenda kutambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu katika Wizara. Kwa namna ya pekee namshukuru sana Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya (Mb) Naibu Waziri, kwa ushirikiano mkubwa anaonipa. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Bi. Maimuna Kibenga Tarishi; Manaibu Makatibu Wakuu; Profesa Simon Samwel Msanjila na Dkt. Leonard Douglas Akwilapo, Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Wakuu wa Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara yangu kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku. Napenda pia kuwashukuru, Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi, Watumishi wa Wizara, Wanataaluma, Wanafunzi na wadau wote wa Elimu kwa ushirikiano wao katika kuendeleza Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi.

**136. Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru wadau wote wa sekta ya elimu, sayansi, teknolojia na ufundi wakiwemo Washirika wa Maendeleo, viongozi mbalimbali na kwa namna ya pekee wananchi ambao wamechangia sana katika kufanikisha utekelezaji wa mipango ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi.

**137. Mheshimiwa Spika**, washirika mbalimbali wa Maendeleo na wadau wa Elimu wamechangia katika kufanikisha mipango ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa kuwa si rahisi kuwataja wote. Napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya Wizara yangu, kuwashukuru na kuwatambua baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za Algeria, Canada, China, Cuba, India, Italia, Japan, Urusi, Denmark, Finland, Norway, Marekani, Mauritius, Msumbiji, Misri, Norway, Sweden, Uingereza, Ujerumani, Korea Kusini, Uturuki na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**138. Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuyashukuru mashirika yaliyochangia katika kufanikisha programu za Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi ambayo pamoja na: Aga Khan Education Services, Airtel, Barclays Bank, Benki Kuu, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Taifa ya Biashara, British Council, Campaign for Female Education (CAMFED), Care International, Children International, Children's Book Project, Commonwealth Secretariat, Benki ya CRDB, DAAD, DfID, Education Quality Improvement Programme (EQUIP(T)), FEMINA, Ford Foundation, GIZ, Global Partnership for Education, International Labour Organisation (ILO), International Reading

Association, Irish Aid, Inter University Council of East Africa (IUCEA), Japan International Cooperation Agency (JICA), Korea International Cooperation Agency (KOICA), National Micro Finance Bank (NMB), Peace Corps, Plan International, Rockefeller, Swedish International Development Agency (Sida), Sight Savers International, Tanzania Education Network / Mtandao wa Elimu Tanzania (TENMET), Tigo, Umoja wa Nchi za Ulaya, United Nations Development Programme (UNDP) , UNESCO, UNICEF na WaterAid.

## **7.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2016/17**

**139. Mheshimiwa Spika**, ili kuwezesha utekelezaji wa malengo yaliyopangwa katika mwaka 2016/17, Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi **1,396,929,798,625.00** ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**140. Mheshimiwa Spika**, katika maombi haya:

(i) Shilingi **499,272,251,000.00** zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara ambapo Shilingi **386,904,995,000.00** ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi **112,367,256,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo;

(ii) Shilingi **84,132,297,000.00** zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Idara na Vitengo. Kati ya hizo, Shilingi **57,246,945,000.00** ni kwa ajili ya mishahara, na Shilingi **26,885,352,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo;

(iii) Shilingi **415,139,954,000.00** zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Taasisi. Kati ya hizo, Shilingi **329,658,050,000.00** ni kwa ajili ya mishahara, na Shilingi **85,481,904,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; na

(iv) Shilingi **897,657,547,625.00** zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo, Shilingi **620,693,856,575.00** ni fedha za ndani na Shilingi **276,963,691,050.00** ni fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo.

**141. Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wizara yangu, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anwani ya: <http://www.moe.go.tz>.

**142. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono sasa tutamsikia Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA  
JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA  
UFUNDI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 PAMOJA NA  
MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI  
YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017  
KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI**

**MHE. HUSSEIN M. BASHE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA  
BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika,  
nitaomba ripoti ya Kamati yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2016, napenda kwanza kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii inayohusu maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati juu ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii yenye jukumu la Kikanuni, Nyongeza ya Nane 6(5)(c) iliyo chini ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kusimamia shughuli za Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi. Aidha, katika Nyongeza hiyo ya Nane, Kanuni ya 7(1)(a) inaeleza jukumu la Kamati zote za kisekta ikiwemo Kamati hii la kushughulikia bajeti ya Wizara inazosisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati hii ina jukumu la kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoishia 2015/2016 pamoja na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha unaoishia ili kufanya ulinganisho kuhusu makadirio ya matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata wa 2016/2017. Lengo ni kuweza kuishauri Serikali namna bora ya kwenda ili kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuwapunguzia mzigo Watanzania kufuatia agizo lake la kufuta ada na michango mbalimbali katika elimu ya msingi na sekondari. Pamoja na changamoto zilizopo, Kamati inaamini Serikali itazifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Uchambuzi wa Taarifa kuhusu ukusanyaji wa maduhuli kama ilivyo kwenye taarifa mliyopewa.



Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Wizara hii (Fungu 46) iliidhinishiwa Sh.511,525,227,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka yaani Machi 2016, Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha Sh.316,402,868,828 sawa na asilimia 68.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bajeti ya maendeleo, Kamati imebaini kuwa katika robo tatu ya mwaka wa fedha, Wizara imepokea jumla ya Sh.360,922,754,359.61 sawa na asilimia 61.9 ya fedha iliyoidhinishwa Sh.582,670,597,884.49. Kamati imebaini kuwa kiasi hiki cha fedha kisichokidhi mahitaji ni moja ya sababu ya kutotekelezwa kwa miradi ya maendeleo ipasavyo. (Rejea Kielelezo Na. 2)

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo na matokeo ya miradi ya maendeleo iliyokaguliwa. Mradi wa kutoa Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Katika mwaka wa fedha wa 2015/2016, Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi (Fungu 46) iliidhinishiwa Sh.418,300,000,000/= kwa ajili ya miradi ijulikanayo kama "*Higher Education Students Loans*" ambao ni Mradi wa kutoa Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Mradi huu ulipangiwa kutekelezwa chini ya Kifungu 7001 - Elimu ya Juu (*Higher Education*) cha Fungu 46.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukaguzi huo Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto kadhaa kama vile kuchelewa kupokea fedha za mkopo kutoka Serikalini. Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2016 ambayo ni robo tatu ya mwaka wa Fedha 2015/2016, Bodi ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 245 sawa na asilimia 55 tu ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Fedha hizo zimetumika kutoa mikopo kwa ajili ya wanafunzi 122,786. Tafsiri ni kwamba kama fedha hizo zingetolewa zote kwa asilimia 100 basi wanafunzi wengi zaidi wangepata mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili. Kamati pia ilifanya ukaguzi wa Mradi wa Upanuzi na ukarabati wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili - Mloganzila. Ujenzi wa mradi huu unalenga katika kuboresha Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili kwa kujenga tawi la Chuo na hospitali ya kisasa kwa ajili ya kufundishia na kutoa huduma. Tawi hili likikamilika, Chuo kitaweza kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 4,010 wa sasa hadi kufikia wanafunzi 15,000 jambo ambalo pia litaongeza wataalam wa afya nchini. Mradi ulianza rasmi tarehe 10 Machi 2014 na unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 9 Juni 2016. Mradi huu unatokana na mkopo wa riba nafuu kutoka *African Development Bank* wa kiasi cha dola za kimarekani bilioni 9.4 na mchango wa Serikali wa dola za kimarekani 755,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imetembelea mradi, ujenzi ulikuwa umefikia asilimia 82. Hata hivyo, Kamati ilijulishwa pia kiasi cha fedha ambacho



kilipaswa kutolewa kama mchango wa Serikali kilikuwa hakijatolewa. Ni imani ya Kamati kuwa fedha hizo zitatoka katika mwaka huu wa fedha 2015/2016 ili kukamilisha mradi na kitakachokuwa kimebaki ni ununuzi wa vifaa ambapo Kamati ilielezwa umepangwa katika mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2015/2016:-

(i) Kamati imebaini kuwa katika Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili – Mloganzila hakuna fedha iliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Walimu. Kamati imeshangazwa mradi mkubwa kama huu kutotengewa fedha za ujenzi wa nyumba za watumishi na inajiuliza watumishi hawa wataenda kukaa wapi? Kamati inaitaka Serikali itenge fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi ili mradi utakapoanza kufanya kazi na nyumba hizo ziwe tayari.

(ii) Kamati imebaini kuwa vijana wengi wenye alama za kuwawezesha kuendelea na masomo ya elimu ya juu wameshindwa kuendelea kutokana na kutokuwa na uwezo wa kujilipia. Uwepo wa mikopo hii ingekuwa ni fursa njema kwao kujiendeleza kielimu na hivyo kuongeza idadi ya wasomi nchini wenye uwezo wa kuleta tija kwenye maendeleo ya nchi. Kamati imeona ni vyema sasa wanafunzi wengi zaidi waendeleo kupewa mikopo kwa miaka ijayo ili kulifanya Taifa letu kuwa na idadi kubwa ya wasomi kama zilivyo nchi nyingine ambao watachochea maendeleo ya endelevu ya nchi. Mchumi Maarufu Duniani na Mhadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Havard Sen aliwahi kusema, *“Economic growth without investment in human development is unsustainable and unethical”*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati, katika mwaka wa fedha 2015/2016. (Kiambatisho Na. 1).

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa mpango wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara inaomba jumla ya Sh.1,396,929,798,625/=. Kati ya Fedha hizo, Sh.499,272,251,000/= sawa na asilimia 35 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.897,657,547,625/= sawa na asilimia 64 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kiasi hiki kinachoombwa ni nyongeza ya Sh.30,733,973,736 sawa na asilimia 27 ya kiasi cha Sh.1,094,195,824,888 kilichotengwa katika mwaka wa fedha 2015/2016. Kamati inaipongeza Serikali kwa ongezeko hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya uchambuzi ili kuona bajeti ya Wizara hii ni sawa na asilimia ngapi ya Bajeti Kuu ya Serikali na ilibaini kuwa kiasi hiki kinachoombwa katika mwaka huu wa fedha 2016/2017 ni sawa na asilimia

4.4 tu ya Bajeti Kuu ya Serikali. Ipo haja ya kuwekeza zaidi kwenye elimu kwa kutenga bajeti ya kutosha kwani usalama wa nchi tafsiri yake siyo uwepo wa Jeshi Imara tu bali pia elimu bora kwani madhara ya elimu duni katika usalama wa nchi ni makubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya elimu nchini kwetu inasikitisha na ni hatari kwa usalama na uhai wa Taifa letu. Tathmini na tafiti nyingi duniani zimethibitisha elimu bora ni ile inayoweza kumsaidia raia kukabiliana na changamoto ili kujenga Taifa imara na salama zaidi. Usalama wa nchi huimarika zaidi raia wake wanapoweza kukabiliana na mahitaji ya wakati na jamii husika. Taifa letu limejenga mfumo wa elimu ambayo haikidhi dira na mahitaji ya nchi. Tunahitaji kujenga Taifa la viwanda lakini hatuna wataalam wa sayansi. Dira ya nchi haifungamani na mkakati wa elimu, wale wanaofeli ndiyo huandaaliwa kufundisha katika elimu ya msingi na sekondari na wale wanaomaliza chuo kikuu wenye ufaulu mzuri wa daraja la kwanza kwa maana ya *1st class* ndiyo wanaobaki kufundisha vyuo vikuu, hili ni jambo la hatari sana kwani Kamati inaona ni sawa na kujenga msingi wa nyumba mbovu na kumalizia na paa zuri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo na ubora wa elimu kuanzia mwaka 2005 umekuwa ukishuka kwa kiwango cha kutisha, mnaweza mkaona (Kielelezo Na. 4). Huu ni ukweli usiosema sana na ambao kama Taifa lazima tuukubali. Toka mwaka 1961 mpaka leo tumekuwa tukiangalia *quantity* na siyo ubora *quality* ya elimu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ualimu imekuwa ni fani isiyo na thamani. Imefika wakati sasa kama Taifa kuamua ualimu na elimu vipewe thamani yake kwa kutambua kwamba ualimu siyo chaka la watu waliofeli na wala siyo kazi ya wito bali ni kazi kama ilivyo taaluma nyingine inayotakiwa kuheshimika, kuthaminika kwa kujenga mfumo wa kutambua na kuboresha mazingira ya kazi na watoa elimu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti zinaonyesha kuwa uwezo wa watoto kujifunza kusoma na kuhesabu ni mdogo sana hapa nchini. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Taasisi ya Twaweza mwaka 2014 inakadiriwa kuwa asilimia 45 pekee ya watoto wa darasa la tatu wanaweza kusoma kwa ufasaha hadithi ya Kiswahili ya darasa la pili, wakati asilimia 19 pekee ya watoto hao hao wa darasa la tatu wanaweza kusoma kwa ufasaha hadithi ya Kingereza ya darasa la pili. Hii ni hatari kubwa sana, Taifa letu linazalisha watumwa na mabwana ndani ya mfumo wetu wa kuendesha, kusimamia na kugharimia elimu, kwa sababu watoto wanaoshindwa kujifunza darasani ni wale wanaotoka familia maskini, zenye vipato duni na wasiojiweza. Hawa ndiyo ambao hawawezi kusoma wala kuandika na hata kuhesabu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa Twaweza umebaini pia kuna pengo kubwa kati ya maskini na matajiri katika mfumo wa elimu kwani inakadiriwa kuwa watoto watatu kati ya 10 wenye umri kati ya miaka 13 wanatoka katika familia maskini (*ultra-poor households*) ndiyo walifaulu zoezi la kusoma hadithi za Kingereza na Kiswahili. Hii maana yake ni kuwa watoto saba kati ya 10 ya familia maskini zaidi wote hawana uwezo wa kusoma wala kuhesabu. Hii maana yake hawa watakuwa watumwa wa watoto wa matajiri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya kidato cha nne mwaka 2015 yameonesha hali ambayo Serikali na sisi kama Bunge tunatakiwa kuchukua hatua. Shule 50 za kwanza zilizofanya vizuri ni shule za binafsi. Matokeo ya aina hii yanathibitisha dhana aliyowahi kutolewa na Prof. Marjorie Mbilinyi kuwa elimu bora inauzwa na watoto maskini hawatapata elimu hii. Umefika wakati kama Taifa tukubali uhalisia kuwa elimu bora inahitaji uwekezaji na elimu ni uhai wa Taifa. Tusipochukua hatua sasa tutajenga aina mpya ya ubaguzi kutokana na mfumo wa elimu wenye tabaka ambalo halitoi haki ya elimu bora kwa maskini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Mahusiano ya Wizara ya Elimu na TAMISEMI. Kamati imebaini kuwa takribani asilimia 80 ya Bajeti ya Serikali inayoelekezwa kwenye sekta ya elimu ya msingi na sekondari inatekelezwa na Ofisi ya TAMISEMI kutokana na mfumo wa ugatuzi wa madaraka (*D by D*). Suala hili limekuwa na changamoto katika usimamizi, uendeshaji, udhibiti na ugharamiaji wa mfumo wa elimu nchini. Kwa sasa sera ipo chini ya Wizara lakini utekelezaji wa elimu ya msingi na sekondari upo chini ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini pia inapotokea wanafunzi wameshindwa katika mitihani yao ya kuhitimu anayeulizwa ni Waziri wa Elimu wakati waendeshaji, wasimamizi, wagharamiaji wa elimu kwa maana ya miundombinu, walimu na watendaji wengine wapo chini ya Ofisi ya TAMISEMI. Vilevile, Waziri wa Elimu haina mamlaka juu ya nidhamu, maslahi na mafunzo ya wasimamizi wa elimu. Kamati inataka suala hili liangaliwe upya kuepuka sekta hii kuwa katika usimamizi wa Wizara zaidi ya moja. Aidha, sera, usimamizi, uendeshaji, ugharamiaji ufanywe na Wizara ya Elimu na suala la kuendeleza na kusimamia miundombinu lifanywe na Ofisi ya Rais- TAMISEMI. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mara baada ya uhuru aliwahi kutangaza maadui watatu wa Taifa kuwa ni ujinga, maradhi na umaskini. Hivyo basi, hatuna budi kuhakikisha wananchi wanakuwa na elimu ambayo itawaondoa katika maadui hawa watatu. Hii itawezekana kwa kutenga fedha za kutosha ili mazingira ya elimu yawe ya kuvutia kuanzia mishahara ya Walimu, miundombinu kama madarasa, mabweni, nyumba za Walimu, maabara, vyoo, vifaa kama vitabu

na madawati vyote vinahitaji fedha. Kama ilivyoonyesha awali, bajeti ya Wizara ya Elimu haiendani kabisa na mpango wa kujikwamua kielimu. Ni ukweli ulio wazi kuwa kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya elimu, kupunguza umaskini na maendeleo endelevu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu hubadilisha maisha ya watu kwa kuwawezesha kuwa na ujuzi wa kuboresha maisha yao kwa kujishughulisha katika sekta zilizo rasmi na zile zisizo rasmi. Aliyekuwa Rais wa Afrika ya Kusini Marehemu Nelson Mandela aliwahi kusema, *“Education is the most powerful weapon which you can use to change the world”*. Kamati inaamini kuwa elimu ni silaha muhimu ya kubadilisha ulimwengu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo Kamati inashauri:-

(i) Serikali iwekeze kwenye elimu kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu kwa kutenga bajeti ya kutosha angalau tutimize Azimio la Incheon la kutenga kati ya asilimia 15-20 ya Bajeti Kuu ya Serikali kwenye sekta ya elimu tofauti na ilivyo sasa ambapo Serikali inatenga kwa ujumla wake Wizara zote asilimia 11 tu.

(ii) Serikali iangalie namna ya kuweka uwiano kati ya bajeti ya elimu ya msingi na elimu ya juu kwani Kamati imebaini kuwa katika fedha za miradi ya maendeleo ni asilimia 17 tu ndiyo inatengwa kwa ajili ya elimu ya msingi wakati elimu ya juu imetengewa asilimia 48. Ikumbukwe kuwa bila kuwa na msingi imara huku chini elimu ya juu inakuwa haina maana. (Makofi)

(iii) Bajeti ya Wizara ya Elimu inaonekana kuwa kubwa sana kitarakimu, kiasi cha shilingi trilioni 1.3 na kati ya hizo shilingi bilioni 427.554 sawa na asilimia 30.6 ya bajeti yote ya Wizarani ni kwa ajili ya Bodi ya Mikopo. Aidha, bajeti hii ya Bodi ya Mikopo pia ni sawa na asilimia 47 ya bajeti ya maendeleo ya Wizara hii. Hali hii ni inaifanya Wizara kuonekana kuwa na bajeti kubwa sana wakati kiuhalisia si sahihi. Kamati inashauri fedha za Bodi ya Mikopo kuwa na fungu lake linalojitegemea ili kuweza kuongeza ufanisi na ufuatiliaji wa mikopo na kuifanya bajeti ya Wizara ya Elimu kuwa na uhalisia. (Makofi)

(iv) Kamati imebaini kuwa sekta ya elimu ina taasisi takribani 88 ambazo zinasaidia katika utekelezaji wa majukumu yake ambapo inapelekea taasisi hizo kutumia asilimia 84 ya bajeti nzima ya sekta ya elimu na kufanya sekta hii kubakiwa na asilimia 16 tu kwa ajili ya kugharimia maendeleo ya sekta ya elimu. Kamati inaona hii siyo sawa na hivyo Serikali iweke uwiano mzuri wa fedha kati ya taasisi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu bila malipo. Pamoja na maelezo ya ufafanuzi yaliyotolewa na Waziri Mkuu wakati akiwasilisha bajeti yake kuhusu mahitaji ya msingi ya mtoto (sare za shule, michezo, madaftari, kalamu na

chakula na kadhalika) kuendelea kutolewa na wazazi, Kamati inatambua changamoto nyingi zilizopo kutokana na Waraka huu ambao Kamati inazitolea maoni na ushauri ufuatao:-

(i) Miundombinu ya kusomea kama madarasa, mabweni na vyoo bado havitoshi na hivyo Kamati inaitaka Serikali iandae mpango mkakati wa haraka kuhakikisha inatenga Bajeti Maalum ya kuwezesha miundombinu kupatikana ili suala hili liwe na tija kwani kuongeza idadi ya wanafunzi bila kuboresha miundombinu ni kazi bure. Bajeti ya kiasi cha asilimia 4 tu ya bajeti yote ya sekta ya elimu kilichotengwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwa ajili ya elimu bure kwenye shule za sekondari hakitoshi kabisa na hakina uhalisia katika kugharamia mpango wa elimu bure nchini. Kamati inaitaka Serikali iweke bajeti yenye nia ya dhati ya kutoa elimu bure. *(Makofi)*

(ii) Kamati inashauri utekelezaji wa maoni yaliyopelekwa kwenye Kamati ya Bajeti ikiwa ni pamoja na TEA kupewa fedha zitakazowezesha kujenga miundombinu ya elimu hasa madarasa ili kukabiliana na changamoto ya ongezeko la wanafunzi.

(iii) Idadi ya Walimu iongezwe ili kuweza kukabiliana na changamoto ya ongezeko la wanafunzi wanaojiunga na shule kutokana na hamasa ya wazazi kupunguziwa mzigo.

(iv) Elimu zaidi iendelee kutolewa kwa jamii kuhusu wajibu wa jamii katika kutekeleza Waraka huu wa Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uainishaji wa vyuo vikuu (*university classification*). Kamati inaona ni jambo jema nchi kuwa na vyuo vingi kwani ndiyo fursa ya kuongeza idadi ya wanafunzi wanaomaliza elimu ya juu ambao ndiyo wanaotegemewa kuleta maendeleo ya nchi. Kuwa na vyuo vingi visivyo na ubora na pia kama hakuna uwiano kati ya idadi ya wanafunzi na ile ya Walimu ni kazi bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inajiuliza hivi ni nani mwenye jukumu la kuwasimamia Wahadhiri wa vyuo vikuu hapa nchini? Kamati inajiuliza swali hili kwani imebaini kuwa vyuo hivi vimekuwa vikiongezeka wakati Wahadhiri wanaoongezeka ni kidogo sana, matokeo yake unakuta Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ndiyo huyo huyo pia anafundisha Chuo Kikuu cha Dodoma ambayo pia ina maana masomo ya kufundishwa kwa kipindi cha miezi mitatu yanafundishwa kwa muda mfupi zaidi mfano mwezi mmoja au wiki mbili ili kukimbizana na muda. Sio hivyo tu, Kamati inajiuliza tena, je, nini kinachangia haya yote? Je, ni mishahara midogo ndiyo inasababisha Wahadhiri wafanye haya kama njia ya kujiongezea kipato ikiwa ni pamoja na

kufanya kazi nyingine nyingi za ushauri ambazo zinachukua muda wao mwingi ambao kiukweli wanapaswa kuutumia kufundisha? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujiuliza maswali haya, Kamati inapendekeza yafuatayo:-

(i) Serikali ifanye uanishaji (*classification*) ya vyuo hivyo kulingana na kiwango cha ubora wake katika utoaji wa elimu. Hii itasaidia kuongeza ushindani wa wanafunzi waliopo sekondari na hivyo kusoma kwa bidii. Kamati inaamini kuwa wanafunzi wengi watapenda kusoma chuo chenye sifa ya juu. Kwa mfano Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kiwekwe katika kiwango cha kufanana na Chuo cha Harvard au Yale au Chuo Kikuu cha Dodoma kiwe Oxford na kadhalika. (Makofi)

(ii) Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha maslahi ya Wahadhiri wa Vyuo Vikuu yanazingatiwa ili kuwaepusha kufanya kazi katika chuo zaidi ya kimoja ili kupata muda wa kutosha kufundisha wanafunzi. Hii iende sambamba na kuongeza idadi ya Wahadhiri ili kuleta uwiano kati yao na wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maslahi ya Walimu. Maendeleo ya elimu nchini yanategemea namna Walimu wanavyoweza. Usitegemee Mwalimu ana manung'uniko ya kutolipwa maslahi yake akafundisha kwa morali. Ukienda nchi nyingine kuwa Mwalimu ni suala la kujivunia lakini hapa kwetu Ualimu siyo fani ya kujivunia kabisa. Imezoeleka kwamba ni wito, Walimu hawaheshimiki yaani ni fani inayotoa wanaoenda tu ili mradi maisha yaende. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaamini kuwa fani ya Ualimu ni fani kama fani nyingine. Walimu ni nguzo muhimu ya maendeleo endelevu ya nchi na hivyo Serikali haina budi kuwawezesha ili waweze kutoa mchango wao stahiki kwa kuhakikisha maslahi yao yanalindwa. Kwa kuanzia Kamati inaitaka Serikali kulipa madai yao yote yanayofikia kiasi cha shilingi bilioni 408. Ikumbukwe kwamba viongozi wote tukiwemo sisi Waheshimiwa Wabunge tumepita mikononi mwa Walimu. Kamati inashauri, Serikali kuwalinda, kuwaheshimu na kuwajali Walimu wa nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa elimu. Mwaka 1981 Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius K. Nyerere aliunda Tume ya Makwetta ili kuchunguza Mfumo wa Elimu nchini na kutoa Ripoti yake mwaka 1982 ambayo ilisaidia kuboresha mfumo wa elimu nchini ikiwemo uanzishwaji wa shule za kata nchini. Aidha, mwaka 1983 aliyekuwa Rais wa Marekani Ronald Regans naye aliunda Tume Maalum ya Kuchunguza Changamoto ya Mfumo wa Elimu nchini Marekani na namna bora ya kwenda. Tume hiyo ilikuja na ripoti iliyojulikana '*A Nation at Crisis: The Imperative for Educational Reform*' ambayo naweza kusema ndiyo historia ya mafanikio ya mfumo wa elimu ya Marekani.



Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwa Taifa ambalo tunataka kwenda kwenye uchumi wa kati, inatupasa kujiuliza maswali matano (5) yafuatayo:-

(i) Je, maudhui ya elimu yetu yakoje na yanazingatia mahitaji ya nchi yetu?

(ii) Viwango na matarajio, je, ni kwa kiasi gani tupo makini kuhusu upandishaji wa madaraja ili kuwa na viwango vinavyofaa?

(iii) Muda wa masomo kwa wanafunzi wa shule ya msingi na wale wa sekondari ukoje, ni masaa mangapi wanatumia kusoma?

(iv) Maslahi ya Walimu, hapa lazima tujiulize, je, mishahara ya Walimu inaendana na ushindani wa taaluma yao pamoja na utendaji kazi wao?

(v) Rasilimali fedha, Serikali inafahamu kuwa ina wajibu wa kusaidia ili kufikia mahitaji ya wanafunzi kama wale waliobarikiwa kuwa na vipawa mbalimbali, walemavu ikiwa ni pamoja na miundombinu yao kwa kuwapa msaada wa fedha lakini pia mafunzo ya utafiti na elimu ya juu? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya tafakuri hiyo, Kamati inaona ni wakati sasa wa kubadili mfumo wa mzima wa elimu nchini kutoka katika mfumo tulionao wa makundi mawili, kundi la matajiri na kundi la maskini. Kamati inaitaka Serikali kuangalia upya mfumo wetu wa elimu kwa kuunda Tume Maalum ya Kitaalam ya kufanya mapitio makubwa ya mfumo wa elimu nchini na kuchunguza hali ya elimu (*state of education*) ili kwenda sambamba na kasi kubwa ya mabadiliko ya kiuchumi duniani. Tume hii iwe Tume ya Rais ya Kitaalam na ripoti yake ilete Bungeni ili Bunge nalo lijadili na kutoa mapendekezo ya kiseru, kisheria kwa Serikali ili kuokoa elimu yetu. Kamati inashauri Tume hiyo iangalie kuhusu sera za elimu, mfumo wa upatikanaji wa Walimu, mfumo wa motisha kwa Walimu, muda wa elimu ya msingi, sekondari na chuo kikuu, usimamizi wa elimu, uendeshaji na ugharamiaji wake. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tuzo ya Udhamini. Kamati inaona ni wakati sasa wa kuwekeza kwenye elimu na kuongeza ushindani kwa kutoa Tuzo za Udhamini kwa wanafunzi wanaomaliza kidato cha sita ambao wamefanya vizuri katika mitihani yao ya Taifa. Kamati inapendekeza tuzo hii iitwe '*Presidential Scholarship Award*' ambapo wanafunzi 50 watakaofanya vizuri katika mitihani ya kidato cha sita wapewe udhamini wa kusoma katika vyuo bora duniani kama Harvard, Yale, Cambridge, Oxford, MIT na kadhalika na wagawanywe katika fani tofauti ikiwemo sayansi, uchumi, sanaa, siasa na kadhalika. (Makofi)



Mheshimiwa Naibu Spika, nchi za Asia ambazo zinajulikana kama 7 Asian Tigers ukisoma historia yake utagundua karibu zote (Singapore, Malaysia, Korea, Hong Kong, Thailand, Indonesia na Taiwan) ukiacha mambo mengine, ziliwekeza sana kwenye elimu. Tukiangalia nchi kama Korea ya Kusini miaka ya 1960 ilikuwa katika uchumi wa chini zaidi hata ya Tanzania lakini kwa mujibu wa taarifa kutoka IMF mwaka 2015 Korea ilikuwa nchi ya 13 kati ya nchi 180 duniani zenye pato la kati la Taifa. Kwa mujibu wa mwandishi wa Kitabu kinachoitwa *"Upside –Down Success Story for Korean Economic Development"* Ndugu Choi ni kwamba Serikali ya Korea ya Kusini iliamua kutoa ufadhili kwa wanafunzi wanaofanya vizuri na wenye vipaji mbalimbali wanaotoka katika familia masikini kwenda kusoma katika vyuo bora duniani katika nchi za Marekani, Ujerumani na Uingereza hali iliyoongeza Wasomi ambao wamesaidia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya uchumi wa nchi hiyo. Kamati inaamini kabisa ufadhili huu utakuwa chachu na utaongeza morali ya wanafunzi kusoma kwa bidii na hatimaye kuwa na wasomi wazuri wenye taaluma mbalimbali ambazo ni muhimu kwa maendeleo endelevu ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mahusiano ya ongezeko la idadi kubwa ya watu katika elimu. Mchumi Todaro katika Kitabu cha Maendeleo ya Uchumi (*Economic Development 11th Edition*) amebainisha kuwa idadi ya watu duniani imekuwa ikiongezeka kwa kasi kubwa na kila mwaka zaidi ya watu milioni 75 wanaongezeka na takribani asilimia 97 ni kutoka nchi zinazoendelea. Aidha, inakadiriwa kuwa hapa nchini kila mwanamke huzaa wastani wa watoto sita. Siyo hivyo tu, takribani asilimia 44 ya wanawake wanapata mimba ya kwanza wakiwa na umri wa miaka 19. Kwa mujibu wa takwimu zas ya mwaka 2012, idadi ya watoto kati ya umri wa miaka 2-6 ilizidi wale wa umri wa miaka 10-14. Endapo ukuaji huu utaendelea basi miaka 25 ijayo Serikali itakuwa na mzigo mkubwa ikiwemo kuongeza idadi ya shule pamoja na Walimu kwani idadi ya wanafunzi wanaopaswa kujiunga na elimu ya msingi itakuwa 333,169 kwa miaka mitano ijayo na ikiwa kila darasa litakuwa na wanafunzi zaidi ya 40 basi yatatakiwa madarasa mapya 8,000 kwa mwaka na kwa miaka mitano madarasa 41,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo inabidi Serikali idhibiti ongezeko la idadi ya watu. Hii itawezekana kwa njia mbalimbali ikiwemo kusomesha zaidi wanawake kwani tafiti zinaonesha kuwa mwanamke anapopata muda zaidi wa kusoma anachelewa kuolewa na kuzaa pia atazaa watoto wachache ambao watakuwa na afya bora lakini pia ambao ataweza kuwasomesha. Serikali iendelee kutoa elimu ya uzazi wa mpango ili kupunguza idadi ya watoto wanaozaliwa kwa kila mwanamke mmoja angalau tufikie wastani wa watoto watatu kwa kila mwanamke. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ina laani vikali wale wote wanaowapa mimba wanafunzi wakiwa shule za msingi na sekondari na inaitaka Serikali

kuwapa adhabu kali wale wote wanaobainika kufanya vitendo hivi. Aidha, Kamati inaona haina maana kuwafukuza masomo watoto wa kike wanaopata mimba na badala yake Kamati inashauri mara baada ya kujifungua wanafunzi hao wapewe nafasi ya kurudi tena masomoni kwa ustawi wao, watoto wao na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vyuo vya ufundi. Pamoja na kuwekeza katika vyuo vikuu, vyuo vya ufundi navyo ni vizuri zaidi katika kuzalisha wataalam wa fani mbalimbali ambao wanasaidia sana katika mapinduzi ya viwanda. Dira ya Maendeleo ya 2025 inalenga katika kuibadili Tanzania kutoka katika nchi yenye uchumi wa chini wa uzalishaji mdogo wa kilimo kwenda kwenye uchumi wa kati wa viwanda na watu wenye elimu ya juu. Sasa basi ili kuweza kufikia lengo hilo, ni wakati sasa Serikali kuanza kuweka msisitizo kwenye elimu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**WABUNGE FULANI:** Aongezewe muda kidogo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bashe naomba umalize dakika mbili. *(Makofi)*

**MHE. HUSSEIN M. BASHE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII):** Umeniongezea?

**MBUNGE FULANI:** Umeongezewa dakika mbili.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali lazima ihakikishe kila mkoa una kuwa na vyuo hivi na ambavyo mitaala yake itaendana na mahali. Kwa mfano, vyuo vilivyopo Kanda ya Ziwa na Pwani ni vyema vikawa na mitaala ya uvuvi na vile vilivyopo katika mikoa yenye kilimo kingi basi vikawa na mitaala ya aina hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ada elekezi. Kamati imebaini kuwa Serikali ipo kwenye mchakato wa kuandaa Waraka wa Ada Elekezi. Kamati haiamini katika ada elekezi kutokana na ukweli kuwa Serikali imeshakuja na Waraka wake wa kutoa elimu bure basi haina budi kuhakikisha elimu inayotolewa inakidhi viwango. Hii itasaidia kupanua wigo na hivyo wazazi wengi watapata nafuu na kuamua kuwapeleka watoto wao katika shule. Pamoja na hayo, Kamati inaitaka Serikali kufanya jukumu lake la kuboresha elimu kwa kuziwezesha shule za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Utumishi. Kamati inashauri Tume hii ipewe uhuru kamili wa kuweza kusimamia sekta ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nimeomba taarifa yetu yote iingie katika Kumbukumbu za Bunge, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa kufanya kazi za Kamati na hususan uchambuzi wa Taarifa kwa weledi, nisingependa kuwatambua kwa majina. Napenda kukushukuru wewe binafsi Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Kamati kwa kuliongoza Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako ni mtu *honesty*, mkweli na Naibu Waziri wake. Nawashukuru watumishi wa Bunge wote, Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Dkt. Kasilillah kwa ushirikiano mzuri wanaotupa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali na kuridhia kuidhinisha makadirio ya mapato ya matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia jumla ya Sh.1,396,929,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (Makofi/Kicheko)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, napenda kwanza kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii inayohusu Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati juu ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati hii ndiyo yenye jukumu la kikanuni (Nyongeza ya nane(6) (5) (c) iliyo chini ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kusimamia shughuli za Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi. Aidha, katika Nyongeza hiyo ya Nane, Kanuni ya 7 (1) (a) inaeleza jukumu la Kamati zote za Kisekta ikiwemo Kamati hii la kushughulikia Bajeti ya Wizara inazosisimamia.

Pia kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1-2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Kamati hii ina jukumu la kutembelea na kukagua Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha unaoishia ambao ni 2015/2016 pamoja na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha unaoishia ili kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha unaofuata wa 2016/2017. Lengo ni kuweza kuishauri Serikali namna bora ya kuenenda ili kuleta Maendeleo ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 14 na 15 Aprili, 2016, Kamati ilikutana na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi Dar es Salaam kwa lengo la kupitia na kuchambua Taarifa ya utekelelezaji wa kazi za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuwapunguzia mzigo Watanzania kufuatia agizo lake la kufuta ada na michango mbalimbali katika Elimu ya Msingi na Sekondari. Pamoja na changamoto zilizopo Kamati ina amini Serikali itazifanyia kazi.

**Mheshimiwa Spika**, Muundo wa Taarifa hii umezingatia Kanuni ya 123 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 na hivyo inatoa maelezo ya kina kuhusu masuala manne (4) yafuatayo:-

- i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
- ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016;
- iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
- iv) Maoni, Ushaurina Mapendekezo ya Kamati.

## **2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIWAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016**

### **2.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016**

**Mheshimiwa Spika**, katika kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajetikwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, Kamati ilizingatia namna makusanyo ya Maduhuli yalivyokuwa ikilinganishwa na lengo la kiwango cha ukusanyaji, na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za Wizara kama zilivyoainishwa kwenye Mpango wake. Kamati ilipitia Taarifa ya Wizarana kuhoji ili kupata ufafanuzi pale ilipohitajika.


**Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa Bunge lako linapata picha halisi ya ukusanyaji wa Maduhuli na upatikanaji wa fedha, Kamati imetumia vielelezo mbalimbali yakiwemo majedwali katika Uchambuzi kwenye Taarifa hii.

#### **2.1.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2015/2016, Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi ilipanga kukusanya jumla ya shilingi **263,825,112,771.47**, kati ya hizo shilingi **9,268,463,100**sawa na **asilimia 3.5** zikiwa ni makusanyo ya Wizara na shilingi **254,556,649,671.47**sawa na **asilimi 96.5** zikiwa ni makusanyo kutoka Taasisi zilizo chini ya Wizara.


**Mheshimiwa Spika**, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi kufikia Februari, 2016 makusanyo yalikuwa shilingi **181,060,205,382.49** sawa na asilimia **71.1** ya makadirio. Kati ya makusanyo hayo shilingi **4,291,190,118.38** sawa na **asilimia 46.2** ya makadirio ya makusanyo ya Wizara yalikusanywa na Wizara na shilingi **176,769,015,264.11** sawa na **asilimia 69.4** ya makusanyo yalikusanywa na Taasisi zilizo chini ya Wizara. **(Rejea Kielelezo Na 1).**

**Kamati inaona mwenendo wa ukusanyaji wa Mapato siyo mbaya sana, inaendelea kulisitiza kuwa hadi kufikia Mwisho wa Mwaka wa Fedha 2015/2016, Wizara na Taasisi zake zihakikishe ziwe zimefikia lengo na ikibidi livuke.**

**Kielelezo Na.1: UKUSANYAJI WA MAPATO KWA MWAKA 2015/2016****2.1.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, Wizara hii (**Fungu 46**) iliidhinishi washilingi **511,525,227,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida. Hadi kufikia robo ya tatu ya Mwaka Machi 2016 Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi **316,402,868,828.00** sawa na **asilimia 61.8**.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu Bajeti ya Maendeleo, Kamati imebaini kuwa katika robo tatu ya Mwaka wa Fedha, Wizara imepokea jumla ya **360,922,754,359.61** sawa na asilimia **61.9** ya fedha ili yoidhinishwa **582,670,597,884.49**. Kamati imebaini kuwa kiasi hiki cha fedha kisichokidhi mahitaji ni moja ya sababu ya kutotekelezwa kwa Miradi ya Maendeleo ipasavyo. (**Rejea Kielelezo Na. 2**)

**Kielelezo Na. 2: UPATIKANAJI WA FEDHA KWA MWAKA 2015/2016**

## **2.2 Maelezo na Matokeo ya Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha wa 2015/2016. Kamati iliweza kufanya ziara ya Ukaguzi wa Miradi miwili (2) ifuatayo kati ya Miradi iliyotengewa fedha:-

### **2.2.1 Mradi wa kutoa Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi (**Fungu 46**) iliidhinishiwa **shilingi 418,300,000,000/=** kwa ajili ya Mradi Namba PT4340 uliojulikana kama **“Higher Education Students Loans”** ambao ni Mradi wa kutoa Mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu. Mradi huu ulipangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 7001 - Elimu ya Juu (Higher Education) cha Fungu 46.

**Mheshimiwa Spika**, Katika ukaguzi huo Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto kadhaa kama vile kuchelewa kupokea fedha za Mikopo kutoka Serikalini. Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2016 ambayo ni robo tatu ya Mwaka wa Fedha 2015/2016, Bodi ilikuwa imepokea jumla ya shilingi **Bilioni 245** sawa na **asilimia 55.9** tu ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Fedha hizo zimetumika kutoa Mikopokwajumla ya **wanafunzi 122,786**. **Tafsiri ni kwamba kama fedha hizo zingetolewa zote kwa asilimia 100 basi, wanafunzi wengi zaidi wangepata Mikopo hiyo.**

### **2.2.2 Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilifanya ukaguzi wa Mradi wa Upanuzi na ukarabati wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili (MUHAS) – Mloganzila. Ujenzi wa Mradi huu unalenga katika kuboresha Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili kwa kujenga tawi (Campus) la Chuo na Hospitali ya kisasa kwa ajili ya kufundishia na kutoa huduma. Tawi hili likikamilika, Chuo kitaweza kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 4,010 wa sasa hadi kufikia wanafunzi 15,000 jambo ambalo pia litaongeza wataalam wa afya nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi ulianza Rasmi mnamo tarehe 10 Machi 2014 na unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 9 Juni 2016. Mradi huu unatokana na mkopo wa riba nafuu kutoka *African Development Bank* (AfDB) wa kiasi cha **dola za kimarekani bilioni 9.4** na mchango wa Serikali ya Tanzania wa **dola za kimarekani 755,000**.

**Mheshimiwa Spika**, wakati Kamati inatembelea Mradi, ujenzi ulikuwa umefikia asilimia **82**. Hata hivyo, Kamati ilijulishwa pia kiasi cha fedha ambacho kilipaswa kutolewa kama Mchango wa Serikali kilikuwa hakijatolewa. **Ni imani ya Kamati kuwa fedha hizo zitafika katika Mwaka huu wa Fedha 2015/2016 ili**



**kukamilisha Mradi na kitakachokuwa kimebaki ni ununuzi wa vifaa ambao Kamati ilielezwa umepangiwa fedha katika Mwaka wa Fedha 2016/2017.**

### **2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatoa Maoni, Ushaurina mapendekezo yafuatayo kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016:-

a) Kamati imebaini kuwa katika Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili – Mloganzila hakuna fedha iliyotengwa kwaajili ya Ujenzi wa Nyumba za Walimu. Kamati imeshangazwa Mradi mkubwa kama huu kutotengewa fedha za ujenzi wa nyumba za Watumishi na inajiuliza watumishi hawa wataenda kukaa wapi?**Kamati inaitaka Serikali itenge fedha kwaajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi ili Mradi utakapoanza kufanya kazi na nyumba hizo ziwe tayari.**

b) Kamati imebaini kuwa Miradi mingi pamoja na kuwa iliidhinishiwa Fedha katika Mwaka wa Fedha 2015/2016, Lakini haikutekelezwa ipasavyo kutokana na kutopatiwa fedha za kutosha na mingine kutotekelezwa kabisa. **Kamati inaitaka Serikali kuchagua Miradi michache ya kipaumbele na kuipatia fedha ili iweze kukamilika kwa wakati, ukamilikaji wa Miradi hii utatoa nafasi kwa miaka inayofuata kuendelea na Miradi mingine badala ya kutoa fedha kidogo kidogo au kutokutoa kabisa wakati Miradi imeanza kutekelezwa.**

c) Kamati imebaini pia kumekuwepo na ongezeko la gharama za Miradi kunakotokana na makisio ambayo hufanywa kwa kuzingatia sarafu ya nchi (TSH) wakati Utekelezaji wake unategemea pia sarafu za nchi nyingine. **Kamati inaona kuwa kutokana na ukweli kwamba dola ya kimarekani ndiyo imekuwa ikitumika zaidi kama sarafu ya kufanya manunuzi, ni vyema sasa makisio hayo yakafanyika katika mfumo huo wa dola ili pale dola inapopanda au kushuka isiweze kuathiri Utekelezaji wa Miradi.**

d) Kamati imebaini kuwa vijana wengi wenye alama za kuwawezesha kuendelea na masomo ya elimu ya juu wameshindwa kuendelea kutokana na kutokuwa na uwezo wa kujilipia, uwepo wa Mikopo hii ingekuwa ni fursa njema kwao kujiendeleza kielimu na hivyo kuongeza idadi ya wasomi nchini wenye uwezo wa kuleta tija kwenye Maendeleo ya nchi, **Kamati imeona ni vyema sasa wanafunzi wengi zaidi waendeleo kupewa Mikopo kwa miaka ijayo ili kulifanya Taifa letu kuwa na idadi kubwa ya Wasomi kama zilivyo nchi nyingine ambao watachochea Maendeleo ya endelevu ya nchi. Mchumi Maarufu Duniani na Mhadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Havard Amartya sen**

**aliwahi kusema “Economic growth without investment in Human Development is unsustainable and unethical”.**

## **2.4 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016, Kamati ilitoa jumla ya Maoni, Ushauri na mapendekezo 17. Wizara imeweza kutekeleza baadhi ya Maoni hayo na mengine Utekelezaji wake unaendelea. (**Rejea Kiambatisho Na. 1**). Kamati itaendelea kuyasisitiza Maoni ambayo bado hayajatekelezwa ili Wizara na Serikali iweze kuyatekeleza kwani ni muhimu sana kutekelezwa kama ilivyopangwa kwa Maendeleo ya Sekta hii na Taifa kwa ujumla.

## **SEHEMU YA PILI**

---

## **3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**

### **3.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka huu wa Fedha wa 2016/2017 Wizara imeainisha jumla ya malengo yake Makuu manne(4) ambayo Kamati ina amini kabisa kama yatafanywa kazi ipasavyo ni dhahiri kuwa Wizara hii pamoja na Sekta zake zote zitakuwa na Maendeleo.

### **3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato**

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi (**Fungu 46**) katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 inatarajia kukusanya jumla ya shilingi **333,075,815,485.21** ikilinganishwa na kiasi cha shilingi **263,825,112,771.47** zilizokadiriwa katika Mwaka wa Fedha wa 2015/2016 ikiwa ni ongezeko la shilingi **69,250,702,713.74** sawa na **asilimia 26.2**.

**Mheshimiwa Spika**, Katika makadirio ya makusanyo hayo, **kifungu 7001** kinachohusu **Elimu ya juu** ndicho chenye makadirio makubwa zaidi yamakusanyo ya Mapato ya shilingi **252,013,955,942.21** sawa na **asilimia 75.6** yamakadirio ya makusanyo ya Mapato yote ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Sababu kubwa ya kuongoza ni kutokana na asili ya kazi zinazofanywa ambazo ni Elimu ya Juu kwa hiyo vyuo vyote vipo chini ya kifungu hiki na hivyo ukusanyaji wa ada unachangia kwa kiasi kikubwa ukusanyaji huu wa fedha.

Aidha, katika uchambuzi huo Kamati imebaini kuwa **kifungu 8001** kinachohusu **Sayansi, Teknolojia na Ubunifu** ndicho chenye makadirio madogo zaidi ya shilingi **13,565,567,151.00**sawa na **asilimia 4.0** yamakadirio ya makusanyo ya Mapato yote ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kutokana na asili ya kazi zake na idadi ndogo ya Taasisi zilizo chini yake ambazo ni 5 tu ukilinganisha na 14 za Elimu ya Juu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ina amini kwamba bado kiwango cha makadirio ya Makusanyo ni kidogo na Wizara inaweza kukusanya zaidi. **Ni rai ya Kamati kuwa, Motisha itolewe kwa kifungu ambacho kitakusanya zaidi hii itafanya kila kitengo kuongeza juhudi za makusanyo.**


### 3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara inaomba jumla ya shilingi **1,396,929,798,625.00** Kati ya Fedha hizo shilingi **499,272,251,000.00**sawa na **asilimia 35.7** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **897,657,547,625.00**sawa na **asilimia 64.3**kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kiasi hiki kinachoombwa ni nyongeza ya shilingi **302,733,973,736.51**sawa na **asilimia 27.6** ya kiasi cha shilingi **1,094,195,824,888.49**kilichotengwa katika Mwaka wa Fedha 2015/2016.**Kamati inaipongeza Serikalikwa ongezeko hili.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi ili kuona bajeti ya Wizara hii ni sawa na asilimia ngapi ya Bajeti kuu ya Serikali na ilibaini kuwa kiasi hiki kinachoombwa katika Mwaka huu wa Fedha 2016/2017 **NI SAWA NA ASILIMIA 4.4 TU YA BAJETI KUU YA SERIKALI. Ipo haja ya kuwekeza zaidi kwenye Elimu kwa kutenga Bajeti ya kutosha kwani Usalama wa nchi tafsiri yake siyo uwepo wa Jeshi Imara tu bali pia Elimubora kwani madhara ya Elimu duni katika usalama wa nchi ni makubwa**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa jumla kuangalia viwango mbalimbali vya Elimu kama uwiano wa idadi ya Walimu na Wanafunzi. Katika uchambuzi huo Kamati imebaini bado Tanzania tupo nyuma kwani pamoja na kiwango cha Nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara kuwa na uwiano wa Mwalimu 1 kwa wanafunzi 42 katika Mwaka 2012 na 2013 katika shule za Msingi, Tanzania bado tuna uwiano mkubwa wa Mwalimu 1 kwa wanafunzi 45 na 43 kwa miaka hiyo 2012 na 2013.**(Rejea Kielelezo Na. 3)**

**Kielelezo Na3. Uwiano waWalimukwa  
Wanafunzi Shule za Msingi**




**Chanzo: UNESCO**

### **3.4 Hali ya Elimu Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, hali ya Elimu nchini kwetu inasikitisha na ni hatari kwa usalama na uhai wa Taifa letu. Tathmini na tafiti nyingi Duniani zimethibitisha Elimu bora ni ile inayoweza kumsaidia raia kukabiliana na changamoto ili kujenga Taifa imara na salama zaidi. Usalama wa nchi huimarika zaidi raia wake wanapoweza kukabiliana na mahitaji ya wakati na jamii husika. Taifa letu limejenga mfumo wa **ELIMU** ambayo haikidhi DIRA **NA MAHITAJI YA NCHI**. Tunahitaji kujenga Taifa la Viwanda lakini hatuna Wataalam wa Hesabu na Sayansi. Dira ya nchi haifungamani na Mkakati wa Elimu, wale wanaofeli ndiyo huandaaliwa kufundisha katika Elimu ya Msingi na Sekondari na wale wanaomaliza Chuo Kikuu wenye wenye ufaulu mzuri wa daraja la kwanza (*1st class*) ndo wanabaki kufundisha vyo vikiu hili ni jambo la hatari sana kwani Kamati inaona ni sawa na **kujenga msingi wa nyumba mbovu na kumalizia na paa zuri**.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo na ubora wa Elimu kuanzia Mwaka 2005 umekuwa ukishuka kwa kiwango cha kutisha (**Rejea Kielelezo Na. 4**), huu ni ukweli usiosema sana na ambao kama Taifa lazima tuukubali. Toka Mwaka 1961 mpaka leo tumekuwa tukiangalia wingi (Quantity) na siyo ubora (Quality).

**Kielezo Na. 4 : WANAFUNZI WALIOFAULU MITIHANI YA SHULE YA MSINGI NA SEKONDARI KATI YA MWAKA 2005 NA 2014**



**Mheshimiwa Spika,** Ualimu umekuwa ni fani isiyo na thamani, umefika wakati sasa kama Taifa kuamua Ualimu na Elimu vipewe thamani yake kwa kutambua kwamba Ualimu siyo chaka la watu waliofeli na wala siyo kazi ya wito bali ni kazi kama ilivyo taaluma nyingine inayotakiwa kuheshimika, kuthaminika kwa kujenga Mfumo wa kutambua na kuboresha Mazingira ya kazi na watoa Elimu.

**Mheshimiwa Spika,** tafiti zimeonyesha kuwa uwezo wa watoto kujifunza kusoma na kuhesabu ni mdogo sana hapa nchini. Kwa mujibu wa Utafiti uliofanywa na Taasisi ya Twaweza Mwaka 2014 inakadiriwa kuwa **asilimia 45** pekee ya watoto wa darasa la 3 wanaweza kusoma kwa ufasaha hadithi ya Kiswahili ya darasa la 2, wakati **asilimia 19** pekee ya watoto hao hao wa darasa la 3 wanaweza kusoma kwa ufasaha hadithi ya kingereza ya darasa la 2. Hii ni hatari kubwa sana, Taifa letu linazalisha watumwa na mabwana ndani ya mfumo wetu wa kuendesha, kusimamia na kugharimia elimu, kwa sababu watoto wanaoshindwa kujifunza darasani ni wale wanaotoka familia masikini, zenye vipato duni na wasiojiweza. Hawa ndio ambao hawawezi kusoma wala kuandika na hata kuhesabu.

**Mheshimiwa Spika,** Utafiti wa Twaweza umebaini pia kuna pengo kubwa kati ya masikini na matajiri katika mfumo wa elimu kwani inakadiriwa kuwa watoto 3 kati ya 10 wenye umri kati ya miaka 13 wanatokea katika familia masikini sana (*ultra-poor households*) ndio walifaulu zoezi la kusoma hadithi za kingereza na kiswahili. Hii maana yake ni kuwa watoto 7 kati ya 10 ya familia masikini zaidi wote hawana uwezo wa kusoma wala kuhesabu. Hii maana yake hawa watakuwa watumwa wa watoto wa matajiri.

**Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya kidato cha nne 2015 yameonesha hali ambayo Serikali na sisi kama Bunge tunatakiwa kuchukua hatua. Shule 50 za kwanza zilizofanya vizuri ni Shule za Binafsi. Matokeo ya aina hii yanathibitisha Dhana aliyowahi kuandika Prof. Marjorie Mbilinyi kuwa **ELIMU BORA** inauzwa na waoto maskini hawatapata Elimu hii. Umefika wakati kama Taifa tukubali uhalisia kuwa **ELIMU BORA** inahitaji uwekezaji na **ELIMU NI UHAI WA TAIFA**. Tusipochukua hatua sasa tutajenga aina mpya ya Ubaguzi kutokana na mfumo wa Elimu wenye tabaka ambalo halitoi **HAKI YA ELIMU BORA KWA MASKINI**.

## SEHEMU YA TATU

---

### 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza uchambuzi wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, sasa naomba nitoe Maoni, Ushaurina Mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

#### 4.1 Mahusiano ya Wizara ya Elimu na TAMISEMI

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa takribani **asilimia 80** ya Bajeti ya Serikali inayoelekezwa kwenye Sekta ya Elimu ya Msingi na Sekondari inatekelezwa na Ofisi ya Rais –TAMISEMI kutokana na mfumo wa ugatuzi wa madaraka (D by D). Suala hili limekuwa na changamoto katika usimamizi, uendeshaji, uhibitaji na ugharamiaji wa mfumo wa elimu nchini. Kwa sasa Sera ipo chini ya Wizara lakini utekelezaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari upo chini ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI. Kamati imebaini pia inapotokea Wanafunzi wameshindwa katika mitihani yao ya kuhitimu anayeulizwa ni Waziri wa Elimu wakati wa uendeshaji, wasimamizi, wagharamiaji wa Elimu kwa maana ya Miundombinu, Walimu na Watendaji wengine wapo chini ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Vile vile, Waziri wa Elimu hana mamlaka juu ya nidhamu, maslahi, mafunzo na usimamizi wa walimu. **Kamati inataka suala hili liangaliwe upya kuepuka Sekta hii kuwa katika usimamizi wa Wizara zaidi ya moja. Aidha, Sera, usimamizi, uendeshaji, ugharamiaji ufanywe na Wizara ya Elimu na suala la kuendeleza na kusimamia Miundombinu lifanywe na Ofisi ya Rais- TAMISEMI.**

#### 4.2 Bajeti

**Mheshimiwa Spika**, Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mara baada ya uhuru aliwahi kutangaza maadui watatu wa Taifa kuwa ni **Ujinga, Maradhi na Umaskini**, hivyo basi hatuna budi kuhakikisha wananchi wanakuwa na Elimu ambayo itawaondoa katika maadui hawa watatu. Hii itawezekana kwakutenga fedha za kutosha ili mazingira ya Elimu yawe ya kuvutia kuanzia mishahara ya Walimu, miundombinu kama madarasa,

mabweni, nyumba za Walimu, maabara na vyoo, vifaa kama vitabu na madawati vyote vinahitaji fedha. Kama ilivyoonyesha awali, Bajeti ya Wizara ya Elimu haiendani kabisa na Mpango wa kujikwamua Kielimu. Ni ukweli ulio wazi kuwa kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya Elimu, kupunguza umaskini na Maendeleo endelevu. Elimu hubadilisha maisha ya watu kwa kuwawezesha kuwa na ujuzi wa kuboresha maisha yao kwa kujishughulisha katika sekta zilizo rasmi na zile zisizo rasmi. Aliyekuwa Rais wa Afrika ya Kusini Nelson Mandela aliwahi kusema **"Education is the most Powerful weapon which you can use to change the World"** Kamati inaamini kuwa Elimu ni silaha muhimu ya kubadilisha Ulimwengu. Ni kwa msingi huo Kamati inashauri:-

a) **Serikali iwekeze kwenye Elimu kwa ajili ya Maendeleo ya Taifa letu kwa kutenga Bajeti ya kutosha angalau tutimize Azimio la Incheon la kutenga kati ya asilimia 15-20 ya Bajeti kuu ya Serikali kwenye Sekta ya Elimu tofauti na ilivyo sasa ambapo Serikali inatenga asilimia 11.1 tu (Wizara ya Elimu na TAMISEMI)**

b) **Serikali iangalie namna ya kuweka uwiano kati ya bajeti ya Elimu ya msingi na Elimu ya juu kwani Kamati imebaini kuwa katika fedha za Miradi ya Maendeleo ni asilimia 17 tu ndiyo inatengwa kwa ajili ya Elimu ya msingi wakati Elimu ya Juu imetengewa asilimia 48. Ikumbukwe kuwa bila kuwa na msingi imara huku chini elimu ya juu inakuwa haina maana.**

c) **Bajeti ya Wizara ya Elimu inaonekana kuwa kubwa sana kitarakimu, kiasi cha shilingi trilioni 1.396 na kati ya hizo shilingi bilioni 427.554 sawa na asilimia 30.6 ya Bajeti yote ya Wizarani kwa ajili ya Bodi ya Mikopo. Aidha, bajeti hii ya Bodi ya Mikopo pia ni sawa na asilimia 47 ya Bajeti ya Maendeleo ya Wizara hii. Hali hii ni inaifanya Wizara kuonekana kuwa na bajeti kubwa sana wakati kiuhalisia si sahihi. Kamati inashauri Fedha za Bodi ya Mikopo kuwa na fungu lake linalojitegemea ili kuweza kuongeza ufanisi wa ufuatiliaji wa Mikopo na kuifanya Bajeti ya Wizara ya Elimu kuwa na uhalisia.**

d) **Kamati imebaini kuwa Sekta ya Elimu ina taasisi takribani 88 ambazo zinasaidia katika utekelezaji wa majukumu yake. Ambapo inapelekea Taasisi hizo kutumia asilimia 84% ya bajeti nzima ya Sekta ya Elimu na kufanya Sekta hii kubakiwa na asilimia 16 tu kwa ajili ya kugharimia Maendeleo ya Sekta ya Elimu. Kamati inaona hii sio sawa na hivyo Serikali iweke uwiano mzuri wa fedha kati ya Taasisi na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.**

#### **4.3 Elimubila malipo (Waraka Na. 5 wa 2015)**

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na maelezo ya ufafanuzi yaliyotolewa na Waziri Mkuu wakati akiwasilisha Bajeti yake kuhusu mahitaji ya msingi ya mtoto (sare za shule na michezo, madaftari, kalamu na chakula, nauli) kuendelea



kutolewa na wazazi Kamati inatambua changamoto nyingi zilizopo kutokana na waraka huu ambazo Kamati inazitolea Maoni na Ushauri ufuatao:-

a) Miundombinu ya kusomea kamamadarasa, mabweni na vyoo bado havitoshi na hivyo **Kamati inaitaka Serikali iandae Mpango Mkakati wa haraka wa kuhakikisha inatenga Bajeti Maalum ya kuwezesha miundombinu kupatikanaili suala hili liwe na tija kwani kuongeza idadi ya wanafunzi bila kuboresha miundombinu ni kazi bure. Bajeti ya kiasi cha asilimia 4 tu kati ya bajeti yote ya Sekta ya Elimu kilichotengwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano kwa ajili ya Elimu bure kwenye shule za sekondari hakitoshi kabisa na hakina uhalisia katika kugharamia mpango wa elimu bure nchini. Kamati inaitaka Serikali iweke bajeti yenye nia ya dhati ya kutoa elimu bure.**

b) **Kamati inashauri utekelezaji wa Maoni yaliyopelekwa kwenye Kamati ya Bajeti ikiwa ni pamoja na TEA kupewa fedha zitakazoweza kujenga Miundombinu ya Elimu hasa madarasa ili kukabiliana na changamoto ya Ongezeko la Wanafunzi.**

c) **Idadi ya Walimu iongezwe ili kuweza kukabiliana na changamoto ya ongezeko la wanafunzi wanaojiunga na shule kutokana na hamasa ya wazazi kupunguziwa mzigo.**

d) **Elimu zaidi iendeleo kutolewakwa jamii kuhusu wajibu wa wazazi katika kutekeleza waraka huu wa Elimu bure.**

#### **4.4 Uainishaji wa Vyuo Vikuu (University Classification)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona ni jambo jema nchi kuwa na vyuo vingi kwani ndiyo fursa ya kuongeza idadi ya wanafunzi wanaomaliza Elimu ya juu ambao ndiyo wanaotegemewa kuleta Maendeleo ya nchi. Kuwa na vyuo vingi visivyo na ubora na pia kama hakuna uwiano kati ya idadi ya Wanafunzi na ile ya Walimuni kazi bure.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inajiuliza hivi ni nani mwenye jukumu la kuwasimamia Wahadhiri wa Vyuo vikuu hapa nchini? Kamati inauliza hili kwani imebaini kuwa Vyuo hivi vimekuwa vikiongezekawakati Wahadhiri wanaoongezeka ni kidogo sana, matokeo yake unakuta Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ndiyo huyo pia anafundisha Chuo Kikuu cha Dodoma ambayo pia ina maana masomo ya kufundishwa kwa kipindi cha miezi mitatu (3) yanafundishwa kwa muda mfupi zaidi mfano mwezi mmoja (1) au wiki mbili (2) ili kukimbizana na muda. Sio hivyo tu, Kamati inajiuliza tena je nini kinachangia haya yote? Je ni mishahara midogo ndiyo inasababisha Wahadhiri wafanye haya kama njia ya kujiongezea kipato ikiwa ni pamoja na kufanya kazi nyingine

nyingi za ushauri ambazo zinachukua muda wao mwingi ambao kiukweli wanapaswa kuutumia kufundisha?

**Baada ya kujiuliza maswali haya, Kamati inapendekeza kuwa:-**

a) **Kwanza Serikali ifanye uanishaji (classification) ya vyuo hivyo kulingana na kiwango cha ubora wake katika utoaji wa Elimu. Hii itasaidia kuongeza ushindani wa wanafunzi waliopo sekondari na hivyo kusoma kwa bidii. Kamati ina amini kuwa wanafunzi wengi watapenda kusoma chuo chenye sifa ya juu. Kwa mfano Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kikawekewa kiwango cha kufanana na Havard au Yale au Chuo Kikuu cha Dodoma kiwango cha Oxford, n.k.**

b) **Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha maslahi ya wahadhiri wa vyuo vikuu yanazingatiwa ili kuwaepusha kufanya kazi katika chuo zaidi ya kimoja ili kupata muda wa kutosha kufundisha wanafunzi. Hii iende sambamba na kuongeza idadi ya Wahadhiri ili kuleta uwiano kati yao na wanafunzi.**

#### **4.5 Maslahi ya Walimu**

**Mheshimiwa Spika**, Maendeleo ya Elimu nchini yanategemea namna Walimu wanavyowezeshwa. Usitegemee Mwalimu ambaye ana manung'uniko ya kutolipwa maslahi yake akafundisha kwa morali. Ukienda nchi nyingine kuwa Mwalimunisuala la kujivunia (*Prestige*), lakini hapa kwetu ualimu sio fani ya kujivunia kabisa imezoeleka kwamba ni wito. Walimu hawaheshimiki yani ni fani ambayo watu wanaenda tu ili mradi maisha yaende. **Kamati ina amini kuwa fani ya Ualimu ni fani kama fani nyingine. Walimuni nguzo muhimu ya Maendeleo endelevu ya nchini hivyo Serikali haina budi kuwawezesha ili waweze kutoa mchango wao stahiki kwa kuhakikisha maslahi yao yanalindwa kwa kuanzia Kamati inaitaka Serikali kuwalipa madai yao yanayofikia kiasi cha shilingi bilioni 408. Ikumbukwe kwamba viongozi wote tukiwemo sisi Waheshimiwa Wabunge tumepita mikononi mwa Walimu. Kamati inashauri, Serikali kuwalinda, kuwaheshimu na kuwajali walimu wa nchi hii.**

#### **4.6 Mfumo wa Elimu**

**Mheshimiwa Spika**, Mnamo Mwaka 1981 Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius.K. Nyerere aliunda Tume ya Makwetta ili kuchunguza Mfumo wa Elimu nchini na kutoa Ripoti yake Mwaka 1982 ambayo ilisaidia kuboresha Mfumo wa Elimu nchini ikiwemo uanzishwaji wa Shule za Kata nchini. Aidha, Mwaka 1983 aliyekuwa Rais wa Marekani Ronald Regans naye aliunda Tume Maalum ya kuchunguza changamoto ya Mfumo wa Elimu nchini Marekani na namna bora ya kuenenda. Tume hiyo ilikuja na ripoti iliyojulikana '**A Nation at Risk: The Imperative for Educational Reform**' ambayo naweza sema ndiyo historia ya mafanikio ya mfumo wa Elimu Marekani.

**Mheshimiwa Spika**, tukiwa Taifa ambalo tunataka kwenda kwenye Uchumi wa Kati yatupasa kujiuliza maswali matano (5) yafuatayo juu ya Mfumo wetu wa Elimu:-

(vi) Je Maudhui ya Elimu yetu yakoje? Na Je yanazingatia mahitaji ya nchi yetu?

(vii) Viwango na matarajio, Je ni kwa kiasi gani tupo makini kuhusu upandishaji wa madaraja ilikuwa na viwango vinavyofaa?

(viii) Muda wa masomo kwa wanafunzi wa shule ya msingi na wale wa Sekondari ukoje, ni masaa mangapi wanatumia kusoma?

(ix) Maslahi ya Walimu, hapa lazima tujiulize je mishahara ya Walimu inaendana na ushindani wa taaluma yao pamoja na utendaji kazi wao?

(x) Rasilimali Fedha: Serikali ina fahamu kuwa ina wajibu wa kusaidia ili kufikia mahitaji ya wanafunzi kama wale waliobarikiwa kuwa na vipawa mbalimbali, walemavu ikiwa ni pamoja na miundombinu yao kwa kuwapa msaada wa fedha lakini pia mafunzo ya utafiti na Elimu ya juu?

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya tafakuri hiyo, Kamati inaona **ni wakati sasa wa kubadili mfumo wa mzima wa Elimu nchini kutoka katika mfumo tulionao wa makundi mawili, kundi la matajiri na kundi la maskini. Kamati inaitaka Serikali kuangalia upya mfumo wetu wa Elimu kuunda TUME MAALUM YA KITAALAM ya kufanya mapitio makubwa ya mfumo wa Elimu nchini na kuchunguza Hali ya Elimu (State of Education) ili kwenda sambamba na kasi kubwa ya mabadiliko ya kiuchumi duniani. Tume hii iwe Tume ya Rais ya kitaalam na Ripoti yake ilewe Bunge ili Bunge nalo lijadili na kutoa mapendekezo ya Kisera, Kisheria kwa Serikali ili kuokoa Elimu yetu.**

**Kamati inashauri Tume hiyo iangalie kuhusu Sera za Elimu; Mfumo wa upatikanaji wa Walimu; Mfumo wa Motisha kwa Walimu; Muda wa Elimu ya Msingi, Sekondari na Chuo Kikuu; Usimamizi wa Elimu, Uendeshaji na Ugharamiaji wake.**

#### **4.7 Tuzo ya Udhhamini (Scholarship Award)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona ni wakati sasa wa kuwekeza kwenye Elimu na kuongeza ushindani kwakutoa tuzo za udhamini kwa wanafunzi wanaomaliza kidato cha sita ambao wamefanya vizuri katika mitihani yao ya Taifa. Kamati inapendekeza tuzo hii iitwe **'Presidential Scholarship Award'** ambapo wanafunzi 50 watakaofanya vizuri katika mitihani ya kidato cha sita wapewe udhamini wa kusoma katika vyuo bora duniani kama Harvard,

**Yale, Cambridge, Oxford n.k. na wagawanywe katika fani tofauti ikiwemo Sayansi, Uchumi, Sanaa, Siasa n.k.**

**Mheshimiwa Spika**, nchi za Asia ambazo zinajulikana kama 7 **Asian Tigers** ukisoma historia yake utagundua karibu zote (Singapore, Malaysia, Korea, Hong Kong, Thailand, Indonesia na Taiwan) ukiacha mambo mengine, ziliwekeza sana kwenye Elimu. Tukiangalia nchi kama Korea ya Kusini mnamo miaka ya 1960 ilikuwa katika Uchumi wa chini zaidi hata ya Tanzania, lakini kwa mujibu wa taarifa kutoka International Monetary Fund (IMF) Mwaka 2015 Korea ilikuwa nchi ya 13 kati ya nchi 180 duniani zenye Pato la Taifa kubwa. Kwa mujibu wa Mwandishi wa Kitabu kinachoitwa “**Upside –Down Success Story for Korean Economic Development**” Joong-Kyung Choi ni kwamba Serikali ya Korea ya Kusini iliamua kutoa ufadhili kwa wanafunzi wanaofanya vizuri na wenye vipaji mbalimbali wanatoka katika familia masikini kwenda kusoma katika vyuo bora duniani katika nchi za Marekani, Ujerumani na Uingereza hali iliyoongeza Wasomi ambao wamesaidia kwa kiasi kikubwa Maendeleo ya Uchumi wa nchi hiyo.

**Kamati ina amini kabisa ufadhili huu utakuwa chachu na utaongeza morali ya wanafunzi kusoma kwa bidii na hatimaye kuwa na Wasomi wazuri wenye taaluma mbalimbali ambazo ni muhimu kwa Maendeleo endelevu ya nchi yetu.**

#### **4.8 Mahusiano ya Ongezeko la Idadi kubwa ya watu katika Elimu**

**Mheshimiwa Spika**, Mchumi Michael Todaro katika Kitabu chake cha Maendeleo ya Uchumi (*Economic Development 11th Edition*) amebainisha kuwa idadi ya watu duniani imekuwa ikiongezeka kwa kasi kubwa na kila Mwaka zaidi ya watu **milioni 75** wanaongezeka na takribani **asilimia 97** ni kutoka nchi zinazoendelea. Aidha, inakadiriwa kuwa hapa nchini kila Mwanamke huzaa wastani wawato **6**. Siyo hivyo tu, takribani **asilimia 44** ya wanawake wanapata mimba ya kwanza wakiwa na umri wa **miaka 19**. Kwa mujibu wa Takwimu za Sensa ya Mwaka 2012 idadi ya watoto kati ya umri wa miaka 2-6 ilizidi wale wa umri wa miaka 10-14 kwa **1,665,843**. Endapo ukuaji huu utaendelea basi **miaka 25** ijayo Serikali itakuwa na mzigo mkubwa ikiwamo kuongeza idadi ya shule pamoja na Walimu kwani idadi ya wanafunzi wanaopaswa kujiunga na Elimu ya msingi itakuwa kwa **333,169** kwa miaka mitano ijayo, na ikiwa kila darasa litakuwa na wanafunzi **40** basi yatatakiwa madarasa mapya **8,392** kwa mwaka na kwa miaka mitano madarasa **41,646**.

**Ni kwa msingi huo :**

a) **Serikali idhibiti ongezeko la idadi ya watu. Hii itawezekana kwa njia mbalimbali ikiwemo kusomesha zaidi wanawake kwani tafiti zinaonesha kuwa mwanamke anapopata muda zaidi wa kusoma anachelewa kuolewana kuzaa,**

**pia atazaa watoto wachache ambao watakuwa na afya bora lakini pia ambao ataweza kuwasomesha.**

**b) Serikali iendeele kutoa Elimu ya Uzazi wa Mpango ili kupunguza idadi ya watoto wanaozaliwa kwa kila mwanamke mmoja angalau tufikie wastani wa watoto 3 kwa kila mwanamke.**

**c) Kamati ina laani vikali wale wote wanaowapa mimba wanafunzi wakiwa shule za Msingi na Sekondari na inaitaka Serikali kuwapa adhabu kali wale wote wanaobainika kufanya vitendo hivi. Aidha, Kamati inaona haina maana kuwafukuza masomo watoto hao wakike na badala yake Kamati inashauri mara baada ya kujifungua wanafunzi hao wapewe nafasi ya kurudi tena masomoni kwa ustawi wao, watoto wao na Taifa kwa ujumla.**

#### **4.9 Vyuo vya Ufundi**

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kuwekeza katika vyuo vikuu, vyuo vya ufundi navyo ni vizuri zaidi katika kuzalisha wataalam wa fani mbalimbali ambao wanasaidia sana katika Mapinduzi ya Viwanda. Dira ya Maendeleo ya 2025 inalenga katika kuibadili Tanzania kutoka katika nchi yenye Uchumi wa chini wa uzalishaji mdogo wa kilimo kwenda kwenye uchumi wa kati wa viwanda na watu wenye Elimu ya Juu. Sasa basi ili kuweza kufikia lengo hilo, ni wakati sasa Serikali kuanza kuweka msisitizo kwenye Elimu ya Mafunzo ya Ufundi ili kuzalisha vijana wenye taaluma na ubunifu ambao utakuwa chachu katika Maendeleo ya Sekta ya viwanda nchini ambayo ni Sekta muhimu katika utoaji wa ajira kwa kufanya yafuatayo:-

**a) Serikali lazima ihakikishe kila Mkoa una kuwa na vyuo hivi na ambavyo mitaala yake itaendana na mahali. Kwa mfano vyuo vilivyopo kanda ya Ziwa na Pwani ni vyema vikawa na Mitaala ya Uvuvi na vile vilivyopo kwenye Mikoa yenye kilimo kingi basi vikawa na mitaala ya aina hiyo.**

**b) Kwa kuwa imeonekana kuna Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ambavyo havitumiki, Kamati inashauri Serikali ivitumie vyuo hivyo kwa kuvibadilisha kuwa vyuo vya VETA ili kupunguza gharama za ujenzi wa vyuo vipya.**

**c) Serikali ianzishe Vyuo vya Ufundi (Technical Schools) kama ilivyokuwa kwa Dar Tech, Arusha Tech n.k. Kamati inapendekeza Mikoa kama Kigoma, Mwanza, Rukwa kuwa na vyuo vya ufundi vya aina hii ili viweze kuchochea Uchumi wa Viwanda.**

**4.10 Mamlaka ya udhibiti wa Elimu nchini (Education Regulatory Authority)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kuwa kumekuwepo na Idara ya Ukaguzi wa Elimu katika Wizara hii ambayo ndiyo yenye jukumu la kusimamia ubora wa Elimu nchini. Kamati haikubaliani na Idara hii kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za Idara hii kutokuwa huru lakini pia kutowezeshwa kifedha ili kutekeleza majukumu yake hali ambayo imekuwa ikichangia kushuka kwa viwango vya ubora na ufaulu kutokana na kutokuwepo kwa ukaguzi na ufuatiliaji. Takwimu zinaonesha (BEST 2015) ni **asilimia 19.1** tu ya shule za msingi na **asilimia 21.4** pekee ya shule za sekondari ndizo hukaguliwa kwa Mwaka. Tafsiri yake ni kuwa huichukua Serikali takribani miaka mitano (5) kukamilisha ukaguzi wa shule zote za Umma zilizopo nchini. Au maana yake pia ni kuwa shule hukaguliwa mara moja kila baada ya miaka mitano (5).

**Ni kwa sababu hiyo Kamati inaona kuna umuhimu wa kuwa na Mamlaka ya Udhiditi wa Elimu nchini ambayo itaangalia ubora wa Elimu kuanzia Elimu ya awali hadi Chuo kikuu kwa shule zote za Serikali na Binafsi kwa kuhakikisha Elimu inayotolewa ndiyo ambayo inategemewa hii itasaidia kuwa na kiwango cha Elimu kinachokidhi viwango na ubora. Kwa kufanya hivi tutafikia lengo namba 4 la Malengo ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals) linalohusu ubora wa Elimu (Quality Education) ambayo itatutoa katika umaskini huu kama ambavyo Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO Bi. Irina Bokova alivyowahi kusema “We know the power of education to eradicate poverty, transform lives and make breakthroughs on all the Sustainable Development Goals.”**

#### **4.11 Ada Elekezi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa Serikali ipo kwenye mchakato wa kuandaa waraka wa Ada Elekezi kwa shule Binafsi na katika Mwaka huu shule binafsi zimezuwa kuongeza ada. **Kamati haiamini katika Ada elekezikutokana na ukweli kuwa Serikali imeshakuja na Waraka wake wa kutoa Elimu bure, basi haina budi kuhakikisha Elimu inayotolewa inakidhi viwango hii itasaidia kupanua wigo na hivyo Wazazi wengi watapata nafuu na kuamua kuwapeleka watoto wao katika shule hizo za Serikali na wale watakaopeleka watoto wao shule binafsi basi itakuwa ni kwa utashi wao.**

**Pamoja na hayo Kamati inaitaka Serikali kufanya jukumu lake la kuboresha Elimu kwa kuziwezesha shule za Serikali ili ziwe kama ilivyokuwa zamani kwamba kila mtu alikuwa anatamani kusoma katika shule hizo kama Tabora Boys, Mirambo, Msalato, Kilakala, Pugu, Loleza na nyingine, kutokana na Ubora wa Elimu iliyokuwa inatolewa na Shule hizo.**

#### **4.12 Tume ya Utumishi wa Walimu (Teachers Service Commission)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa pamoja na kuunda kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (**Teachers Service Commission**) mnamo Mwaka 2015 ambayo jukumu lake ni pamoja na kuajiri, kupandisha vyeo na kusimamia nidhamu ya watumishi lakini imenyimwa kipengele muhimu cha kulipa



mishahara ambayo ingeipa nguvu Tume kwani hakuna sababu ya kuwa Mwajiri wakati hauna jukumu la kulipa Mishahara. Pia, Kamati imebaini kuwa pamoja na Tume hii kusimamia masuala ya Walimu lakini ipo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMIkiwa imetengewa bajeti ya **shilingi bilioni 10 (Fungu 02)** kwaajili ya uendeshaji. Kutokana na hali hii-

a) ***Kamati inarudia ushauri wake wa kutaka mambo yote yanayohusu Sekta ya Elimu yawe chini ya Wizaramoja ili kupunguza usumbufu huu.***

b) ***Kamati inaitaka Serikali kuipa Tume hii jukumu la kulipa mishahara ili kurahisisha ushughulikiaji wa masuala yote ya walimu na kuwapunguzia usumbufu ambao wanaendelea kuupata.***

c) ***Kutokana na kutokuwa na Bodi ya Taaluma ya Ualimu (Teachers Profession Board) Kamati inaitaka Serikali kuunda Bodi hii ambayo itasimamia Taaluma ya walimu ili kuhakikisha viwango vya Taaluma ya Walimu vinazingatiwa hii itasaidia katika kipindi hiki ambapo kumekuwa na soko huru na hivyo kuwepo kwa walimu wengi ambao wengine hawakidhi viwango vinayotakiwa.***

#### **4.13 Taasisi ya Elimu Tanzania (Tanzania Education Authority)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa kumekuwepo na ucheleweshaji wa upatikanaji wa vitabu katika shule mbalimbali za msingi na sekondari nchini kutokana na Makampuni yanayopewa jukumu la kuandika na kuchapa kuwa na uwezo mdogo.

a) ***Kamati inaitaka Taasisi hii kuliangalia suala hili upya kwa kuwapa Zabuni hiyo Makampuni yenye kukidhi vigezo na viwango ili vitabu hivi viweze kutoka mapema kwani hadi Kamati inakutana na Wizara mwezi Aprili, kuna vitabu ambavyo vilipaswa kuanza kutumika katika Mwaka huu wa masomo vilikuwa bado havijatoka. Kamati inajiuliza wanafunzi hao waliopaswa kufundishwa na kusoma masomo hayo itakuwaje?***

b) ***Kamati inaitaka Taasisi hii kuanza kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu ya Elimu ya Msingi na Sekondari ya shule za Umma kwa kuipatia fedha za kusaidia Halmashauri katika Ujenzi wa miundombinu.***

#### **4.14 Wanafunzi wanaojiunga na Vyuo Vikuu**

**Mheshimiwa Spika,** Mfumo wetu waElimu nchini umepitia mambo mengi ya ajabu na ya kusikitishasana. Kama tunavyofahamu, Mamlaka ya Vyuo Vikuu (TCU) inajukumu la kudahiri wanafunzi wenye Elimu ya kidato cha sita na diploma kwa ajili ya kujiunga na Vyuo Vikuu. Katika Mwaka 2013/2014 kuna takribani wanafunzi 1000 waliomaliza kidato cha nnewalidahiriwa na kujiunga na Chuo/Vyuo vikuu. Kamati imeshtushwa na hili na inajiuliza hivi kuna sera



yeyote inayoeleza na kuruhusu Mwanafunzi aliyehitimu Kidato cha nne kujiunga na Elimu ya Juu? Na kama ipo ilitungwa lini? Sio hivyo tu bado Kamati inajiuliza je walipewa Mikopona Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu? Kama kweli je ni kwa vigezo vipi?

**Kamati inaona hapa kuna kizungumkuti na hivyo inamtaka Waziri alieleze Bunge lako Tukufu kuhusu suala hili lakini pia afanye uchunguzi kwa Taasisi zote zilizohusika na zichukuliwe hatua za kinidhamu pale zitakapobainika kwamba zilifanya uzembe au kukiuka utaratibu.**

#### 4.15 Jengo laElimu

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na utaratibu wa Taasisi nyingi za Serikali zikiwemo za Wizara hii kuamua kujenga majengo yao kwa Matumizi ya Ofisi hata kama taasisi ina watumishi wachache. Kamati inaona ujenzi huu hauna tija na ni gharama kubwa kwa Taifa letu ambalo bado lipo katika listi ya nchi zenye uchumi wa chini.

**Kamati inapendekeza Taasisi zote zilizochini ya Wizarahii kujenga jengo moja litakalojulikana kama ELIMU TOWER na kila Taasisi ikapata Ofisi ndani ya jengo hilo ambayo itapunguza gharama lakini pia itasaidia wadau wanaokuja kupata huduma zinazohusu masuala ya Elimu kuzikuta taasisi zote sehemu moja na hivyo kurahisisha upatikanaji wa huduma.**

#### 4.16 Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu

**Mheshimiwa Spika**, Bodi ya Mikopo ndiyo moyo wa Taifa hili kwani Mikopo ya Elimu ya Juu imesaidia kuongeza idadi ya wanafunzi wanaomaliza vyuo vikuu ambalo ni jambo jema sana. Hata hivyo zipo changamoto ambazo Kamati inaona ni muhimu kuzitolea Maoni na Ushauri.

a) Pamoja na lengo zuri la utoaji wa Mikopo kwa wanafunzi, Kamati imebaini kuwa bado watu wengi hawafahamu nini hasa maana ya hii Mikopo na hivyo kuona hawana wajibu wa kulipa mara wanapopata kipato/ajira. **Kamati inashauri Elimu zaidi iendelee kutolewa kupitia vyombo mbalimbali kama Radio, Magazeti, Televisheni na hata vipeperushi.**

b) Katika kuhakikisha kila mtu aliyepata mkopo anarejesha kwa wakati, **Kamati inapendekeza Bodi iangalie utaratibu wa kutoa leseni badala ya vyeti mara wanafunzi wanapohitimu na vyeti kutolewa mara baada ya kurejesha mkopo kama nchi nyingine kama vile Uingereza inavyofanya. Mbinu, hii itasaidia Mikopo mingi kurejeshwa kwa wakati na hivyo kuwezesha Wanafunzi wengi zaidi kupata Mikopo. Kwa kuanzia Kamati inashauri kutoa majina ya waliokopa wote kwenye magazeti ya Umma na kupeleka orodha hiyo kwa waajiri wote ili kuwabaini na kuanza kulipa.**

c) **Kamati inapendekeza kuanzia Mwaka wa Masomo 2016/2017, Wanafunzi wote wanaojiunga na Elimu ya Juu nchini wapewe Vitambulisho vya Taifa vinavyoweza kutambulika na Mabenki ili kuhakikisha kuwa kila**

**mwanafunzi mwenye kupata mkopo anaunganishwa na Kitengo cha Uratibu wa Mikopo (Credit Reference Bureau) kilichopo Benki Kuu (BOT) ili kuunganisha Taarifa zake na mabengi na Taasisi nyigine za fedha. Hii itawezesha wanufaika wa mikopo kulipa mikopo hiyokabla ya kupewa mikopo mipya na Benki husika. Kamati inashauri kila mwanafunzi aliyepo kwenye chuo aunganishwe na mfumo huo na hivyo tutakuwa tumemaliza kabisa tatizo la watu kutolipa mikopo yao kwa wakati.**

d) Kutokana na changamoto ya uendeshaji wa Bodi inayotokana na kutojua idadi kamili ya wanafunzi ambao wanapaswa kupata Mikopo kila mwaka, **Kamati inapendekeza kuwa Serikali iamue kuweka idadi kamili ya wanafunzi (fixed number) ya wanafunzi wanaopaswa kupata Mikopo ili Bodi iweze kujipanga tofauti na utaratibu wa sasa wa kutoa Mikopo kulingana na kiwango cha ufaulu.**

e) Kamati ilisikitishwa na changamoto ya ucheleweshaji wa utaoji wa Mikopo kwa wanafunzi ambao wengi wao ni wale wanaotoka kwenye familia duni na hivyo wazazi wao hawana uwezo wa kuwasaidia, **Kamati inaitaka Bodi ya Mikopo kuanza kutoa Mikopo hiyo kwa wakati ili kuepuka wanafunzi hao kujiingiza katika vitendo visivyofaa kama njia ya kujipatia kipato cha kuweza kujikimu kama vile kufanya biashara ya ngono.**

f) Kamati imebaini kuwa takribani asilimia 48 ya fedha yote ya Miradi ya Maendeleo ya Fungu 46 kwa Mwaka huu 2016/2017 ni fedha kwaajili ya Mikopo ya Elimu ya Juu hali inayofanya Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kuonekana kubwa wakati kiuhalisia siyo sawa. **Kamati inashauri kuwa fedha za Mikopo ya Elimu ya juu isiwe sehemu ya Bajeti ya Maendeleo ya Wizara bali iwe ni fedha inayotoka moja kwa moja Hazina (Direct Transfer) au iwe na Fungu lake linalojitegemea.**

#### **4.17 Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela- Arusha**

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi hii ni muhimu sana katika zama hizizi Sayansi na Teknolojia kwani ndiyo inatumika kuendeleza umahiri na weledi katika Maeneo ya Sayansi na Teknolojia. **Kamati imebaini kwamba Taasisi hii ipo kwenye mpango wa kuanza kufundisha masomo mengine ya Biashara na Utawala kitu ambacho Kamati ina amini halikuwa dhumuni la uanzishwaji wake. Kamati inaona kwa kuwa vipuo vingi vinavyo fundisha masomo haya ya Biashara na Utawala ni vyema Chuo ikaviachia vipuo hivyo kufundisha masomo hayo na chenyewe kikajikita kwenye masomo ya Sayansi na Teknolojia kama lilivyo lengo la uanzishwaji wake ili kuzalisha wataalam tarajiwa.**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuweza kutoa matokeo tarajiwa, Kamati inaona pia bado Taasisi hii haijawezeshwa vya kutosha ili kutimiza lengo na hivyo **Kamati inaitaka Serikali kuongeza Bajeti ya Taasisi hii.**


#### 4.18 Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Sheria ya Bunge No. 7 ya Mwaka 1986 COSTECH ndiyo chombo pekee cha kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu masuala yote yanayohusu Utafiti wa Sayansi na Teknolojia. COSTECH imekuwa ikigharamia Tafiti za kisayansi na kuboresha mazingira ya utafiti ikiwemo miundombinu na vitendea kazi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika zama hizi za Sayansi na Teknolojia hatuna budi kuhakikisha kwamba Tume hii inafanya kazi ipasavyo. Kamati imebaini kuwa pamoja na umuhimu wa Tume hii lakini bado Serikali haijawa na dhamira ya dhati kuiwezesha ili iweze kutoa matokeo mazuri ambayo ni msingi muhimu kwa Maendeleo ya nchi. Kwa mujibu wa UNESCO Institute of Statistics nchi zilizoendelea katika kipindi cha miaka sita (2008-2013) zimekuwa zinatumia wastani wa **asilimia 2.4** ya Bajeti yake ya Matumizi kwa mwaka kwenye Utafiti na Maendeleo wakati nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara zimekuwa zinatumia wastani wa **asilimia 0.4 tu** kwa kipindi hicho. Aidha, kwa mujibu wa Taarifa za Wizara na Vitabu vya Bajeti kiasi kilichotengwa kwaajili ya Mradi wa Utafiti na Maendeleo (*Research and Development*) ulio chini ya COSTECH ni shilingi **Bilioni 10.9 tu** kati ya **Trilioni 23.9** sawa na **asilimia 0.04 tu** ya Bajeti yote ya Serikali kwa Mwaka huu wa Fedha 2016/ 2017, kiasi ambacho ni kidogo sana ukilinganisha na umuhimu wake kwa Maendeleo ya nchi yetu. (**Rejea Kielelezo Na. 4**)

**Kamati inaitaka Serikali kuipatia Taasisi hii fedha nyingi zaidi ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi na kuleta tija.**

**Kielelezo Na.4: % YA FEDHA ZA UTAFITI NA MAENDELEO**



**Chanzo: UNESCO**

#### 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa kufanya kazi za Kamati na hususan uchambuzi wa Taarifa kwa weledi wa hali ya juu. Taarifa hii

ni matokeo ya kazi yao nzuri ambayo wamekuwa wakifanya kwa kipindi chote tangu Kamati hii imeundwa.

Kwa namna ya kipekee napenda kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Peter Joseph Serukamb, Mb	Mwenyekiti
2. Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb	M/Mwenyekiti
3. Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb	Mjumbe
4. Mhe. Dkt. Charles J. Tizeba, Mb	Mjumbe
5. Mhe. Peter Ambrose Lijualikali, Mb	Mjumbe
6. Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi, Mb	Mjumbe
7. Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mb	Mjumbe
8. Mhe. Kasuku Samson Bilago, Mb	Mjumbe
9. Mhe. Dkt. Elly Marko Macha, Mb	Mjumbe
10. Mhe. Lucia Michael Mlowe, Mb	Mjumbe
11. Mhe. Dkt. Jasmine Tiisekwa, Mb	Mjumbe
12. Mhe. Neema William Mgaya, Mb	Mjumbe
13. Mhe. Susan Anselm Lyimo, Mb	Mjumbe
14. Mhe. Juma Selemani Nkamia, Mb	Mjumbe
15. Mhe. Seleman Said Bungara, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Zitto Zuberi Ruyagwa Kabwe, Mb	Mjumbe
17. Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb	Mjumbe
18. Mhe. Bernadetha Kasabango Mushashu, Mb	Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuliongoza vema Bunge hili la 11.

**Mheshimiwa Spika**, namshukuru Waziri waElimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi Pro. Joyce Ndalichako (Mb), Naibu Waziri Eng. Stella Manyanya, Katibu Mkuu Ndg. Maimuna Tarishi, Naibu Katibu Mkuu Prof. Simon Msanjila na Dkt.Leonard Akwilapo pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah kwa ushirikiano mzuri ambao Kamati imekuwa ikipewa. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman B. Hussein, Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Kamati yetu Ndg. Dickson M. Bisile pamoja na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Agnes Nkwera na Ndg. Pamela Pallangyo kwa kufanya kazi kwa weledi na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati na Msaidizi wa Kamati Ndg. Mwimbe John pamoja na Watumishi wote wa Bunge kwa utendaji kazi wao mzuri unaosaidia Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo naomba sasa Bunge lako Tukufu, likubali na kuridhia kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi (**Fungu 46**) jumla ya shilingi **1,396,929,798,625.00 (Trilioni Moja, Bilioni Mia tatu tisini na sita, Milioni Mia tisa ishirini na tisa, laki saba tisini na nane elfu na mia sita ishirini na tano)**.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono Hoja.

Mussa A. Zungu, Mb  
**MAKAMU MWENYEKITI**  
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA**  
**MAENDELEO YA JAMII**

26 MEI, 2016

**KIAMBATISHO NA. 1**

SN	HOJA / USHAURI	MAJIBU/ MAELEZO
<b>UTENDAJI USIORIDHISHA WA IDARA YA UKAGUZI WA ELIMU</b>		
5.1 (i)	Idara ya Ukaguzi wa Elimu kuwa Wakala ya Serikali.	Kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii, Wizara imewasiliana na Ofisi ya Waziri Mkuu ili kuomba kibali cha kuanzisha Wakala wa Ukaguzi wa Shule kwa barua yenye Kumb. Na. HA.1188/212/03/142 ya tarehe 14 Mei, 2015.
5.1 (ii)	Idara ya Ukaguzi kuongezewa Bajeti.	Serikali imeendelea kuongeza bajeti ya Idara ya Ukaguzi mwaka hadi mwaka. Katika mwaka wa fedha 2013/14 kiasi cha <b>shilingi 18,308,674,045</b> kilitengwa, <b>shilingi 18,792,457,200</b> zilitengwa mwaka 2014/15 na <b>shilingi 25,823,307,000</b> zimetengwa katika mwaka 2015/16 sawa na ongezeko la asilimia <b>41</b> ukilinganisha na kiasi cha fedha kilichotengwa 2013/14.
<b>MPANGO WA KUTEKELEZWA KWA MATOKEO MAKUBWA SASA (BRN) KATIKA SEKTA YA ELIMU</b>		
5.2	Serikali ihakikishe kunakuwa na utaratibu wa kupima matokeo ya miradi ambayo inatekelezwa kwa utaratibu wa BRN ili jamii iweze kutathmini mafanikio yanayopatikana na kutofautisha na	Ushauri huu umepokelewa na unafanyiwa kazi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2015/2016 serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 4.6 kupitita Mamlaka ya Elimu Tanzania kwa ajili ya kuwezesha uratibu, ufuatiliaji, uendeshaji na tathmini ya miradi ya elimu

SN	HOJA / USHAURI	MAJIBU/ MAELEZO
	miradi inayotekelezwa kwa utaratibu mwingine	ikiwemo miradi ya BRN
<b>MWENENDO WA UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA WIZARA NA TAASISI ZAKE</b>		
5.3 (i)	Wizara iimarisha ukusanyaji wa maduhuli kwa zile taasisi zake ambazo zimeonesha udhaifu mkubwa katika eneo la ukusanyaji kama Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu	Mwelekeo wa Serikali kwa sasa ni kuzifanya Taasisi kujiendesha zenyewe kwa kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza vyanzo vya mapato kwa kuendelea kusimamia kwa ufanisi bajeti za mapato, matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo.
5.3 (ii)	Wizara iangalie namna ya kutumia mfumo wa Kielektroniki katika ukusanyaji na udhibiti wa mapato kwa taasisi zake	Maelekezo ya ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya wizara na taasisi kwa kutumia mfumo wa Kielektroniki yamepokelewa. Kwa sasa asilimia kubwa ya makusanyo ya Wizara yanafanywa kupitia benki.
5.3 (iii)	Taasisi ambazo hazikufanya vizuri katika makusanyo ni vyema zikajifunza kutoka kwenye taasisi zilizofikia au kuvuka malengo	Ushauri wa kisisitiza Taasisi kuwa wabunifu na kuongeza makusanyo ya maduhuli umezingatiwa
5.3 (iv)	Wizara ibuni vyanzo vipya vya makusanyo ili kuongeza mapato	Mikakati iliyowekwa na Taasisi kubuni vyanzo vingine vya kukusanya mapato (Maduhuli) badala ya kutegemea ada za wanafunzi peke yake ni kama vile kufanya tafiti na huduma za ushauri wa kitaalamu. Aidha kwa taasisi ambazo zinasimamia ubora wa elimu ya juu (TCU na NACTE) zimebuni ada (fee) ambayo inachangiwa na kila mwanafunzi ili kudhibiti ubora wa elimu ya juu nchini.
<b>MKAKATI WA WIZARA KUTEKELEZA VIPAUMBELE</b>		
5.4	Wizara izingatie vigezo vya SMART wakati wa kutekeleza vipaumbele vya majukumu yake	Wizara inatumia Mpango mkakati ambao ni wa mwaka 2014/2015 katika kutekeleza majukumu yake. Mpango huu hutumika pamoja na Mpango wa Kati wa Matumizi ya Bajeti ya Wizara (MTEF) katika kutekeleza vipaumbele vilivyopangwa.
<b>MWENENDO WA UPATIKANAJI WA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO</b>		
5.5	Serikali iangalie uwezekano wa kutenganisha fedha za mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu katika fedha za maendeleo ili kutoa picha	Wizara ilikwishapeleka maombi ya kuhamishia tengeo la fedha za Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kutoka Wizara ya Elimu kwenda Hazina, hoja hii ilipoletwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya

SN	HOJA / USHAURI	MAJIBU/ MAELEZO
	halisi ya bajeti ya maendeleo na mwenendo wa utoaji wa fedha hizo kwa miradi husika	Huduma za Jamii mwaka 2013/2014. Hata hivyo, Hazina waliamua tengeo hili lihamishiwe kutoka katika fedha za Matumizi mengineyo na lijumuishwe kwenye Matumizi ya Maendeleo kama inavyoonekana sasa. Wizara inaiomba Kamati kwa mamlaka yake iishawishi Hazina kuhamisha tengeo hili kama ilivyoagizwa na kamati.
<b>UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2014/2015</b>		
5.6 (i)	Mradi wa ukarabati na upanuzi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe kutopatiwa fedha	Pamoja na kutopatikana kwa fedha kwa mwaka 2014/2015, Serikali imeendelea kutenga fedha za miradi ya maendeleo ambapo katika mwaka fedha 2015/2016 jumla ya shilingi bilioni 1.05 ilitengwa. Aidha, katika mwaka wa fedha 2016/2017 kiasi cha shilingi bilioni 3.5 kimetengwa kwa ajili ya kukamilisha mradi huo.
5.6 (ii)	Mradi wa ukarabati na upanuzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kutokamilika kutokana na mkandarasi kutolipwa fedha zake	Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya chuo. Vile vile, katika mwaka wa fedha 2016/2017 kiasi cha shilingi bilioni 4 kimetengwa kwa ajili ya upanuzi wa chuo kikuu cha Kilimo cha Sokoine..
5.6 (iii)	Mradi wa ujenzi wa Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutokamilika kutokana na kutopatiwa fedha za maendeleo	Pamoja na kutopatikana kwa fedha katika mwaka wa fedha 2014/2015, Serikali imeendelea kutenga fedha za miradi ya maendeleo kwa chuo hiki ambapo katika mwaka 2015/2016 chuo kilitengewa jumla ya shilingi bilioni 4 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 kiasi cha shilingi bilioni 5 ilitengwa kwa ajili ya kukamilisha miradi hiyo.
<b>MAFUNZO YA UALIMU KWA VITENDO (BTP)</b>		
5.7	Mafunzo ya Ualimu kwa Vitendo (Block Teaching Practice-BTP) yanafanyika kwa wiki 2 badala ya Wiki 8 kama ilivyokuwa hapo mwanzo. Kitendo hiki kinaathiri ubora wa elimu.	Kulingana na Mtaala wa Mafunzo ya Ualimu, mafunzo kwa vitendo hutolewa kwa namna mbalimbali ikiwemo ufundishaji kiduchu, mafunzo ya muda mfupi ndani ya chuo na ya muda mrefu kwa wiki 8. Wanachuo waliohitimu mafunzo haya mwaka 2015 walifanya mafunzo kwa muda wa wiki 5 (wiki 3 walipokuwa mwaka wa kwanza, wiki 2 walipokuwa mwaka wa pili). Hata hivyo muda huo hautoshi. Muda wa mafunzo kwa vitendo



SN	HOJA / USHAURI	MAJIBU/ MAELEZO
		<p>umepungua kutokana na upatikanaji wa fedha hasa kwa mwaka 2013/14 na 2014/15. Ili kuhakikisha kuwa mwalimu mwanafunzi anapata muda wa kupata uzoefu wa kutosha wa mafunzo kwa vitendo, Serikali iliweka zaidi msisitizo kwenye mafunzo ya muda mfupi (mafunzo kiduchu) ili kuhakikisha kiwango cha ubora wa Elimu kinazingatiwa na kinaendelea kukua.</p> <p>Aidha, kwa mwaka 2015/16 tengeo limewekwa la kutosha wiki nane. Ikiwa bajeti hii itapitishwa na kutolewa kama zilivyoombwa suala la mafunzo kwa vitendo yatafanywa kwa muda mrefu kama inavyotakiwa.</p>
<b>UKOSEFU WA UFANISI KATIKA MFUMO WA KUHUDUMIA WALIMU (TEACHERS SERVICE DELIVERY SYSTEM)</b>		
5.8 (i)	Ni mwingiliano wa majukumu gani unaosababisha mchakato wa kuundwa kwa Bodi ya Kitaalam ya walimu usubiri kuundwa kwa chombo kimoja cha ajira ya walimu?	Kuna mwingiliano wa baadhi ya majukumu kati ya Chombo kimoja cha Ajira ya Walimu na Bodi ya Kitaalamu ya Walimu ambapo vyombo vyote viwili vina majukumu ya <b>kusajili</b> na kushughulikia <b>nidhamu kwa walimu</b> . Hivyo Serikali imeona ni busara kuunda kwanza chombo kimoja cha ajira ya walimu na kisha ndipo ikamilishe uundaji wa Bodi ya Kitaalamu ya Walimu ili kuondoa mwingilio unaoweza kujitokeza
5.8 (ii)	Serikali iangalie namna ambavyo eneo la huduma za walimu kuwa sehemu ya Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN)	Katika utekelezaji wa mikakati ya mpango wa BRN, kipaumbele namba 9 kinahusiana na walimu.
<b>WALIMU NA MAZINGIRA MAGUMU YA KAZI</b>		
5.9	Walimu waliopo katika mazingira magumu wapatiwe fursa za kujiendeleza wakiwa kazini kwa lengo la kuwajengea uwezo katika taaluma yao	Utaratibu wa walimu kupata nafasi za kujiendeleza upo chini ya utaratibu unaowekwa na mwajiri husika.
<b>UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA VETA</b>		
5.10	Serikali iangalie namna ya kuiongezea uwezo zaidi VETA ili iweze kutimiza wajibu wake	Mpango wa ushirikiano kati ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na OWM – TAMISEMI katika

SN	HOJA / USHAURI	MAJIBU/ MAELEZO
	kikamilifu ikiwa ni pamoja na kuvisaidia vyuo vya Maendeleo ya wananchi	<p>kuvitumia vyuo 55 vya Maendeleo ya wananchi (FDCs) wa kutoa mafunzo ya ufundi stadi yatolewayo na vyuo vya VETA ulianza kutekelezwa Januari, 2013. Vyuo 25 vya Maendeleo ya Wananchi kati ya 55 vilianza kudahili wanachuo 50 kila chuo na hivyo kufanya jumla ya wanchuo 1,250 kudahiliwa.</p> <p>Mwaka 2013 mamlaka ya VETA ilitoa mafunzo kwa walimu 100 kutoka vyuo 25 vya FDC. Mafunzo yalilenga kuwajengea uwezo walimu waweze kufundisha kwa umahiri fani zilizoainishwa kufundishwa kulingana na makubaliano ya kuanza kutoa mafunzo ya ufundi stadi yatolewayo na vyuo vya VETA katika vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.</p>
<b>UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI (NACTE)</b>		
5.11	Upungufu katika Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Mafunzo ya Ufundi (NACTE) yafanyiwe kazi kuipa mamlaka zaidi ya kusimamia kikamilifu ubora wa mafunzo ya elimu na ufundi stadi nchini	Mapungufu yaliyopo katika Sheria za NACTE yamefanyiwa kazi katika Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 kwa ajili ya kufanya maboresho ya Sheria hizi.
<b>IDADI YA WANUFAIKA WA MIKOPO YA ELIMU YA JUU</b>		
5.12 (i)	Serikali iangalie namna ya kubuni utaratibu utakaowawezesha wahitimu wa baadhi ya taaluma kufanya kazi katika maeneo ya pembezoni	Ushauri umepokelewa na utafanyiwa kazi na mamlaka husika ili wakati wa kupanga walimu wapya wazingatie maeneo ya pembezoni.
5.12 (ii)	Watoto wanaotoka familia duni wapewe mikopo licha ya kuwepo utaratibu wa kutoa mikopo kwa kuzingatia masomo ya vipaumbele.	Ushauri unapokelewa. Aidha, Sheria Na. 9 ya mwaka 2004 iliyorekebisha mwaka 2007 iliyoanzisha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, inataka mikopo kutolewa kwa wanafunzi ambao ni wahitaji. Uhitaji huu hupimwa kwa kuzingatia uwezo wa mwanafunzi kuchangia gharama za elimu ya juu kama Sera ya Elimu ya Juu inavyoelekeza. Utaratibu huu unawezesha watoto wanaotoka familia duni kupewa mikopo hata kama hawasomi masomo ya kipaumbele.
5.12 (iii)	Kuwepo na mkakati wa makusudi wa kukusanya marejesho ya mikopo ya Elimu ya Juu.	Ushauri unapokelewa. Mikakati mbalimbali ya kuwezesha wanufaika wa mikopo kutambuliwa ipo na imekuwa ikitekelezwa na Bodi. Katika mwaka wa fedha wa 2014/15, Bodi kwa kushirikiana na NIDA

SN	HOJA / USHAURI	MAJIBU/ MAELEZO
		inatekeleza mpango wa kuwapatia vitambulisho vya kitaifa wanafunzi wote wanaosoma katika Taasisi za Elimu ya Juu. Hadi kufikia tarehe 30 Mei,2015 wanafunzi wa vyuo vyote vilivyoko Dar es salaam wameandikishwa na uandikishwaji wa wanafunzi katika vyuo vilivyoko nje ya jiji la Dar es salaam unaendelea. Uandikishaji huu utaiwezesha Bodi kuwatambua kwa urahisi wakopaji hawa baada ya kuwa wamehitimu masomo yao
<b>MPANGO WA MAFUNZO YA KUANDIKA, KUSOMA NA KUHEBABU (KKK)</b>		
5.13	Uhitaji wa programu maalum ya mafunzo ya walimu kazini ikiwemo mafunzo ya KKK (Kusoma, Kuandika na Kuhesabu)	Kuna mpango wa kuhushia Mitaala ya Mafunzo ya Ualimu kawa kuchopeka kipengele cha mafunzo ya KKK ili wahitimu waweze kuwa na weledi mkubwa katika eneo hilo. Aidha, kuna mpango wa mafunzo kazini wa KKK kwa walimu 17,030 wa shule za msingi kutoka katika mikoa 14. Mafunzo hayo yanatarajiwa kuzinduliwa tarehe 07.02.2015 katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na mpango huu ni endelevu. Programu ya mafunzo hayo kwa Mikoa 7 iko chini ya mradi wa EQUIP-T, Mikoa 3 iko chini ya UNICEF na Mkoa 1 uko chini ya USAID
<b>WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUM</b>		
5.14	Kuwe na Idara kamili inayoshughulika na wanafunzi wenye mahitaji maalum na itakayotengewa fedha za kutosha.	Ushauri umepokelewa Serikali itaifanyia kazi ili kuona uwezekano wa kutekeleza ushauri huu.
<b>ELIMU YA JUU KUTENGANISHWA NA ELIMU MSINGI NA SEKONDARI</b>		
5.15	Elimu ya Juu itenganishwe na Elimu Msingi na Sekondari ili kuongeza ufanisi wake.	Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 36 Rais ndiye mwenye mamlaka ya kuanzisha na kufuta nafasi za madaraka ya namna mbalimbali katika utumishi wa Jamhuri ya Muungano, ikiwemo uanzishwaji wa Wizara mbalimbali, Idara Zinazojitegemea na Taasisi za Umma. Muundo wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi uliithinishwa na Rais kwa kuzingatia majukumu ya Wizara.
<b>ELIMU YA WATU WAZIMA KUKOSA MKAKATI WA KUPUNGUZA TATIZO LA KUTOJUA KUSOMA NA KUANDIKA</b>		

SN	HOJA / USHAURI	MAJIBU/ MAELEZO
5.16	Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima iwe na mikakati maalum kukabiliana na kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK).	<p>Katika kupambana na tatizo la kutokujua kusoma, kuandika na kuhesabu kuna mipango ifuatayo:</p> <ol style="list-style-type: none"> <li>1. Kuhuisha mitaala mafunzo ya wataalamu wa elimu ya watu wazima ili wawe mahiri katika kukuza stadi za Kusoma, Kuhesabu na Kuandika (KKK), kuboresha na kuchapa vitabu vya KKK (literacy primers), na kuvisambaza kwa ajili ya kuendeleza watu wazima.</li> <li>2. Kuendelea kutumia wanachuo wa Stashahada wa Elimu ya Watu Wazima kufundisha katika vituo vya elimu ya watu wazima katika mikoa mbalimbali kama sehemu ya mafunzo kwa vitendo ili kusaidia kupunguza uhaba wa walimu wenye weledi wa KKK. Taasisi imeanza na vitua 76 katika Manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam na vituo 7 katika Manispaa ya Morogoro.</li> <li>3. Taasisi itashirikiana na Halmashauri za Wilaya katika kufuatilia utekelezaji wa mkakati wa kukuza stadi za KKK katika vituo 10 kila wilaya chini ya mpango wa LANES.</li> <li>4. Kuandaa, kuboresha na kuendeleza kampeni za kisomo</li> <li>5. Taasisi itaendelea kuandaa wataalam watakaosimamia uandaaji na utekelezaji wa mipango ya Elimu ya Watu Wazima katika Mikoa, Wilaya na Kata kupitia mafunzo ya Stashaha na Shahada.</li> <li>6. Kupitia mpango wa Ndio Naweza (YES I CAN), vituo vimefunguliwa na kuwawezesha wanakisomo 3556 kuweza kusoma, kuhesabu na kuandika kuanzia Septemba, 2014 hadi sasa.</li> </ol>
<b>MAAZIMISHO YA WIKI YA ELIMU</b>		
5.17	Serikali iendeleo kuboresha maazimisho ya wiki ya elimu ili iwe chachu ya kuinua kiwango cha nchini	<p>Suala la kuwatambua wanafunzi na shule zilizofanya vizuri na kutunuku zawadi ni mafanikio ya Wizara na zoezi endelevu. Kupitia maadhimisho ya Wiki ya Elimu kitaifa yanayofanyika kila mwaka kuanzia mwaka 2014, WEMU kwa kushirikiana na OWM – TAMISEMI zimekuwa na utaratibu wa kuwatambua wanafunzi na shule zilizofanya vizuri na kuwazawadia. Kwa mwaka 2015 maadhimisho haya yalifanyika kuanzia tarehe 11 – 15, Mei, 2015 mkoani Dodoma.</p>

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI MHESHIMIWA SUSAN ANSELIM JEROME LYIMO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KATIKA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI**

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sote uhai na kutuwezesha kuliona Bunge la Kumi na Moja tukiwa salama. Pili, napenda kumshukuru kwa dhati kabisa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe kwa imani kubwa aliyo nayo kwangu kwa kuendelea kuiteua kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa vipindi vitatu mfululizo. Ninaahidi kuendelea kuchapa kazi kwa bidii na kwa hakika sitaangusha Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika wajibu huu niliopewa wa kuisimamia Serikali katika sekta ya elimu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru familia yangu ikiongozwa na mume wangu mpenzi Boniventure Ngowi na wanangu wote. Kipekee namshukuru sana Naibu Waziri wangu, Mheshimiwa Dkt. Suleiman Ally Yussuf kwa ushauri wake. Vilevile nawashukuru sana BAWACHA Mkoa wa Kichama wa Kinondoni kwa kunichagua kuwakilisha hapa kama kawaida sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwapongeza viongozi wote wakuu wa vyama vinavyounda Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA), kwa kazi kubwa na nzuri walioyoifanya ya kuwaongoza Watanzania kuchagua mabadiliko katika Uchaguzi Mkuu wa tarehe 25 Oktoba 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ukiukwaji mkubwa wa haki na demokrasia uliofanywa na vyombo vya dola dhidi ya upinzani katika uchaguzi huo, ikiwemo kuvamia, kuwakamata na kuwanyang'anya vifaa vya kazi wataalamu wa UKAWA waliokuwa wakijumlisha matokeo ya uchaguzi huo, bado wananchi walionesha imani kubwa sana kwa upinzani kwa kuupigia kura nyingi na kwa mara ya kwanza katika historia ya vyama vingi hapa nchini, upinzani umepata viti 116 ikiwa ni ongezeko la asilimia 23.3 kutoka viti 89 vilivyopatikana katika uchaguzi Mkuu wa 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kura za Rais, licha ya mbinu zote zilizofanywa na vyombo vya dola kuchakachua ushindi wa upinzani, bado upinzani kupitia UKAWA umeongeza kiwango chake cha ushindi hadi kufikia asilimia takriban 40 tofauti na miaka iliyopita. Ushindi huu umetokana na

kuporomoka vibaya kwa Chama cha Mapinduzi katika ngazi ya Rais kutoka ushindi wa asilimia 80 mwaka 2005, asilimia 61 mwaka 2010 na kufikia asilimia 58 mwaka 2015. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hesabu hizi ni wazi 2020 CCM itakuwa historia kama vile ilivyokuwa kwa chama cha KANU nchini Kenya na vyama vingine katika nchi za kifaraka ambavyo vinakaa madarakani vikikataliwa wananchi kutokana na utawala wa muda mrefu. Kuporomoka huku ni matokeo ya wazi kabisa kuwa chama hiki kimepoteza mvuto kwa wananchi kutokana na kushindwa kuondoa umaskini pamoja na kushindwa kusambaza huduma toshalezi za kijamii hasa elimu na afya kwa miaka yote ya utawala wake wa miaka 55 sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na aibu hii ya kushindwa kuondoa umaskini kwa wananchi na kutokana na hofu ya Serikali kuhojiwa na Bunge kuhusu utendaji wake; sasa Serikali hii ya Awamu ya Tano inayojinasibu kwa kauli mbiu ya Hapa Kazi Tu imeamua kulinyamazisha Bunge kwa kupiga marufuku vyombo vya habari kurusha moja kwa moja mijadala inayoendelea Bungeni kuhusu utendaji wa Serikali na kuhusu mgawanyo wa fedha za umma katika bajeti ya Serikali. Aidha, kutokana na hofu ya kukosolewa kutokana na kutojiamini kwa mambo inayoyafanya, Serikali sasa imeanza kuingilia hotuba za Wasemaji Wakuu wa Upinzani na kuzifanyia censorship kinyume kabisa na Kanuni za Bunge hili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016, inasema kwamba:-

*"Baada ya Waziri kuwasilisha hotuba ya bajeti kwa mujibu wa fasili ya (1), Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia makadirio husika na Msemaji wa Kambi ya Upinzani watatoa maoni yao kwa muda usiozidi dakika thelathini kila mmoja".*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni haijalelekeza kwamba watatoa maoni yao baada ya kupitiwa na Kamati ya Kanuni. Kwa hiyo, kitendo kilichofanyika tarehe 16 Mei, 2016 cha kuondoa Mezani hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili ikachakachuliwe na Kamati ya Kanuni ni kinyume kabisa na Kanuni za Bunge na ni kinyume kabisa na mila na desturi za uendeshaji wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakemea kwa nguvu zote na inaitaka Serikali kuacha mara moja tabia hii ya kuingilia shughuli za kikanuni za Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa kutumia mgongo wa Bunge. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu yetu na hatma ya Tanzania. Dhambi kubwa na mbaya kuliko zote kuwahi kufanywa na Serikali hii ya CCM ni

kuwanyima Watanzania elimu bora, kupandikiza elimu nyepesi, potofu na tegemezi kwa vizazi vingi vya Taifa hili, dhambi ya kuwachanganya na kuwavuruga watoto wa Taifa hili kwa sera dhaifu, mitaala isiyo na dira na vitabu visivyokuwa na tija kwa maendeleo ya yao na ya Taifa lao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ipo hivyo kwa sababu ya elimu duni. Umaskini, ujinga na maradhi vinavyotesa Taifa hili ni matokeo ya elimu mbovu iliyotolewa na Serikali ya CCM kwa zaidi ya miaka 50 tangu tupate uhuru. Taifa linalotoa elimu bure halifanani hata kidogo na jinsi Tanzania yetu ilivyo. Hizi ni zama za kuelezana ukweli, hata mkitufungia humu Bungeni wananchi wasituone *live* bado ukweli utaendelea kupasua kuta za Bunge hili na kuwafikia Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwanafasihi mashuhuri wa nchi yetu, Afrika ya Mashariki na Barani Afrika, Hayati Shaaban Robert, katika kitabu chake cha Kusadikika aliandika hivi:-

*“Msema kweli hukimbiwa na rafiki zake, nikipatwa na ajali kama hiyo sitawaonea wivu wale wanaodumu na marafiki zao siku zote. Siwezi kuikana kweli kwa kuhofia upweke wa kitambo na kujinyima furaha ya milele inayokaribia kutokea baada ya kushindwa kwa uongo”. Mwisho wa kunukuu. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maneno haya ndiyo msimamo wangu na ndiyo msimamo wa Kambi kwa ujumla wake, kwani siku zote Wabunge wa Upinzani tumeonekana kama maadui na kunyanyapaliwa na Serikali hii ya CCM kwa sababu ya kusema ukweli kuhusu madhaifu ya Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwanafalsafa Herbert Spencer aliwahi kusema, namnukuu:-

*“The great aim of education is not knowledge but action”.*

Mheshimiwa Naibu Spika, alikuwa na maana kwamba lengo kuu la elimu si ufahamu, bali vitendo. Tafiti zinaonyesha ni asilimia 39 tu ya wahitimu wa vyuo vikuu hapa nchini wanaajirika kutokana na kile kinachoitwa kukosa ujuzi (*lack of skills*). Kambi ya Upinzani inauliza hivi ni lini Serikali itawekeza vizuri kwenye elimu katika ngazi zote?

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya utekelezaji wa elimu bure. Kupitia Sera Mpya ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 iliyofuatiwa na Tamko la Utekelezaji katika Waraka Na.5 wa mwaka 2015, imeagiza kufutwa kwa ada za masomo katika shule za sekondari kuanzia Kidato cha 1 - IV na michango ya aina yoyote ile kwa shule za msingi.



Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya agizo hili la elimu bila ada na uchangiaji wa elimu katika shule za umma ulifanywa kwa ushirikiano baina ya Serikali pamoja na wazazi. Hata hivyo, upatikanaji wa pesa shuleni ulikuwa wa shida. Mathalani Serikali iliweza kupeleka wastani wa Sh.4,000/= hadi Sh.5,000/= tu kama ruzuku kwa shule za msingi badala ya Sh.10,000/= zilizotakiwa na Sh.12,000/= hadi Sh.15,000 kwa kila mtoto kwa mwaka kama ruzuku kwa shule za sekondari badala ya Sh.25,000/=. Kwa kuzingatia hali hiyo, ili Serikali iweze kugharamia utoaji wa elimu pasipo wazazi kuchangia ni lazima katika mpango wake wa bajeti kuanzia bajeti ya mwaka huu itenge kiwango cha fedha kama kugharamia elimu kama ifuatavyo:-

- (i) Shilingi bilioni 161.5 kwa ajili ya ruzuku ya elimu ya msingi na awali kwa wanafunzi milioni 8.9 kwa Sh.10,000 kila mwanafunzi;
- (ii) Shilingi bilioni 40 kwa ajili ya ruzuku elimu ya sekondari kwa wanafunzi milioni 1.5 kwa Sh.25,000 kila mwanafunzi kwa shule za umma;
- (iii) Shilingi bilioni 31 kufidia ada ya Sh.20,000/= kwa kila mwanafunzi katika shule za sekondari za umma kwa wanafunzi milioni 1.5;
- (iv) Shilingi milioni 198 kufidia program za uji ambazo zilikuwa zinachangiwa na wazazi maana sasa wazazi hawachaji chochote na shule nyingi zimeacha kutoa uji; na
- (v) Shilingi trilioni 1.4 kwa ajili ya kutatua changamoto za miundombinu kwa shule za msingi na sekondari kama vile vyoo, madarasa, madawati na ukamilishaji wa maabara za shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa uchambuzi uliofanywa na Haki Elimu katika majedwali yanayoonekana, namba 1, 2 na 3 hapo chini, kwa kuzingatia takwimu za idadi ya wanafunzi, shule na mahitaji, kila mwaka Serikali itapaswa kutenga kiasi cha shilingi trilioni 1.7 nje ya mahitaji mengine ya kissekta. Hivyo, tunaitaka Serikali ituambie fedha hizo ziko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha kiwango hicho kinajumuishwa katika bajeti ya sekta ya elimu ya mwaka huu wa fedha ili kutekeleza kwa ufanisi azma yake ya utoaji wa elimu bure. Vinginevyo utakuwa ni usanii mtupu na dhana ya elimu bure inaweza kuwa chanzo kingine cha anguko kuu la ubora wa elimu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zinazowakabili Walimu nchini. Elimu bora inategemea sana morali ya Walimu na si madawati au madarasa yenye viyoyozi. Pamoja na uhalisia kwamba Serikali hii ya CCM imekuwa ikiwatumia sana Walimu kutekeleza majukumu yao mengine tofauti na kufundisha kama vile uendeshaji wa sensa ya watu na makazi, uandikishaji wa wapiga kura na usimamizi wa mazoezi ya kupiga na kuhesabu kura lakini baada ya shughuli hizo, Serikali huwa inawasahau kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu wanakabiliwa na changamoto nyingi sana jambo ambalo linakwamisha matamania ya kuinua ubora wa elimu nchini. Tumelisema hili tangu Bunge la Tisa, la Kumi na sasa la Kumi na Moja lakini Serikali haionekani kuzipa kipaumbele changamoto hizo ili kuzitatua. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutatua changamoto zinazowakabili Walimu kama zilivoorodheshwa hapo chini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Vitabu. Mwaka 1991 Serikali ya Tanzania ilitangaza Sera mpya ya Vitabu iliyoruhusu wachapishaji binafsi (*private publishers*) kuchapisha vitabu vya shule na vyuo nchini. Uamuzi huo ulifanyika baada ya miaka mingi ya ukosefu wa vitabu kutokana na kutaifishwa kwa makampuni ya uchapishaji na kuanzishwa kwa mashirika ya umma ya uchapishaji (kama *TPH, EAEPL*) ambayo yalilenga kuchapisha vitabu ambavyo vingemandikwa na Taasisi ya Elimu. Sera hiyo ilipanga majukumu kama ifuatavyo: Wizara ya Elimu kuhusika na sera, mipango na ukaguzi; Taasisi ya Elimu kufanya utafiti, tathmini, kutunga mitaala, mihutisari ya miongozi, kutoa mafunzo juu ya ukuzaji wa mitaala na kudhibiti ubora wa vifaa vya elimu, huku wachapishaji wakiwa na jukumu la kupokea kazi za waandishi, kuchapisha vitabu na kusambaza vitabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera mpya iliyotangazwa na Kamishna wa Elimu kupitia Waraka wa Elimu Namba 4 wa mwaka 2014 inafuta Sera ya mwaka 1991 na kurejesha majukumu ya uandishi na uchapishaji wa vitabu vya shule mikononi mwa Taasisi ya Elimu. Sera hiyo inadai kuwa wachapishaji binafsi wanaweza kuchapisha vitabu vya ziada ambavyo vinaitwa *reference books*. Inasemekana vitabu hivyo vipya vya Taasisi ya Elimu havifai na tumesikia kuwa baadhi ya wafanyakazi waliohusika katika usimamizi wa kazi hiyo wamesimamishwa kazi lakini hadi sasa watoto wako madarasani wakisubiri vitabu vipya vya Taasisi ya Elimu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Elimu ina mwelekeo wa ukuzaji mitaala na si kuandika na kuchapisha vitabu. Ilichukua muda mrefu hadi Wizara ya Elimu katika miaka ya 1990 kutambua hivyo. Ni heri Wizara ya Elimu ikabidhi jukumu la uandishi na usambazaji wa vitabu kwa wachapishaji binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kadhia hii ya vitabu kukosekana mashuleni, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza yafuatayo:-

(i) Serikali irejeshe Sera ya Vitabu ya 1991 ambayo ina mafanikio makubwa; na

(ii) Serikali iweke pembeni mitaala mipya ya Taasisi ya Elimu (*Tanzania Institute of Education – TIE*) ya 2016 na badala yake iunde Tume ya Elimu

itakayotathmini Mfumo na Utendaji wa Elimu nchini na kutoa mapendekezo mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa kisiasa unavyoathiri ubora wa elimu nchini. Serikali ya CCM kwa muda mrefu sasa imekuwa na tabia ya kufanya uamuzi wa kisiasa katika masuala ya elimu na kuweka kando utafiti au ushauri wa kitaalamu, jambo ambalo limeathiri sana ubora wa elimu nchini. Mifano iko mingi lakini nitoe michache. Mfano mwaka 2014, Serikali ya CCM iliwashusha Walimu Wakuu wa Shule mbalimbali za Sekondari za Serikali nchini na nafasi zao za ukuu wa shule eti kwa sababu walifunga shule kutokana na ukosefu wa chakula uliosababishwa na wazabuni wa chakula mashuleni kushindwa kusambaza vyakula hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine ni kuhusu matokeo ya kidato cha nne mwaka 2012 yaliyokuwa mabaya kuliko matokeo yoyote kutokea hapa nchini ambapo zaidi ya asilimia 95 walipata daraja la 0 na IV. Hali hii ilipelekea Serikali kufanya *standardization* pamoja na upangaji wa matokeo kutoka madaraja kwenda GPA. Jambo hili halikukubalika siyo tu na Kambi Rasmi ya Upinzani bali hata kwa wadau mbalimbali wa elimu. Leo hii baada ya kelele nyingi za wadau wa elimu Serikali imerudi tena kwenye utaratibu wa zamani wa madaraja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kuionya Serikali kuacha siasa katika masuala muhimu kama ya elimu kwani yanachangia sana katika kuporomoka kwa elimu nchini. Aidha, ili kuondokana na maamuzi ya kisiasa kwenye elimu, tunarudia kupendekeza tena kwamba Serikali ianzishe Chombo cha Udhhibiti wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Tanzania (*Tanzania Education and Training Regulatory Authority - TETRA*) kitakachoweka viwango vya ubora wa elimu. Haiwezekani Wizara hii ndiyo iwe mtungaji wa sera, iwe mtoaji wa elimu, iwe mdhibiti wa elimu, iwe mtungaji na msahihishaji wa mitihani huku ikiwa pia mmiliki wa baadhi ya shule, haki itatoka wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mkanganyiko uliopo kuhusu ada elekezi na katazo la Serikali la kuongeza ada kwa shule zisizo za Serikali kwa mwaka wa masomo 2016, zipo baadhi ya shule zisizo za Serikali zimeendelea kuongeza ada kwa mwaka huu wa masomo 2016 na kwenda mbali zaidi kuwatoza wazazi faini ya hadi shilingi laki moja kwa kuchelewa kulipa ongezeko hilo ndani ya siku saba. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa kwamba shule ya awali ya *Al Muntazir Union Nusery School* ya Dar es Salaam imeongeza ada kutoka shilingi milioni 1.5 mwaka 2015 hadi kufikia milioni 1.98 mwaka 2016 sawa na ongezeko la shilingi 400,000/=. Aidha, shule ya msingi ya

*Al Muntazir Boys Primary School* ya Dar es Salaam imeongeza ada kutoka shilingi 1.8 million mwaka 2015 hadi shilingi milioni 2.4 mwaka huu sawa na ongezeko la shilingi 460,000/= Pamoja na barua mbalimbali zilizoandikwa na Katibu Tawala pamoja na Kamishna wa Elimu bado shule hiyo imeendelea kutoza ada hiyo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa msimamo wake kuhusu katazo lake na ongezeko la ada kwa shule zisizo za Serikali na namna inavyosimamia utekelezaji wa agizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, upangaji wa bajeti ya Wizara ya Elimu. Kumekuwa na changamoto ya muda mrefu ya upangaji wa matumizi katika sekta ya elimu. Mara zote upangaji wa bajeti ya sekta umeshindwa kuzingatia uwiano unaokubalika kati ya matumizi ya kawaida na yale ya maendeleo. Uchambuzi wa bajeti ya Wizara unaonesha kuwa kati ya shilingi bilioni 897 za bajeti ya Wizara zilopangwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo, shilingi bilioni 427 ambazo ni sawa na asilimia 47.6 zimepangwa kwa ajili ya kugharamia mikopo ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, athari ya kupanga fedha za mikopo katika bajeti ya maendeleo ili bajeti ya maendeleo inaonekane kuwa kubwa lakini kimsingi fedha inayokwenda kutekeleza miradi halisi ya maendeleo ni kidogo sana na hivyo kutokidhi mahitaji. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji kama mkopo wa mafunzo ni uwekezaji kwa nini bajeti za mafunzo ya maafisa wa Wizara (*training domestic na training outside*) yako kwenye bajeti ya matumizi ya kawaida? Mafunzo kwa ajili ya Walimu 7,000 wa sayansi na lugha katika kasma 4001 ya SEDP yako katika bajeti ya matumizi ya kawaida. Kwa nini bajeti ya mafunzo ya Program 20 kasma ndogo 2001 ambayo ni shilingi bilioni 3.9 na Program 70 yako kwenye bajeti ya matumizi ya kawaida? Upangaji huu wa bajeti ni kushindwa kuwa na msimamo unaowiana na hii husababisha miradi mingi ya maendeleo katika sekta ya elimu kutotekelezwa kama vile ukarabati wa shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto za kibajeti za ukaguzi. Ni dhahiri kwamba moja ya sababu zinazochangia kushuka kwa viwango vya ubora na ufaulu katika shule zetu za umma ni kutokuwepo kwa ukaguzi na ufuatiliaji. Kwa mujibu wa Takwimu za Elimu Tanzania (*BEST 2015*) ni asilimia 19.1 tu ya shule za msingi na asilimia 21.4 ya shule za sekondari ndizo mbazo hukaguliwa kwa mwaka. Hii inamaanisha kwamba Serikali huchukua takriban miaka mitano kukamilisha ukaguzi wa shule zote za umma zilizopo. Kwa maneno mengine ni kwamba shule hukaguliwa mara moja kila baada ya miaka mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika bajeti ya mwaka huu pamoja na kwamba inaonekana Kitengo cha Ukaguzi kimetengewa shilingi bilioni 24.1 lakini fedha hizo zinakwenda katika matumizi ya kawaida, inabaki

shilingi bilioni 2 pekee ndiyo inayokwenda kwenye ukaguzi. Kambi ya Upinzani inauliza, je, shilingi bilioni 2 zitatoshwa kweli ukaguzi kwa nchi nzima? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wa utekelezaji wa Sera Mpya. Itakumbukwa kwamba sekta ya elimu sasa inasimamiwa na Sera Mpya ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 iliyoinduliwa Februari 2015 na kuanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2015/2016. Katika sera hii, Serikali imeazimia kutekeleza pamoja na mambo mengine utoaji elimu msingi na sekondari bila ada, kuongeza ubora wa elimu kwa kuimarisha ukaguzi shuleni, kuboresha miundombinu na kuhakikisha kuna upatikanaji wa vifaa stahili vya kujifunzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Sera hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi inahitaji itengenezewe miongozo (*guidelines*) na mpango wa utekelezaji. Hata hivyo, pamoja na kwamba baadhi ya matamko ndani ya sera hii yamekwishaanza kufanyiwa kazi, mfano utoaji elimu bure lakini bado mpango wa utekelezaji wa sera hii haujakamilika mpaka hivi sasa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya Bunge lako ni kwa nini mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Elimu haujakamilika na kuanza kutumika hadi leo huku baadhi ya matamko yakiwa yameanza kutekelezwa? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi waliohamishwa kutoka vyuo vya St. Joseph. Kwa muda mrefu Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliomba Serikali kuhamisha vijana hao kutokana na mazingira mabovu ya kujifunzia na kufundishia. Hii ni pamoja na ukosefu wa Walimu wenye sifa na programu zisizo na ulinganifu na vyuo vingine. Nilifuatilia jambo hili hadi kufanya ziara katika vyuo hivi na kujionea hali mbaya isiyokubalika. Baada ya kupiga kelele nyingi humu Bungeni, Naibu Waziri wa wakati huo Mama Anne Kilango aliahidi kwenda pamoja na TCU kuona hali halisi katika vyuo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kustaajabisha ni kwamba alituletea ripoti ya hovyoyao na ya kisiasa zaidi na kusema kuwa hali ni shwari lakini jambo linaloshangaza zaidi ni kwamba leo wanafunzi wale wamehamishwa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa majibu ya kina ni kwani nini mwaka jana watendaji wa TCU na wa Wizara walisema hakuna tatizo na watendaji hao hao mwaka huu wameona kuna tatizo la msingi na kuwahamisha wanafunzi hao? Je, wanafunzi hao watalipwa nini kwa muda waliopoteza na ni nini hatma ya vyuo hivyo? Jambo linalonikera zaidi ni baadhi ya vijana hawa sasa wamekwama kwenye vyuo walivyohamia kwa kuwa kozi walizokuwa wanasoma zinatofautiana na pia kutokana na kuwa na mihula tofauti, wengi wao wamelazika kurudia mwaka wa masomo au semester. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha Waziri wa Elimu kuvunja Bodi ya TCU, jana tarehe 25 Mei, 2016 kutokana na kudahili wanafunzi wasio na sifa

kujiunga vyyo vikuu siku moja kabla ya mjadala wa hotuba yake ya bajeti, ni kujaribu kwa hila kulizuia Bunge kujadili kwa kina udhaifu mkubwa wa Serikali kupitia TCU katika kusimamia ubora wa elimu hapa nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili ni hatua gani za ziada zitachukuliwa kwa wajumbe hao wa Bodi kwa kuwa wamewaharibia wanafunzi maisha yao na kupoteza fedha za umma kutokana na maamuzi yao mabovu! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Maboresho ya Mfumo wa Elimu Nchini; kwa muda mrefu sana Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikitoa angalizo kuwa mfumo wetu wa elimu umepitwa na wakati. Hivyo, upitiwe upya na kufanyiwa marekebsho ili uendane na mabadiliko yanayotokea katika nyanja mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa matatizo yanayoikumba sekta ya elimu hapa nchini yamekuwa yakijirudiarudia na kwa kuwa mara kadhaa Serikali imekuwa ikifanya maamuzi ya kisiasa zaidi kukabiliana na changamoto inayoikumba zaidi ya kitaalam; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kwa hatua ya sasa kuunda Tume ya Kitaalam kwa ajili ya kupitia upya mfumo wetu wa elimu inayotolewa Tanzania ili pamoja na kukuza ubora wake, lakini pia elimu hiyo iweze kwenda sambamba na kasi ya mabadiliko ya kiuchumi duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dhana ya Ugatuzi Kamili wa Madaraka; katika utekelezaji wa dhana ya ugatuzi, yaani *D by D*, huduma nyingi za kijamii zikiwemo afya, elimu zimeshushwa katika ngazi ya Serikali za Mitaa. Pamoja na utaratibu huo kutajwa kuwa una tija na nia njema kwa wananchi, lakini utaratibu huo umeleta mkanganyiko mkubwa sana katika usimamizi wa Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuona matatizo ya ugatuzi hapa nchini, niliamua kusoma vitabu vingi vinavyohusu dhana ya ugatuzi na nimegundua kuwa Tanzania kimsingi haitekelezi kabisa dhana ya *D by D*, bali tunachokifanya ni *D by C*, yaani *Decentralization by Deconcentration* na ndio maana mambo hayaendi. Hivyo, basi nashauri serikali isome vitabu vinavyoelezea dhana hii kwa kina ili waelewe undani wake na kuweza kuitekeleza. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ubunifu katika Sayansi; hakuna Taifa duniani lililoendelea bila kuwekeza kwenye sayansi na teknolojia. Mageuzi ya sayansi na teknolojia yanaleta hamasa na ubunifu, pamoja na kuvutia zaidi ushiriki wa sekta binafsi katika kuendeleza sayansi na teknolojia na ubunifu. Ni wazi mageuzi haya yanahitaji fedha nyingi hasa za utafiti!



Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kusikitisha ni kwamba, Serikali haitoi fedha kwa ajili ya utafiti. Kwa mfano, bajeti ya 2015/2016, sekta hii ilikuwa na upungufu mkubwa na hata baada ya agizo la tengeo la asilimia moja ya pato ghafi la Taifa (*GDP*). Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze ni kiasi gani cha pato ghafi la Taifa limetengwa kwa ajili ya utafiti katika bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Inasikitisha sana kuona *COSTEC*, ambacho ni chombo pekee cha kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu utafiti, sayansi na teknolojia, kilichoanzishwa na Sheria Namba 7 ya mwaka 1986, lakini bado Serikali haijaweza kuipata Tume hii angalau asilimia moja ya pato ghafi la Taifa. Mathalani kwa mwaka huu, Tume imetengewa asilimia 0.04 tu ya Bajeti yote ya Serikali. Halafu tunategemea nchi itaendelea kwa utaratibu huu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuipa kipaumbele Tume hii ili iweze kufanya tafiti zake na kusaidia taasisi nyingine zilizo chini yake. Haiwezekani kasma 8001 inayohusu Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ipate asilimia nne tu ya bajeti ya Wizara. Ndiyo sababu inayopelekea wabunifu kushindwa kuendeleza ubunifu wao na hivyo kuishia mitaani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika; Marejesho Kandamizi ya Mikopo; Bodi ya mikopo imeweka kiwango cha adhabu kwa wanaochelewa kurejesha mikopo (*penalty amount*) na kiwango cha kulinda kuporomoka kwa thamani ya shilingi (*retention of value charges*). Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haikubaliani kabisa na kiwango kilichowekwa na Bodi cha kulinda kuporomoka kwa thamani ya shilingi (*value retention*) ya takriban asilimia 50 ya deni lote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama jedwali linavyoonyesha hapo chini, linaonesha kabisa ni jinsi gani vijana wetu wanakandamizwa na Sheria hii. Kwa hiyo, tunaomba kabisa, hii *Value Retention fee*, ifutwe ili kufanya vijana wetu waweze kurejesha mikopo wao, lakini vile vile, izingatie ajira nayo ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Unyanyasaji wa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu Wanaohisiwa Kuunga Mkono Upinzani; kumekuwapo na tabia mbaya sana ya baadhi ya Wakuu wa Vyuo hapa nchini kuwanyanyapaa na kuwadhalilisha na hata kudiriki kuwafukuza chuoni wanafunzi ambao kwa hisia zao wanafikiri wanaunga mkono harakati za Vyama vya Upinzani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa kwamba, aliyekuwa kiongozi wa Serikali ya Wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Dodoma amesimamishwa masomo kwa hisia tu kuwa mfuasi wa CHADEMA. Aidha, aliyekuwa Makamu wake, tena msichana, aliamriwa na uongozi wa



chuo hicho kukabidhi madaraka yake, kwa uongozi mwingine wa Serikali ya Wanafunzi ambao haukuchaguliwa na wanafunzi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanafunzi huyu ambaye ni msichana alitakiwa kupongezwa na uongozi wa chuo kwa kuthubutu kugombea nafasi hiyo na kuonesha uwezo mkubwa wa uongozi, lakini alisakamwa na uongozi wa chuo na kutishiwa maisha. Naamini Wakuu wa wako hapa na wananisikia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hukumu imetoka na binti ameshinda, lakini bado utawala wa chuo umedharau amri ya mahakama ya kumrejesha na kumpa ushirikiano. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya Bunge lako Tukufu ni kwa nini haijamchukulia Mkuu wa Chuo hicho cha Dodoma hatua za kinidhamu kwa kuendeleza unyanyapaa na unyanyasaji wa wazi kwa wanafunzi wa chuo hicho kwa hisia tu kwamba wanafunzi hao wanatoka UKAWA. Hii ina maana kwamba UDOM ni kwa ajili ya wanafunzi wa CCM? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Utumishi wa Walimu; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa muda mrefu imezungumzia suala zima la uanzishaji wa Tume ya Utumishi wa Walimu, lakini Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuwaarifu Walimu wote kwamba Serikali ya CCM haijawahi kuwa na nia ya dhati ya kutatua kero zake, ila inakaa na Walimu kimkakati tu kwa malengo ya kubembebeza kura zao na wakishapiga kura hizo matatizo yanaendelea kubaki palepale. Ndiyo maana hadi leo pamoja na Tume hiyo ya Utumishi wa Walimu kutengewa fedha bado wajumbe hawajateuliwa ikiwa ni miezi tisa tangu ianzishwe.

Pili, vifungu vingi vya Sheria hiyo ni vya muundo wa majukumu ya Tume hiyo pamoja na makatazo na adhabu na haioneshi jinsi gani kero za Walimu zitashughulikiwa. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ilete Bungeni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria hiyo ili vifungu vyote vyenye upungufu viweze kufanyiwa marekebisho ili sheria hiyo iwe na ubora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhamishwa kwa Mafunzo ya Walimu kutoka Kurugenzi ya Walimu Wizarani hadi NACTE; tangu tupate uhuru, nchi hii imekuwa ikifanya mipango na mikakati ya kutoa elimu bora kwa ajili ya wananchi wake. Serikali imekuwa inaweka vyombo au taasisi mbalimbali kuelekeza jukumu la utoaji wa elimu!

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kushangaza ni kuwa, bila utafiti wowote wa kisayansi wala ushiriki wa wadau wa elimu kwa niaba ya wananchi, mafunzo ya ualimu (*Teachers Education*) yamehamishwa kutoka Kurugenzi ya Ualimu na kupelekwa Mafunzo ya Elimu ya Ufundi (NACTE).

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya kufanya uhamisho huu ni sawa na kuweka mafunzo ya Ualimu kama fani ya ufundi tofauti na Ualimu kama taaluma inayojitegemea kama sheria, uhasibu au ununuzi na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imesikitishwa sana na jambo hili na inaitaka Serikali kutoa majibu mbele ya Bunge hili juu ya maswali yafuatayo:-

Kulikuwa na sababu gani, yaani (*rationale*) ya kuhamisha mafunzo ya walimu toka Kurugenzi ya Mafunzo ya Wizara ya Elimu kwenda NACTE? Je, wadau walihusihwa kwa jambo hili? Kuna mikakati gani iliyowekwa kuhakikisha kuwa ubora wa elimu hautaathirika?

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya jumla, yanaonekana hapo, niende kwenye hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, aliyekuwa Rais wa Marekani, Abraham Lincoln aliwahi kusema, namnukuu;

*"The philosophy of the school room in one generation will be the philosophy of Government in the next", yaani "Falsafa ya elimu inayotolewa darasani kwenye kizazi cha leo ndiyo itakayokuwa hatma ya Serikali yetu ya kesho". Kama tutaendelea kuzalisha wahitimu wanaotokana na elimu duni inayotolewa, iliyogubikwa na maamuzi mabovu ya kisiasa na vitendo vya ufisadi, ni dhahiri kuwa Taifa letu halitaweza kupata viongozi bora wa kuliongoza huko tuendako. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kuchukua hatua za kunusuru elimu yetu ni sasa. Ni lazima tubadilike. Haitawezekana kamwe kutatuliwa na elimu hii duni tuliyopandikiza kwa watoto wetu. Tunahitaji mapinduzi na mageuzi makubwa ya kielimu kuikoa Tanzania hapa ilipo na kuipeleka kwenye *level* nyingine. Suala la kuwa nchi yetu ni ya uchumi wa kati, nchi ya viwanda litaendelea kuwa ni hadithi za Bulicheka ikiwa hatutaondoa upungufu mwingi tulioukabili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia hotuba yangu kwa kusema kwamba, sera ya elimu bure ilianzishwa na CHADEMA. Ipo katika Ilani ya Uchaguzi ya CHADEMA chini ya mwavuli wa UKAWA tangu 2005, 2010 na hatimaye 2015. Lengo lilikuwa ni kutoa huduma ya elimu bure kwa ukamilifu wake kuanzia shule za awali hadi chuo kikuu. Maigizo ya Ilani ya CHADEMA yaliyofanywa na CCM, yameishia kuondoa ada tu na michango...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan Lyimo, dakika mbili umalizie.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ELIMU, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie, Maigizo ya Ilani ya CHADEMA au UKAWA yaliyofanywa na CCM, yameishia kuondoa ada tu na michango midogomidogo ya uendeshaji wa shule hadi kidato cha nne tu, huku kukiwa na sintofahamu kubwa juu ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika shule hizo. Hali inayopelekea kuporomoka zaidi kwa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna msembo usemao: “*If education is expensive, try ignorance*”, yaani kama elimu au kuelimika ni gharama basi jaribu ujinga. Tanzania tumeamua kujaribu ujinga, kwa kutowekeza vya kutosha katika elimu na ndiyo maana elimu yetu imeporomoka na kufikia hapa ilipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Elimu katika Awamu ya Kwanza Marehemu Jackson Makwetta alisema kwamba: “Tanzania ni kama mama mjamzito ambaye siku za kujifungia zimefika, lakini hajifungui. Hivyo Tanzania inahitaji mabadiliko vinginevyo itaendelea kudidimia kielimu na kiuchumi”. Kwa sababu hiyo; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutazama upya mfumo wa elimu wa sasa kwa kuunda Tume Maalum ya kupitia upya na kutoa mapendekezo ili Taifa hili liweze kuwa na mfumo bora wa elimu unaokidhi viwango vya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Mungu ibariki Afrika, Mungu ibariki Tanzania! *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Lyimo. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI  
KATIKA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI  
MHESHIMIWA SUSAN ANSELIM JEROME LYIMO (MB), AKIWASILISHA  
BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU  
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KATIKA  
WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17 KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sote uhai na kutuwezesha kuliona Bunge la 11 tukiwa salama. Pili napenda kumshukuru kwa dhati kabisa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaali Mbowe (Mb) kwa imani kubwa aliyo nayo kwangu kwa kuendelea kuiteua

kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa vipindi vitatu mfululizo. Ninaahidi kuendelea kuchapa kazi kwa bidii, na kwa hakika sitaangusha Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika wajibu huu niliopewa wa kuisimamia Serikali katika sekta ya Elimu nchini.

**Mheshimiwa Spika**, naishukuru familia yangu ikiongozwa na mume wangu Boniventure Ngowi na wanangu wote. Kipekee namshukuru sana Naibu Waziri wangu Dr. Suleiman Ally Yussuf kwa ushauri wake. Vilevile nawashukuru sana BAWACHA Mkoa wa kichama wa Kinondoni kwa kunichagua kuwawakilisha hapa kama kawaida sitawaangusha.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kuwapongeza viongozi wote wakuu wa vyama vinavyounda Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA), kwa kazi kubwa na nzuri walioyoifanya ya kuwaongoza wataanzania kuchagua mabadiliko katika Uchaguzi Mkuu wa tarehe 25 Oktoba 2015.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na ukiukwaji mkubwa wa haki na demokrasia uliofanywa na vyombo vya dola dhidi ya upinzani katika uchaguzi huo, ikiwemo kuvamia, kuwakamata na kuwanyang'anya vifaa vya kazi wataalamu wa UKAWA waliokuwa wakijumlisha matokeo ya uchaguzi huo, bado wananchi walionyesha imani kubwa sana kwa upinzani kwa kuupigia kura nyingi; na kwa mara ya kwanza katika historia ya vyama vingi hapa nchini, upinzani umepata viti 116 ikiwa ni ongezeko la asilimia 23.3 kutoka viti 89 vilivyopatikana katika uchaguzi Mkuu wa 2010.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa kura za rais, licha ya mbinu zote zilizofanywa na vyombo vya dola kuchakachua ushindi wa upinzani, bado upinzani kupitia UKAWA umeongeza kiwango chake cha ushindi hadi kufikia asilimia takriban 40 tofauti na miaka iliyopita. Ushindi huu umetokana na kuporomoka vibaya kwa Chama cha Mapinduzi katika ngazi ya Rais kutoka ushindi wa asilimia 80 mwaka 2005 hadi asilimia 61.17 mwaka 2010 na kufikia asilimia 58 mwaka 2015. Kwa hesabu hizi ni wazi 2020 CCM itakuwa historia kama vile ilivyokuwa kwa chama cha KANU nchini Kenya na vyama vingine katika nchi za kifaraka vilivyoondolewa madarakani kwa kukataliwa na wananchi kutokana na utawala wa ki-imla wa muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika**, kuporomoka huku ni matokeo ya wazi kabisa kuwa chama hiki kimepoteza mvuto kwa wananchi kutokana na kushindwa kuondoa umasikini pamoja na kushindwa kusambaza huduma toshelezi za kijamii hasa elimu na afya kwa miaka yote ya utawala wake wa miaka 55 sasa.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na aibu hii ya kushindwa kuondoa umasikini kwa wananchi; na kutokana na hofu ya Serikali kuhojiwa na bunge kuhusu utendaji wake; sasa Serikali hii ya awamu ya tano inayojinasibu kwa kauli mbiu ya *'hapa kazi tu'* imeamua kulinyamazisha bunge kwa kupiga marufuku vyombo vya habari kurusha moja kwa moja mijadala inayoendelea bungeni kuhusu utendaji wa Serikali na kuhusu mgawanyo wa fedha za umma katika bajeti ya serikali. Aidha, kutokana na hofu ya kukosolewa kutokana na kutojiamini katika mambo inayoyafanya; Serikali sasa imeanza kuingilia hotuba za Wasemaji Wakuu wa Upinzani na kuzifanyia *copyright* kinyume kabisa na Kanuni za Bunge hili.

**Mheshimiwa Spika**, Kanunu ya 99(9) ya Kanuni za Bunge toleo la Januari, 2016, inasema kwamba: *"Baada ya Waziri kuwasilisha hotuba ya bajeti kwa mujibu wa fasili ya kwanza; Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia makadirio husika na Msemaji wa Kambi ya Upinzani watatoa maoni yao kwa muda usiozidi dakika 30 kila mmoja"*. Kanuni haijalelekeza kwamba watatoa maoni yao baada ya kupitiwa na Kamati ya Kanuni. Kwa hiyo Mheshimiwa Spika; kitendo kilichofanyika tarehe 16 Mei, 2016 cha kuiondoa mezani hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili ikachakachuliwe na Kamati ya Kanuni, ni kinyume kabisa na Kanuni za Bunge; na ni kinyume kabisa na mila na desturi za uendeshaji wa mabunge ya Jumuiya ya Madola.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakemea kwa nguvu zote na inaitaka Serikali kuacha mara moja tabia hii ya kuingilia shughuli za kikanuni za Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa kutumia mgongo wa Bunge.

## 2. ELIMU YETU NA HATMA YA TANZANIA

**Mheshimiwa Spika**, dhambi kubwa na mbaya kuliko zote kuwahi kufanywa na Serikali hii ya CCM ni kuwanyima Watanzania elimu bora; kupandikiza elimu nyepesi, potofu na tegemezi kwa vizazi vingi vya taifa hili; dhambi ya kuwachanganya na kuwavuruga watoto wa Taifa hili kwa sera dhaifu, mitaala isiyo na dira na vitabu visivyokuwa na tija kwa maendeleo yao na ya Taifa lao.

**Mheshimiwa Spika**, Nchi yetu ipo hivi ilivyo kwa sababu ya elimu duni. Umaskini, ujinga na maradhi vinavyotesa Taifa hili ni matokeo ya elimu mbovu iliyotolewa na Serikali ya CCM kwa zaidi ya miaka 55 tangu tupate uhuru. Taifa linalotoa elimu bora halifanani hata kidogo na jinsi Tanzania yetu ilivyo.

**Mheshimiwa Spika**, hizi ni zama za kuelezana ukweli, hata mkitufungia humu Bungeni wananchi wasituone 'Live' bado Ukweli utaendelea kupasua kuta za Bunge hili na kuwafikia Watanzania. Mwanafasihi mashuhuri wa nchi yetu, Afrika ya Mashariki na Barani Afrika, Hayati Shaaban Robert, katika kitabu chake cha

KUSADIKIKA aliandika hivi, **"Msema kweli hukimbiwa na Rafiki zake, nikipatwa na Ajali kama hiyo sitawaonea Wivu wale wanaodumu na marafiki zao siku zote. Siwezi kuikana Kweli kwa kuhofia Upweke wa kitambo na kujinyima Furaha ya milele inayokaribia kutokea baada ya kushindwa kwa Uongo"** mwisho wa kunukuu. Maneno haya ndio msimamo wangu na wa Kambi kwa ujumla wake, kwani siku zote wabunge wa Upinzani tumeonekana kama maadui na kunyanyapaliwa na Serikali hii ya CCM kwa sababu kusema ukweli kuhusu madhaifu ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, nchi zilizoendelea zinafanya mambo mengi ya kimaendeleo kwa kuwatumia wataalam wao wa elimu ya juu – University graduates. Wataalam wa vyuo vikuu wanatengenezwa kwa kutegemea pia elimu bora ya msingi na sekondari. Tanzania nayo ina vyuo vikuu. Lakini leo ipo haja ya Bunge hili kujiuliza nini hasa maana ya Chuo kikuu – **"A University is an institution of higher learning where people's minds are trained for clear thinking, for independent thinking, for analysis and for problem solving at the highest level, is the centre for advancing the frontiers of knowledge"**. Kwamba: Chuo Kikuu ni taasisi ya elimu ya juu inayoandaa watu kuwa na fikra pevu, fikra huru kwaajili ya kuwa na uwezo mkubwa wa kiuchambuzi na kwaajili ya kutatua matatizo kwa kiwango cha hali ya juu, ni kituo cha kuendeleza maarifa.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imekuwa na Mawaziri wengi tu waliopita vyuo vikuu, lakini bado wameliingiza Taifa hili kwenye hasara kubwa kwa maamuzi mabovu, kwa kuingia mikataba isiyojali maslahi ya taifa na kwa utendaji usio na ufanisi. Hivi hawa wana-fit kweli kwenye definition hii ya Chuo Kikuu? Ukweli ni kuwa hata Serikali yenyewe haiwaamini wataalam wake wanaozalishwa na vyuo vikuu hasa kwenye Sekta ya Sayansi na Teknolojia. Na hili lipo wazi; leo Tanzania ina madini, gesi na mafuta, lakini watafiti, wachimbaji na wavunaji wakubwa wa rasimali hizi, wenye mashine kubwa na za kisasa, na zenye kutumia teknolojia ya hali ya juu si Watanzania.

**Mheshimiwa Spika**, Mwanafalsafa Herbert Spencer aliwahi kusema, namnukuu **"The great aim of education is not knowledge but action"** – kwamba "lengo kuu la elimu si ufahamu, bali vitendo". Tafiti zinaonyesha ni 39% tu ya wahitimu wa vyuo vikuu wanaajirika kutokana na kile kinachoitwa kukosa ujuzi "lack of skills". Kambi ya Upinzani inauliza hivi ni lini serikali itawekeza vizuri kwenye elimu katika ngazi zote?!!

### 3. BAJETI YA UTEKELEZAJI WA ELIMU BURE

**Mheshimiwa Spika**, kupitia Sera Mpya ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, iliyofuatiwa na Tamko la utekelezaji katika Waraka namba 5 wa Mwaka 2015, imeagiza kufutwa kwa ada za masomo katika shule za sekondari kuanzia Kidato cha 1 –IV na michango ya aina yoyote kwa shule za msingi.



**Mheshimiwa Spika**, Kabla ya agizo hili la elimu bila ada na uchangiaji wa elimu katika shule za umma ulifanywa kwa ushirikiano baina ya serikali pamoja na wazazi. Hata hivyo upatikanaji wa pesa shuleni ulikuwa wa shida. Mathalani serikali iliweza kupeleka wastani wa Tsh. 4,000/= hadi 5,000/= tu kama ruzuku kwa shule za msingi badala ya Tsh 10,000/= zilizotakiwa kwa kila mtoto kwa mwaka. Aidha, Serikali iliweza kutoa wastani wa Tsh 12,000/= hadi 15,000 kwa kila mtoto kwa mwaka kama ruzuku kwa shule za sekondari badala ya 25,000/= zilizostahili (BRN report 2015).

**Mheshimwa Spika**, kwa kuzingatia hali hiyo, ili serikali iweze kugharamia utoaji wa elimu pasipo wazazi kuchangia ni lazima katika mpango wake wa bajeti kuanzia bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/17 itenge kiwango cha fedha kama kugharamia elimu kama ifuatavyo:-

- Shilingi bilioni 161.5 kwa ajili ya ruzuku elimu ya msingi na awali kwa wanafunzi 8,987,031 kwa shilingi 10,000 kila mwanafunzi.
- Shilingi bilioni 40 kwa ajili ya ruzuku elimu ya sekondari kwa wanafunzi 1,575,254 kwa shilingi 25,000 kila mwanafunzi kwa shule za umma.
- Shilingi bilioni 31 kufidia ada ya shilingi 20,000/=kwa kila mwanafunzi katika shule za sekondari za umma kwa wanafunzi 1,575,254.
- Shilingi 198 kufidia program za uji ambazo zilikuwa zinachangiwa na wazazi maana hivi sasa wazazi hawachaji chochote na shule nyingi zimeacha kutoa uji kwa wanafunzi.
- Shilingi bilioni 1,438 kwa ajili ya kutatua changamoto za miundombinu kwa shule za msingi na sekondari kama vile vyoo, madarasa, madawati na ukamilishaji wa maabara za shule ya kata.

**Mheshimiwa Spika**,kwa minajili hiyo, ili kugharamia utoaji elimu bure serikali inapaswa kufidia pesa za ada iliyokuwa ikitolewa na wazazi kwa shule za sekondari na fedha ya gharama za chakula (uji) kwa wanafunzi wa shule za msingi kuanzia darasa la awali mpaka la saba. Serikali pia inapaswa kulipia gharama za uboreshaji na ujenzi wa miundombinu inayohitajika kwa mwaka. Shule nyingi zina mrundikano wa wanafunzi zaidi ya 400 kwa darasa la kwanza walioandikishwa mwaka 2016.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa uchambuzi uliofanywa na Haki Elimu katika jedwali namba 1, 2 na 3 hapo chini, kwa kuzingatia takwimu za idadi ya wanafunzi, shule na mahitaji, kila mwaka serikali itapaswa kutenga kiasi cha fedha kisichopungua shilingi **bilioni 1,797.5 (takriban shilingi trilioni 1.8)** nje ya mahitaji mengine ya kisékta ili kugharamia elimu bila malipo.



**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuhakikisha kiwango hicho kinajumuishwa katika bajeti ya sekta ya elimu ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 ili kutekeleza kwa ufanisi azma yake ya utoaji wa elimu bure, vinginevyo utakuwa ni usanii mtupu, na dhana ya elimu bure inaweza kuwa chanzo kingine cha anguko kuu la ubora wa elimu nchini.

**Jedwali 1: Gharama za kufidia ada na ruzuku shuleni kwa ajili ya vifaa, gharama za mitihani na gharama za uendeshaji**

	Kiasi (Tshs)	Idadi ya wanafunzi	Jumla
Msingi	10,000	8,987,031	Bil. 90
Sekondari	25,000	1,575,254	Bil. 40
Ada Sekondari	20,000	1,575,254	Bil. 31.5
<b>Jumla ya Ruzuku Msingi na Sekondari</b>			<b>Bil 161.5</b>

Chanzo: (BEST 2015)

**Jedwali 2: Gharama za kufidia ujenzi wa miundombinu uliokuwa ukichangiwa na wazazi**

	Upungufu	Gharama (Tshs)	Jumla
Madawati	1,170,827	80,000	Bil.90
Matundu ya vyoo	150,000	1,000,000	Bil. 150
Madarasa	95,945	12,000,000	Bil.1,150
Maabara	Shule 1,560	30,000,000	Bil. 47
<b>Jumla kuu ya gharama za kufidia ujenzi wa miundombinu</b>			<b>Bil.1,438</b>

Chanzo: (BEST 2015)

**Jedwali 3: Gharama za kufidia utoaji uji shuleni**

<b>Watoto wa darasa la awali</b>			
Bei ya Uji kwa siku	Siku za Masomo	Idadi ya wanafunzi	Jumla
Sh. 100	198	992,356	Bil 20
<b>Wanafunzi wa msingi (Darasa la I – VII)</b>			
Sh.100	198	8,987,031	Bil. 178
<b>Jumla ya fidia utoaji uji shule za awali na msingi</b>			<b>Bil 198`</b>
<b>Jumla Kuu</b>			<b>Bil 1,797.5</b>

#### 4. CHANGAMOTO ZINAZOWAKABILI WALIMU NCHINI

**Mheshimiwa Spika;** Elimu bora inategemea sana morali ya walimu na sio madawati au madarasa yenye viyoyozi. Pamoja na uhalisia kwamba Serikali hii ya CCM imekuwa ikiwatumia sana walimu kutekeleza majukumu mengine tofauti na kufundisha kama vile uendeshaji wa sensa ya watu na makazi; uandikishaji wa wapiga kura na usimamizi wa mazoezi ya kupiga na kuhesabu kura, lakini baada ya shughuli hizo, Serikali huwa inawasahau kabisa.

**Mheshimiwa Spika,** walimu wanakabiliwa na changamoto nyingi sana jambo ambalo linakwamisha matamano ya kuinua ubora wa elimu nchini. Tumelisema hili tangu bunge la tisa, bunge la kumi na sasa bunge la kumi na moja lakini Serikali haionekani kuzipa kipaumbele changamoto hizo ili kuzitatua.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutatua changamoto zinazowakabili walimu kama ifuatavyo:

- i. Kuongeza posho ya kufundishia kwa walimu ili kufidia muda wa mwalimu kufanya kazi kwani ualimu ndio kada pekee inayofanya kazi kwa saa 24 hasa nyakati za kutunga na kusahihisha mitihani, kupanga matokeo n.k.
- ii. Kujenga vyumba vya madarasa vya kutosha na kuviwekea samani za kutosha ili kupunguza mlundikano wa wanafunzi darasani na hivyo kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunza.
- iii. Kuwapandisha madaraja kwa wakati sambamba na kuwapandishia mishahara walimu waliokidhi vigezo vya kupandishwa madaraja ili kuwapa motisha wa kufundisha.
- iv. Kuwe na chombo kimoja cha ajira kwa walimu, na kwa maana hiyo; Tume ya Walimu ianze mara moja kazi ya kutatua kero za walimu.
- v. Muda wa mafunzo kwa vitendo (BTP) kwa walimu uzingatiwe ili walimu-wanafunzi waweze kupata uzoefu wa kutosha wa kufundisha kuliko inavyofanyika hivi sasa ambapo mafunzo hayo yanafanyika chini ya wiki nane kila mwaka.
- vi. Serikali ishughulikie kero ya Walimu wanaostaafu na kutolipwa stahiki zao mapema na pia kutorudishwa makwao kwa mujibu wa kanuni za utumishi.
- vii. Serikali iwalipe walimu posho ya mazingira magumu ya kazi ili kuvutia kufanya kazi maeneo ya vijijini.
- viii. Ajira mpya ziingizwe kwenye payroll mapema ili kuondoa kero ya kucheleweshwa kwa maslahi ya walimu kutokana na majina yao kutokuwepo kwenye payroll.

## 5. SERA YA VITABU

### **Mheshimiwa Spika,**

Mwaka 1991 Serikali ya Tanzania ilitangaza sera mpya ya vitabu iliyoruhusu wachapishaji binafsi (private publishers) kuchapisha vitabu vya shule na vyuo nchini. Uamuzi huo ulifanyika baada ya miaka mingi ya ukosefu wa vitabu kutokana na kutaifishwa kwa makampuni ya uchapishaji na kuanzishwa kwa mashirika ya uma ya uchapishaji (km TPH, EAEPL) ambayo yalilenga kuchapisha vitabu ambavyo vingehandikwa na Taasisi ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, Uamuzi huo wa kuondokana na dhiki na mahangaiko ya kukosekana kwa vitabu vya shule uliwekewa utaratibu maalumu wa utekelezaji ukiratibiwa na kitengo cha Book Management Unit (BMU), makao makuu ya Wizara ya Elimu. Baadae Wizara ya Elimu iliunda kitengo cha kudhibiti ubora wa vitabu kiitwacho, Educational Materials Approval Committee (EMAC).

**Mheshimiwa Spika,** Tangu 1991 wachapishaji wazalendo wamepiga hatua kubwa katika fani hii. Wanachapisha vitabu bora vya kiada vya ngazi zote za elimu. Tatizo la kutokuwapo kwa vitabu vya kiada halipo tena. Tatizo sasa ni kwamba serikali hainunui vitabu vya kutosha na kwa muda. Pia wachapishaji wanachapisha vitabu vya hadithi mbalimbali kwa ajili ya watoto wa ngazi zote za msingi na sekondari – hususan chini ya CBP kwa mfano kuna aina za vitabu (titles) zisizopungua 350 za vitabu vya hadithi na rejea pale CBP. Pia wachapishaji hao wametoa machapisho mengine kama kamusi, atlas, chati mbalimbali, n.k.

### **Sera mpya ya vitabu ya mwaka 2014**

Mheshimiwa Spika, Sera mpya iliyotangazwa na Kamishna wa Elimu kupitia Waraka wa Elimu Namba 4 wa mwaka 2014 inafuta sera ya Serikali ya vitabu ya mwaka 1991 na kurejesha majukumu ya uandishi na uchapishaji wa vitabu vya shule mikononi mwa Taasisi ya Elimu. Sera hiyo inadai kuwa wachapishaji binafsi wanaweza kuchapisha vitabu vya ziada – ambavyo anaviita ‘reference books’.

**Mheshimiwa Spika,** Mwaka jana (2015) Taasisi ya Elimu iliendesha semina kwa walimu wakuu wa shule za msingi nchini kote kuhusu ufundishaji unaotekeleza mitaala mipya hususan darasa la kwanza na la pili kwa utaratibu wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). Walimu waliopewa semina waliahidiwa kupatiwa vitabu vipya vinavyokidhi mitaala mipya mwezi Januari au Februari 2016 ili waanze kuvitumia

madarasani. Shule zimesubiri vitabu hivyo hadi sasa, karibu nusu ya mwaka, bila kupatiwa vitabu hivyo.

**Mheshimiwa Spika**, Inasemekana vitabu hivyo vipya vya Taasisi ya Elimu havifai. Pia tumesikia kuwa baadhi ya wafanyakazi waliohusika katika usimamizi wa kazi hiyo wamesimamishwa kazi. Lakini hadi sasa watoto wako madarasani wakisubiri vitabu vipya vya Taasisi ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, *Mwandishi* ni msanii kama alivyo mchoraji, mwimbaji, mchezaji wa ngoma au mwigizaji. Kundi hili lina watu wenye vipaji maalumu. Uandishi siyo kazi anayoamriwa au kupangiwa mtu kuifanya ila naifanya kwa utashi wake. Pia haitegemei elimu ya mtu, kwa mfano, Shaaban Robert alikuwa na elimu ya darasa la IV tu lakini aliandika vitabu vilivyo bora sana ambavyo vinatumika hadi vyuo vikuu.

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Elimu ina mwelekeo wa *ukuzaji mitaala* na siyo kuandika na kuchapisha vitabu. Ilichukua muda mrefu hadi Wizara ya Elimu ya miaka ya 1990 kutambua hivyo. Ni heri Wizara ya Elimu ikabidhi jukumu la uandishi na usambazaji wa vitabu kwa wachapishaji binafsi.

**Mheshimiwa Spika, Kutokana na kadhia hii ya vitabu kukosekana mashuleni**, Kambi rasmi ya Upinzani inapendekeza yafuatayo:

(a) Serikali irejeshe Sera ya Vitabu ya 1991 ambayo ina mafanikio makubwa

(b) Serikali iweke pembeni mitaala mipya ya TIE ya 2016 na badala yake iunde Tume ya Elimu itakayotathmini Mfumo na Utendaji wa Elimu nchini na kutoa mapendekezo mapya

(c) Vitabu vilivyopo tangu mfumo mpya wa elimu wa 1991, viendeele kutumika shuleni hadi tume imalize kazi yake.

## 6. UAMUZI WA KISIASA UNAVYOATHIRI UBORA WA ELIMU NCHINI

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ya CCM kwa muda mrefu sasa imekuwa na tabia ya kufanya uamuzi wakisia katika masuala ya elimu na kuweka kando utafiti au ushauri wa kitaalamu jambo ambalo limeathiri sana ubora wa elimu nchini.

**Mheshimiwa Spika**, mifano iko mingi; kwa mfano mwaka 2014, Serikali ya CCM iliwashusha walimu wakuu wa shule mbalimbali za Sekondari za Serikali nafasi zao za ukuu wa shule eti kwa sababu walifunga shule kutokana na ukosefu wa chakula uliosababishwa na wazabuni wa chakula mashuleni kushindwa kusambaza vyakula kutokana na ukosefu wa fedha kwa kuwa Serikali ilikuwa haiwalipi wazabuni hao.

**Mheshimiwa Spika**, mfano mwingine ni kuhusu matokeo ya kidato cha nne mwaka 2012 yaliyokuwa mabaya kuliko yote kutokea ambapo zaidi ya asilimia 95 walipata daraja la 0 na IV. Hali hii ilipelekea Serikali kufanya **'standardization'**, uamuzi ambao kimsingi ulikuwa ni wa kisiasa ili kuwafurahisha wanafunzi na wazazi ili waendeleo kuipigia kura CCM. Haikuishia hapo, Serikali baadaye ikapanua magoli kwa kubadili mfumo wa upangaji wa matokeo kutoka madaraja (division) kwenda GPA (wastani). Jambo hili halikukubalika sio tu na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni bali hata wadau mbali mbali wa elimu. Leo hii baada ya kelele nyingi za wadau wa elimu; Serikali imerudi tena kwenye utaratibu wa zamani wa madaraja.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kuionya Serikali kuacha siasa katika masuala muhimu kama ya elimu kwani yanachangia sana katika kuporomoka kwa elimu nchini. Aidha, ili kuondokana na maamuzi ya kisiasa kwenye elimu, tunarudia kupendekeza tena kwamba Serikali ianzishe chombo cha udhibiti wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi (Tanzania Education and Training Regulatory Authority - TETRA) kitakachoweka viwango vya ubora wa elimu kwa mujibu wa mitaala iliyopitishwa na Serikali, kudhibiti utungaji, usahihihaji na upangaji wa matokeo ya mitihani, kudhibiti gharama za elimu (ada na michango mingine) baina ya shule na taasisi nyingine za elimu za uma na binafsi ili kuwa na mfumo mmoja wa elimu unaoeleweka kuliko sasa ambapo kuna tofauti kubwa za kinfumo baina ya shule na taasisi za elimu binafsi na zile za umma. Haiwezekani Wizara hii iwe ndio mtungaji ya sera elimu, mtoaji wa elimu, mdhibiti wa elimu, mtungaji na msahihihaji mitihani huku ikiwa pia mmiliki wa baadhi ya shule. Haki itatoka wapi?!!

## **7. UKIUKAJI WA KATAZO LA SERIKALI LA KUONGEZA ADA KWA SHULE ZISIZO ZA SERIKALI KWA MWAKA WA MASOMO 2016**

**Mheshimiwa Spika**; Pamoja na mkanganyiko uliopo kuhusu ada elekezi na katazo la Serikali la kuongeza ada kwa shule zisizo za Serikali kwa mwaka wa masomo 2016, zipo baadhi ya shule zisizo za Serikali zimeendelea kuongeza ada kwa mwaka huu wa masomo 2016 na kwenda mbali zaidi kuwatoza wazazi faini ya hadi shilingi laki moja kwa kuchelewa kulipa ongezeko hilo ndani ya siku saba.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa kwamba shule ya awali ya AL MUNTAZIR UNION NUSERY SCHOOL ya Dar es Salaam imeongeza ada kutoka shilingi 1,580,000/= mwaka 2015 hadi kufikia shilingi 1,980,000/= mwaka 2016 sawa na ongezeko la shilingi 400,000/=. Aidha, shule ya msingi ya AL MUNTAZIR BOYS PRIMARY SCHOOL ya Dar es Salaam imeongeza ada kutoka shilingi 1,820,000/= mwaka 2015 hadi shilingi 2,480,000/= mwaka 2016 sawa na ongezeko la shilingi 460,000/=

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na barua mbalimbali zilizoandikwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar na Kamishna mwenyewe ambayo kopi yake tunayo bado shule hii imeendelea kukaidi. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua, hii shule ya AL MUNTAZIR inapata wapi nguvu ya kukaidi maagizo ya Serikali waziwazi? sambamba na hilo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa msimamo wake kuhusu katazo lake la ongezeko la ada kwa shule zisizo za Serikali, na namna inavyolisimamia utekelezaji wa agizo hilo.

## 8. UPANGAJI WA BAJETI YA WIZARA YA ELIMU

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na changamoto ya muda mrefu ya upangaji wa matumizi katika sekta ya elimu. Mara zote upangaji wa bajeti ya sekta umeshindwa kuzingatia uwiano unaokubalika kati ya matumizi ya kawaida na yale ya maendeleo. Uchambuzi wa bajeti ya wizara unaonesha kuwa kati ya **shilingi bilioni 897.6** za bajeti ya Wizara zilopangwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo, **shilingi bilioni 427.5** ambazo ni sawa na asilimia 47.6% zimepangwa kwa ajili ya kugharamia mikopo ya elimu ya juu.

**Mheshimiwa Spika**, athari ya kupanga fedha za mikopo katika bajeti ya maendeleo ili bajeti ya maendeleo inaonekane kuwa kubwa lakini kimsingi fedha inayokwenda kutekeleza miradi halisi ya maendeleo ni kidogo sana na hivyo kutokidhi mahitaji.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji, kama mkopo wa mafunzo ni uwekezaji kwa nini bajeti za mafunzo ya maofisa wa Wizara (Training domestic na Training outside) yako kwenye bajeti ya Matumizi ya Kawaida? Mafunzo kwa ajili ya walimu 7000 wa sayansi na lugha katika kasima 4001 ya SEDP yako katika bajeti ya matumizi ya kawaida. Kwa nini bajeti ya mafunzo ya Program 20 kasima ndogo 2001 ambayo ni shilingi bilioni 3.9 na Program 70 kasima ndogo 7001 yako kwenye bajeti ya matumizi ya kawaida? Upangaji huu wa bajeti ni kushindwa kuwa na msimamo unaowiana na hii husababisha miradi mingi ya maendeleo katika sekta ya elimu kutotekelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwa na vigezo vya bajeti ya maendeleo katika wizara hii tofauti na ilivyo sasa ambapo fedha zinazoonekana dhahiri kuwa ni za matumizi ya kawaida zinawekwa kwenye bajeti ya maendeleo ili bajeti iungwe mkono wakati ki-uhalisia hakuna maendeleo yenye tija yatakayofanyika kutokana na upungufu mkubwa wa fedha za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kama Serikali inadai kwamba mikopo ya elimu ya juu ni fedha za maendeleo kwa kigezo kwamba huo ni uwekezaji kwenye maendeleo ya rasilimali watu; basi isiwadai wanafunzi wanaopewa fedha hizo kugharamia

elimu ya juu kwa kuwa ni uwekezaji kama uwekezaji mwingine wa miradi ya maendeleo ambayo serikali hugharamia bila kudai kurudishiwa fedha hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haioni sababu ya Serikali kuwadai wahitimu wa vyuo vikuu kurejesha fedha waliyokopeshwa kugharamia elimu waliyoipata kwa sababu gharama hiyo wataifidia kupitia kodi ya mapato (Pay As You Earn) pindi watakapojiriwa. Kodi hiyo itakuwa ndio faida (economic returns) ya kuwalipia wanafunzi wa elimu ya juu ambayo inachangia moja kwa moja kwenye pato la taifa na uchumi kwa jumla. Serikali itambue pia kwamba fedha inazowakopesha wanafunzi wa elimu ya juu inatokana pia na kodi waliyolipa wazazi wa wanafunzi hao.

## **9. CHANGAMOTO ZA KIBAJETI ZA UKAGUZI NA UHAKIKI WA UBORA WA ELIMU NCHINI.**

**Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kwamba moja ya sababu zinazochangia kushuka kwa viwango vya ubora na ufaulu katika shule zetu za umma ni kutokuwepo kwa ukaguzi na ufuatiliaji. Kwa mujibu wa Takwimu za Elimu Tanzania (BEST 2015) ni asilimia 19.1 tu ya shule za msingi na asilimia 21.4 pekee ya shule za sekondari ambazo hukaguliwa kwa mwaka.

**Mheshimiwa Spika**, tafsiri ya takwimu hizo ni kwamba, serikali huchukua takribani miaka mitano kukamilisha ukaguzi wa shule zote za umma zilizopo. Kwa maneno mengine ni kwamba, shule hukaguliwa mara moja kila baada ya miaka mitano!

**Mheshimiwa Spika**, kwa mfano, katika bajeti ya Mwaka 2016/2017, jumla ya **shiligi bilioni 24.1** zimetengwa kwa ajili ya idara ya ukaguzi na vitengo vyake kwa ajili ya matumizi ya kawaida lakini takribani **shilingi bilioni 22** zimetengwa kwa ajili ya mishahara na maslahi mengine ya watumishi katika matumizi ya kawaida. Hivyo kiasi cha takribani **shilingi bilioni 2** pekee ndicho kilichobaki kwa ajili ya shughuli halisi za ukaguzi kama ununuzi wa mafuta ya gari, posho za wakaguzi, ukarabati wa magari, mawasiliano na programu za mafunzo au uelimishaji.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuona umuhimu wa ukaguzi na uhakiki wa ubora wa elimu na hivyo kutenga fungu rasmi katika mwaka mpya wa fedha 2016/17 lenye fedha za kutosha kukagua angalau asilimia 80 ya taasisi za elimu zinazostahili kukaguliwa hapa nchini.

## **10. MWONGOZO WA UTEKELEZAJI WA SERA MPYA YA ELIMU**

**Mheshimiwa Spika**, Itakumbukwa kwamba sekta ya elimu sasa inasimamiwa na Sera Mpya ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, iliyozinduliwa Februari 2015 na



kuanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2015/2016. Katika sera hii serikali imeazimia kutekeleza, pamoja na mambo mengine; utoaji elimu msingi na sekondari bila ada, kuongeza ubora wa elimu kwa kuimarisha ukaguzi shuleni, kuboresha miundombinu na kuhakikisha kuna upatikanaji wa vifaa stahili vya kujifunza na kufundishia pamoja na kuongeza ubora wa walimu kwa kutoa mafunzo, motisha na kuimarisha udhibiti wa taaluma ya ualimu.

**Mheshimiwa Spika**, ili Sera hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi, inahitaji itengenezewe miongozo (Guidelines) na Mpango wa utekelezaji (Strategy). Hata hivyo pamoja na kwamba baadhi ya matamko ndani ya sera hii yamekwishaanza kufanyiwa kazi (mfano utoaji elimu bure), bado mpango wa utekelezaji wa sera hii haujakamilika mpaka hivi sasa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya bunge hili kwa nini mkakati wa utekelezaji wa sera ya elimu haujakamilika na kuanza kutumika hadi leo huku baadhi ya matamko yakiwa yameanza kutekelezwa?

## 11. WANAFUNZI WALIOHAMISHWA KUTOKA VYUO VYA ST.JOSEPH

**Mheshimiwa Spika**, kwa muda mrefu Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliomba Serikali kuhamisha vijana hao kutokana na mazingira mabovu ya kujifunzia na kufundishia. Hii ni pamoja na ukosefu wa walimu wenye sifa na program zisizo na ulinganifu na Vyuo vingine. Nilifuatilia jambo hili hadi kufanya ziara katika Vyuo hivi na kujionea hali mbaya isiyokubalika. Baada ya kupiga kelele nyingi humu Bungeni, Naibu Waziri aliahidi kwenda pamoja na TCU kuona hali halisi katika vyuo hivyo. Jambo la kustaajabisha ni kwamba walituletea ripoti ya hovyoyao na ya kisiasa zaidi na kusema kuwa hali ni shwari; lakini jambo linaloshangaza zaidi ni kwamba leo wanafunzi wale wamehamishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa majibu ya kina ni kwani nini mwaka jana watendaji wa TCU na wa Wizara walisema hakuna tatizo na watendaji hao hao mwaka huu wameona kuna tatizo la msingi na kuwahamisha wanafunzi wa vyuo hivyo?. Je, wanafunzi hao watalipwa nini kwa muda waliopoteza?. Na ni nini hatma ya vyuo hivyo??

**Mheshimiwa Spika**, jambo linalokera zaidi ni baadhi ya vijana hawa sasa wamekwama kwenye vyuo waliovyohamia kwa kuwa kozi walizokuwa wanasoma zinatofautiana na pia kutokana na kuwa na mihula tofauti wengi wao wanalazika kurudia mwaka wa masomo ausemista.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji ni kwanini TCU ilivisajili vyuo hivi na kuvipa ithibati? Pili ni kwanini vyuo hivi vina mihula tofauti na vyuo vingine? Na pia ni fedha kiasi gani zimepotea katika kuwalipia mikopo vijana

hawa na sasa hawajui ni lini watahitimu masomo yao? Ni nini hatma ya vyuo hivyo na ni mfumo gani wa elimu yetu unaoruhusu wahitimu wa kidato cha nne kujiunga na vyuo vikuu kwa kisingizio cha special programs?!!

**Mheshimiwa Spika**, kitendo cha Waziri wa Elimu kuivunja bodi ya TCU jana tarehe 25 Mei, 2016 kutokana na kudahili wanafunzi wasio na sifa kujiunga vyuo vikuu siku moja kabla ya majadala wa hotuba yake ya bajeti ya Elimu ni kujaribu kwa hila kulizuia bunge kujadili kwa kina udhaifu mkubwa wa Serikali kupitia TCU katika kusimamia ubora wa Elimu ya juu hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili ni hatua gani za ziada itachukuwa kwa wajumbe hao wa bodi kwa kuwa wamewaharibia wanafunzi maisha yao na kupoteza fedha za umma kutokana na maamuzi yao?

## 12. MABORESHO YA MFUMO WA ELIMU NCHINI

**Mheshimiwa Spika**, kwa muda mrefu sasa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikitoa angalizo kuwa mfumo wetu wa elimu umepitwa na wakati; hivyo upitiwe upya na kufanyiwa maboresho ili uendane na mabadiliko yanayotokea katika nyanja mbalimbali duniani.

**Mheshimiwa Spika**, elimu ya nchi yetu imekumbwa na matatizo mengi ya ki-mfumo jambo ambalo pamoja na madhaifu mengine limechangia sana kushuka kwa ubora wa elimu ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa matatizo yanayoikumba sekta ya elimu hapa nchini yamekuwa yakijirudia rudia; na kwa kuwa mara kadhaa serikali imekuwa ikifanya maamuzi ya kisiasa zaidi kukabiliana na changamoto zinayoikumba sekta ya elimu jambo ambalo halijatoa ufumbuzi wa kudumu wa kuondokana na changamoto hizo; na kwa kuwa wadau wote wa elimu wana matamano ya kuona ubora wa elimu yetu unaongezeka; Hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kwa hatua ya sasa kuunda tume ya kitaalamu kwa ajili ya kuupitia upya mfumo wa elimu inayotolewa Tanzania ili pamoja na kukuza ubora wake lakini pia elimu hiyo iweze kwenda sambamba na kasi kubwa ya mabadiliko ya kiuchumi duniani.

## 13. DHANA YA UGATUZI KAMILI WA MADARAKA (DECENTRALIZATION BY DEVOLUTION) NA MKANGANYIKO WA USIMAMZI WA SEKTA YA ELIMU NCHINI

**Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa dhana ya ugatuji kamili wa madaraka, yani D by D, huduma nyingi za kijamii zikiwemo afya na elimu zimeshushwa katika ngazi ya Serikali za Mitaa na Wizara za sekta husika

zimeachwa na jukumu la kusimamia sera za sekta husika na kusimamia taasisi chache tu kulingana na itakavyopangwa na wizara husika.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja utaratibu huo kutajwa kuwa una nia njema ya kuwapa wananchi madaraka zaidi kupitia serikali zao za mitaa, lakini utaratibu huo umeleta mkanganyiko mkubwa sana katika usimamizi wa sekta ya elimu nchini.

**Mheshimiwa Spika**, nasema hivi kwa sababu tuliona jinsi matatizo ya walimu yalivyokuwa yanashindikana kutatuliwa kutokana na kuwa na mamlaka nyingi mno zinazoshughulika na walimu hadi tukafikia uamuzi wa kupendekeza kwamba kuwe na chombo kimoja kitakachoshughulikia masuala ya walimu yani TETRA – Tanzania Education and Training Authority, jambo ambalo mpaka sasa halijatekelezwa na Serikali. Hata hivyo, haiwezekani kutokana na mfumo wa D by D, waziri awe na mamlaka tu na vyuo vya ualimu na vyuo vikuu na kuacha taasisi nyingine zote za elimu na kazi zake katika mamlaka nyingine.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na hali hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia upya mfumo wake wa ugatuzi madaraka ili usilete mwingiliano wa kiutendaji katika ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa lakini pia kuweka mfumo ambao kutakuwa na chombo kimoja kikuu cha kitaifa kitakachoshughulikia kwa ukamilifu masuala ya elimu kuliko ilivyo sasa.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuona matatizo ya ugatuaji hapa nchini, niliamua kusoma vitabu vingi vinavyohusu dhana ya ugatuzi na nimegundua kuwa Tanzania hatutekelezi kabisa dhana ya D by D bali tunachofanya ni D by C yaani **Decentralization by Deconcentration** na ndio maana mambo hayaendi, Hivyo basi nashauri serikali isome vitabu vinavyoelezea dhana hii ili waelewe kwa undani.

#### 14. UBUNIFU KATIKA SAYANSI NA TEKNOLOJIA

**Mheshimiwa Spika**, hakuna Taifa duniani lililoendelea bila kuwekeza kwenye Sayansi na Teknolojia. Ni ukweli usioplingika kuwa, Sayansi na Teknolojia vinachangia sana katika maendeleo ya Taifa lolote. Mageuzi ya Sayansi na Teknolojia yanaleta hamasa ya ubunifu, pamoja na kuvutia zaidi ushiriki wa sekta binafsi katika kuendeleza Sayansi ya Teknolojia na ubunifu. Ni wazi mageuzi haya yanahitaji fedha nyingi hasa za utafiti. Jambo la kusikitisha ni kwamba, Serikali haitoi fedha kwa ajili ya utafiti; kwa mfano, bajeti ya 2015/2016 sekta hii ilikuwa na upugufu mkubwa na hata baada ya agizo la tengeo la 1% ya pato ghafi la Taifa (GDP). Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze ni kiasi gani cha pato ghafi la Taifa limetengwa kwa ajili ya utafiti katika bajeti ya 2016/17?

**Mheshimiwa Spika,** Inasikitisha sana kuona COSTEC ambacho ni chombo pekee cha kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu utafiti, sayansi na Teknolojia kilichoanzishwa na sheria Namba 7 ya mwaka 1986 lakini bado Serikali haijaweza kuipata Tume hii walau 1% ya pato ghafi la Taifa. Mathalani kwa mwaka huu Tume imetengewa 0.04% ya Bajeti yote ya Serikali. Halafu tunategemea nchi itaendelea kwa utaratibu huu?

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuipa kipaumbele Tume hii ili iweze kufanya tafiti zake na kusaidia Taasisi nyingine. Haiwezekani kasma 8001 inayohusu Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ipate asilimia 4 tu ya bajeti ya Wizara. Ndio sababu inayopelekea wabunifu kushindwa kuendeleza ubunifu wao na hivyo kuishia mitaani.

**Mheshimiwa Spika,** tulielezwa hapa kuwa COSTEC iliishauri kutoa mwongozo wa matumizi na Teknolojia ya kisasa itwaayo (Unmanned Aerial Vehicle UAV) itumiayo helicopters zinazoendeshwa bila rubani (drones). Teknolojia hii ni muhimu sana kwa ajili ya uhibitaji wa majangili kuandaa mipango miji, upimaji ardhi na katika matukio kama mafuriko. COSTEC ilishauri Serikali kuainisha Teknolojia hii kama kipaumbele cha kufanya utafiti na hivyo Tanzania kuwa mstari wa mbele ikiwa taasisi zake zataitumia. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Serikali kulieleza Bunge hili kama ilitekeleza ushauri iliopewa na COSTEC kuhusu teknolojia hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka 2015/2016 Sekta hii ya Sayansi na Teknolojia ilipata fedha kidogo sana huku tukitamba tuko kwenye karne ya Sayansi ya Teknolojia. Kwa mfano mwaka jana iliyokuwa Wizara ya Sayansi na Teknolojia na Mawasiliano ilipokea hadi Aprili, 2015 shilingi bilioni 4.79 fedha za maendeleo sawa na 18.46% ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako tukufu.

## 15. MAREJESHO KANDAMIZI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU

**Mheshimiwa Spika,** yapo malalamiko ya Wahitimu wa vyuo vikuu walionufaika na mikopo ya elimu ya juu kwamba utaratibu unatumika wa kufanya marejesho ya mikopo hiyo ni kandamizi na hauzingatii mazingira magumu ya ukosefu wa ajira wahitimu hao wanayokumbana nayo mara tu baada ya kuhitimu elimu ya chuo kikuu. Kwa mujibu wa taarifa ya baadhi ya wahitimu wa elimu ya juu ni kwamba; badala ya Bodi ya mikopo kudai marejesho ya mikopo peke yake, bodi hiyo imeweka gharama nyingine juu ya mikopo hiyo.

**Mheshimiwa Spika;** Bodi ya mikopo imeweka kiwango cha adhabu kwa wanaochelewa kurejesha mikopo (penalty amount) na kiwango cha kulinda kuporomoka kwa thamani ya shilingi (retention of value charges). Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni haikubaliani na kiwango kilichowekwa na bodi cha kulinda

kuporomoka kwa thamani ya shilingi (value retention fee) ya takriban asilimia 50 ya deni lote.

**Mheshimiwa Spika**, ufuatao ni mfano wa hati ya madai ya marejesho wa mkopo kwa mhitimu wa chuo kikuu. Inasomeka kama ifuatavyo: *“Kindly be informed that the deductions for the loans board will begin effectively May, 2016 and the deduction Percentage will be 8% from the basic salary.*

*If you have a complaint in accordance to this information, kindly see from HESLB*

Chek no	Index	Full name	Principle Amount	Penalty	Loan Admin fee	Value Retention fee	Total Loan Amount	Outstanding debt
			6,946,000.	694,600	69,460	2,833,344	10,543,404	10,543,404

## CHANZO: HESLB

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kufuta gharama ya **‘Value Retention Fee’** inayowatoza wahitimu wanaporejsha mikopo ili kuwapunguzia ukali wa maisha wahitimu hao ukizingatia wengi wao bado hawajapata ajira na waliopata ajira bado mishahara yao ni midogo. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni bado inasimamia msimamo wake wa kuitaka Serikali kutowadai wahitimu wa elimu ya juu kwa kuwa fedha inayowapatia ni bajeti ya maendeleo ya wizara husika kama ilivyo kwa wizara nyingine na hivyo Serikali haipaswi kudai fedha hizo kama ambavyo haidai kurejeshewa fedha inazotoa katika miradi mingine ya maendeleo.

## 16. UNYANYASAJI WA WANAFUNZI WA VYUO VIKUU WANAHOISIWA KUUNGA MKONO UPINZANI

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na tabia mbaya sana ya baadhi ya wakuu wa vyuo vikuu hapa nchini kuwanyanyapaa na kuwadhalilisha na hata kudiriki kuwafukuza chuoni wanafunzi ambao kwa hisia zao wanafikiri wanaunga mkono harakati za vyama vya upinzani.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa kwamba aliyekuwa kiongozi wa Serikali ya Wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Dodoma amesimamishwa masomo kwa hisia tu kwamba alikwa mfuasi wa CHADEMA. Aidha, aliyekuwa makamu wake, tena **msichana**, aliamriwa na uongozi wa chuo hicho kukabidhi madaraka yake, kwa uongozi mwingine wa serikali ya wanafunzi ambao haukuchaguliwa na wanafunzi (uliteuliwa na utawala wa chuo) kinyume kabisa na katiba inayoongoza Serikali ya Wanafunzi wa chuo hicho.

**Mheshimiwa Spika**, mwanafunzi huyu (msichana) alitakiwa kupongezwa na uongozi wa chuo kwa kuthubutu kugombea nafasi hiyo na kuonyesha uwezo mkubwa wa uongozi, lakini alisakamwa na uongozi wa chuo na kutishiwa maisha, jambo lilomfanya afungue shauri mahakamani kupinga kulazimishwa kuachia madaraka. Hata hivyo, zilipoonekana dalili za yeye kushinda, chuo kilimwandikia barua ya kumfukuza chuo kabla ya hukumu.

1. **Mheshimiwa Spika**, hukumu imetoka na huyo mwanafunzi ameshinda kesi. Utawala wa chuo hicho umedharau amri ya Mahakama ya kumrejeshwa na kumpa ushirikiano kiongozi huyo halali wa Serikali ya Wanafunzi kwa nafasi ya Makamu wa Rais; mwanafunzi huyo ananyanyapaliwa na uongozi wa chuo kikuu cha Dodoma jambo ambalo kwa vyovyote vile litaathiri masomo yake ikizingatiwa kwamba zimebaki wiki chache kabala hajafanya mtihani wa kuhitimu shahada yake ya kwanza. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya bunge hili ni kwa nini haijamchulia Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma hatua za kinidhamu kwa kuendeleza unyanyapaa na unyanyasaji wa wazi kwa wanafunzi wa chuo hicho kwa hisia zake tu kwamba wanafunzi hao ni wafuasi wa CHADEMA/UKAWA? Ina maana UDOM ni kwa ajili ya wanafunzi wa CCM? **TUME YA WALIMU (TEACHERS SERVICE COMMISSION)**

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani kwa muda mrefu imekuwa ikipinga utaratibu wa walimu kuwa chini ya mamlaka tofauti za ajira jambo linaloleta mkanganyiko kwao hasa pale wanapokuwa na madai mbalimbali kuhusu maslahi yao. Walimu walikuwa wakipata tabu kujua ni mamlaka ipi kati ya Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma au Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, au Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi .

**Mheshimiwa Spika, Baada ya kelele nyingi**, hatimaye serikali ilileta muswada wa Sheria ya kuanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu (Teachers Service Commission) mwezi Julai, 2015. Nia ya Serikali kuleta muswada ule ililenga kuwalaghai walimu ili waipigie CCM kura katika uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2015, na ndio maana uliletwa Julai, 2015 tena kwa matangazo na mbwembwe nyingi hadi kufikia hatua ya Rais wa wakati huo Jakaya Mrisho Kikwete kuupigia kampeni kwa Chama cha Walimu (CWT) na wadau wengine wa elimu tofauti na njia za kawada za Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii kukutana na wadau ili mradi tu ionekane kwamba Serikali ilikuwa inawajali walimu sana.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuwaarifu walimu wote nchini kwamba Serikali hii ya CCM haijawahi kuwa na nia ya dhati ya kutatua kero zake, ila inakaa na walimu kimkakati tu kwa malengo ya kubembebeza kura zao, na wakishapiga kura hizo matatizo yanaendelea kubaki palepale **ndio maana hadi leo pamoja na Tume hiyo ya Utumishi wa Walimu**



**kutengewa fedha bado wajumbe hawajateuliwa ikiwa ni miezi tisa tangu sheria hiyo itungwe; Pili vifungu vingi vya Sheria hiyo ni vya muundo na majumumu ya tume hiyo pamoja na makatazo na adhabu na haionyeshi kero za walimu zitashughulikiwa namna gani.** Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ilete Bungeni muswada wa sheria ya marekebisho ya sheria hiyo ili vifungu vyote vyenye mapungufu viweze kufanyiwa marekebisho ili sheria hiyo iwe bora na yenye kutatua kero za muda mrefu za walimu.

### **KUHAMISHWA KWA MAFUNZO YA WALIMU KUTOKA KURUGENZI YA WALIMU YA WEST HADI NACTE (NATIONAL COUNCIL FOR TECHNICAL EDUCATION)**

**Mheshimiwa Spika,** tangu tupate uhuru, nchi imekuwa ikifanya mipango na mikakati ya kutoa elimu bora kwa ajili ya wananchi wake. Serikali imekuwa inaweka vyombo au taasisi mbali mbali kutekeleza jukumu la utoaji ya elimu. Ili kuhakikisha tunaenda vizuri, serikali imekuwa inafanya mapitio ya utoaji wa huduma hasa elimu. Mapitio hayo (reviews) yamekuwa yanategemea kwanza; utafiti wa kisayansi, na pili ushirikishwaji mpana wa wadau wote.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo la kushangaza ni kuwa bila utafiti wowote wa kisayansi wala ushiriki wa wadau wa elimu kwa niaba ya wananchi, MAFUNZO YA UALIMU (Teachers Education) yamehamishwa kutoka Kurugenzi ya Ualimu ya WEST na kupelekwa Mafunzo ya Elimu ya Ufundi (NACTE).

**Mheshimiwa Spika;** malengo na makusudi ya mafunzo ya walimu yanatofautiana sana na malengo na makusudi ya mafunzo yanayotolewa chini ya NACTE.

**Mheshimiwa Spika,** Makusudi ya Elimu ya Ufundi ni inayotolewa chini ya NACTE ni kama ifuatavyo; naomba kunukuu:-

- *Technical Education objective is to prepare graduates for occupations categorised as skilled crafts below engineering profession and hence employees are called technicians guided by 1996 National Technical Education Policy.*
- *NACTE quality controls and regulates technical education.*
- 

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya kufanya uhamisho huu ni sawa na kuweka mafunzo ya Ualimu kama fani ya ufundi tofauti na Ualimu kama taaluma inayojitegemea kama sheria, Uhasibu au ununuzi ambazo zote zina bodi zake.

**Mheshimiwa Spika;** Kambi Rasmi ya Upinzani ina mtazamo kwamba, uamuzi huo wa Serikali usipobatilishwa, basi Changamoto zafuatazao zitatokea.

- i. Kuongezeka kwa gharama za uendeshaji kutokana kubadilika kwa muundo wa utawala (organizational structure).



- ii. Kutakuwa na shida ya kupata wanafunzi wa kujiunga na vyuo kwa vile vyuo vikuu navyo vinawaangalia hao hao kutoa vyeti na diploma.
- iii. Kutokwepo harmonization kati ya TCU na NACTE juu ya mafunzo ya walimu hasa ubora wake.
- iv. Ugumu wa kuendesha vyuo kwa vile serikali haitapeleka fedha tena.
- v. Falsafa (philosophies) mbali mbali za vyuo vya binafsi na umma na hivyo kuongeza kwa mkanganyiko.

**Mheshimiwa Spika;** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa majibu mbele ya Bunge hili juu ya maswali yafuatayo:-

- i. Kulikuwa na sababu gani (rationale) ya kuhamisha mafunzo ya walimu toka Kurugenzi ya Mafunzo ya Wizara ya Elimu kwenda NACTE?
- ii. Je, kuna utafiti gani wa kisayansi uliofanyika kuhalalisha mabadiliko hayo?
- iii. Je, wadau walihusihwa kuhusu jambo hili?
- iv. Kuna faida na hasara gani ya kufanya huu uhamisho huo?
- v. Kuna mikakati gani iliyowekwa kuhakikisha kuwa ubora wa elimu hautaathirika?
- vi. Kuna mikakati gani iliyowekwa kuhakikisha uandikishaji wa walimu wanafunzi kukidhi mahitaji ya vyuo husika?
- vii. Vyuo hivi vitawezaji kuwa endelevu bila ruzuku ya serikali?
- viii. Je, mitaala itawezaje kuwa harmonized kwa ajili ya vyuo vyote?

## **17. MAPENDEKEZO YA JUMLA YA KUBORESHA SEKTA YA ELIMU NCHINI**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa imebainika dhahiri kwamba elimu ya Tanzania imekuwa inaporomoka kwa sababu ya uwekezaji hafifu katika rasilimali watu katika sekta hiyo – yaani taaluma na mafunzo kwa walimu; na kwa kuwa imebainika pia kwamba mitaala mibovu isiyokidhi viwango imechangia sana kushuka kwa ubora wa elimu hapa nchini; hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwa Serikali kufanya mambo yafuatayo:

1. Kuboresha Mitaala elimu ili ishabihiane na mahitaji ya jamii na mabadiliko makubwa yanayoendelea kutokea duniani katika nyanja mbalimbali.
2. Kuelekeza na kusimamia matumizi ya kitabu kimoja cha kiada ili kufanya vijana wetu wasitofautiane katika ufahamu wa mada zinazofundishwa kwani wanafanya mitihani mmoja.

3. Kusimamia utungaji na uchapaji wa vitabu na kuhakikisha kuwa vina ubora wa hli ya juu kwani vitabu ndio kiongozi kwa walimu.
4. Kuongoza majadiliano na wadau wa elimu na kuweka msimamo juu ya Lugha ya kufundishia katika ngazi zote za elimu kwani bado ni tatizo kubwa. Haiwezekani katika nchi moja baadhi ya shule zitumie Kiswahili na nyingine Kiingereza.
5. Kuwekeza katika Vifaa vya kufundishia na kujifunza ili kuondoa vikwazo katika utekelezaji wa mataala.
6. Kuboresha Miundo mbinu na mazingira ya shule. Miundo mbinu iliyopo bado ni mabovu sana; ukosefu wa vyoo, madarasa n.k. watafiti wamesema ni asilimia nne tu ya shule za sekondari nchini ndizo zinazokidhi vigezo vya chini kabisa vya hadhi ya sekondari. Hii ni takribani shule 160 tu kati ya shule za sekondari zaidi ya 4000 zilizopo nchini.
7. Mafunzo kwa walimu ni muhimu mno ili waendane na mabadiliko yanayojitokeza. Taarifa ya CAG inafafanua kwa undani tatizo hilo kwamba ni walimu 61,531 (31%) tu kwa shule za msingi na 11% kwa walimu wa Sekondari.
8. Mazingira ya walimu ni mabaya sana kama nilivyoeleza awali hivyo, tunaamini mwalimu ni wakala mzuri wa kubadilisha hali mbaya ya elimu nchini. Bila kurekebisha maslahi ya mwalimu hata uwekeze vipi kwa kujenga madarasa kwa dhahabu vitakuwa kazi bure, sambamba na hili pawepo usimamizi thabiti kuhakikisha walimu wanatimiza wajibu wao.
9. Motisha kwa walimu ninajua baadhi ya walimu wanajituma sana hivyo, Serikali iwatambue na kutunzwa ili kuwatia moyo na kuwahamasisha wengine.
10. Kuajiri walimu wenye sifa stahiki – yaani waliofuzu na kufaulu vizuri katika taaluma inayokidhi mahitaji katika shule husika,

## 18. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, aliyekuwa Rais Marekani, Abraham Lincoln aliwahi kusema, namnukuu;

***“The philosophy of the school room in one generation will be the philosophy of government in the next”*** - kwamba ***“Falsafa ya elimu inayotolewa darasani kwenye kizazi cha leo ndiyo itakayokuwa hatma ya serikali yetu ya kesho”***.

Kama tutaendelea kuzalisha wahitimu wanaotokana na elimu duni inayotolewa, iliyogubikwa na maamuzi mabovu ya kisiasa na vitendo vya

ufisadi, ni dhahiri kuwa Taifa letu halitaweza kupata viongozi bora wa kuliongoza huko tuendako.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchukua hatua za kunusuru elimu yetu ni sasa. Ni lazima tubadilike. Matatizo ya nchi hii hayataweza kamwe kutatuliwa kwa elimu hii duni tunayopandikiza kwa watoto wetu. Tunahitaji mapinduzi na mageuzi makubwa ya kielimu kuitoa Tanzania hapa ilipo na kuipeleka kwenye *level* nyingine. Suala la kuwa nchi ya uchumi wa kati, nchi ya viwanda, litaendelea kuwa ni hadithi za Bulicheka tu ikiwa hatutaondoa mapungufu mengi yanayokabili mfumo wetu wa elimu.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumalizia hotuba yangu kwa kusema kwamba, sera ya elimu bure ilianzishwa na CHADEMA. Ipo katika ilani ya uchaguzi ya CHADEMA chini ya mwavuli wa UKAWA tangu mwaka 2005, 2010 na hatimaye 2015. Lengo lilikuwa ni kutoa huduma ya elimu bure kwa ukamilifu wake kuanzia shule za awali hadi chuo kikuu. Maigizo ya ilani ya CHADEMA yaliyofanywa na CCM, yameishia kuondoa ada tu na michango midogomidogo ya uendeshaji wa shule hadi kidato cha nne tu, huku kukiwa na sintofahamu kubwa juu ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika shule hizo. Hali hii inapelekea kuporomoka zaidi kwa elimu.

**Mheshimiwa Spika**, kuna msemo usemao, ***'If education is expensive try ignorance'***, tafsiri yake ni kwamba; kama elimu/ kuelimika ni gharama basi jaribu ujinga. Tanzania tumeamua kujaribu ujinga, kwa kutowekeza vya kutosha katika elimu na ndio maana elimu yetu imeporomoka na kufikia hapa ilipo.

**Mheshimiwa Spika**, Waziri wa Elimu katika awamu ya kwanza Marehemu Jackson Makwetta alisema kwamba: ***"Tanzania ni kama mama mjamzito ambaye siku zake za kujifungia zimefika lakini hajifungui, hivyo Tanzania inahitaji mabadiliko vinginevyo itaendelea kudidimia kielimu na kiuchumi."*** Kwa sababu hiyo; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuutazama upya mfumo wa elimu sasa kwa kuunda tume maalum ya kuupitia upya na kutoa mapendekezo ili Taifa liweze kuwa na mfumo bora wa elimu unaokidhi viwango vya kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Susan Anselm Jerome Lyimo (Mb)  
**WAZIRI KIVULI NA MSEMAJI MKUU WA  
KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI**

26 Mei, 2016

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mwongozo wa Spika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Angellah Kairuki, Mheshimiwa Angellah unaomba nini? *(Makofi)*

Endelea Mheshimiwa Angellah.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7)...

**NAIBU SPIKA:** Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba tumsikilize, Mheshimiwa Angellah Kairuki tafadhali, Mheshimiwa Angellah unaomba nini?

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), kuhusu mambo ambayo yamesemwa na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara hii ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, yote yaliyoelezwa katika ukurasa wa pili na katika ukurasa wa tatu hususan katika hoja kwamba, vyombo vya dola vimekiuka demokrasia katika uchaguzi uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba, vyombo vya dola vimechakachua ushindi wa upinzani na ya tatu kwamba, Serikali imekuwa ikifanya *Censorship* kwa mujibu wa taarifa za upinzani na kwamba ni kinyume cha Kanuni hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yote haya yalioelezwa katika ukurasa huu wa pili na wa tatu, si ya kweli na kwa kweli ni ukiukwaji mkubwa wa matakwa ya Kanuni. Kwa hiyo, naomba Mwongozo wako ni hatua gani zinaweza zikachukuliwa kwa msemaji huyo, kwa kulipotosha Bunge hasa ukizingatia kwamba, uchaguzi ulikuwa ni uchaguzi halali, matokeo yalikuwa halali na Serikali hii imepata uhalali wake kupitia kwa wananchi na imepata ushindi wa zaidi ya asilimia 74 kwa Wabunge na zaidi ya asilimia...

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila utaratibu kuashiria kutokubaliana na maneno ya mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA (MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako dhidi ya msemaji huyu. *(Makofi)*

**MHE. AMINA S. MOLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mwongozo wangu. Naomba Mwongozo kwa Kanuni ya 68(7), lakini vile vile, nanukuu kupitia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 14. Ibara ya 14 inasema:

“Kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka katika jamii hifadhi ya maisha yake, kwa mujibu wa Sheria”.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na matukio yakitokea katika, Mikoa ya Kanda ya Ziwa hasa Mkoa wa Manyara pamoja na Mkoa wa Mara. Hapo jana, kumefanyika mauaji ya familia moja, ambayo ni baba na mama na wamekatwakatwa mapanga na cha kusikitisha zaidi huyo mama alikuwa ni mjamzito!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kauli ya Serikali, kwa mwongozo wako wewe unisaidie, ili basi, tupate kauli kutoka kwa Serikali, kwa sababu mauaji haya yamekuwa yakitokea kwa watu wasio na hatia. Ni lini au ni nini wajibu wa Serikali katika kuhakikisha kwamba raia wote wa Tanzania wanaishi kwa amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, asante.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wako, Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nape Nnauye.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, WASANII NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa Kanuni ya 64(1)(a), inayosema kwamba, Mheshimiwa Mbunge hatatoa ndani ya Bunge lako taarifa ambazo hazina ukweli.

Wakati, Mheshimiwa...

**MBUNGE FULANI:** *Please! Please!*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, WASANII NA MICHEZO:** Kawaida yenu.

Wakati Mbunge wa Mbeya Mjini, anaomba mwongozo wako, alinukuu gazeti la Mwananchi la tarehe 24 mwezi wa Tano na kudai kwamba lilieleza

jambo lililotokea Mwanza kwenye tamasha la muziki, lakini amefanya hivyo, kulidanganya Bunge lako, akijua wazi kwamba, gazeti la tarehe 25 la Mwananchi liliikanusha habari hiyo kwa sababu haikuwa ya kweli na wakaiweka kwenye ukurasa wa mbale. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote aliyoyanukuu, lakini kwenye ile shughuli tulikuwa na Mawaziri wengine, ambao ni mashahidi na jana Kaimu Waziri Mkuu hapa alikuwa akizungumza na Wachungaji zaidi ya 400, ambao walilizungumza suala la Bunge “live”, na katika maelezo walimshangilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, ambalo linapotoshwa sana na amesema kwa uongo, anaendelea kudanganya kwamba, suala hili ni suala la Serikali. Kwa kweli, nimesimama kwa sababu, Sugu nimemzoea, angeweza akasema nikampuuza, lakini ameihusisha Serikali hapa na jambo ambalo Serikali halihusiki nalo na limekuwa likizungumzwa hapa mara kwa mara kwamba Serikali haihusiki nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba mwongozo wako kwa mtu ambaye ameamua kutumia *Platform* ya Bunge lako, kwanza kuleta taarifa za uongo, lakini pili, kuendelea kuihusisha Serikali na jambo ambalo Serikali haihusiki nalo.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wako, Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Japhary, naomba ukae tafadhali!

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka nilichukua miongozo miwili mwanzo, sasa hivi nimechukua mingine. Kwa hiyo, maana kuna watu walishaanza kunyanyua midomo, wanataka kuona kama kuna namna ambayo si nzuri. Sasa hivi nimechukua miongozo mitatu, nitaitolea maelezo baadaye kidogo!

Tunaendelea, Waheshimiwa Wabunge, uwasilishaji umekwisha. Nitaita Mbunge atakayeanza kuchangia, Mheshimiwa Mary Chatanda, atafuatiwa na Mheshimiwa Nkamia. Mheshimiwa Mary Chatanda.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya mwanzo ili niweze kuchangia. Kwanza kabisa naomba niuunge mkono hoja juu ya bajeti aliyowasilisha Waziri wa Elimu kwamba, amewasilisha kiufundi kabisa, nampongeza. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi ya kumpa pole Naibu Waziri wa Elimu kwa msiba ambao umempata. Basi, namwombea kwa Mwenyezi Mungu

amtie nguvu na Marehemu Roho yake iweze kuwekwa mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Waziri na Naibu Waziri, Wakuu wa Wizara kwa kazi ambayo wamekuwa wakiifanya pamoja na changamoto nyingi ambazo wanakabiliana nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kusema kwamba, elimu ndiyo ufunguo wa maisha. Bila elimu hakuna viwanda, bila elimu hakuna kilimo chenye tija, bila elimu hakuna afya bora na kadhalika. Hivyo, ningeomba sana, Wizara ya Elimu ifanye kazi ya kuboresha suala zima la elimu. Suala zima la elimu likiboreshwa, tunaweza tukawapata wasomi wazuri, watakaoweza kuendesha nchi hii na kuweza kuingia kwenye soko la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Wizara ya Elimu, kwa kuanza kutazama upya ufaulu wa darasa la saba. Ufaulu wa darasa la saba uanze sasa kwak kuzingatia vigezo vya kuingia kwenye elimu ya sekondari. Utaratibu wa mitihani wa kuchagua alama za a, b, c, d, tunawapata wanafunzi ambao wanakwenda sekondari wasiojua kusoma na kuandika. Hawa wanafunzi ambao wengine wana vipaji vile vya kubahatisha, wanabahatisha halafu wanaingia kwenye elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakiingia kwenye elimu ya sekondari wanawapa tabu Walimu wa sekondari namna ya kuwafundisha, kwa sababu inabidi sasa waanze kuwafundisha kwa uelewa zaidi, masomo yale ambayo yalikuwa ni ya darasa la saba wanaanza kuwafundisha huku sekondari. Kwa hiyo, naomba sana utaratibu ule wa awali, uliokuwepo mara ya kwanza uweze kurejewa ili kuondoa usumbufu kwa Walimu wa shule za sekondari kuanza kuwafundisha wale wanafunzi ambao hawakufaulu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara irejeshe utaratibu wa zamani wa kufanya masomo kwa kufikiri badala ya kufanya masomo kwa kuchagua. Wakifanya hivyo tutawapata watoto wanaojitambua, itawarahisishia Walimu kuwa na watoto wenye uelewa na ufaulu wenye tija kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sasa uboreshaji wa elimu uende sambamba na uboreshaji wa maslahi ya Walimu na stahiki zao. Baadhi ya stahiki za Walimu wala hazihitaji kuwa na shida kiasi kwamba Walimu wanapata matatizo, wanapata shida za kuhangaika kufuata stahili zao. Walimu inajulikana siku zao za likizo, mwezi wa Sita ni mapumziko na mwezi wa 12 ni mapumziko, hivyo niiombe Wizara, kinapofika kipindi hicho, wanapojua kwamba Walimu wanataka kwenda likizo mwezi wa Sita, wale Walimu wanaotakiwa kwenda wawe wameandaliwa tayari nauli zao miezi miwili kabla, fedha zao zipelekwe kwenye Halmashauri ili Walimu hawa wanapokuwa wanakwenda likizo,



wapewe nauli zao badala ya kuwakopa kwamba waende halafu watakuja kurudi ndipo wapate nauli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la *teaching allowance*. Walimu hawa, ndugu zangu, wanafanya kazi kubwa, wanafanya kazi kiasi kwamba hawana nafasi ya kupumzika, hawana nafasi ya kufanya shughuli nyingine za kuwaongezea kipato. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie utaratibu wa kurejesha *teaching allowance* ili Walimu hawa wapate moyo wa kufanya kazi, kwa sababu hawana njia nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wengine wanapata muda wa kwenda kufanya kazi kujiongeza kipato, lakini Walimu hawana nafasi ya kufanya hivyo kwa sababu wanakuwa na shughuli nyingi ambazo zinawafanya waendeleo kufanya maandalizi kwa ajili ya wanafunzi kwa kesho yake. Kwa hiyo, ni matarajio yangu kwamba Serikali, ombi hili ni la muda mrefu, ni vizuri basi wakaliangalia ili Walimu hawa walipwe hiyo *teaching allowance* ili iweze kuwasaidia katika kujikimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala zima la madarasa haya ya awali. Madarasa ya awali, Serikali kwa kweli imefanya kazi kubwa kuona kwamba watoto wote waende shule. Hata hivyo, niombe basi kwa kuwa Walimu hakuna wa madarasa la awali, sana sana wanawachukua wale Walimu ambao ni watu wazima ndiyo wamewapangia kufundisha madarasa ya awali. Niombe sasa waandaliwe Walimu maalum watakaokuwa wanafundisha madarasa haya ya awali, badala ya kuwatumia wale Walimu ambao wanaona ni watu wazima waliopo kwenye madarasa mengine na kuwaleta kwenye madarasa haya ya awali. Vile vile iende sambamba na suala zima la kuwapa vile vitendeakazi vya kufundishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali, kwa sababu ruzuku inapelekwa kwa wanafunzi wale wa shule za msingi, basi ruzuku vile vile ya watoto wa shule ya awali, iunganishwe kwa kupelekwa kwenye shule za msingi ili angalau na wenyewe waingie kwenye hesabu, kwa sababu safari hii walipokuwa wamepeleka zile ruzuku, hawakuingiza kwenye orodha ya watoto ambao wako shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena nizungumzie suala la upandishwaji wa madaraja. Naomba upandishwaji wa madaraja uende sambamba na mabadiliko ya mishahara ya Walimu...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chatanda, hiyo ni kengele ya pili!

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Juma Nkamia!

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema leo na nawashukuru Wabunge wenzangu wote mlionipa pole wakati nimepata maradhi juzi; nashukuru sasa niko salama na nimejiunga na ninyi. Pili nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kumteua Mheshimiwa Profesa Ndalichako na Mheshimiwa *Engineer* Manyanya kuwa Mawaziri katika Wizara hii, lakini pia nimpe pole sana dada yangu, Mheshimiwa *Engineer* Manyanya kwa msiba uliompata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima ya kipekee kabisa nimpongeze Mheshimiwa Bashe kwa uwasilishaji mzuri wa taarifa ya Kamati yetu. Hata dada yangu, Mheshimiwa Susan naye leo kapendeza na anayafahamu kidogo mambo ya elimu kwa sababu alikuwa warden pale Chuo Kikuu akigawa vyumba kwa wanafunzi kwa muda mrefu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na jambo la kwanza, nataka kuzungumzia hili suala la ada elekezi, nasikia kwamba Serikali ina mpango wa kuja na mfumo huo. Nadhani suala la ada elekezi lazima Serikali ikae iliangalie kwa kina sana, kwa sababu hakuna mtu anayelazimishwa kumpeleka mtoto shule ya kulipia. Suala lililopo hapa ni kwa Serikali kusimamia na kuhakikisha shule zote za Serikali zinakuwa bora, lakini leo kumwambia mzazi, ama kumwambia mwenye shule, kwanza kuendesha shule ni gharama kubwa, hata yale mabasi tu wanalazimishwa kupiga rangi. Kwa kweli upo umuhimu mkubwa wa Serikali kuliangalia jambo hili na sidhani kama ni jambo la busara sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nataka niseme tu kwamba, kuhusu hiki Chuo Kikuu cha *Saint Joseph*, mimi ni mmoja kati ya watu walioathirika kwa sababu mtoto wa marehemu kaka yangu alikuwa anasoma kule Arusha. Chuo hiki kimefungwa, waliofanya makosa ni *TCU*, wamekifunga chuo hiki na wenyewe ndiyo waliotoa kibali cha kuanzishwa kwake. Mheshimiwa Waziri leo amesema amevunja Bodi, hivi watoto hawa walioathirika, nani atawalipa? Pia kukipa chuo kibali cha kuendesha elimu ya chuo kikuu kuna hatua zinafuatwa na hata kukifungia kuna hatua zinafuatwa. Wanafunzi wale wamepelekwa Moshi pale, wengine wamepelekwa Morogoro, leo wanaambiwa wale ambao walikuwa wanapata mikopo hawatapewa tena mikopo kwa sababu wameongezewa semester moja. Ni kosa la wanafunzi hawa au kosa la Serikali? Kwa hiyo, naomba Serikali mliangalie vizuri sana jambo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Mheshimiwa Waziri hebu chunguza watu wako; hivi walikifunga chuo hiki kwa halali ama kulikuwa na mbinu nyingine? Kwa hiyo, nikuombe sana, kwa sababu tulioathirika ni sisi wazazi.

Wanafunzi wanahamishwa, wengine wamekuja UDOM hapa wanaambiwa kwa sababu kule sijui walichelewa, waongezewe semester moja, waliokuwa wanapewa mikopo hawatapewa tena mikopo. Nani sasa atakayelipia hiyo gharama wakati ninyi ndiyo mlifanya kosa? Angalieni kwa kina sana; namwomba Mheshimiwa Waziri alichunguze sana jambo hili. Pamoja na hatua nzuri aliyochukua hebu awachunguze vizuri watu wake wa TCU, walitenda haki kwenye kukifunga chuo hiki ama kulikuwa na mbinu za chini kwa chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, naomba nizungumzie kidogo suala la shule ambazo zinapewa hadhi ya kwenda A Level, hasa katika shule hizi za Kata. Shule nyingi hizi zina miundombinu duni na nimshukuru Mheshimiwa Waziri, ameniahidi kwamba atanisaidia kupata fedha ya kuchimba kisima cha maji katika Shule ya Sekondari ya Farkwa na Shule ya Sekondari ya Msakwalo. Shule hizi zina miundombinu duni sana, wakati mwingine sisi Waheshimiwa Wabunge tumekuwa sasa ndiyo kama walezi wa shule hizi, kila jambo lazima sisi tusimame kidete, wakati mwingine magodoro hakuna, Wabunge wanatoa, hiki hakuna, Wabunge wanatoa. Niiombe Serikali iziangalie vizuri shule hizi, mnapopandisha hadhi ya shule mjiridhishe kwanza, kwamba, je, inakidhi! Hili ni jambo ambalo nadhani mkiliangalis vizuri linaweza kutusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nataka kuzungumzia huu mfumo wetu wa D by D, kwenye Kamati wamesema, lakini na mimi tena nichangie. Hebu uangalieni vizuri huu mfumo, nimesema kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, nimesema kwenye Wizara nyingine, angalieni, fanyeni kwanza review, unatusaidia kiasi gani! Leo Waziri wa Elimu naweza kusema mwisho wake hapa Dodoma ni Dodoma Sekondari na Msalato, akifika kule, Waziri anayeshughulika na shule zile Mheshimiwa Simbachawene. Waziri akifika huyu kule mgeni kabisa, halafu akienda kwenye Halmashauri Waziri wa Elimu anasimamia tu kile kitengo cha ukaguzi, lakini Maafisa wengine wote wapo chini ya TAMISEMI. Nadhani kuna tatizo hapa, hebu kaeni chini muangalie namna gani, sisi kazi yetu ni kushauri tu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho, na mimi naomba leo niseme kidogo jamani. Uchaguzi uliopita umepita na mshindi kajulikana; mshindi CCM. Mpira hauwezi kwisha, tena unataka kuja kulalamika nje, uchaguzi umekwisha. Leo mtu anasimama hapa anasema oh, tuliibiwa kura, ninyi mlikuwa wapi wakati mnaibiwa! Acheni kutafuta sababu, tafuteni chanzo cha kwa nini mlishindwa. Ninyi mnajua kabisa kwamba timu ya mpira yenye wachezaji 11, mchezaji mmoja anapoumia anaingia wa timu ile ile, ninyi ilikuwaje mkachukua mchezaji wa upinzani mkamuweka! Mchezaji wa Simba kaumia, mmechukua wa Yanga mkaweka pale, amefungisha leo mnakuja kulalamika hapa! Kabisa tu, eeh, lazima tuseme tu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine tunakaa kimya humu sio kwamba hatuna uwezo wa kusema, tuna uwezo wa kusema. Mchawi mwenyewe, unaanza kutafuta mchawi, mchawi utatoa wapi wakati mchawi ni wewe. Kwa hiyo, niwaombe tu, muwe mnatafakari kwanza! Wewe nyoosha mdomo, fanya nini, lakini *that's the truth*, utaongea sana, utapiga kelele sana, ukweli ndiyo huo na umekuingia vizuri. Eeh! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kelele wala hainisumbui. Nataka niwaambie, nataka niwashauri *in future* kama mnataka kuwa chama kizuri cha Upinzani, miaka minne ijayo na miaka 20 ijayo, anzeni kutafuta wachezaji wenu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tusikilizane. Mheshimiwa Magereli, Mheshimiwa Matiko tusikilizane. Mheshimiwa Nkamia malizia! (Makofi)

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Ninyi tukaneni lakini ukweli ndiyo huo. Wenye akili wanajua, wapiga kelele wanajua na najua imewaingia vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, kwanza naunga mkono hoja...  
(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila utaratibu)

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** ...We piga kelele! Kwanza meno yako yameoza, endelea kupiga kelele humu! (Makofi)

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliendelea kuongea bila utaratibu)

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Nataka niwambie tu. Kuna baadhi yenu humu...

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Mheshimiwa Nkamia, malizia tafadhali!

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Ahsante, namalizia. Nataka niwape mfano mmoja. Benard Tapie aliwahi kusema kwamba, kuna baadhi ya watu wakiamba asubuhi wakijiangalia kwenye voo, wana sura mbaya wanatamani kutapika. Sasa ninyi mnaoshangilia humu, mna sura mbaya mnatamani kutapika. (Makofi)

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliendelea kuongea bila utaratibu)

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Nitasoma majina ya wachangiaji wa mchana. Kwa sababu uchangiaji tumeanza leo, *list* ni ndefu sitawasoma wote, kwa hiyo, nitasoma wachache watakaoanza.

Tunao Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mheshimiwa Juliana Shonza, Mheshimiwa Kangi Lugola, Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi na Mheshimiwa Hassan Elias Masala. Halafu Mheshimiwa Dkt. Elly Marco Macha, Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mheshimiwa Zainab Mussa Bakar, halafu Mheshimiwa Dkt. Suleiman Ally Yussuf, Mheshimiwa Yussuf Kaiza Makame. Wengine *list* yao itaendelea kusomwa mchana, sijawasoma wote.

Waheshimiwa Wabunge, kuna miongozo mitatu iliyoombwa. Nitaanza na mwongozo wa mwisho wa Mheshimiwa Nape Nnauye kuhusu maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Joseph Mbilinyi kuhusu tamasha la Mwanza. Nilitoa maelezo kwamba mwongozo ule aliokuwa ameuomba Mheshimiwa Joseph Mbilinyi haukuwa mwongozo kwa mujibu wa Kanuni, lakini kwa kuwa yale maneno yalisemwa humu ndani yameombewa mwongozo na Mheshimiwa Nape Nnauye. Sasa mwongozo wangu kwenye hili ni kwamba kwa kuwa yale maneno ya asubuhi aliyoyasema Mheshimiwa Joseph Mbilinyi nimeyakataa kuwa mwongozo, basi hoja ya Mheshimiwa Nape na kile alichokisema Mheshimiwa Mbilinyi pia kinakufa. (*Makofi*)

Mwongozo wa Mheshimiwa Amina Molel kuhusu Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na haki ya kuishi na mauaji yanayotokea Kanda ya Ziwa. Kwanza nianze kwa kusikitika sana kwa niaba yenu Waheshimiwa Wabunge, kwamba haya mauaji yamekuwa yakiendelea kila wakati, lakini tutakumbuka Waheshimiwa, wiki hii, nadhani Jumatatu ama Jumanne, tulisikia kauli ya Serikali kwamba wanafanya nini, lakini sasa haya mauaji yametokea tena jana kwa ripoti ya Mheshimiwa Molel. Nikumbushe tu masikitiko yetu makubwa ni kwamba haya mauaji yanaendelea, tunaomba Serikali tafadhali ifuatilie kwa karibu ili yaweze kukomeshwa.

Waheshimiwa Wabunge, lakini la kukumbushana, jambo kama hili haliombewi mwongozo kama nilivyosema asubuhi. Jambo kama hili linaletwa kwa kutumia Kanuni nyingine ambayo sio Kanuni ya kuomba Mwongozo wa Spika, kwa sababu Mwongozo wa Spika unaombwa kwa jambo lililotokea humu Bungeni mapema.

Waheshimiwa Wabunge, mwongozo wa mwisho ni mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Angellah Kairuki kuhusu hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, kwamba ukurasa wa pili mpaka wa tatu, nadhani na wa nne, hotuba inaishia pale, yale maneno ya utangulizi, kwamba ni maneno ya uongo.

Mheshimiwa Angellah Kairuki amejielekeza zaidi kwenye hoja ambayo iko ukurasa wa tatu inayohusu uchakachujaji wa matokeo.

Waheshimiwa Wabunge, pia ukurasa wa pili, nadhani wote tumeshagawiwa hizi nakala, ukurasa wa pili alioombea Mheshimiwa Angellah Kairuki, nadhani wote tuko hapo, *paragraph* ya mwisho ina hayo maneno hapo. Pia ukienda ukurasa wa tatu na ukurasa wa nne una maneno ambayo yananitaka nitoe maelezo kidogo ili kuweka kumbukumbu sawasawa.

Waheshimiwa Wabunge, ukurasa wa tatu, sentensi ya mwisho inasomeka hivi: "Aidha, kutokana na hofu ya kukosolewa kutokana na kutojamini katika mambo inayoyafanya; Serikali sasa imeanza kuingilia hotuba za Wasemaji Wakuu wa Upinzani na kuzifanyia *copyright* kinyume kabisa na Kanuni za Bunge hili." (*Makofi*)

Ukurasa wa nne, sentensi ya mwisho pia, inaanza kwa maneno yafuatayo, inasema: "Kwa hiyo Mheshimiwa Spika; kitendo kilichofanyika tarehe 16 Mei, 2016 cha kuiondoa mezani hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili ikachakachuliwe na Kamati ya Kanuni, ni kinyume kabisa na Kanuni za Bunge na ni kinyume kabisa na mila na desturi za uendeshaji wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola."

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka tarehe 16, Mheshimiwa Mwenyekiti aliagiza Kamati ya Kanuni ikutane ili iweze kuiangalia hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani na namna ambavyo inaendana na Kanuni ama kuvunja Kanuni. Alipoagiza hivyo, Kamati ya Kanuni ilienda kukutana ikamletea Mwenyekiti mapendekezo yake ambayo mapendekezo hayo aliyasoma hapa ndani.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ili kuweka kumbukumbu sawasawa, twende Kanuni ya 5(1) ambayo inasema hivi: "Katika kutekeleza majukumu yake yaliyotajwa katika Ibara ya 84 ya Katiba, Spika ataongozwa na Kanuni hizi na pale ambapo Kanuni hazikutoa mwongozo, basi Spika atafanya kazi kwa kuzingatia Katiba, Sheria nyingine za nchi, Kanuni nyingine zilizopo, maamuzi ya awali ya Maspika wa Bunge pamoja na mila na desturi za Mabunge mengine."

Waheshimiwa Wabunge, wachache wenu mlikuwa Wabunge huko nyuma, mwaka 2013 mambo kama haya yalishaamuliwa mara tatu. Moja, yaliamuliwa kwamba Kamati ya Kanuni ikakutane ili ikaangalie ile *report* na ikaleta mapendekezo kwamba ile *report* ama hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani ifutwe maneno fulani na ndicho kilichofanyika. 2013, *Hansard* ziko hapa.

Maamuzi mengine yaliyotolewa hiyo hiyo 2013 katika pia vikao vya bajeti, ilitokea ugomvi humu kati ya chama cha CHADEMA na CUF kwa yale maelezo yaliyokuwa yametolewa na Mheshimiwa Ezekia Wenje. Sasa katika kujaribu kutatua ule mzozo, Spika aliagiza Kamati ya Maadili ikakutane kwa sababu jambo lililokuwa linagombaniwa lilikuwa linahusu maadili na uzuri wake Mheshimiwa aliyesoma hotuba hii ya Kambi Rasmi ya Upinzani wakati huo alikuwa Mbunge na alikuwepo na jina lake lipo kwenye hizi *Hansard*.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo, kwa kutumia hayo maamuzi ya Maspika wa Bunge lile ambalo lilikuwepo 2010 - 2015, naagiza, kuanzia ukurasa wa pili, wa tatu na wa nne, maneno yale ambayo yako kinyume na Kanuni yaondolewe. *(Makofi)*

Kwa kuwa nimeagiza kwamba *records* lazima zikae sawasawa, ile hotuba iliyoagizwa kuondolewa hapa mezani ilikuwa na mambo matatu. Jambo la kwanza lilikuwa linakwenda kinyume na Kanuni ya 64(1)(c) na ndivyo Mwenyekiti alivyosoma. Kanuni hiyo inakataza Bunge hili kujadili jambo ambalo lilikwishaamuliwa, hilo ni moja.

La pili, ilikuwa ni kinyume na Kanuni ya 117(10) na 12 ambazo ikiwa Kamati ya Bunge inashughulikia jambo hilomtu haruhusiwi kulisema kwa sababu Kamati inafanya shughuli zake kwa faragha.

Jambo la tatu lilikuwa linajadili na kichwa cha habari kilisema, tabia ya Rais na Kanuni ya 64(1)(e) inasema ukitaka kujadili mwenendo wa mtu yeyote, pamoja na Rais lazima ulete hoja mahususi. Kwa hiyo, kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawasawa, hakuna mtu aliyeikataza hiyo hotuba lakini kwa maeneo yaliyokuwa yanavunja Kanuni zetu za Bunge yasingeweza kusomwa hapa ndani kwa mujibu wa maelezo ambayo nimeshayatoa kuhusu maamuzi yaliyopata kutolewa na Bunge lililopita.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema haya, wapo wageni walioingia baadaye na hawa ni wageni 50 wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni ma-secretary kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanaoshiriki mkutano unaofanyika hapa Dodoma, wote wasimame kwa pamoja. Karibuni sana wageni wetu, tumefurahi kuwaona. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi kamili leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*



*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:** Hoja za Serikali; hoja ya Waziri wa Elimu Sayansi Teknolojia na Ufundi kwamba sasa Bunge likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa Mwaka wa fedha 2016/2017.

### **HOJA ZA SERIKALI**

#### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 - Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaanza majadiliano kuna tangazo moja hapa naomba nilisome. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika kwa mamlaka aliyopewa chini ya kanuni ya 116(3) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari 2016 amefanya mabadiliko ya baadhi ya Wajumbe wa Kamati za Bunge kwa kuzingatia maombi ya Wajumbe husika pamoja na mahitaji mapya yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa shughuli za Kamati za Bunge. Mabadiliko haya yamefanywa tarehe 24 Mei, 2016. Wabunge wote watagawiwa nakala za waraka wa Mheshimiwa Spika leo hii humu ukumbini.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala wetu na tunaanza na Mheshimiwa Joseph Hasunga na baaadaye Mheshimiwa Edwin Sanda na Mheshimiwa Juliana shonza akae tayari.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza jina langu naitwa Japhet Hasunga, siyo Joseph.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kwanza kushukuru kwa kupata nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii. Pia napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa na mchanganuo mzuri ambao ameuwasilisha leo hii, kwa kweli nimefurahi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuipongeza Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa uchambuzi wa kina walioufanya na kuiwasilisha katika Bunge lako Tukufu. Kwa kweli ni nzuri sana na imejenga msingi mzuri wa nini kinatakiwa kufanyika katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuchangia katika Sera ya Elimu ya shule za msingi na sekondari ya mwaka 2014. Sera hii ni nzuri sana ambayo imeandaliwa na iliwasilishwa na ilishirikisha wadau mbalimbali ambayo

imeweka bayana hatua ambazo zinatakiwa kuchukuliwa na Serikali kuhakikisha kwamba nchi yetu inabadilika kwa hali tuliyonayo na kwenda mahali ambapo ni pazuri. Elimu ni kitu muhimu sana, elimu ndiyo msingi mkubwa wa maendeleo ya nchi yoyote na hii ndiyo itakayotusaidia kutufikisha kuwa nchi ya kipato cha kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika elimu hii sasa hivi vijana wetu wengi ambao wamekuwa wanamaliza elimu ya msingi, wanamaliza wakiwa ni wadogo sana, wengi wanaanza darasa la kwanza wakiwa na miaka mitano, miaka sita wanamaliza shule ya msingi wakiwa na miaka kumi na mbili, kumi na tatu. Hivyo hawa-qualify kujitegemea wala hawawezi kujiajiri wala kuajiriwa, kwa sababu itakuwa ni kinyume na sheria za ajira. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hilo sera hii ilikuwa inasema elimu ya msingi sasa itajumuishwa na elimu ya sekondari mpaka kidato cha nne. Mtoto akianza shule ya awali aende moja kwa moja shule ya msingi, akimaliza shule ya msingi anaunganisha moja kwa moja kwenda kidato cha kwanza. Kwa hiyo, ina maana watoto wote sasa watakuwa wanakwenda mpaka kidato cha kwanza wanamaliza mpaka kidato cha nne. Hapa mpaka wanamaliza sasa watakuwa wamefikisha umri ule ambao kidogo wanaweza wakaanza kujitegemea au wakaajirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili nafikiri ni la msingi sana. Sasa nataka Wizara wakati wa majumuisho itupe maelezo ni hatua gani au mikakati gani wameiweka kuhakikisha kwamba sera hii sasa inaanza kutekelezwa kama ambavyo tulikusudia. Kwa sababu ifikapo mwaka 2018 ni kesho kutwa tu tutakuwa tumefika. Tungependa kikifika kipindi hicho watoto wote sasa wawe na uwezo wa kufika hadi kidato cha nne, badala ya kuishia darasa la saba ambapo wanakuwa kidogo hawajaandaliwa vya kutosha hilo ni la msingi sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kuna suala la watoto wanaopata mimba wakiwa shuleni. Mimba inapatikana kwa bahati mbaya, nasema ni kwa bahati mbaya siyo kwa makusudi, watoto wengi wamekuwa wakipata mimba kwa bahati mbaya mashuleni. Sasa watoto hawa wanapopata mimba, ni bahati mbaya unakuta kwamba baada ya muda wanaondolewa mashuleni kwa sababu eti wana mimba. Hii inakuwa ni kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini pia ni kinyume na dira ya Wizara ya Elimu ambayo imeitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ninukuu, ukurasa wa nne pale, ameeleza dira vizuri sana, kwamba dira ya Wizara ni kuwa na Mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa, stadi, umahiri, uwezo na mitazamo chanya ili kuweza kuchangia katika kuleta maendeleo ya Taifa. Hivi ndivyo dira

inavyosema na hii dira haijabagua mtoto wa kike wala kiume. Kwa hiyo ina maana watoto wote ni muhimu na mtoto wa kike sasa hivi ndiyo muhimu sana kumwelimisha kuliko hata mtoto wa kiume. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kabisa kwamba hawa watoto ambao kwa bahati mbaya wanapata mimba basi wapewe nafasi ya kuendelea kusoma pale wanapokuwa wamejifungua ili kusudi waendeleo kuelimika maana nao ni Watanzania kama Watanzania wengine. Hili ni la msingi sana na litatusaidia kuhakikisha kwamba sasa jamii yote ya Kitanzania Watanzania wote wanapata elimu sawa na ile ambayo tulikuwa tunakusudia. Nadhani kwamba hilo ni suala la msingi sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa nichangie katika hii Wizara ni kuhusu Mitaala. Mitaala ya elimu yetu kuanzia shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu lazima hii mitaala iangaliwe kwa undani ili iendane na maarifa na stadi zinazohitajika sokoni. Iwaandae vijana wetu kujitegemea, iandae wataalam watakaochangia na watakaoweza kushiriki katika maendeleo ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa mitaala yetu haijaainisha vipaumbele ambavyo Taifa kama Taifa linahitaji. Watu wanasoma tu wengine wanajiunga katika vyuo mbalimbali, sasa vyuo hivi viendane na mahitaji halisi ya soko, ndiyo itatusaidia sana kwenda na wakati. Hili ni la muhimu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa nilichangie ni kuhusu tafiti yaani *research* na *project* mbalimbali ambazo vyuo mbalimbali vimekuwa vikiwapa vijana wanafanya katika maeneo mbalimbali. Sasa hivi vyuo vingi havijatilia mkazo sana katika upande wa utafiti, vyuo vikuu vingi havifanyi utafiti wa kutosha. Bila kufanya utafiti wa kutosha hatuwezi kupata wataalam, hatuwezi kupata maendeleo halisi. Lazima vifanye utafiti na Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kuhakikisha hao wataalam wetu wanafanya utafiti. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti hizi ndizo zinatakazosaidia kuboresha mazingira na kuleta maendeleo katika nchi yetu. Kuna maeneo mengi ambayo vijana huwa wanafanya na kuna baadhi ya *project* ambazo vijana huwa wanapewa wakiwa mashuleni. Wanafanya *project* nzuri sana. Naishauri Wizara iandae utaratibu mzuri wa kuhakikisha zile *project* ambazo vijana wanafanya wakiwa vya zingine zinafaa sana kuendelezwa, zingine zingefaa sana katika kuanzisha viwanda vidogo na kadhalika. Wanafanya ubunifu mzuri sana ambao nafikiri ni muhimu sana kama Wizara itakuwa na utaratibu mzuri, wa kuziangalia hizo *project* na kuangalia namna ambavyo Serikali inaweza ikazi-fund ili ziweze kuchangia maendeleo ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa nichangie ni kuhusu Vyuo vya Ufundi, Vyuo vya VETA, pamoja na Vyuo Vikuu, Jimbo langu ni Makao Makuu ya Mkoa mpya wa Songwe na hiyo naipongeza Serikali sana. Pamoja na kuwa ni Makao Makuu ya Mkoa sasa hivi hatuna chuo hata kimoja, hatuna chuo cha Serikali wala cha watu binafsi. Sasa ni wakati muafaka naomba Wizara yako iangalie utaratibu, iweke utaratibu wa kuhakikisha kwamba Jimbo la Vwawa hasa Wilaya ya Mbozi tuna jenga chuo cha VETA ambacho kitawaajiri vijana mbalimbali waliopo katika Wilaya ile. Wale vijana wako maeneo mengi, iwe ni katika fani mbalimbali wapate ule ujuzi ambao utasaidia sana katika kuchangia maendeleo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Vyuo vya Elimu ya Juu kikiwemo Chuo Kikuu Huria, tungeomba vianzishe matawi haraka ili wananchi wale ambao ni wengi sana katika ile Wilaya waweze kupata elimu ile ambayo inahitajika katika hili eneo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa nichangie ni kuhusu suala la hii *SDL*, hii kodi ambayo sekondari za watu binafsi na vyuo vya watu binafsi vinatakiwa kulipia, *SDL ya five percent*. Kwanza naomba ku-declare interest kwamba mimi ni mdau na nina maslahi katika hili, hili suala sasa hivi sekondari zote za watu binafsi pamoja na vyuo binafsi vinaendelea kudaiwa *SDL* kwamba lazima vilipwe, wakati navyo vinatoa mafunzo ya ufundi ambao vinawaandaa vijana wale wale na sera za nchi hizi zinasema elimu siyo sehemu ya biashara, elimu ni kutoa huduma. Sasa kama ni huduma kwa nini vidaiwe *SDL* badala ya kupata mgao kutoka Serikalini unaotokana na hizi fedha, wanaambiwa wao wachangie. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili kwa kweli halikubaliki kabisa, ningependa kabisa kabisa kwa dhati Serikali ili iangalie upya ili hizi shule za watu binafsi, vyuo vya watu binafsi, vipewe msaada, vipewe mgawo wa hii *SDL* ili viweze kujenga ujuzi, stadi na maarifa mbalimbali yanayohitajika katika nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri haya masuala ya msingi sana na naamini tukiweka misingi mizuri ya kuimarisha elimu yetu nchi yetu itapiga hatua sana. Wale wanaobeza kwamba nchi yetu elimu yetu inashuka, hapana haishuki tuendeleo kuiboresha, tuweke mikakati mizuri, tuiimarishe, naamini nchi yetu itapiga hatua sana. Wenzangu wale ambao wanategemea kwamba eti mwaka 2020 tutaishia hapa labda CCM itaporomoka, nataka niwaambie CCM mwaka 2020 tutashinda huenda Viti vyote vya Ubunge kwa sababu ya kazi nzuri ambayo tutaifanya. Hii Wizara naomba ifanye kazi nzuri na mambo yatakwenenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Hasunga. Sasa hivi tunaendelea na Mheshimiwa Ester Mmasi.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii adhimu nami niweze kuchangia kwenye Bunge lako Tukufu. Kabla sijajikita kwenye hoja kwanza kabisa ningependa kumpongeza Rais wa Jamhuri wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kutupatia Profesa Joyce Ndalichako. Profesa Ndalichako namfahamu, mama huyu si Mwanasiasa, kama ni siasa tumfundishe sisi humu ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa Mama Joyce Ndalichako huyu ni mama ambaye ni *result oriented character*, hivyo ndivyo ninavyoweza kum-define. Kwa hiyo, Profesa Ndalichako nakupa moyo sana, kazi yako inaonekana na kwa hili tunamrudishia sifa na heshima Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye hoja za msingi. Sasa hivi pamoja na kwamba Mheshimiwa Rais ameonesha nia dhahiri ya kuweza kuongeza fursa za mkopo kwa vijana wetu wa vyuo vya elimu ya juu, kwa maana ya kwamba kuongeza fursa za rasilimali fedha ili vijana wetu waweze kupata mikopo na kuweza kujimudu kule mashuleni, lakini pia tumekuwa na changamoto kubwa na Mheshimiwa Waziri hapa amekiri, ya masuala mazima ya urejeshaji wa fedha hizi za mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jana tu nimepata taarifa kwamba katika *target* za Wizara hii au Taasisi hii ya *Loans Board* ilikuwa ipate bilioni 37 hadi ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha huu yaani tarehe 30 Juni, lakini mpaka mwezi jana ninapoongelea tarehe 30 Aprili kumekuwa kuna marejesho ya shilingi bilioni 22 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nimsaidie Mheshimiwa Waziri, nimesikia hapa akisema pengine ni namba ya *defaulters*, *defaulters* wamekuwa ni wengi. Mheshimiwa Waziri naomba nikiri hapana, yawezekana ndiyo kuna namba ya *defaulters* lakini tatizo si hivyo tunavyoliona leo. Tuna tatizo kubwa ambalo nafikiri bado halina *commitment* ya Serikali, tatizo hili ni masuala mazima ya ajira kwa kijana mhitimu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tumeshuhudia Mawaziri wetu wengi hapa wamekuja wamefanya mawasilisho ya bajeti. Hata hivyo, nilikuwa makini, *of course* nilitoka kidogo, niliporudi nikasikiliza vyema, mikakati ya kumtoa kijana aliyehitimu kuingia kwenye soko la ajira. Nikasikia mipango mingi, nimesikia pale kuna masuala ya *skills mismatch program* ambayo hii ni mkakati wa kuwajengea uwezo vijana wahitimu kwenda kuingia kwenye ajira. Hapa nimejiuliza kijana yupi kwa ajira ipi tuliyoandaa hapa? Tunahitaji *commitment*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumesikia *plan* ambayo imetoka Wizara ya Ardhi kwamba, kutakuwa na *land tenant support system* ambayo ina mpango wa kurasimisha kwa kuwapa wakulima wadogowadogo hati za kimila ili waweze kukopesheka katika mabenki ambayo ni mabenki ya *TIB*, ambayo kuna Mabenki ya Kilimo. Hata hivyo, nikajiuliza hili kijana mhitimu leo anafaidikaje kwenye dirisha hili la *TIB*, kijana huyu anafaidikaje kwenye mkopo huu ambao tunaambiwa wa Benki ya Kilimo kwa zile rasilimali fedha zilizowekwa pale bilioni 60? hii inakatisha tamaa, tunahitaji *commitment* ya Serikali kuweza kuwanasua vijana wetu kwenye suala zima la changamoto ya ajira. Tusikae tukijikita kwenye masuala ya *defaulters*, hakuna kitu kama hicho kuna zaidi ya hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumesikia maelekezo kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu akitoa maagizo pale TAMISEMI kwamba, isitokee Ofisi ya TAMISEMI inapitisha mpango wa ardhi na matumizi *unless* kutaonesha ni kiasi gani cha ardhi kitatengwa katika kusaidia wakulima au vijana hawa kuingia kwenye suala zima la kilimo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kutenga ardhi tu mbona haitoshi pembejeo ziko wapi? Inasikitisha sana. Mimi nimetoka Kilimanjaro, vijana wangu pale wameshuka mabega, vijana wamepata vilema vya mabega, wamekuwa *potters* katika kubebea wazungu mizigo yao. Jana tumesikia hapa Kilimanjaro ilivyobarikiwa na suala zima la maliasili, lakini vijana wale wamekata tamaa, mabega yamewashuka, wameishia kuvuta bangi, ni nini hiki? Tunahitaji *commitment* ya Serikali kwenye suala zima la ajira. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona pale na nitamfuata kaka yangu Japhary anisaidie, Kilimanjaro nimeona pale kuna *White Elephant* moja imejengwa na *NSSF*, kama kweli kulikuwa na *visibility study* katika jengo lile, Jengo lile limejengwa kwa bilioni 67 lakini mpaka leo ninavyoongea, mwaka wa tatu huu, kama kurudisha lile jengo siyo zaidi ya bilioni moja. Inasikitisha sana mipango na sera hai-*reflect* changamoto tulizonazo katika suala zima la ajira. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesimama Waziri hapa leo akatueleza changamoto ambayo imetokana na, niseme tu mipango haiko makini katika taasisi zetu hizi. Tumesikia suala la *Saint Joseph* ambalo naamini kila mtu atakayesimama hapa ataliongela kwa uchungu wa aina yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TCU* naifahamu vizuri, nimefanya kazi Kurugenzi ya Elimu ya Juu na nilifanya pale niki-*head* ile *section* baada ya Mama Sawasawa kuondoka. Mheshimiwa Mama Ndalichako mume wake amenifundisha kazi, Profesa wangu alikuwa pale juu asubuhi hii. (Makofi)



Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi ni mdau na nasema haya kwa sababu nimeyafanyia kazi ofisi kwangu. Hii TCU imegeuka kibanda cha kuchangisha upatu kwa wananchi wasio na uwezo. Pale TCU leo unaenda kusoma nje ya nchi ukirudi ukiwa una *degree* yako moja unatakiwa utoe shilingi 50,000, kwa *masters degree* 150,000, kwa *PHD* unatakiwa utoe karibu 200,000. Unaambiwa hii kupata *accreditation letter*, *accreditation letter* ipi na wakati kuna *list* ya *accredited institution* unapata kwenye mtandao wa TCU kupata not even *authentication letter* hii ni *accreditation letter* ambayo tayari pale kuna *list* unapata. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaumiza sana TCU hawa wanaenda leo kuwakagua Saint Joseph tumeona, badala ya TCU wao kwenda kuwakagua wanawa-charge mpaka fees, inasikitisha sana, *audit fee* Saint Joseph wanalipa na wamelipa kwa miaka yote, leo hii wanawarudisha wanafunzi 489 majumbani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu wanapata *psychological torture* na mimi kama kijana mwenzao ambaye nimesoma kwa uchungu, sitakaa kimya kwenye Bunge lako hili Tukufu, nasema kwa uchungu, naomba vijana sasa waangaliwe, hatutakubali na hatutakuwa wa kupiga makofi kama vijana hawatatengewa hazina yao, kama vijana hawatapewa stahiki yao katika hii nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoongelea TCU kuna masuala yanayonisikitisha sana, tumeambiwa hiki ni kitengo katika kuangalia ubora wa shule, tunasema *quality assurance*, nimejiuliza wana-*insure* nini? Mimi nimefanya ofisi ya *postgraduate*, nilikuwa napokea *dissertations* zote, wote mliopita hapa, nimekaa nimesoma *dissertation* ya kila mmoja wenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti inasikitisha sana, unakuta *dissertation* moja inakuwa *submitted* pale OUT chuo kishiriki, *the same dissertation* inakuwa *submitted in university of Dar es Salaam*, tunasema tuna Board inayo-*insure quality for good sake*, no haiwezekani. Tumeona vitu vya kutisha kwenye Board hii, wamekaa wanacheza mchezo wa kibati halafu wanakuja kusema wana-*insure quality, for good sake*, hili tutalisema bila kumumunya maneno. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wamesimamishwa hawa, tumeambiwa pale Bodi imesimamishwa lakini haitoshi. Kuna *psychological torture* ya vijana 489 wako mtaani. Inaumiza sana sisi tumezaa matumbo yetu yamezaa tuwasemee hawa watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo vitu vinavyosikitisha, leo anatoka kijana amepata *discontinuation* kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; lakini mwanafunzi huyo huyo anakwenda kuwa *admitted* kile Chuo cha pale,



kinaitwa *not CBE*, wanaenda kuwa *admitted* kwenye vyuo vingine na hali wameshafeli na wanapewa mkopo, hii inasikitisha sana. Una-*transfer credit* za mwanafunzi ambaye ameshafeli na Bodi inamwongezea mkopo, hii tunasema hapana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao vijana waliokuwa *misplaced* kwenye hili, inabidi tulisemee. Leo kuna vijana waliomaliza kidato cha nne wanakwenda kusoma *degree* ya ualimu, kwenye fani ya sayansi, unampeleka pale Chuo Kikuu cha Dodoma; *for good sake* tunawafahamu, baadhi wako *funded* na *World Bank*, lakini wapo wengine wamekuwa *misplaced* baada ya mkorogano wa Chuo cha *Saint Joseph*, wamepelekwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unataka kutengeneza Mwalimu, *ethics* za ualimu anazipata wapi pale kwenye mihadhara ya Chuo Kikuu? Hatuwezi kujenga Taifa lililoelimika, hatuwezi kujenga uchumi wa nchi wakati tunapuuza suala zima la ujuzi na maarifa kwa vijana wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kupata maelezo ya kina, juzi Mama Sitta alisimama hapa akashika shilingi kwenye Bunge lililopita, tulidai tuwe na *Teachers Professional Board*, hili nitalidai pia, kwa udi na uvumba katika Bunge hili. Tunahitaji kuwa na chombo ambacho kita-*insure quality* ya elimu ya juu kwa vijana wetu hawa, inasikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimetoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, napenda ku-*declare interest*. Kuna suala zima tunaita *institution charter*, kile ni kivuli cha kuficha maovu ndani ya vyuo vikuu. Nilimwomba Mheshimiwa Waziri tushuke twende naye tukaone maovu yanayofanyika kule, viko vitu vya kutisha. Unakuta kiongozi wa Chuo ana magari matatu, ana gari la kubebea mbwa chakula, la kumpeleka mama kwenye *kitchen party* na la baba. Hatuwezi kukubali, wafanyakazi wetu wanateseka...(Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mmasi muda wako umekwisha. Tunaendelea na Mheshimiwa Juliana Shonza na baadaye Mheshimiwa Kangi Lugola ajiandae.

**MHE. JULIANA DANIEL SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nichukue nafasi hii kushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia, lakini vile vile nimpongeze Waziri wa Elimu pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite moja kwa moja kujadili suala la Bodi ya Mikopo. Tatizo kubwa ambalo linawa-face wanafunzi wengi wa elimu

ya juu ni suala la mikopo. Tumeshuhudia katika vyuo vingi kwamba wanafunzi wamekuwa wakifanya maandamano, wakipinga Sera ya Bodi ya Mikopo ambayo kwa kweli ni tatizo kubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano, tutakumbuka miaka ya nyuma ukisikia migomo katika Vyuo Vikuu, ilikuwa ni migomo ambayo inapinga sera. Kuna mgomo ambao ulifanyika 1969 ulikuwa ni mgomo wa kupinga sera ya wanafunzi kwenda *JKT*, kuna mgomo mwingine ukafanyika miaka ya 90, ambao moja kwa moja ilikuwa ni kupinga, suala la *cost sharing* katika elimu ya juu. Nisikitike kwamba migomo ya sasa hivi imekuwa ni tofauti, wanafunzi wa sasa hawapingi masuala ya sera kama ambavyo ilikuwa zamani. Agenda yao kubwa ni Bodi ya Mikopo, suala la mikopo limekuwa ni jipu kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia chimbuko la matatizo ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu ni Sheria ambayo imeunda Bodi ya Mikopo. Kuna vigezo ambavyo vimeainishwa, ukisoma Sheria ya hiyo, kifungu cha 17, kimeainisha vigezo vya mwanafunzi kuweza kupata mikopo, kigezo cha kwanza awe ni Mtanzania. Sote tunatambua kwamba zaidi ya asilimia 90 ya wanafunzi ni Watanzania, kwa hiyo, bado hiki sioni kama ni kigezo cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kigezo kingine lazima awe ni mwanafunzi ambaye anaendelea na amefaulu katika mwaka husika, bado siyo kigezo. Kigezo kingine cha tatu, lazima awe ameandika barua, sidhani kama kuna mwanafunzi nchi hii ambaye atashindwa kuandika barua. Kigezo kingine ni lazima mwanafunzi huyo awe amedahiliwa katika Chuo ambacho kimesajiliwa na Serikali. Sote, tunashuhudia katika nchi ya Tanzania kwamba, kuna utitiri mkubwa sana wa vyuo. Kwa hiyo, suala la mwanafunzi kuweza kudahiliwa bado siyo kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa makini hivi vigezo ndivyo vinavyopelekea kuwa na migomo, wanafunzi wanalalamika, wale ambao wanastahili kupata mikopo hawapati na wale ambao hawastahili mara nyingi ndiyo tumekuwa tukishuhudia wakipata mikopo. Kwa hiyo, napenda kuishauri Serikali, ni vyema ikaangalia hili suala kwa umakini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna mkanganyiko mkubwa sana katika suala hili la Bodi ya Mikopo. Suala la kwanza, ni suala la kimtazamo, kwamba kama Bodi yenyewe haijajitambua, kwamba ule mkopo wanaotoa je, ni mkopo au ni hisani na ndiyo maana mpaka leo hii tunashuhudia kwamba hakuna vigezo ambavyo wameviweka, ambavyo mwanafunzi akipata mkopo, vinambana mwanafunzi huyo aweze kurejesha ili wanafunzi wengine waweze kwenda kutumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkanganyiko wa pili, kwamba hata yule anayepewa mikopo, bado yeye mwenyewe hajajitambua, kwamba je, huu ni mkopo au ni hisani na tumeshuhudia Waheshimiwa Wabunge wengi ambao tupo katika Bunge hili tumesomeshwa na hizi kodi za Watanzania, lakini tuulizane ni nani ambaye ameweza kurudisha mkopo huo. Hata Mheshimiwa Waziri ameligusia asubuhi, lakini kusema kwamba Wabunge twende kulipa bado halitoshi, kusema kwamba atatoa majina kwenye magazeti bado haitoshi; lazima kama Wizara, kama Bodi ya Mikopo, mje na mkakati, mje na *system* ambayo itambana yule ambaye anapewa mikopo na Serikali ili basi aweze kurudisha kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia hata kwa wafanyakazi wanaofanya kazi Serikalini, wanasema kwamba hawajaambiwa wameanza kukatwa, wanashuhudia tu kwenye *salary slip* wamekatwa, hawajui mikopo hiyo watakatwa mwisho lini. Hii ni changamoto kubwa ya Bodi ya Mikopo na inaonesha kwamba Bodi kimsingi haijajipanga kwa suala hili la kuhakikisha kwamba, hizi fedha wanazozitoa ziweze kuwa *revolving fund*, ili mtu anapopata na wanafunzi wengine waweze kuja kuzipata. Ndiyo maana tunashuhudia migomo katika nchi yetu haiishi kwa sababu Bodi ya Mikopo haijajipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ya Bodi ya Mikopo, tumeshuhudia kwamba mikopo hiyo inatolewa Dar es Saalam. Nimeshindwa kuelewa , kwamba Bodi ya Mikopo ipo Dar es Salaam, mwanafunzi atoke Mbozi, Ileje, mimi nikienda Dar es Salaam, watajuaje kama kweli Shonza ana sifa ya kupata mikopo. Siyo rahisi kuweza kumtambua, kwa hiyo hii nayo ni changamoto kubwa sana ambayo kama Wizara ihakikishe kwamba inalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuishauri Serikali pamoja na Wizara, Mama yangu Ndalichako tunatambua kwamba wewe ni mweledi, una uwezo mkubwa, lakini bado kuna upungufu mkubwa katika Wizara hii ya Elimu. Nishauri Serikali, kwanza sisi kama Wabunge lazima tukubaliane kwamba, mahali tulipofika mpaka sasa hivi ni ngumu kwa Serikali kuweza kutoa michango kwa asilimia mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipofika ni ngumu na wala tusijidanganye, lazima Serikali ije na njia mbadala kuhakikisha kwamba hizi fedha ambazo zilikwishanza kutolewa miaka mingi, kama zingekuwa *revolving fund*, leo hii tusingekuwa tunajadili bajeti ya mikopo humu ndani, kwa sababu fedha ambazo zimeshatolewa ni nyingi na zingekuwa zimeshazunguka na zingesaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka kuishauri Serikali, la kwanza ni vyema wakahakikisha kwamba wanaanzisha mfumo wa kutoa *scholarship*, kwa wanafunzi wanaofanya vizuri, kwamba kigezo pekee cha kuweza kupata

mkopo, iwe ni ufaulu. Mwanafunzi ambaye amekaa kule Mbozi, ajue kabisa kwamba ili nipate mkopo, lazima nipate *division one*. Tofauti na ilivyo sasa hivi, kwamba aliyepata *division three* anapata mkopo, aliyepata *division one* hapati mkopo. Hiyo ni changamoto kubwa sana, kwa hiyo, kama Wizara tuwe na utaratibu wa kuzawadia bidii, itatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nataka kuishauri Serikali ihakikishe kwamba inatoa mikopo asilimia mia kwa zile taaluma ambazo ni taaluma za huduma, kwa mfano Walimu pamoja na Madaktari. Hii itasaidia pia zaidi kuweza kuleta motisha, katika kozi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu, niombe pia Serikali, iangalie namna ya kuhakikisha kwamba Bodi ya Mikopo isihusike moja kwa moja katika kutoa mikopo hiyo. Ni vema mikopo ikatolewa katika Wilaya zetu, kwa sababu kule kwenye Wilaya kuna Taasisi za kifedha, leo hii Serikali imeingia taaluma ambayo naweza nikasema kwamba siyo ya kwake, ni taaluma ya kibenki. Taaluma ya kukopa na kukopeshana ni taaluma za kibenki siyo taaluma ya Serikali. Kwa hiyo Serika iache kufanya biashara, kwa kupitia Bodi ya Mikopo na kuna Taasisi ambazo zipo ambazo ni za kifedha, ziachiwe kazi hizo, hao ndio waratibu zoezi zima la kutoa mikopo, kwenye Wilaya zetu, kwa kuangalia kwamba ni nani anafaa ni nani ambaye hafai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo, naamini kwamba itasaidia ili fedha hizo ziweze kuzunguka kama ambavyo tumeshuhudia nchi za wenzetu suala la mikopo mzazi anafanya jitihada kuhakikisha kwamba anamwepusha mtoto wake na mikopo, lakini Tanzania kwa sababu ni bure, ndiyo maana kila mtu ambaye ana uwezo, asiye na uwezo anaomba apate mkopo, kwa sababu ni bure. Naomba suala hili lifanyiwe kazi na likifanyiwa kazi masuala ya migomo yatakuwa yamekwisha katika nchi yetu, lakini wananchi wengi na wanaostahili watapata nafasi ya kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nizungumze kwamba, nimesikiliza kwa makini sana hotuba ya Kambi ya Upinzani. Wamezungumza kwamba, Serikali ya Chama cha Mapinduzi ndiyo ambayo inawanyanyasa wanafunzi ambao ni wa UKAWA. Mimi niseme kwamba, hilo siyo kweli, mimi mwenyewe nilikuwa ni mwanafunzi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na nilikuwa upande wa CHADEMA, nilishawahi kuongoza migomo na nikakamatwa nikaenda ndani siku mbili, lakini hakuna siku ambayo nilifukuzwa chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote ni mashahidi, hata Mama yangu ambaye amewasilisha hotuba hiyo tulikuwa naye pale Chuoni na alikuwa aki-support, hakuna siku ambayo mwanafunzi amerudishwa. Nami kama mwanzilishi wa CHASO katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mama yangu alikuwa akini-

support vizuri sana na wala sikuwahi kufukuzwa. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge tuwe wa kweli. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile suala la kusema kwamba Mheshimiwa Nape amezomewa Mwanza, naomba Waheshimiwa Wabunge, sote humu ndani ni waelewa na kwa sisi ambao ni waelewa wa haya mambo tunafahamu, kwamba haya mambo wanapanga nani asiyejua CHADEMA kwamba wanawapa viroba vijana waende kuwazomea viongozi wa Chama cha Mapinduzi, nani asiyejua? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Nape, wewe endelea na kazi yako, piga kazi Watanzania tuko nyuma yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Kangi Lugola na Mheshimiwa Dkt. Eli Macha, pamoja na Dkt. Suleimani Ally Yussuf wajiandae.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kutoa mchango wangu kwenye hotuba ya bajeti, ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda pengine nianzie alipomalizia Mheshimiwa Shonza, amenikumbusha, hii hoja ya kwamba UKAWA wananyanyaswa vyuoni, ni bahati nzuri sana nimkumbushe Mheshimiwa Ally Saleh na Mheshimiwa James Mbatia, nikiwa pamoja na mimi, tulikuwa Chuo Kikuu, tukaonekana tunashiriki mambo ya siasa, tukashughulikiwa na Serikali, hatukuwa UKAWA. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala la Serikali kushughulika na wanafunzi kwenye vyuo, ni jambo lingine na suala la kushughulikia wanafunzi kivyama si sahihi kulihusisha na chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru sana hotuba nzuri ya Mheshimiwa Ndalichako.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kangi Lugola naomba ukae. Mheshimiwa Mbatia taarifa.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lugola namheshimu sana, naomba aweke rekodi sahihi, wanafunzi tuliofukuzwa 10 Chuo Kikuu yeye hakuwa mmojawapo. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kangi Lugola unapokea hiyo taarifa?

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Sikuwa mmojawapo kwa sababu mimi sikuwa *lean leader*, yeye ndiye alikuwa *lean leader* ndiyo alishughulikiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kangi Lugola endelea.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti imekuja katika wakati ambao ni muafaka, wakati ambao tunataka kuzungumzia suala la elimu kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na ukurasa wa 24 wa hotuba. Ukurasa wa 24 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, imejaribu kutoa majibu, kwenye hoja ambayo Mheshimiwa Chumi aliiwasilisha Bungeni hapa kama hoja binafsi, juu ya wanafunzi 489 ambao wanaonekana kwamba hawana sifa za kudahiliwa kusoma kozi ya Ualimu wa Sayansi katika Chuo Kikuu cha Mtakatifu Joseph.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie ukweli Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Wabunge naomba mnisikilize kwa makini, Wizara ya Elimu imekuwa na tatizo la kubomoa na kufumuafumua mifumo ya elimu katika Taifa letu. Mambo haya yanafanywa, kila Waziri anayekuja, anafumua mifumo iliyotengenezwa na Mawaziri wengine. Ni lini tutakuwa na mifumo ambayo inaheshimika? Ina maana kwamba, kwenye Wizara ya Elimu, hawa ambao ni Maprofesa wameshindwa kabisa kuja na mitaala, mifumo ambayo itatupeleka miaka mingi bila kufumuliwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uingereza tunasema kuna *Cambridge*, mpaka leo *Cambridge* haifi, hivi Tanzania tumeshindwa kuwa na *Cambridge* ya Watanzania; kila anapokuja Waziri anafumua mifumo ya elimu. Kwa nini nasema mifumo ya elimu inafumuliwa? Inaniuma sana baada ya kuwa na matatizo ya Walimu wa sayansi katika nchi yetu, tukaona kwamba kwa sababu wanafunzi wanapomaliza kidato cha nne, wanapokwenda kidato cha tano, wale ambao wanachukuliwa wamefaulu sayansi, wakimaliza *forms six*, hawataki kwenda kwenye kozi za Ualimu wa sayansi au kozi za Ualimu,

wanaenda *engineering*, wanaenda kuchukua kozi zingine. matokeo yake shule zetu za Kata na shule za Serikali tumeshindwa kuwa na mikakati ya kuzalisha Walimu wa sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie tu hawa wanafunzi waliomaliza kidato cha nne, wale ambao wana *credit* nzuri kuanzia C, ndio wanaofaulu kwenda kidato cha tano, wale wanaobaki na alama za D, ndiyo wanaonekana wamefeli. Sasa kukawa na utaratibu, kwamba kwa nini kama wanafunzi wanakwepa kusoma Ualimu wa sayansi, kwa nini tusianzishe utaratibu maalum, ambao waliuita *five years integrated bachelor degree program*, ili mtaala huu, uweze kuwachukua wanafunzi wa kidato cha nne, ambao wana alama za D, waweze kusoma miaka mitano na siyo miaka mitatu. Katika kipindi cha miaka mitano wawalee, wawanoe, wawapike, iwe kama wamesoma *certificate, diploma* mpaka *degree* na wanakuwa wamechujwa hapa katikati, wale wanaofeli wanaondoka, kumaliza miaka mitano tunakuwa na Mwalimu tuliye mfundisha sayansi ili wafundishe shule zetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake Mheshimiwa Waziri anakuja hapa anatuambia kwamba hawakustahili, hawana sifa, wakati wamekuwa na sifa ndani ya mtaala maalum ambao umewasilishwa na Chuo cha Mtakatifu Joseph; kuna nini hapa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma tulipokuwa na mahitaji ya Walimu, tulianzisha Walimu wa UPE na wenyewe hawakuwa na sifa, lakini tukawa-*qualify* na ndiyo wametufundisha sisi, nimefundishwa na Mwalimu wa UPE mimi. Vile viel tulipoona kuna mahitaji ya Walimu, tulianzisha programu miezi mitatu, kumfundisha Mwalimu, wakabatizwa jina la yeboyebo, sijui voda fasta, yote hiyo ilikuwa ni kwa sababu ya mahitaji ya Walimu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tulipokuwa na mahitaji ya Walimu tulianzisha *combination* ambazo unasoma *HG Education, PC Education, CB Education*, yote hiyo ilikuwa ni kutatua matatizo ya Walimu. Sasa leo kupitia mtaala maalum mnawaita hawa watoto ni vihiyo haiwezekani, hawa siyo vihiyo. Mheshimiwa Ndulichako, kuniambia kwamba wengine walikuwa *arts*, kwa nini wameenda kusoma, kwenye *arts* wanasoma *biology* pamoja na *mathematics* masomo mawili hayo ni sayansi hata kama wako *arts*, wakienda kusoma masomo hayo wamesoma sayansi, leo unasema ni vihiyo; matokeo yake umewafukuza wanafunzi 489. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii haiwezekani, huu ni ukatili, unyama na kama umesema umemshirikisha Mheshimiwa Rais, umemshirikisha kwa kumpotosha. Umemweleza mambo ambayo si sahihi na ndiyo maana, Mheshimiwa Ndulichako anataka tucheze muziki anaotulazimisha kucheza sisi, haiwezekani!



Niliwahi kusema hapa kwamba, hatuwezi kukubali kuchezesha kama Joyce wowowo hapa. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Ndalichako wanafunzi hawa wamedahiliwa na TCU, wamepewa mikopo na Serikali, itakuwaje wawe wahanga, muwafukuze. Hatutakubali, utakapokuja kuhitimisha, tunataka majibu kwa nini wanafunzi hawa umewafukuza, lazima muwarejeshe hatuwezi kukubali, tumepoteza fedha za Serikali kwa sababu ya matatizo yenu huko TCU, matatizo yenu yasije yakatuletea uhanga kwa wanafunzi hawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye ada elekezi. Hii ada elekezi mnaelekeza kitu gani? Mkitaka shule za binafsi wapunguze ada, mkitaka shule za binafsi zife ni shule za Serikali kuwalipa Walimu vizuri, kuwa na madarasa, kuwa na nyumba za Walimu, kuweka msosi yaani chakula, hakuna mtu binafsi atakayepandisha ada na ninyi kama mtaendelea kuhakikisha mazingira haya hamyajengi kila mtu ana uchaguzi kupeleka mtoto Ulaya, kupeleka mtoto shule binafsi. Shule binafsi mmezirundikia kodi nyingi sana, mara wapake magari rangi, mara sijui wafanya nini, sasa watarudishaje hizo fedha mnazowaambia wapake rangi magari, kodi kede kede, tunakwenda wapi! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, CCM ni gari kubwa na Serikali yetu ya Awamu ya Tano ni gari kubwa tukiacha gari ku....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kangi Lugola muda wako umemalizika.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Elly Macha.

**MHE. DKT. ELLY M. MACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kupata nafasi hii ya kuchangia jioni ya leo. Awali ya yote napenda kumpongeza Waziri wa Elimu na Naibu Waziri pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Elimu kwa kutayarisha Hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa pole Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye amefiwa na mama yake mpenzi, Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Kabla sijachangia kwenye hotuba hii kwanza kabisa ninalo ombi, ombi langu ni kwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na Waheshimiwa Mawaziri. Wapo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanatumia *dehumanizing terminologies* kwa mfano vilema, siyo wote nimesema baadhi na pia kuna baadhi ya Mawaziri wanatumia neno kama vilema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapotumia neno vilema, maana yake vi ni *non-living object* yaani ni kitu ambacho hakina uhai tunasema viti, vikombe, vijiko lakini watu wenye ulemavu ni watu. Kwa hiyo, naomba tutumie lugha ya kuwathamini na kuwapa utu watu wenye ulemavu, kwamba ni watu wenye ulemavu na sio vilema. Ahsante naona hilo limeshakuwa *noted*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kuchangia hotuba, kwanza napenda kumshukuru Waziri alipokuwa akitoa Hotuba yake alisema kwamba, elimu maalum ameipa kipaumbele katika Wizara yake, hiyo nashukuru. Katika kuipa elimu maalum kipaumbele, napenda kuchangia kwa kuanzia ule mtambo wa kuchapisha vitabu vya nukta nundu ambapo upo chini ya Wizara ya Elimu, upo pale Uhuru Mchanganyiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule mtambo ulianzishwa katika miaka ya 70 kwa msaada wa Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la CIDA kwa ajili ya kuisadia Wizara ya Elimu iweze kutoa maandishi ya nukta nundu kwa wanafunzi wasioona pamoja na maandishi makubwa kwa wanafunzi wenye uoni hafifu, pamoja na kutengeneza zile *hearing aids* kwa wale wanafunzi ambao wana upungufu wa kusikia. Hata hivyo, baada ya Shirika la Sweden kusitisha msaada wake kwenye miaka ya 80, ufanisi wa ule mtambo wa kuchapisha vitabu vya maandishi ya *braille* ambao ni mtambo pekee hapa Tanzania, Tanzania nzima, mashule yote ya msingi pamoja na sekondari yanategemea mtambo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanisi wa mtambo huu umekuwa ni duni, jengo limechakaa, mashine ni mbovu, Mheshimiwa Waziri mwenyewe alishafika pale anajua. Wafanyakazi wanaopelekwa pale ni wafanyakazi wasiokuwa na uwezo na mara nyingi Wizara ya Elimu imekuwa ikipeleka wafanyakazi ambao wana matatizo, wale wanaohitaji *light duty* ndiyo wanapelekwa kufanya kazi pale. Matokeo yake hivi tunavyoongea katika shule zote za watoto wasioona na wale wenye uoni hafifu, msingi pamoja na sekondari hawana vitabu vya *text book* na hawana vitabu vya kiada. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu fikiria mwanafunzi anaingia darasani, wenzake wanapata vitabu vya masomo yote jiografia, historia, lakini mwanafunzi asiyeona hana kitabu chochote anachosoma, anaingia pale kusikiliza na kuondoka bila kupata vitabu, ni kwa sababu uzalishaji wa vitabu vya namna hiyo umekuwa ni duni na umekuwa na matatizo, mashine hakuna zilizopo ni mbovu, rasilimali hakuna wenye uwezo. Kwa hiyo, *production* ya ile *Braille Press* imekuwa chini kiasi kwamba shule zetu sasa hivi wanafunzi wetu wasioona na wale wenye uoni hafifu hawana vitabu vyovyote vya kusoma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri ambaye hili suala analijua afanye jitihada kuona kwamba ule mtambo umekuwa *equipped*, jengo limetengeneza, wanapelekwa pale wataalam wenye uwezo wa ku-*produce* hiyo *braille press* ili *supply* ya vitabu vya nukta nundu mashuleni liweze kutosheleza, ambapo sasa hivi hakuna kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna tatizo la kile chuo kimoja tu Tanzania nzima, Chuo cha Patandi ambacho kinatoa elimu maalum kwa Walimu wa elimu maalum. Mpaka 2010 Tanzania hii ilikuwa na *shortage* ya Walimu wa elimu maalum 16,000 na sasa hivi wameongezeka. Chuo cha Patandi ambacho kina miundombinu ambayo ni mibaya, inahitaji matengenezo, hawana vifaa vya kufundishia wala vya kujifunzia, kinahitaji kupewa vipaumbele na Wizara ya Elimu ili kiweze kutoa Walimu wa elimu maalum wa kutosha. Kwa mwaka wanatoa Walimu kati ya 150 mpaka 250 tu, lakini nimesema upungufu hadi sasa ni zaidi ya 16,000 wa elimu maalum wanaohitajika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo shule za msingi ambazo zinakaribia 90 ambazo zinachukua wanafunzi mbalimbali wasioona na walemavu wa aina nyingine. Tunazo shule za sekondari, lakini pamoja na hayo Walimu wa elimu maalum ni wachache na chuo ni kimoja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2009, Wizara ya Elimu ilitoa *inclusive and special need education frame work* ambapo ilisema kati ya 2009 mpaka 2017 vyuo vingine vitakuwa vinatoa dozi ya elimu maalum kwa ajili ya kwamba Walimu wanapohitimu wanakuwa na ufahamu wa jinsi ya kuwashughulikia au jinsi ya kuwapokea na kuwafundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mpaka sasa hivi ile *frame work* bado haijatekelezwa. Namwomba Mheshimiwa Waziri afuatilie hiyo *education frame work* ya *inclusive education* ili tuweze kuona inafanya kazi na vyuo vingine vyote vinapata *component* ya *special education* ili waweze kuwapokea wanafunzi wenye elimu maalum katika shule zao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija suala la elimu bure, Waziri sijaona ni mipango gani ameainisha kwenye hotuba hii, jinsi wanafunzi wenye ulemavu nao watakavyofaidika na huu mpango wa elimu bure. Wapo wengi ambao wana umri wa kwenda mashuleni wapo majumbani, shule zilizopo hazitoshelezi na sijaona mikakati ambayo ipo kwa ajili ya kuwafaidisha wanafunzi au watoto wenye umri wa kwenda shule wenye ulemavu na wao wafaidike na hii elimu bure. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la wanafunzi viziwi, mpaka sasa hivi wanafunzi hawa wana matatizo ya kupata Walimu wakalimani wa lugha ya alama wa kuwafundisha katika mashule. Kwa hiyo, naomba pia kuwe na mkakati wa kuimarisha mafunzo ya lugha ya alama ili wanafunzi hao nao wapate nafasi ya kupata elimu kama wanavyopata wengine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri wa Elimu awasiliane na Waziri anayeshughulika na sera kuhusu watu wenye ulemavu. Kuna *Treaty* ya Kimataifa ambao inaitwa *Marrakesh Treaty*, hii *Treaty* inatakiwa iwe *ratified* na nchi 20 ili iweze kufanya kazi na inasema kwamba inawalazimisha *publishers* au wachapishaji waweze kutoa maandishi ya vitabu vyao wanavyochapisha katika *accessible format*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ikiwa imeshasaini na kuridhia, Serikali ina uwezo wa kuwalazimisha *publishers* waweke maandishi yao katika maandishi ambayo yanaweza kusomwa na watu wasioona pamoja na watu wengine ambao wana matatizo ya kusoma maandishi ya kawaida kama watu wenye *Dyslexia* au kama watu wenye *down syndrome* ama kama watu wenye uoni hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hii sheria kama itaridhiwa itasaidia pia ile wanaita *cross border literature*, ni kwamba kama kuna nchi moja inatoa vitabu ambavyo vinaweza kutumia katika nchi nyingine, hiyo sheria inawataka wale watu wenye *copyright* waruhusu kazi zao ziweze kusafirishwa katika nchi nyingine ili wanafunzi wenye matatizo ya kusoma maandishi ya kawaida waweze kupata nafasi ya kusoma vitabu hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi itilie mkazo somo la *computer* kwa wanafunzi wenye ulemavu waweze kwenda na teknolojia. Wanafunzi wenye ulemavu wakipata nafasi ya kujua teknolojia, ya kujua kompyuta watakuwa na uwezo zaidi wa ku-access *information*, wataweza kwenda kwenye vyo vikiu bila matatizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Macha, tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Suleiman Ally Yussuf, baadaye Mheshimiwa Silafu pamoja na Mheshimiwa Hassan Elias na Mheshimiwa Halima Bulembo wakae tayari.

**MHE. DKT. SULEIMAN A. YUSSUF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanah Wataala* na kumsalia Mtume wake *Muhammad Swallallahu Alayhi Wassalam*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza mchango wangu naanza kwa masikitiko makubwa kwamba alipokuja Waziri nilidhani anakuja kutuambia kwamba elimu yetu imekwama na kutufahamisha njia ambazo tutakwamuka, lakini badala yake Waziri amekuja hapa, akaja na majibu ya maswali ya kawaida, ukweli hicho si sahihi. Hata hivyo, kwa upande mwingine namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati, ukweli namfahamisha Waziri kwamba atupe zile karatasi zake achukue ushauri wa Kamati, ni mzuri na utamwelekeza pazuri pia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naanza mchango wangu kwa kutoa ushauri, nasema kwamba, elimu hapa kwetu imekwama na nadhani Wizara ya Elimu inajua vizuri sana kwamba elimu kwetu imekwama, lakini hatujui ni namna gani tujikwamue kutoka hapo tulipo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa tunalolifanya hapa kwetu la kusababisha elimu ikawa duni na haina thamani ni kwambakatika udahili tunachukua wanafunzi ambao wame-fail fani nyingine, wameshindwa, tunawachukua wale ndiyo tunawapeleka kwenye ualimu. Tunapanda mbegu mbovu, tunategemea tupate matunda gani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ili tufanikiwe tuwe na elimu yenye thamani, tuchukue wanafunzi ambao wame-pass vizuri sana kuanzia O-level mpaka kufikia A-level na tuwashawishi namna gani ya kuwashawishi hawa, tunaweza kuwashawishi kwa kuwapa mishahara minono kama mishahara ambayo tunawapa Madaktari na fani nyingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kukwambia kwamba hakuna mtu ambaye ni muhimu baada ya mzazi kuliko Mwalimu. Ndiyo sababu tunapokuja katika ulinganisho, tunasema nani ambaye ni bora Mwalimu ama mzazi. Husemi Mwalimu au Dokta, husemi mzazi au Daktari, husemi mzazi au Mwanasheria bali ni Mwalimu pamoja na mzazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, fani zote ni muhimu, lakini fani ya ualimu ni muhimu zaidi. Ukitaka kuwa Rais ni lazima uende kwa Mwalimu, ukitaka kuwa Waziri Mkuu ni lazima uende kwa Mwalimu, ukitaka kuwa Spika, ni lazima uende kwa Mwalimu, ukitaka uwe Mwenyekiti wa Bunge, ni lazima uende kwa Mwalimu, ukitana uwe Mbunge ni lazima uende kwa Mwalimu, ukitaka Ukurugenzi, ni lazima uende kwa Mwalimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mwalimu ni mtu muhimu kupita kiasi na ndio sababu mshairi mmoja wa Kiarabu anakwambia *kumli Imuallimi wafii ttamijina kaadha Imuallimu an-yakuna rasula, alimta akrama au ajalla mina lladhi yubni, wayunshiu jabni, wayunshiu anfusan waankula*. Anakwambia msimamie mwalimu na mtukuze kwa hali yoyote ya utukufu, kwa sababu

Mwalimu anakaribia kuwa Mtume. Je, unamjua mkaribu zaidi na mtukufu zaidi kuliko yule ambaye anajenga nafsi za watoto na akili zao, kuna mtukufu kuliko huyo? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo la kwanza hilo kama tunataka tufanikiwe katika elimu tuchukue wanafunzi waliokuwa bora kwa kuwapa mishahara minono Walimu wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili hapo hapo kwa Walimu kila siku tunazungumzia upungufu wa Walimu katika vijiji, kuna shule zina Walimu wawili, kuna shule zina Walimu watatu, jamani sababu yake mnajua. Sababu yake ni kwamba kule vijijini mazingira ni mabovu, kwa hivyo, Mwalimu anapopelekwa kijijini, huyu ni kama anaadhibiwa. Ili kuwafanya Walimu wakae vijijini, ni muhimu sana hawa tukawazidishia mishahara kwanza, halafu kuna posho ya mazingira magumu, ni lazima tuwape. Mahali hakuna barabara, hakuna umeme, hakuna kilichopo, hata kuja mjini ni matatizo, ni lazima tuwanyanyue, tuwape hadhi nzuri hawa ili waishi maisha yaliyokuwa bora kule shamba. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo lakini nataka nisizungumze upungufu wa Walimu vijijini tu, nataka Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa, atueleze ni Walimu wangapi ambao hivi sasa tunao, hitajio letu ni Walimu wangapi kwa jumla na upungufu wa Walimu tulionao. Pia atueleze ni jitihada gani ambazo Wizara inachukua ili kuhakikisha kwamba tunaziba lile gape lililopo, nataka akija hapa atujibu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naelekea katika masuala ya elimu kwa upande wa Zanzibar. Nataka Mheshimiwa Waziri pia atakapokuja hapa anifahamishe ni nini maana ya elimu ya juu, maana yake nashindwa kuelewa elimu ya juu ni ipi, kwa sababu gani? Kwa sababu leo tunakuta mitihani ya *form four*, mitihani ya *form six*, Zanzibar inafanywa mitihani kutoka bara na nijuavyo mimi *A-level* na *O-level* sio elimu ya juu, siyo mambo ya Muungano, ni kwa nini vijana wale wanafanya mitihani kutoka hapa, wakati hata mitaala inatungwa hapa na mara nyingine inachelewa kufikishwa kule, kadhalika inaweza ikapita miezi sita kabla ya kupewa elimu ya mitaala ambapo hapa Bara tayari wanakuwa watu wameshapatiwa elimu hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unategemea wale vijana mitihani waifanye vipi kama ni kusema kwamba, wanataka tuwasaidie, ikiwa wanataka kusaidiwa kule Zanzibar hata mitihani wa *form four* na *form six* naiambia Serikali ya Zanzibar haifai ikae chini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu masuala madogo madogo kama hayo ni masuala ya mtu kufanya mwenyewe, kwa hiyo, kama hawayawezi basi

wakae pembeni wampe mtu ambaye wanamjua ambaye ni Maalim Seif. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika nataka kujua haki ya Wazanzibar katika mikopo ya elimu ya juu. Kwa sababu elimu ya juu ni suala la Muungano, lakini mpaka dakika hii Wazanzibar hawajui haki yao ni ipi katika mkopo ule bali wanachotewa kama watu waliokuwa wanafadhiliwa tu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunafanyiwa vitendo kama hivyo! Nataka atakapaokuja hilo pia anijibu. Nimetoa baadhi ya ushauri na kwa sababu muda umekwenda sana lakini sidhani kama ushauri huu utafanya kazi na sababu kubwa nahisi kwamba Mheshimiwa Waziri kavishwa koti ambalo limemzidi kimo, koti alilovalishwa ni kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu Mheshimiwa Waziri alikuwa Katibu Mtendaji wa NECTA. Lakini akafukuzwa kwa kushindwa kazi leo, ghafla anaibuka eti ni Waziri, ni mkombozi huyo, atatukomboa kitu gani! Wanasema waarabu *faqidu shei la yuutwi* (aliyekuwa hana hawezi kutoa) na yeye ikiwa kashinda pale padogo hapa pakubwa hapawezi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naam halafu kaja tu anafanya mambo Mheshimiwa Waziri kwa kukurupuka anatusifu...

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Suleiman, umemaliza muda wako.

**MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Silafu Jumbe.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kuweza kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii ya Waziri wa Elimu. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia nguvu kwa kuniwezesha mimi kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani za dhati na kumpongeza ndugu yangu Profesa Ndalichako kwa kazi nzuri ambayo ameanza nayo katika kipindi hiki kifupi na kuleta matumaini kwa wale wanohitaji elimu bora katika nchi hii, ahsante sana Mheshimiwa Waziri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili napenda kutoa shukrani kwa dada yangu Stella Manyanya Naibu Waziri. Awali ya yote tunamuomba Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema mama yetu mpenzi na mwanga wa milele umwangazie. (Makofi)



Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujikita katika suala zima la msingi wa elimu. Elimu ni kila kitu ndugu Waheshimiwa Wabunge, hakuna kitu ambacho kitakachozanzishwa ama kitakachofanyika katika nchi au mahali popote pale pasipokuwa na elimu, kwa hiyo elimu ndio msingi wa maisha yote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi ninapenda kuzungumzia kwenye suala zima la elimu ya awali. Tumeweza kuanzisha madarasa katika shule za msingi madarasa ya awali lakini bahati mbaya walimu husika na kufundisha madarasa yale ya awali hawapo walimu hao na kama wapo hawatoshelizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachozungumzia kwamba, hawapo ni kwa sababu katika shule zetu walimu wakuu wanachukulia sifa ya kumpatia mwalimu kufundisha darasa la awali ni mwalimu ambaye amefundisha kwa muda mrefu au ni mwalimu ambaye amebakiwa na miaka miwili au mitatu ya kustaafu ndio anayoelekezwa kwenda kufundisha watoto wa somo la awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hilo sio sahihi, tunaomba Serikali ijipange na ijitoe kuhakikisha ya kwamba inaandaa walimu wa kwenda kufundisha watoto wetu wa madarasa ya awali kwa sababu ndio msingi wa elimu. Bila kuwa na msingi bora ni dhahiri kusema ya kwamba uinujaji wa elimu bora na mafunzo bora katika nchi yetu hautawezekana kwa sababu watoto hawa watakuwa hawajapata msingi bora wa ufundishaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba Serikali, ninaomba Wizara iweke utaratibu maalum wa kufuatilia kwanza, kufatilia katika shule zetu za msingi kuona ile elimu inayotolewa kwa watoto wetu kama inaafiki ama inaswii katika kuhakikisha kwamba wanapata elimu bora. Hapo ndipo tutakapoonda kwamba kweli tumedhamilia kuinua elimu bora na mafunzo katika nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu watoto wasichana, wasichana ni kwa maana ya kwamba, hao ndio watakaokuwa wakina mama wa kesho kama sio wakina mama wa leo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachozungumzia ni ujenzi wa mabweni ya shule za sekondari. Ninawaomba Serikali iliweka msukumo wa kujenga sekondari kila kata na tumejenga sekondari kila kata na katika sekondari zile kuna watoto wasichana na watoto wa kiume, lakini hawa watoto wasichana ambao akina mama wa kesho wanakuwa na mitihani walimu wanawapa mimba, wananfunzi wenzao wanawapa mimba, sisi wenyewe wakubwa tunawapa mimba kwahiyo hawa watoto wanakuwa na mitihani mkubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali ione umuhimu wa kukamilisha mabweni ya watoto wasichana katika mashule yetu kuhakikisha kwamba

samani zinakuwemo ndani ya mabweni hayo vitanda, magodoro na kadhalika ili kujenga mabweni yale yawe ni rafiki kwa watoto wetu wasichana ili angalau wapunguze ile taratibu ambayo wanaopata mimba ambazo zisizokuwa na wakati muafaka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala zima la hawa akina dada, wale wanaowapa mimba wanapobainika ninawaomba wapatiwe adhabu kali tena kali sana. Kwa sababu wanapunguza muonekano wa wale akina mama katika mafunzo yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba ninaiomba Serikali hawa watoto wanaopata mimba ninawaomba wawaandalie fursa muafaka wa kuwawezesha hawa watoto wanapomaliza kujifungua, watoto wabaki wazazi wao, wao waendeleo na masomo jamani, hili limekuwa ni kilio cha kila mara sasa limefikia wakati kwa Mama Ndalichako nafasi kwa Mama Manyanya mmepeleka ninyi wanawake kwa sababu mnauchungu na watoto. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuwaonee uchungu hawa watoto wa kike, tuwaonee uchungu hawa watoto wa kike na tunajua ya wazi kwamba, ukimuelimisha mwanamke mmoja umeelimisha jamii nzima. Sasa kwanini tuwapoteze hawa kwa kuweza kuja kuendeleza nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuweke fursa maalum ya kuhakikisha hawa watoto wa kike wanapomaliza kujifungua watoto wanawaacha nyumbani wao wanaendelea na masomo ili tuweze kupata maendeleo katika nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kulizungumzia suala zima la wanasayansi. Tumesema nchi yetu itakuwa ni nchi ya viwanda, tuanze na viwanda vidogo vidogo, lakini hatuwezi kuwa na viwanda endelevu ikiwa hatuna wataalam wa kisayansi, ni lazima tuandae wanasayansi wa kuja kuendesha hivi viwanda vyetu, ili viwanda vyetu visiweze kufa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanyaje basi, tumeanzisha maabara katika shule za sekondari zote, lakini maabara hizi katika mashule yetu yana changamoto, changamoto iliyopo ni walimu wa sayansi hatuna. Vifaa vya sayansi katika maabara yetu havipo na ukiachia Halmashauri uwezo wa kununua vifaa vile ni aghali sana hawawezi Halmashauri kuweza kutekeleza na kuweka katika maabara zote za Sekondari zetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali natunamuomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atuaeleze amejipangaje na uwekaji wa vifaa au samani za maabara katika mashule yetu ili tupate walimu wa

kutosha na hatimaye tupate wanasayansi wa kuja kuendeleza viwanda vyetu hapa nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ushauri ni vyema wakaweka utaratibu maalum wa kuweka vivutio kwa walimu hawa wa sayansi, na kuweka vivutio kwa wanafunzi hawa wanaopenda sayansi, vinginevyo tutaweza kupoteza maana ya kuhakikisha kwamba, tunajenga viwanda katika nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika suala la walimu, walimu wanaokuja katika maeneo yetu kama sisi Mikoa yetu ya pembezoni Mkoa wa Rukwa, kwenda kule vijijini wamekuwa na taratibu za kuja ku-report wakishaingia kwenye payroll wale walimu wana-disappear katika yale maeneo kwa sababu mazingira yale ni mazingira magumu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulikuwepo utaratibu na hata na baadhi ya Mikoa walijaribu kuanzisha taratibu hizo za kuwawezesha walimu hawa kwenda kuishi kule mfano Rukwa walianzisa Nyerere Fund ambayo kwamba sasa hivi hai-operate vizuri, lakini vilevile na Serikali wangeweza kuweka package nzuri ya kuhakikisha kwamba huyu mwalimu anapokwenda kule anakwenda katika ukamilifu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Rukwa walikuwa wanapewa vitanda, magodoro, vyombo na sehemu kidogo ya kwenda kuanzia maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Wizara iweze kuona suala hili ili tuwe na walimu hawa katika shule zetu, katika ukamilifu. Walimu wanafanya kazi moja kubwa mno, sisi sote hapa tusingekuwepo kama kungekuwa hakuna mwalimu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi tunachokiomba hii Wizara ya TAMISEMI imepewa mambo mengi mno, kwa sababu changamoto zote za walimu, changamoto za wanafunzi zipo TAMISEMI, lakini wanaolaumiwa ni Wizara ya Elimu, tunaomba hii Wizara ya Elimu ijitegemee kwa sababu ina mambo mengi ya kuweza kufanya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba wameanza Tume ya Walimu lakini bado haitoshelezi mahitaji, tunahitaji elimu iwe na Wizara inayojitegemea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu na VETA Mkoa wa Rukwa umeanzishwa nadhani ni mwaka 1974 ama ni 75 lakini mpaka hivi leo Mkoa wa Rukwa hatuna VETA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao vijana wengi wanaomaliza darasa la saba, tunao vijana wengi wanaomaliza darasa la 12 lakini wanakuwa hawana mahali pa kushika, hawawezi kujajiri na wala hawawezi kuajiriwa. Kwa hiyo tunaomba katika Bajeti hii ya 2016/2017 katika mipangilio yao wafanye utaratibu wa kuanzisha VETA katika Mkoa wetu wa Rukwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na napenda kuunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Tunandelea sasa ni Mheshimiwa Hassan Elias Masala na baadaye Mheshimiwa Halima Bulembo ajiandae.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba ya Wizara ya Elimu.

Mimi naomba nijielekeze kwenye mambo yafuatayo; eneo la kwanza mara baada ya kupitia hotuba nzima nilikuwa anajaribu kuangalia eneo la uboreshaji wa miundombinu katika kuboresha kiwango cha elimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa waziri atakapokuja kusimama hapa ni vizuri niungane na wale wenzangu waliotangulia kusema ni kwa kiasi gani wamejipanga kukamilisha ujenzi wa maabara ambao ulishaanza kipindi cha nyuma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivi lengo letu ni kuona tunawezaje kwenda kutatua tatizo la walimu wa sayansi ambalo limekuwa ni tatizo kubwa na hata hapa tunapojadili upungufu wa walimu kwa sehemu kubwa tunaangalia upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna eneo la upungufu wa madarasa na nyumba za walimu naona mkazo mkubwa tumeelekeza zaidi kwenye kujenga madarasa na hii ni kwa sababu ya ongezeko la watoto ambao tumekuwa tumewapokea mara baada ya utekelezaji wa sera hii ya elimu bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni lazima tuangalie mazingira ya walimu wetu, tuone ni namna gani Serikali imejielekeza kujenga nyumba za walimu za kutosha, ukienda kwenye jimbo la Nachingwea ambalo mimi nakaa sehemu kubwa ya walimu wetu hawana makazi ya kudumu yenye kueleweka hivyo hii inaweza ikashusha kiwango cha elimu katika kuboresha elimu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia Mheshimiwa Waziri Profesa Ndalichako nilifikiri tunapojadili elimu ni lazima

tuangalie stahiki za walimu. Walimu wetu wamekuwa kwenye matatizo makubwa ya kudai haki zao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wanapandishwa madaraja lakini hawalipwi pesa zao kwa wakati. Nafikiri umesikiliza na umeona kumbukumbu ya idadi ya watu ambao wanadai na kiasi ambacho Serikali kinadaiwa, kwa hiyo naomba deni hili ili tuweze kuwatia nguvu walimu ni lazima tuweke mkakati wa kuona kupitia bajeti hii tunawezaje kwenda kulipa madeni, ili walimu waweze kufanya kazi ambayo tumewaagiza watusaidie kutufanyia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia liko tatizo, iko tofauti ya upandishwaji wa madaraja kwa walimu ambao wameanza wakati mmoja. Walimu mathalani wanaanza mwaka mmoja lakini baada ya miaka mitatu pamoja na kwamba kuna OPRAS ambayo inapima utendaji wao wa kazi lakini bado kumekuwa na *variation* kubwa katika upandishaji wa madaraja sasa hili ni tatizo na walimu wetu wangependa kupata majibu wakati unahitimisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini kinapelekea utofauti huu mkubwa kwa watu ambao wameanza wakati mmoja kuwa katika viwango tofauti vya madaraja yao na hivyo kupelekea kupokea pesa kidogo tofauti na wale ambao wameanza nao kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kuchangia na mimi niungane mkono na wale wote ambao wameshangazwa na maamuzi yale ambayo kimsingi jana Mheshimiwa Waziri ameshayatolea ufafanuzi. Makosa sio wanafunzi, kilichofanywa na TCU lazima Serikali iende zaidi ya pale ambapo imefanya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa wako watu wamechukuliwa hatua lakini ni lazima tujiulize tatizo mpaka tumelifuga tunachukua wanafunzi, tunawapa mikopo, lazima tujue tatizo ni kwa nani lazima hatua tungependa kuishauri iende zaidi ya hapo ili kuondoa uzembe ambao kimsingi tusingependa kuona vijana wetu wanapata shida na leo tunakuja kuwabebesha mzigo ambalo wao hawahusiki lakini kumbe kuna watu wamepewa dhamana na wameshindwa kusimamia dhamana yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo la mikopo, mim naomba ni-*declare interest*, Mheshimiwa Waziri kati ya watu unaowatafuta kulipa hiyo mikopo nafikiri na mimi mwenywe ni mmojawapo. Nimeshangaa kidogo hapa lakini nafikiri tuna kazi ya kukusaidia kwamba unatafuta waliokopeshwa wako wapi. Bado unajaribu kuangalia *board* toka nimeajiriwa Serikalini kabla sijaacha kazi nimejaribu kufanya mawasiliano zaidi ya mara tatu, mara nne niweze kurejesha mikopo lakini sijaona hatua zozote. Sasa hili ni mapungufu ambayo

yako ndani ya Bodi ya Mikopo, ni usimamizi mbovu ambao bado haujawekewa mikakati. (Makofi)

Mheshimiwa mwenyekiti, leo hii ukiamua nusu ya Wabunge walioko hapa ndani wote ni wanufaika wa hii mikopo, lakini ni Wabunge wangapi wamelipwa hii mikopo nafikiri hakuna au ni wachache watakaokuwa wamefanya hivi, lakini sio makosa yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ulipaji ule mmeweka gharama za kufidia kile ambacho mmekiita wenyewe kwamba ni sumbufu sijui ni nini. Hebu Mheshimiwa Waziri, tutakaa chini tujaribu kuweka utaratibu mzuri, lengo letu sisi kama Wabunge lazima tuwe mfano tulipe hii pesa ili vijana na watoto wetu waweze kupata na wao elimu kama ambavyo sisi tulipata wakati tunasoma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kukuambia mimi niikuwa Rais wa Serikali ya wanafunzi chuo kikuu pale *DUCE* mwaka 2008/2009. Najua kinachofanyika Bodi ya Mikopo ni nini, hebu tumia baadhi wa Wabunge wenzio ulikuwa nao hapa ndani tukusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko *account* mbili mbili zinafunguliwa na Bodi ya Mikopo, wako watu ambao wanapewa pesa lakini kimsingi pesa hii inarudi kwa watendaji wa bodi ya mikopo wenyewe. Sasa ni jambo ambalo linahitaji utulivu, linahitaji sasa wewe ushirikishe wadau mbalimbali ili tuweze kukupa taarifa ili tuweze kurejesha hizi pesa na vijana wetu waweze kusoma na hata wapiga kura nao waweze kunufaika na mikopo ambayo sisi tumenufaika nayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kulichangia ni suala la ukaguzi wa shule zetu. Leo hii nimeipitia bajeti nzima, najaribu kuangalia kiasi cha pesa ambacho kimeombwa kwa ajili ya matumizi ya kuboresha eneo la ukaguzi wa shule zetu, bado sijaona kiasi cha pesa cha kutosha.

Mheshimiwa Waziri na hili naomba nikwambie itakapofika wakati nitakamata mshahara wako, lazima uniambia ni kwa kiasi gani tumetenga pesa kwa ajili ya Idara hii ya Ukaguzi, leo hii ukaguzi haufanyi kazi yoyote ile, shule zetu hazikaguliwi, miaka mitano, miaka kumi shule zinafundisha, walimu wanafundisha lakini hakuna mtu anayeenda kutoa ushauri ni kwa sababu Idara ya Ukaguzi haina mafuta, Idara ya Ukaguzi hawana magari, Idara ya Ukaguzi hawana vitendea kazi na imefika wakati sasa wanatamani warudishe Halmashauri labda wanaweza kupata msaada kuliko kukaa huko ambako wamekaa na hawapati kiasi chochote cha pesa cha kufanya kazi zao. (Makofi)

Mheshimiwa Waziri, nitaomba wakati unakuja kuhitimisha bajeti yako utuambie watu wa ukaguzi umewatengea kiasi gani cha pesa na sio kiasi cha

bilioni mbili ambacho kitaenda kubaki mara baada ya matumizi mengine kwa kadri ulivyoomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la mitaala. Mtaala wetu unaotumiwa na kwa kasi tuliyonayo ya kuhitaji kujenga viwanda bado haiendani. Leo tunahitaji viwanda vya kutosha lakini hatuna wataalam ambao watakwenda kufanya kazi kwenye viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Elimu ya Kujitegemea (EK) mashuleni haifanyi kazi, leo hii tunategemea tuzalishe wasomi, tuzalishe watu ambao wataenda kuhudumia viwanda vyetu, lakini mitaala yetu inapishana. Leo hii ndani ya nchi moja wako watu wanatumia mitaala ya kutoka kwa Malkia ya Cambridge, kuna Watanzania wanaotumia mitaala ya kawaida sijui tunageneza taifa la namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu tumeamua kujipanga vizuri ni vizuri sasa tukaangalia namna ya kurekebisha mitaala yetu *i-match* na kile ambacho tunakwenda kukitengeneza ili tuweze kusaidia Taifa hili na Watanzania kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni wakati ule mitaala inapobadilika, vitabu vinavyotumika mashuleni navyo pia haviendani. Leo hii darasa la kwanza na darasa la pili vitabu wanavyovitumia na mitaala ni vitu viwili tofauti. Wachapaji wa vitabu wamekuwa wengi, vitabu hivi vinapishana kimaudhui, vitabu hivi vinapishana katika *content* ambazo tunategemea zifundishe watu wa aina moja.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri kwa kazi ambayo umeifanya na unaendelea kuifanya ni vizuri maeneo haya yote tukayaweka vizuri ili tuweze kutengeneza kitu ambacho kinafanana na tutengeneze Watu ambao watakuwa sawa katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingineni ufundishaji wa TEHAMA katika shule zetu. Shule za wenzetu zile ambazo Watoto wenye pesa wanaweza kusomesha leo wanapata masomo ya sayansi, wanasoma *computer*, wanasoma vitu vingine, lakini ukienda katika shule zetu za kawaida wanapelekewa vitabu lakini *practically* hawasomi haya masomo kwa ajili ya kuwawezesha na wao kumudu teknolojia hii ya mawasiliano. Kwa hiyo Mheshimiwa katika bajeti yako ni vizuri, nimeona kwamba umetenga kwa jili ya ndugu zetu walemavu lakini bado kwa Watanzania wale walio wengi nao pia ni muhimu ukatueleza eneo hili tumejiweka na tumejipanga vipi ili tuweze kufanya vizuri.



Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho ambalo ningependa kuchangia ni NECTA kwenye suala la utoaji wa vyeti vya kuhitimu masomo. Hapa katikati tumeanza na *division one* mpaka *division zero*, lakini kuna watu wamekuja kutahiniwa kwa kupewa GPA, kuna watu walikuja wakapewa ile mpaka *division five*, leo hii waajiri wanapata shida wakati wa kuajiri kujua ni utaratibu gani unaweza ukatumika.

Naomba nitoe ushauri Mheshimiwa Waziri wakati unahitimisha utuambie, Wizara yako inaweza ikaweka utaratibu gani ili vitoke vyeti vya pamoja ambavyo vitasaidia kuondoa hii sintofahamu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa Halima Bulembo na baadae Mheshimiwa Pauline Gekul pamoja na Mheshimiwa Zubeda Hassan wajiandae.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia na ninaomba nijielekeze moja kwa moja katika mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunajadili bajeti muhimu kuliko bajeti yoyote nchini. Leo tunajadili bajeti inayohudumia Watanzania wengi kuliko bajeti yoyote nchini na leo tunajadili Bajeti ya Taifa la sasa na hasa hasa Taifa la baadaye. Nitawaonyesha takwimu kuthibitisha maelezo yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Watanzania tunakadiriwa kuwa takribani milioni 50, nusu ya Watanzania wana umri wa miaka 17 kwa maana nyingine nusu ya Watanzania ni watoto. Kwa mujibu wa takwimu ya Taifa ndiyo inasema hivyo, kati ya watoto takribani milioni 25, watoto wetu milioni 12 wako katika shule zetu za awali, shule za msingi na shule za sekondari. Nizungumzie shule za awali. Kwa utafiti wa hali ya uchumi mwaka 2014, inaonesha idadi ya wanafunzi wa awali iliongezeka kwa asilimia 1.9 kutoka wanafunzi 1,026,466 mwaka 2013 hadi kufikia wanafunzi 1,046,369. Utafiti huo huo unaendelea kuonyesha idadi ya wanafunzi wanaojiunga na elimu ya msingi inazidi kupungua kutoka wanafunzi 8,202,892 mpaka wanafunzi 8,231,913 sawa na upungufu wa asilimia 0.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti huo huo unaendelea kuonesha wanafunzi wa kidato cha kwanza mpaka cha sita, idadi yao imeendelea kupungua kutoka wanafunzi 1,800,056 mpaka wanafunzi 1,704,130 sawa sawa na upungufu wa asilimia 5.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa *Basic Education Statistics* yaani *BEST*, watoto wa Kitanzania milioni nne wako katika elimu ya msingi na watoto wa Kitanzania milioni nne wako katika elimu za sekondari. Kwa maana hiyo hapa tunazungumzia robo ya Watanzania wako mashuleni, robo ya Watanzania wako madarasani na wengine wamekaa chini kwa kukosa madawati, na wengine matumbo yao hayana kitu kwa kutoka familia fukara na shule hazina chakula na wengine wanagombea kitabu kimoja kwa kuwa hatuna vitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri robo ya Watanzania inafundishwa na walimu wasiokuwa na hamasa na hamasa hii inakosekana kutokana na walimu kutokuwa na mishahara mizuri, kutokupandishwa madaraja katika kazi zao, kutokuwa na makazi yanayoeleweka na wengine kuwa walevi wa kutupa kutokana na *stress* za maisha. Tunajua kila mtu akiwa na *stress* zake anaamua pa kwenda wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna uwezekano mamilioni ya watoto wetu wanafundishwa na walimu walevi, lakini leo hii nani ana mamlaka ya kuwawajibisha hawa walimu walevi ilihali elimu haina ukaguzi mzuri, nani ana mamlaka ya kuwaadhibisha walimu hawa kwakuwa hatuwezi kutatua kero zao, nani ana mamlaka? Hakuna. Robo ya Taifa tunaiweka mashakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, robo ya wananchi wanapata robo ya bajeti. Bajeti ya Wizara ya Elimu ni shilingi trilioni 1.3 kwa pesa za Kitanzania. Tunaambiwa bajeti nyingine ipo TAMISEMI.

Mimi ningeshauri au ningeomba Wizara na Serikali yangu ingeipa bajeti ya Wizara ya Elimu peke yake na bajeti hii ingewekwa kwa uwazi ili tuweze kukokotoa, tujue asilimia 25 ya wananchi wanapata asilimia 25 kweli ya bajeti yao? Tukijumlisha na bajeti inayopelekwa TAMISEMI ambayo tunaambiwa iko TAMISEMI bado bajeti ya Wizara ya Elimu iko chini ya asilimia 10. Tunawakosesha watoto wetu haki ya kuwa na elimu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka miwili ya chekechea na miaka mitatu ya elimu ya msingi ni muhimu sana na wote tunajua kwamba elimu ya awali ni muhimu kwa vijana wetu. Lakini vile vile kama Watanzania tunajua Watoto wetu hawa wana matatizo, hawana msaada wa Kiserikali, hawana msaada wa kiseri na wala hawana msaada wa kisheria kutoka hizi elimu za mwanzoni. Hali hii inabidi ibadilike kama tunataka kweli kujenga Taifa lililoelimika kwa mujibu wa Dira ya Taifa 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo au takwimu za utafiti ya UWEZO inaonesha katika wanafunzi 10 wa darasa la tatu, ni wanafunzi watatu pekee

wanaoweza kusoma sentensi ya darasa la kwanza na ni wanafunzi watatu wanaoweza kukokotoa hesabu za darasa la kwanza. Hii inaonesha kwamba Watoto wetu hawapati fursa nzuri ya kusoma huku tangu awali kwenye hizi elimu zao za mwanzoni. Tukitaka kubadili hali hii inabidi tuwekeze. Tuwekeze katika kupata kizazi cha wanafunzi wanaopenda kujisomea, wanafunzi ambao watakuwa na uwezo mkubwa wa elimu, wadadisi na hata wabunifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 50 ya vijana wanaomaliza elimu ya msingi hawaendi shule za sekondari na asilimia 75 ya wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne hawaendi kidato cha tano na cha sita. Na sera yetu ya elimu sasa hivi inaunganisha elimu ya msingi ya sasa na elimu ya sekondari ya sasa kuwa elimu ya msingi kwa miaka 10. Hawa ambao hawapati fursa za kuendelea wanakwenda wapi? Rasilimali hii ya Taifa inaenda wapi? Na hapa ndiyo tunapokuja kuhitaji ufundi stadi na ufundi mchundo.

Naomba kuipongeza Serikali yangu kwa kuamua kuunganisha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na VETA lakini hapo hapo Serikali ya chama changu, Serikali ya Chama cha Mapinduzi iliahidi kujenga Vyuo vya VETA katika kila Halmashauri ya Wilaya tangu mwaka 2005. Mheshimiwa Waziri, mimi ninaimani kubwa na wewe, naomba usimamie suala hili litekelezwe. Zijengwe hizo VETA katika kila Halmashauri ya Wilaya ili tuwape vijana wetu stadi za maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kutoa ushauri katika suala hili kwamba tuamue kugeuza Jeshi la Kujenga Taifa yaani JKT liwe VETA kwa maana ya kwamba kila kwenye Jeshi la JKT tusajili VETA. Vijana wetu wanapoenda kusoma miaka miwili, mwaka mmoja waweze kupewa *skills* maalum za maisha na baada ya hapo waweze kupewa mikopo ya vifaa, hii itawajengea wenyewe uwezo wao wa kufanya kazi na tutajenga Taifa la watu ambao wanapenda kufanya kazi wao kwa wao, kujiajiri au kuajiriwa na Mheshimiwa Waziri, ningeomba suala hili la VETA liwe mpango maalum na lisimamiwe na Jeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba kuzungumzia walimu. Naomba kuzungumzia walimu wa kada maalum, walimu wa awali kwa maana ya chekechea mpaka darasa la kwanza, kuanzia darasa la kwanza mpaka la tatu. Walimu hawa wawe na mafunzo maalum, wapewe motisha maalum na Vyuo Vikuu vitoe shahada maalum kwa walimu hawa ili tuweze kuwajengea uwezo watoto wetu wanaokua kuanzia chekechea mpaka darasa la kwanza, la pili na la tatu. Na hii tukifanya hivyo tutawapata watu wengi, watoto wetu watakuwa na mwanzo mzuri, wataweza kufanya kazi vizuri kwa bidii lakini pia walimu hawa wa kada maalum wawe walimu maalum na wawe na mishahara maalum siyo wanapewa mishahara ambayo haieleweki Mheshimiwa Waziri. Kwa kufanya hivyo, tutaibadilisha Tanzania yetu katika kizazi kimoja tu kwa kuwekeza kwa walimu, kwa watoto na *let us* ....

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:**Ahsante Mheshimiwa Halima, tunaendelea sasa ni zamu ya Mheshimiwa Pauline Gekul na baadae Mheshimiwa Zubeda ajiandae

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru ili na mimi niweze kuchangia machache katika Wizara hii ya Elimu, Wizara muhimu sana na awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya ambayo anayoendelea kunijaalia ili niweze kutoa mchango wangu katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru wananchi wa Jimbo la Babati Mjini ambao wamenipa dhamana ya kuwa Mbunge wao wa Jimbo na niwaahidi sitowaangusha na baada ya Bunge tutaendelea kuwa pamoja ili tuendeleze Jimbo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niombe Waziri anisaidie kwa sababu hapa tunazungumza suala zima la bajeti. Naomba tu anisaidie katika bajeti yake kabla sijaenda mbele zaidi katika kitabu chake cha *Development*, kwenye *Vote 1003*, amezungumzia suala zima la *rehabilitation of the schools and colleges*. Ametenga shilingi 8,153,000,000 lakini ukienda kwenye randama hii, Mheshimiwa Waziri ulichokiandika huku kwamba unafanya marekebisho ya shule zetu sicho ulichoandika, unaomba na nafikiri umefanya hivyo kwa sababu mkijua wengi Wabunge hatusomi randama, umeandika fedha hizo shilingi bilioni nane unajenga ujenzi wa ofisi ndogo ya Wizara Dodoma pamoja na ukarabati wa Makao Makuu ya Wizara shilingi 6,153,000,000 lakini ukaandika kwamba ni ukarabati na upanuzi wa Taasisi ya elimu ya Watu wazima shilingi bilioni mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo shilingi 8,153,000,000 huku ulivyotuandikia kwamba unafanya *rehabilitation ya schools*, sicho kabisa ni uongo na niombe majibu ya kina kwa sababu shilingi bilioni nane ukigawa kwa idadi ya madarasa ni zaidi ya madarasa 1,000 yanatakiwa yajengwe kwa fedha hizo na nasema hivyo kwa sababu mmekuja na sera ya elimu bure, watoto wanakaa chini Mheshimiwa Waziri kipaumbele chako ni kujenga ofisi yako kwa shilingi bilioni sita na shilingi bilioni mbili ilihali ukijua watoto wa Kitanzania wanakaa chini, chini ya Wizara yako.

Kwa hiyo, nahitaji uniambie ni kwa nini Waziri mwenzetu, mwanamke mwenzetu, mwenye uchungu kwa watoto wa Kitanzania unatenga fedha zaidi ya shilingi bilioni nane kwa ajili ya ujenzi wa ofisi yako ilihali watoto wanakaa chini na Wizara hiyo unaongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa la Kitanzania *literacy level* yetu ni asilimia 67. Watanzania wengi zaidi ya asilimia 30 bado kusoma na kuandika ni tatizo. Lakini kwa hali ya kawaida Taifa hili ambalo linapigana vita, maaskari hawa ambao wako vitani wamesahauliwa kwa asilimia zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa sababu kama Mbunge wa Jimbo nilikaa na walimu wangu kuwafikia kwenye shule zote zaidi ya 30 katika Jimbo la Babati Mjini. Wala haya ninayoyachangia siyabahatishi na maaskari na walimu hawa ambao wanapambana na ujinga katika Taifa la Tanzania na naamini haya nitakayosema ambayo nimeambiwa na walimu wangu wa Babati ndiyo wanayopata walimu katika nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la madaraja walimu wetu. Mmetoa miongozo kwa miaka mitatu mnapandisha madaraja lakini walimu wanaofundisha huko katika shule zetu wanakaa miaka minne hawajapandishwa madaraja, lakini Mheshimiwa Waziri mnawapandisha madaraja kwa *ceiling* ya bajeti. Mimi naomba niishauri Serikali, kwanini mnawagawa walimu na maaskari hawa ambao wanapigana katika Taifa la Tanzania kuondoa ujinga? Kama hakuna fedha msiwagawe walimu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna walimu wanaajiriwa pamoja, kwenye madaraja wanatofautiana, kwenye mishahara wametofautiana, kwa nini? Mnapeleka wachache eti ukomo wa bajeti wengine wasubiri, nani kakwambia hivyo Mheshimiwa Waziri? Huu ni ubaguzi, walimu hawa kama hakuna fedha subirini mkipata muwapandishe hata kwa miaka mitano wote au miaka minne badala ya kuwagawa, hilo naomba majibu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine wanaohamishwa kutoka Mkoa mmoja kwenda mwingine, Halmashauri nyingine kwenda nyingine akifika anaanza upya, daraja halipandi, anaambiwa huko ulikotoka ndiko ambako mambo yako yamekosewa, hebu Waziri tuambie leo hivi kuhamishwa ni dhambi kwenda kusaidia sehemu nyingine? Kwa nini walimu hawa wakihamishwa kwenda Halmashauri nyingine madaraja yao wanaanza upya, hawaendelei na madaraja waliyonayo? Unaongoza hiyo Wizara tupe majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti lakini lingine, hivi Serikali haina mpango kazi kwa walimu? *Transport allowance*? Leo anaibuka Makonda anasema walimu wapande mabasi bure. Msiwalipe *transport allowance* kwa nini? Yaani Serikali mmeacha walimu yeyote aamue kwamba hawa leo wapande bodaboda, hawa wapande mabasi bure, hawa wakejeliwe hivi kwa nini? Muwalipe walimu wetu *transpot allowance*. *Sitting allowance* hamuwalipi, yaani mwalimu hana *shift* yoyote, kwanza wanalalamika muda wanaingia saa moja wanatoka saa kumi, hawana wa kuwapokea wakati madaktari, manesi na fani zingine wana-

*shift* lakini pia wanalipwa *on call allowance*, mwalimu halipwi *housing allowance*, *sitting allowance* wala *transport allowance*, umempeleka kijijini kule hakuna nyumba. Hivi kweli Mheshimiwa Waziri umekaa kwenye Wizara hiyo kwa muda mrefu, haya matatizo unayafahamu, leo nahitaji majibu kwa ajili ya walimu wa Taifa hili la Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Waraka wa Elimu Bure, sawa, mmeiga kutoka kwetu UKAWA elimu bure mkakurupuka mkaanzisha. Haya mtuambie na mimi niliuliza swali kwa Waziri Mkuu, ni kwa nini mmekurupuka katika hili la elimu bure? Mnachokifanya sasa hivi shule zetu hakuna pesa. Shule ya wanafunzi 800 mnapeleka OC ya shilingi 200,000. Madeni katika shule zetu, Mheshimiwa Waziri tangu mwaka jana shule zinadaiwa pesa za ulinzi, za maji, za umeme kila shule yangu niliyopita inadaiwa zaidi ya milioni tano. OC ya shilingi 200,000 inaendeshaje shule? Mnaua elimu ya Tanzania. Mmetuachia huko kwa TAMISEMI mnasema kwamba huko tutafute pesa, hakuna. Mnabadilishia gear angani. Mlituambia kwenye waraka kwamba madawati wazazi hawatachanga leo wazazi wa Babati wanachangishwa Madawati, mnageuzia gear angani. Mtuambie kwanini mnatudanganya? Na hizi fedha mnapeleka lini tunahitaji mtuambie msitudanganye Watoto wetu wanakaa chini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa walimu wa sayansi. Mheshimiwa Waziri, zaidi ya walimu 30,000 wanahitajika wa sayansi katika nchi hii. Nimepita kwenye shule za sekondari, ninauliza hata mwalimu aliyesoma *BAM (Basic Applied Mathematics) A-level* aniambie kama yupo afundishe *mathematics*, hakuna mwalimu wa hesabu kwenye shule za sekondari halafu Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yako unasema ujenzi wa maabara katika shule zetu za sekondari utakamilika mwaka 2018/2019 ndiyo vifaa vya maabara utapeleka huko. Tunapataje walimu wa sayansi ilihali hata maabara huko hakuna vifaa na hampeleki? Mnajenga ofisi zenu kwa shilingi bilioni nane, mnataka walimu wa sayansi wa *mathematics*, wa *chemistry* hawapo kwenye shule zetu, mnategemea mtabadilisha Taifa hili kweli elimu ya nchi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha shule hatuna walimu wa sayansi. Mheshimiwa Waziri nikushauri tu, walimu wa *arts* tunao wakutosha. Boresheni VETA, pelekeni vijana wetu huko VETA muwadahili walimu wa sayansi, mtupelekee walimu wa sayansi kwenye shule zetu. Msitegemee watapatikana huku juu, huku chini hata hayo maabara mmeshindwa kujenga. Waziri nakupa tu ushauri wewe ni Mwananmke mwenzangu naomba tu nikupe ushauri labda utanielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine niurejeshaji wa mikopo. Mheshimiwa Waziri Bunge lililopita tulikuwa tunalipa, mimi ni-*declare interest*, mimi nimelipa nimemaliza. Lakini Bunge lililopita tuliandaliwa mpango hapa, Wabunge wote tumelipa, tumekuwepo Bunge lililopita. Hivi nchi hii kodi mpaka ikusanywe



mpaka Magufuli aende na polisi na mbwa kama alivyoenda bandarini ndiyo mkusanye? Ndiyo mtakusanya? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti mbona sijaona mkakati wa ninyi kukusanya fedha hizi, mtuambie wazi wazi, halafu mnasema mtu akichelewa kulipa eti mnampiga *interest* ya 10% kwa sababu amechelewa, ajira ziko wapi? Wamekaa mtaani hawana ajira baadae unampiga eti *penalty* ya 10%, kweli Mheshimiwa Waziri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani muache kuimba Serikali ya Magufuli, hii nchi ni ya kwetu sote! Isiwe ni *one man show* kwamba Magufuli asipofikiria ninyi Mawaziri mnasubiri leo anaamkaje anasemaje, njoo na mpango kazi wako wa kukusanya hizo fedha, hata hapa basi ungetuita Wabunge wote hapa tujue nani anadaiwa, tulipe hizo pesa. Lakini pia utuambie na hao wengine ambao wameajiriwa kwenye sekta ambazo sio rasmi wanalipaje, sio tunamsubiri Rais akisema basi wote ndiyo tunaenda huko, hapana! Hatuwezi mkaendesha nchi kwa *show* ya kiasi hicho! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala zima la shule za awali. Mheshimiwa Waziri najua utasema iko TAMISEMI, jamani mmechukua sera ya elimu bure, basi tembeleeni! Mtoke na Simbachawene muende hizo shule. Walimu kwanza hawana mitaala na watoto wetu wanakaa chini ya miti, hakuna darasa, mmewaambia Wakurugenzi watafute hizo fedha wajenge, hawana! *Collection* za Halmashauri ndiyo hizo mnasema mnaenda kukusanya wenyewe, mpaka zitoke lini? Watoto wananyeshewa na mvua!

Naomba leo mniambie Mheshimiwa Waziri, Wizara ya Elimu iko chini yako, sera na mambo mengine naomba leo utuambie kwenye hili Bunge, una mkakati gani kwa ajili ya watoto wetu wazuri? Wale wa miaka mitano ambao wanakaa chini, mkituachia Halmashauri tujenge hayo madarasa tutajenga kwa muda gani kama Serikali ya CCM mmejenga VETA kwa miaka 10 hata VETA moja kwa Wilaya haijakamilika! Mnategemea hao watoto...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendele. Mnategemea watajenga shule hizi za msingi....

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ni kengele ya pili hiyo!

Mheshimiwa Gekul hiyo ni ya pili naambiwa! (Makofi)



Tunaendelea na mchangiaji mwingine, Mheshimiwa Zubeda Hassan na baadaye Mheshimiwa Mashimba Ndaki. Mheshimiwa Bonnah Kaluwa na Mheshimiwa Ester Mahawe wajiandae.

**MHE. ZUBEDA H. SAKURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia lakini kabla ya kuanza kuchangia ningependa kushukuru chama changu cha Demokrasia na Maendeleo kwa kunipa nafasi ya kuwa wakilishi wa Mkoa wa Ruvuma kupitia Baraza la Wanawake wa CHADEMA. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kabla sijachangia ningependa kupongeza hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani ambayo imekuja na mawazo mbadala na naamini kwamba Waziri ukiwa makini utaweza kuyachukua mawazo yetu kwa sababu yanaelezea viini vya matatizo lakini pia yanaelezea ni wapi tunaweza kulipeleka Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya Tanzania iko rehani. Leo tunapozungumza, tunazungumza juu ya mtoto wa Kitanzania ambaye anashindwa kushindana katika soko la ajira katika dunia hii. Kwenye dunia ambayo tunaendana na kasi kubwa ya mabadiliko ya kiuchumi na teknolojia, mtoto wa Tanzania leo anajifundisha kuhusu *World War One* lakini *application* yake katika maisha ya kawaida hatuyaoni. Sidhani kama Marekani, nchi zilizoendelea leo wanajifunza kuhusu *Majimaji War* na bado wana mapinduzi katika uchumi wa viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia kuhusu mtoto wa Kitanzania katika ushindani wa soko la ajira, tunampeleka wapi mtoto wa Kitanzania ambaye leo atika mfumo wa elimu kuanzia *primary education* mpaka *secondary education* anasoma kitu kile kile lakini kwa *replication* ya utofauti wa lugha! Kuanzia darasa la tatu mpaka darasa la saba binti wa Kitanzania, kijana wa Kitanzania anasoma kuhusu sayansi kwa lugha ya kiswahili, akienda kusoma *form one* mpaka *form four* anaenda kusoma *the same thing* katika lugha ya kiingereza. Tunaenda mbele au tunarudi nyuma? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna changamoto kubwa ya kuweza kushindana na soko la ajira katika Afrika Mashariki, na nioneshe masikitiko yangu makubwa kwamba kati ya vitu ambavyo Tanzania imeviweka rehani kwa mfano tukizungumzia suala zima la elimu ni pamoja na kubadilishwa kwa mitaala kwa kauli za Mawaziri. (Makofi)

Leo Taifa letu linaendeshwa kutokana na kauli za Mawaziri au *vision* ya Waziri badala ya *vision* ya Kitaifa ya mtaala wa elimu! Akija mmoja leo akifikiria kwamba sayansi ni muhimu kwa watoto wa Kitanzania, basi wote tunasomeshwa sayansi, akija mwingine akiamini kwamba biashara ni muhimu

kwa waototo wa Kitanzania wote tinasomeshwa biashara, tunaelekea wapi kama Taifa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nabado tujue kwamba na nashukuru kwamba Waziri Mkuu katika hotuba yake aliyoitoa Aprili, 2016 alizungumzia kuhusu kutoajirika kwa kijana wa Kitanzania kwa kushindwa kupata elimu na ujuzi wa kuweza kujiajiri na kuajiriwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja ya sisi kama Tanzania, *set aside our political differences*, kuwa na mpango wa Kitaifa utakaoweza ku-match gap kati ya mahitaji ya soko la ajira na kile tunachokizalisha. Leo hii ukimchukua mtotowa Kitanzania kwenda kushindana na mtoto Jumuiya tu ya Afrika Mashariki, mtoto wa Kenya, mtoto wa Kitanzania anakaa wapi? Mhitimu wa Kitanzania anakaa wapi? Tunacheza pata potea kwenye elimu na tumewaweka watoto wa maskini katika ombwe wasijue watafanya nini wanapohitimu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nasikitika sana Serikali inapokuja na hoja ya kuwa na ada elekezi. Unawekaje ada elekezi pale ambapo umeshindwa kuboresha miundombinu ya shule za Serikali? Na niseme tu mimi ni tunda au uzao la shule za Serikali, nimesoma *all government schools*, lakini shule nilizosoma leo ukiangalia matokeo yake na *quality of the output they put in the market is a mess, is a shame*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia kuhusu masuala ya kutoa ada elekezi lazima tuji-reflect katika matendo yetu, miundombinu ambayo tumeiweka katika shule za Serikali ni rafiki? Leo mnazungumzia kuhusu mimba za viherehere na nashukuru sana baadhi ya Wabunge wa upande wa Kambi ya CCM wamezungumzia kuhusu mimba za utotoni, lakini Rais wa Awamu ya Nne aliyekuwa na dhamana alisema ni mimba za viherehere, ni kauli mbaya ambayo haijawahi kutolewa na Mkuu wa Nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kabisa changamoto ya watoto wanaotoka vijijini imetokana na ubovu wa miundombinu, umbali wa shule, lakini pia kutokuwa na miundombinu rafiki kwao. Leo hii tuna wanafunzi ambao wamepewa mimba na walimu wa shule za msingi, *how do we place them katika market?* Nafikiri Waziri kwa sababu wewe ni mwanamke na tupo katika zama za kuweza ku-value mchango wa mtoto wa kike katika kujenga uchumi na kujitegemea, basi naamini kwamba leo utatoa agizo la kufuta *the ban* ya watoto wa shule wanaopata mimba kutorudi shuleni. (Makofi)

Kuna kitu ambacho kinanifurahisha sana. Wakati ukiwa Mkurugenzi wa Baraza la Mitihani la Taifa, *sorry!* Mheshimiwa Waziri ulitoa picha mwanafunzi amechora *zombie* na akachekwa, lakini je, Tanzania tuna wachoraji wa

kutosha kujivunia? Katika mitaala yetu, tuna mitaala ambayo inaweza ku-*accomodate fine and performing arts*? Au sisi tunachagua tu baadhi ya *career*? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo kijana aliyechora *zombie* kama angepewa elimu ya ziada ya kuweza kujifunza *fine and performing arts*, si ajabu alivyochora *zombie* angepata A. leo hii anawekewa *failure* kwa sababu ameshindwa ku-*accommodate* masomo. Na mimi Mheshimiwa Waziri nikuambie Mheshimiwa Mwenyekiti aniruhusu, ni kati ya wanafunzi ambao waliweka *determination* na kuacha kile ambacho niliambiwa nisome. Leo katika Tanzania watoto wengi wanasoma si vile ambavyo wao wanataka bali mfumo unachotaka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazalisha madaktari wengi, juzi katika hoja sikuchangia, lakini katika hoja ya Wizara ya Afya kuna wanafunzi wahitimu karibu 1,000 ambao wamesoma udaktari leo hawana kazi, mfumo umewatenga. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie tena kuhusu migogoro inayoendelea katika vyuo vyetu vikuu. Ni dhahiri, shahiri kuna matabaka ya ushiriki wa wanafunzi katika vyuo vikuu kutokana na matabaka ya utofauti wa itikadi zao. Pamoja na kwamba kuna Mbunge aliongea hapa akaelezea kwamba hakuna u-CHADEMA, hakuna u-CCM, tuna ushahidi wa mwanafunzi ambaye alikuwa *Vice President* wa Chuo cha UDOM ambaye amesimamishwa masomo kwa sababu tu ya kushindwa kufanya kazi kama ambavyo *management* ya chuo ilitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanafunzi huyu Rose Machumu alienda mahakamani akafungua shauri na katika shauri lake mahakama iliona kwamba alikuwa na *legal stand* ya kuwa kiongozi, lakini akapinduliwa. Mapinduzi tu haya ya kawaida tu haya ya kwenye kura za kawaida huku mtaani mnahaha, kwenye vyuo vikuu mnashindwa kushughulikia kwa nini? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niangalie kuna kitabu hiki cha *Africa Development Bail Out* kimeandikwa na Profesa Norman A. S. King ambaye ni mwanachama wenu. Anaelezea na ame-*rank reasons* za kwa nini Tanzania hatuendelei. Mojawapo ya changamoto ambazo ni kwa nini Tanzania na mfumo wa elimu hauendelei ni pamoja na kutokuwa na *match* kati ya uhitaji wa walimu na wanafunzi kitu ambacho ni kweli, lakini kingine anasema *poor quality of teachers in primary school* yaani walimu wa shule za msingi hawakidhi viwango. Lakini pia anasema *lack of housing for teachers*, kukosekana kwa malazi kwa ajili ya walimu kumesababisha kuwa na matokeo mabaya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna changamoto nyingine nyingi ambazo shule zinakumbana nazo na leo hii mimi huwa nashangazwa sana, tunasemaje kwamba kuna upungufu wa madarasa, tunashangiliaje kuwa na ongezeko la madarasa nchini kama kiwango cha utoaji wa elimu kiko duni? Tunawezaje kushangilia ongezeko la wanafunzi wanaofaulu wakati kati ya hao wanaofaulu hawajui kusoma na kuandika? Tunawezaje leo kushangilia kuwa na ongezeko la maabara ambazo kimsingi hizo maabara hazitoweza kufanya kazi mpaka sijui bajeti ya mwaka gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongeleaje kuwa na maendeleo katika sekta ya elimu wakati mwalimu wa Kitanzania hana malipo stahiki wala yenye staha na kumuwezesha kumudu haki zake? Tunazungumzia kwamba kuna mambo mengi ya msingi ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi, kuna kitu ambacho kina-*neglect* na kuvunja moyo sana na kuvunja moyo sana katika Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanaitwa *Tanzania One*, wale vijana waofanya vizuri katika msomo yao, wakishakuja Bungeni, wakipigiwa makofi, wakishapewa zawadi laki moja, laki mbili hatma yao haijulikani. Kwanza nitoe pongezi zangu kwa mwanafunzi Gertrude Clement aliweza kuhutubia UN lakini pia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ZUBEDA H. SAKURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante! Tunaendelea na Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze pia kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri Profesa Ndalichako na Naibu Waziri mama *Engineer* Stella, lakini pia nimpe pole kufiwa na mama yake, Mungu aendeleo kumtia nguvu katika wakati huu mgumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye kujadili hotuba ya Mheshimiwa Waziri na nianze na eneo la ada elekezi. Nilikuwa najiuliza kuna tatizo gani mpaka tuanze na ada elekezi? Tatizo hili linamgusa nani? Na nilikuwa najiuliza, wanaopeleka kwenye shule hizi za binafsi ni akina nani? Si

Mawaziri, sio Makatibu Wakuu, sio Makamishna, sio Wabunge na watu wengine wakubwa wakubwa?

Sasa Mheshimiwa Waziri anapoileta hapa au tunapoiona, mimi najiuliza pia je, hii sio *conflict of interest*? Kwa sababu wanaopeleka watoto kwenye shule hizi ambazo sasa zinatakiwa zipewe ada elekezi ni watu walio na uwezo mkubwa kifedha. Na kama tutakubali ada elekezi kwa shule hizi za binafsi maana yake tunatafuta unafuu wa wakubwa na kama watapata unafuu hawa wakubwa kwenye shule hizi za binafsi basi tusahau shule zetu za Serikali kuboreshwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za Serikali ni nyingi kuliko shule za binafsi. Kama zingekuwa ni bora zingeweza kuchukua watoto wote wanaofaulu kwenda sekondari, kidato cha kwanza mpaka cha nne, kidato cha tano mpaka cha sita na hizi shule za binafsi zingekosa wateja. Lakini sasa kwa nini shule hizi za binafsi zinachukua watoto wetu? Ni kwa sababu shule zetu za Serikali tunazitelekeza, miundombinu yake mibovu, walimu wachache, ndiyo hawa hatuwalipi vizuri, ndiyo hawa ambao Wabunge wanalalamika hapa hawapandishwi madaraja na ndiyo hawa ambao wakitaka pesa ya nauli kwenda likizo hapewi. Lakini kwenye shule hizi hayo yote wanapewa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini huyu mwalimu asifundishe vizuri? Kwa nini huyu anayemiliki shule binafsi anapolipa pesa hii asitengeneze miundombinu mizuri ya madarasa? Nyumba za walimu na mambo mengine? Kwa hiyo. Mheshimiwa Waziri mimi ningekuomba tu ungekuja na mkakati mahsusi kwa ajili ya kuboresha shule zetu za Serikali, tunazo kuanzia ngazi ya kata, kata zote zina sekondari, vijiji vyote vina shule za msingi. Sasa hizi zinatakiwa ziboreshwe. Tuwe na walimu ambao wako *motivated*, tuwe na madarasa yanayotosha, tuwe na vitabu vinavyotosha, mazingira kwa ujumla kwenye shule zetu yawe bora. Hizi shule za binafsi watapunguza wenyewe ada zao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kama shule za Serikali zimekuwa nzuri, zinatoa kile wanachotaka wazazi naniatapeleka mtoto wake shule ya binafsi akalipe laki tano, akalipe milioni au ngapi? Sasa nimesikia kwenye majibu ya Mheshimiwa Waziri alipokuwa anaulizwa swali wakati mmoja kwenye Bunge hili, akasema; tunatafuata namna ya kuzitofautisha hizi ada kulingana na shule hizi za binafsi. Sasa nikawa najiuliza pia tunataka kurudi kule kwenye matabaka ambayo Mwalimu Nyerere aliyakataa? Kuna shule za wenye hela, shule za wasio na hela, shule za weusi, shule za weupe. Mimi nafikiri itatuletea matatizo. Suala la ada elekezi tungeliacha, kwa walioamua kuanzisha hizo shule waziendeshe kwa gharama hizo watakazoweza, kama wanashindwa wazifunge. (Makofi)

Niende kwenye suala lingine la pili. Elimu ya msingi bure. Naipongeza Serikali yangu kwa mkakati wake wa elimu bure. Elimu bure imesaidia kuchukua watoto waliokuwa wanafichwa kwa sababu ya michango mbalimbali na ada mbalimbali zilizokuwepo kwenye shule za msingi na shule za sekondari na matokeo yake kwenye shule za msingi uandikishaji umeongezeka. Sisi kwenye Mkoa wetu wa Simiyu uandikishaji ni 123%; kwenye Wilaya yangu ya Maswa asilimia 130 na kitu. Watoto wengi wameandikishwa na hivyo tunaamini watoto wengi watakata elimu kuanzia ya msingi na hata ya sekondari. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa kutokana na kuongezeka huku kuna tatizo la miundombinu kwenye shule zetu za msingi na shule zetu za sekondari. Hatuna madarasa ya kutosha, hatuna nyumba za walimu za kutosha, hatuna vyoo vya kutosha. Aidha, kwenye shule za sekondari maabara zetu hazijakamilika na mahali pengine bado yameanzishwa tu maboma yakaishia hapo na Serikali ilipoanzisha tena mchango wa madawati ndio basi kabisa habari ya maabara imesahuliwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa ninamsihi Mheshimiwa Waziri kwamba hebu tujaribu kuja na mkakati unaoeleweka kuhusiana na mapungufu haya.

Waheshimiwa Wabunge, wengi wameelezea habari ya mapungufu haya kwa hiyo, hiki ni kielelezo kwamba, kila mahali kuna tatizo kubwa la upungufu wa madarasa, nyumba za walimu, ofisi za walimu, vyoo; upungufu huu ni mkubwa. Tunajitahidi na Halmashauri zetu, lakini ni vizuri Wizara hii kwa sababu, ndio Wizara mama na ndio yenye kuelekeza ubora wa elimu kwenye nchi yetu waje na mkakati ni kwa namna gani tunatatua tatizo hili kwa sababu, tumekazana na habari ya madawati, lakini najiuliza madawati haya yanawekwa wapi? Juani kwenye mti? Kwa sababu madarasa hayapo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule yangu moja ina darasa la kwanza mpaka la saba ina madarasa matatu tu, shule ya Zawa! Lakini tunapeleka madawati pale ambayo tumechangishana kule. Najuliza tunaenda kuyaweka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wetu ambao pia wana madai chungu nzima kama walivyosema wenzangu hawana nyumba za walimu na hasa kwenye Jimbo langu shida ni kubwa sasa matokeo yake napata *allocation* ya walimu anakaa miaka mitatu anaomba uhamisho ahame kwa sababu, nyumba za walimu hazipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikaja na mkakati ni kwa namna gani mkakati unaoeleweka ni kwa namna gani unatatua mapungufu haya ambayo tumeyataja hapa. (Makofi)



*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umemalizika. Naomba tuendelee na Mheshimiwa Bonnah Kaluwa.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga...

**MHE. BONNAH M. KALUWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kushukuru kupata nafasi hii, ili na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara nyeti ambayo inaongoza mustakabali wa elimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kuchangia katika Sera yetu ambayo iko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo inazungumzia elimu bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu bure tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutuletea elimu bure kwa watoto wetu, lakini hii elimu bure imekuwa na changamoto kubwa. Jimbo la Segerea tuna shule 37 na tuna wanafunzi ambao wamejiandikisha kwa sasa ni 8,949. Katika Jimbo la Segerea ukitembelea hizi shule Mheshimiwa Waziri wewe mwenyewe utaona huruma na utashangaa. Najua wewe utasema kwamba, unasimamia sera na hii iko kwa TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama ni sera Mheshimiwa Waziri naomba usimamie hizi shule zipate miundombinu ambayo tunaihitaji kwa sababu mwaka 2013 mlikuja na programu ya kila kata kuweka maabara, lakini kabla hamjamaliza maabara zile kuweka vifaa tumekuja na programu nyingine ambayo ni elimu bure, lakini katika hiyo elimu bure tunaanza sasa kutafuta madawati, tunatafuta miundombinu, tunatafuta mambo ambayo sisi wenyewe inaonekana tulikuwa hatujajipanga vizuri. Na hii inasababisha na inaweza ikatuletea matatizo katika elimu yetu na baadaye kuleta matabaka katika elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Segerea kama nilivyosema lina shule 37, lakini kuna madarasa mengine watoto wa darasa la kwanza wako A, B, C, D yaani ina maana kuna wengine wanaingia asubuhi, wengine wanaingia saa 07.00 mchana, wengine wanaingia saa 10.00 jioni, sasa hii yote ni kuwatesa watoto! Mheshimiwa Waziri tunaomba Waziri wa TAMISEMI hili jambo la elimu bure alishughulikie kwa makini sana kwa sababu, tunapoliachia hili jambo tuna miaka tisa na baadaye tutaona madhara yake. Baadaye mtoto atakayemaliza *form four* atakuwa hawezi kusoma au kuandika jina lake, lakini sisi tutaanza kushangaa kusema kwamba pengine ni wazazi au ni walimu. *(Makofi)*



Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu tunawapa mzigo mkubwa. Unakuta mwalimu amesimama anafundisha hana hata nafasi ya kufundishia. Amesimama hapa wanafunzi wameanzia hapa kukaa chini. Mtoto amekaa chini anaandika, hawezi hata kuona anaandika kitu gani. Halafu baadaye tunasema kwamba elimu yetu imeshuka. Elimu yetu inashuka, sisi wenyewe hatuna msingi, hatujajenga msingi mzuri wa kuboresha elimu ya Tanzania.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri kwanza uangalie zile maabara ambazo tumejenga mwaka 2013 mpaka sasa hivi ziko kama mapambo, hakuna kitu chochote kinachoendelea katika maabara zetu. Naomba usimamie hilo ili hizo maabara ziweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine Mheshimiwa Waziri naomba niongelee wanafunzi wahitimu wanaohitimu wanaomaliza shule kutoka vyuo vikuu. Hapa tuna wahitimu wa aina nyingi, lakini wahitimu ambao wamepata mafunzo ya vitendo ni madaktari, wauguzi na walimu. Hatuwezi kufikia uchumi wa kati wakati sisi hatujawaandaa wahitimu wanaotoka vyuo vikuu waje kupambana na kutengeneza ajira na kuajiri watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ningeomba sana, pamoja na mkakati wako wa kusema kwamba unaboresha miundombinu ya vyuo na mambo mengine, ningeomba pia uwaangalie na hawa vijana wahitimu wanafanyaje kupata ajira au kujitengenezea ajira kutokana na hiyo elimu yao ambayo wameisoma na sio tu kwamba ni elimu wakimaliza wanakuja huku mtaani, na mtaani tunajua kabisa kwamba, Serikali uwezo wake wa kuajiri hatuwezi kuajiri wahitimu wote, lakini kama mhitimu atakuwa ametengenezewa uwezo wa kujijiri na kuajiri yeye mwenyewe, basi tunaweza tukapunguza matatizo ya ajira za kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambacho ninataka niongelee ni kuhusiana na changamoto ambazo zinawapata walimu. Walimu sasa hivi ambao wanafundisha shule za msingi, lakini pia na shule za sekondari; kuna walimu wengine wanashindwa kuingia kwenye vipindi kufundisha kwa sababu ya kudai madai yao. Kuna walimu wengine ambao unakutana nao Manispaa hawaelewi wanaenda kumdai nani na kama tunavyosema sasa hivi tunasema Hapa Kazi Tu, lakini mwalimu kama hajapata mshahara wake hawezi kukaa akamfundisha mtoto, inabidi afuatilie pesa zake, ili aweze kula na familia yake.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri uangalie kwanza masuala ya walimu, lakini pia, uangalie miundombinu ya shule pamoja na kwamba inasimamiwa na TAMISEMI, lakini cha tatu uangalie mitaala ya vyuo vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hawa wahitimu wanavyohitimu vyuo vikuu, lakini pia, muwaandae waweze kupambana na soko la ajira kwa sababu sasa hivi huwezi kumlinganisha mhitimu aliyemaliza chuo kikuu cha Tanzania na mhitimu wa chuo kikuu cha nje, *obvious* huyu wa kwetu hapa atashindwa kwa sababu hajafundishwa kwa vitendo.

Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, najua wewe ni mtaalam na ni mfanyakazi mzuri unaweza ukayasimamia haya mambo na sio mwanasiasa, unaweza ukasimamia vizuri haya mambo yakakaa vizuri ili kesho na keshokutwa tusije tukapata tabaka la watu ambao wamesoma vizuri na watu ambao hawajasoma vizuri ikawa ni matatizo kwetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Bonna, tunaendelea na Mheshimiwa Ester Mahawe na baadae atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanne Mchemba ajiandae,

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza naomba tu ni-*declare interest* mapema kwamba mimi ni mdau wa elimu pia, ni mwalimu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa sera ya elimu bure ama elimu bila malipo, lakini inayogharamiwa na Serikali. Ninajua kila kitu kina mwanzo mgumu, mtoto hazaliwi leo akakimbia, hata nani angekuja na Sera hii na yeye angeweza kuyumbayumba hapa katikati. Hata ndege inapotaka kuruka huwa kuna tatizo mara nyingi na mwisho wa siku ikifika kwenye *cruising point* inasimama sawasawa na inakwenda. Mimi niseme tu niwatie moyo sana Mheshimiwa Waziri Mama Ndalichako pamoja na Mheshimiwa *Engineer* Mama Stella Manyanya, tunawaamini sana akinamama tuko nyuma yenu, pigeni mzigo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kama inavyoeleweka elimu ni ufunguo wa maisha. Na hata neno la Mungu linasema, mkamate sana elimu asiendezake, mshike sana maana huyo ndio uzima wako. Ninaomba tu niombe Serikali yetu sasa, hebu iwekeze sana kwenye elimu. Taifa lolote ambalo elimu yake haijakaa sawasawa linazalisha watumwa ambao watakwenda kutumia matajiri.

Kwa hiyo, mimi naomba tu Serikali yetu iendelee sasa, hii ingekuwa ni Wizara ambayo ilipaswa ipate bajeti kubwa kuliko Wizara nyingine zozote kwa

umuhimu wake. Itoshe sasa walimu na ualimu kutokupewa kipaumbele katika nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu waliopata *division four* karibu na zero ndio wanaokwenda kusoma ualimu, unategemea nini na hawa watu ndio wanaotuanzishia msingi wa elimu nchi hii. Msingi wowote, hata kama ni nyumba unajenga huwezi ukaanza na msingi mbovu huko juu ukaweka zege, hiyo nyumba ni lazima itadondoka *at the end of the day*. Wale aliofaulu wakapata *first class* ndio wanaosubiri kuwapokea hawa watoto watakapofika Chuo Kikuu wakati hawa watoto wana mwanzo mbaya. Ifike mahali walimu nao wapewe nafasi ya *ku-up grade*, waweze kuboresha elimu zao na wapewe nafasi ya kwenda kujiendeleza. Na ikiwezekana hata watu wanaotokea *division one* na *two* waende wakasomee ualimu kwani kuna dhambi gani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo litazamwe sana, imekuwa hivyo kwa miaka mingi, tutaendelea kumtafuta mchawi, mchawi ni sisi wenyewe ambao tunaweka sera mbovu kwenye elimu, mwisho tunabakia kulalamika kila iitwapo leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba tu nizungumzie pia, suala la mitaala. Mitaala hii imekuwa ikibadilishwa kila wakati, ifike mahali kuwe na *Standing Orders* kwenye Wizara ya Elimu, sio kila Waziri anayeingia anaingia na lake, tunachanganywa. Wakati tukiwa tunasoma wengi wetu tulioko hapa, nakumbuka kuna kitabu kimoja cha Kiswahili, kitabu chenye lile shairi linalosema karudi baba mmoja toka safari ya mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka nilikuwa naimba lile shairi nikiwa darasa la kwanza japo haikuwa *level* yangu kwa sababu, lilikuwa linaimbwa na ndugu zangu walionitangulia, kulikuwa kuna *system* nzuri. Nani ametuloga tukaondoa hiyo *system*? Tuangalie tulikoangukia ili tuweze kuboresha elimu yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyowahi ku-*declare interest*, nimesema mimi ni mdau katika shule binafsi. Sheria ya Elimu ya mwaka 1978 inaeleza kwamba shule sio biashara, shule ni huduma. Mwalimu Nyerere alisema watu wa asasi za kidini na wenye mapenzi mema waweze kuisaidia Serikali katika kutoa elimu, lakini leo tunashindwa kuelewa tumekuwa maadui? Kwa nini isifike mahali Serikali ikaona sisi ni *partners* badala ya *competitors* wakati tunawasomesha Watanzania hao hao? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi peke yake ambayo shule zisizo za Serikali zinalipa kodi. Tumetembea nchi mbalimbali humu duniani, wanapata *capitation grant* kutoka kwenye Serikali zao, wanalipiwa walimu wao mishahara. Sisi tunafanya kila kitu wenyewe, tunakopa mikopo 24% *interest*

kwenye mabenki, unanunua ardhi, unajenga shule, unalipa mishahara, unalisha watoto, unafanya kila kitu, leo tunaambiwa ada elekezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hii ni sawa na kwamba mtoto wako mimba umebeba mwenyewe, mtoto umemlea mwenyewe, shule umempeleka mwenyewe, anayekuja kuo anakupangia mahari. Sasa namna hii tutafika? Ikiwa tu bado tuna ukakasi na tuna mahitaji makubwa kwenye shule zetu za Serikali, tutakapoanza tena kuzitibua hizi zisizo za Serikali ambazo hata kwa kunukuu tu niseme, shule 50 bora mwaka jana katika kidato cha nne zilikuwa zimetoka kwa shule binafsi, yaani tunavuruga huku wakati hata huku bado hatujaweka sawasawa! Kwa kweli, hatutendewi haki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mlolongo wa kodi. Ada elekezi si tatizo, lakini mimi nilikuwa ninaishauri Serikali ituondolee huu msururu wa kodi ili kwamba tuwasaidie hata watoto watokao kwenye mazingira magumu. Niseme tu ukweli, mimi shuleni kwangu nina watoto 67 yatima ninaowa-sponsor mwenyewe. Watoto hawa wametelekezwa, ni shule ipi ya Serikali ambayo inaangalia hawa watoto wa namna hii? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamiliki wa shule binafsi wanajitahidi sana kuchukua watoto hawa. Serikali iondoe hizi kodi ili tuweze kuwasaidia watoto wengi wa namna hii, tupunguze wingi wa watoto wa mitaani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalipa kodi zifuatazo, inawezekana Wabunge hawafahamu ama wananchi huko nje hawajui; na hizi kodi unapozi-impose kwetu hakuna mwingine atakayezilipa ni mlaji ambaye ni mzazi. Iko hivi, tunalipa *Land Rent, Property Tax, Business License, Sign Boards Levy, City Service Levy, Corporation Tax, SDL, Workers Compensation Fund, Work Residence Permit Fee, Fire, OSHA*, taja yote tunalipa. Tunafanya biashara gani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaisadia Serikali kusomesha Watanzania, kabla ya hapo watu walikuwa wanasomesha watoto Kenya na Uganda. Tumejitoa muhanga, wengine wamekufa kwa *pressure* kwa ajili ya kudaiwa na mabenki, wengine mna ushahidi hapa wameshindwa kulipa madeni ya benki mtu anakufa na *pressure* na wamiliki wengi wa shule wana-suffer na masuala ya *pressure* na sukari kwa sababu ya ugumu wa kuendesha hizi shule. Leo ni nani mwenye shule ambaye ana biashara nyingine pembeni ya uendeshaji wa shule? Kama ulikuwa unaendesha *nursery school* uta-up grade utafungua *primary*, bado ni elimu ileile! Utatoka *primary* utaanzisha *secondary*, utatoka *secondary* utaenda *colleges*! Yet tunawasomesha Watanzania hawa hawa, kwa nini Serikali isitupatie dawati pale Wizara ya Elimu, ili kwamba, na sisi tuweze kutoa maoni yetu pale? Ili kusaidia mitaala hii inayotungwa watu wakiwa wamejifungia vyumbani bila kupokea maoni ya wadau wengine? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilifanyika semina ya walimu wa darasa la kwanza na la pili hapa Dodoma, hatukuelezwa watu wa shule binafsi kwamba, kuna semina ya namna hiyo na wakati kwenye shule zetu kuna wanafunzi wa namna hiyo. Tunatengwa, sisi tumebaki yatima, Serikali ituangalie sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pia tukaambiwa tupake magari rangi ya njano, tunaongezewa gharama, gari moja ni shilingi milioni tatu mpaka tano, mwingine ana magari 50 ni shilingi ngapi hizo? Nani atazilipa kama sio mzazi wa Kitanzania? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi tukubali, kama ni hiyo ada elekezi basi ije tujue kwamba ada elekezi imekuja, lakini hatulipishwi kodi za namna hii zinaumiza sana. Tuna madeni kwenye mabenki kwa ajili ya kujenga madarasa wanakosoma watoto wa Kitanzania, hata mtu akifa leo anaacha shule inaendelea kusomesha Watanzania, lakini wewe umekufa na *pressure* kwa ajili ya uendeshaji wa shule za namna hii. Tutaendelea hivi mpaka lini? Itafika mahali hawa wadau watafunga hizi shule zao basi turudishe watoto Kenya na Uganda kama ndicho tunachokitafuta. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano wa shule yenye watoto 350 ambao ada yake labda makusanyo kwa mwaka ni kama shilingi milioni 216, lakini shule kama hii inalipa kodi shilingi milioni 85, kwa faida ipi anayotengeneza mwenye shule? Weka tu chakula cha mtoto shilingi 10,000 hata kwa siku 90 anazokaa mtoto shuleni ni shilingi ngapi? Tunaumizwa. Ifike mahali sasa kilio chetu kisikilizwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nilikuwa nafikiri *there is no fair play here*. Wizara ya Elimu ama TAMISEMI ina shule zake, watu binafsi wana shule zao, lakini anayetu-monitor ni Wizara ya Elimu. Ni sawa na mchezaji wa simba awe referee wakati yanga na Simba wanacheza, hivi kweli hatapendelea timu yake? (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. ESTER A. MAHAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Mwanne Mchemba, na baadaye Mheshimiwa Yussuf Kaiza pamoja na Mheshimiwa Zainabu Mussa Bakari wajiandae.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii na mimi niweze kuchangia kutoa machache ambayo niliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kumpongeza Mheshimiwa Profesa Ndalichako, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu, pamoja na watumishi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba nimeipitia, sijasoma yote lakini nimeielewa. Pia nishukuru Mungu kwamba leo Mheshimiwa Simbachawene yupo, kwa hiyo, haya nitakayoyasema na yeye pia yatamgusa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tabora una historia kubwa sana ya suala zima la elimu, ina historia kubwa mno, lakini Tabora inaongoza kwa kuwa na shule zenye vipaji maalum. Shule za vipaji maalum hazijawahi kushika nafasi kumi bora, kwa nini hazijawahi kushika? Shule hizi zimetelekezwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini shule hizi hawasomi wakazi wa Tabora, wanafunzi wa Tabora, ni wanafunzi wa nchi nzima ambao wanapeleka kusoma kama vipaji maalum lakini wakishuka pale getini vipaji maalum havipo. Kwa sababu *Tabora Boys* ina historia hata ya Baba wa Taifa, Milambo ina historia ya Baba wa Taifa, *Tabora Girls* ina historia kubwa mno, viongozi wengi wemetoka *Tabora Girls* hususani wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mazingira yaliyopo katika shule hizi hayafai, watoto wanaokwenda pale wanateseka, miundombinu ni mibovu. Wanafunzi wanaokwenda pale hata kama walikuwa na shida ya kusoma hawawezi kusoma. Miundombinu ambayo naizungumzia hakuna maji, umeme na miundombinu ya shule zile hazijafanyiwa ukarabati miaka dahari na dahari. Kwa hiyo, wale wazazi wanaowapeleka watoto kwa sababu wako mbali anaambiwa tu mtoto amefaulu anampeleka lakini mazingira ni magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali sasa iangalie kwa nini shule hizi hazipati nafasi ya kushika nafasi kumi bora, lakini kama tutakuwa tunawalaumu walimu hatuwatendei haki. Shule ya *Tabora Girls* ni ya wasichana, shule ile tumeomba kujenga uzio takribani sijui miaka 30 sasa, shule ile ni pana, wanafunzi wale mabweni ni mabovu, tunajitahidi sana kusema uzio ule ukamilike lakini wanafunzi wanaogopa kwa sababu panapokuwa hakuna uzio usalama wa watoto wa kike ni mdogo. Usalama wa wanafunzi wale kwa sababu ni wanawake wanaogopa na ni kweli wanateseka, kwa sababu ikifika usiku hawawezi kutoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niiombe Serikali yangu kwa sababu ni sikivu iangalie usalama wa wale wanafunzi wa shule ya sekondari ya wasichana, wanateseka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hilo tu, wanapokosa maji, wanafuzi wa kike, wanawake wote mliomo humu mnajua. Mnajua adha ya mtoto wa kike anapofika katika siku zake anavyoteseka kwenda kutafua maji. Wanawake wenzangumimi niombe Wizara hii ilete mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba shule zote nchi nzima ambazo wasichana wanasoma wapewe kipaumbele za taulo. Kwa sababu kwa kweli aah, mimi siwezi kusema mengi lakini wanawake tunajua. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shule hizi kuna upungufu mkubwa wa walimu wa sayansi, hakuna unategemea nini, niombe madamu tunaita shule za vipaji maalum basi Serikali iwape kipaumbele ili walimu hawa wa sayansi waweze kufika huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia madai ya wazabuni. Wazabuni hawa ndio wanaohudumia hawa watoto, shule hizi ni kama za watoto yatima, wanapokosa huduma chakula ni matatizo, hawana mahali pa kushika. Kwa mfano, kuna wadai wa zabuni wanadai tangu mwaka 2011 Mheshimiwa Ndalichako. Na ndio maana nimesema Mheshimiwa Simbachawene alipate hili, mwaka 2011 wazabuni wanadai, mwaka 2013 wanadai, mwaka 2014 wanadai, hawajapewa fedha zao. Hawa watu wengine wanakwenda kwenye mikopo lakini unategemea watawahudumia wanafunzi? Kwa hiyo mimi niombe hili wasipolitolea ufafanzu wa madai ya wazabuni patakuwa hapatoshi hapa, nitashika mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora, pia tuna chuo cha elimu cha Walimu, nacho kimetelekezwa, miundombinu hovyoy, hivi unategemea mwalimu anayejifunza kwa tabu atakwenda kufundisha huko mnakompeleka? Kwa hiyo ningeomba Chuo cha Ualimu Tabora kiangaliwe na kipewe nafasi ya kukarabati miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hilo tu nizungumzie habari ya Chuo cha VETA. Chuo cha VETA ni kikubwa mno na majengo mazuri sana kuliko Chuo cha Chang'ombe. Lakini VETA Tabora haijatangazika, hakuna, hata ukisoma humu hutapata maelekezo ya Chuo cha VETA Tabora, hakipo. Chuo cha VETA Tabora au nchi nzima watu wengi wanafikiri chuo cha VETA ni wale walioshindwa darasa la saba, sio kweli. Tukiviendeleza vyyo vya VETA nchi nzima tutatoa wataalam wazuri kuliko wa chuo kikuu kwa sababu hawa ni watu ambao wanajituma na hawa watakuwa na uchungu wa maisha. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali yangu iangalie ni jinsi gani itaweza kuwasaidia wanafunzi wanaomaliza VETA kuwapa vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tusipowapa vitendea kazi anamaliza kusoma akishamaliza kusoma unamwambia nenda kajijiri, anaenda kujajiri wapi. Wapewe mikopo, wakishapewa mikopo wanaweza wakafanya



kazi nzuri ambayo itasaidia pia na wao kuwaendeleza katika maisha yao. Lakini nishukuru pia Serikali kuunganisha VETA na FDC. FDC nayo ilikuwa imekufa, ilikuwa haipo, lakini ndio ilikuwa inasaidia mpaka vijijini, kwa sababu vyuo vingi viko mjini, lakini FDC ilikuwa inakwenda mpaka vijijini watu wanapata elimu ambayo ilikuwa inawasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi niombe Wizara ya Elimu na Wizara ya TAMISEMI washirikiane kikamilifu kuisaidia Wizara hii ya Elimu ambayo ndio inayotambuliwa ingawa ni mtambuka, lakini kuipeleka TAMISEMI Wizara ya Elimu ni kama kuionea. Kwa sababu kila mtu anayejua ukimwambia habari ya TAMISEMI haelewi, walimu wana madai yao, wana madai mengi kwa sababu TAMISEMI wameelemewa na mzigo mkubwa, afya imeenda huko, elimu imeenda uko, sijui nini wamepelekewa huko, mara wakusanye kodi huko huko, ardhi huko huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba kwa heshima na taadhima Wizara hizi zikae chini na zifanye mambo ambayo wataanzania wataridhika, wataelewa, jamani msione hivi walimu wanapata taabu kubwa mno tena kuwe na fungu maalum la kuwakopesha walimu hata magari, hivi Serikali inashindwa kudhamini walimu wakopeshwe magari ambayo watakuwa wanakatwa kwenye mishahara yao, hiyo nayo itatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nyumba za walimu, nyumba za walimu hata hizi shule nazosema za vipaji maalum ziko hovyoy, haziko katika mazingira ya kumfanya mwalimu ambaye anastahili kufundisha shule zile. Ahsante nashukuru sana naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mchemba. Tunaendelea na Mheshimiwa Yussuf Kaiza na baadae Mheshimiwa Zainabu Mussa Bakari na Mheshimiwa Oscar Mukasa wajiandaye.

**MHE. YUSSUF KAIZA MAKAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pili niendeleo kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Chake Chake kwa kuniamini, lakini tatu nikishukuru chama changu na niwashukuru pia wananchi wa Chake Chake kwa kuendelea kuyaheshimu maazimio na maagizo ya chama chao. (Makofi)

Baada shukrani hizo naomba sasa nianze kuchangia hoja, na nianze kwa kumnukuu Rais wa mwanzo wa Afrika ya Kusini Iliyohuru, Hayati Nelson Mandela aliwahi kusema; *“education is the most powerful weapon which you can use to change the world.”* Elimu ndio silaha pekee, taaluma ndio silaha pekee inayoweza ikatumika kuubadili ulimwengu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie kiriri hiki, nitumie nyumba hii kusema kwamba elimu ndio silaha pekee ya kuibadili Tanzania, si jambo lingine. Si Jeshi, si Polisi wala si kingine kitakachoweza kuibadili Tanzania isipokuwa tutumie elimu yetu, tu-*invest* kwenye elimu ndio itakayoweza kututoa hapa tulipo tukaenda tunapotaka. *The best way* ni kutumia elimu kwenda kwenye uchumi tunaoutaka wa viwanda, *the best way* ni kutumia elimu kwenda kwenye demokrasia halisi na mambo mengine yenye faida kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la mikopo limezungumzwa na wazungumzaji wengi, wachangiaji wengi wamelizungumza suala hili kwa kina. Ila kwa sababu na mimi ni mdau katika suala hili la mikopo naomba nizungumze kwa mantiki ifuatayo; kwanza niwashukuru kama Serikali niwashukuru kwamba mmeianzishia sheria madum, sheria mlitunga, Namba 9 ya mwaka 2004 ya kwamba isimamie Bodi ya Mikopo ambayo itawezesha kuwapa mikopo vijana wetu wa elimu ya juu, lakini sheria hii ikaeleza kwamba wanaopaswa kupewa mikopo ni wale tu wenye mahitaji ya kupewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si kila Mtanzania kwamba anapaswa kupewa mikopo kwa mujibu wa sheria hii, ila *practically* ni vinginevyo. Wale watu waliosoma katika shule za kayumba wanakoseshwa mikopo na wanapewa watoto wa Mawaziri na watoto wengine wa vigogo. Kwa hiyo, niseme suala hili lina changamoto kubwa, kwanza ucheleweshaji wa mikopo ya wanafunzi, ni changamoto kubwa kwa Serikali na hii ndio inayosababisha migogoro baina ya Bodi ya Mikopo na wanafunzi na Wizara ya Elimu, ucheleweshaji wa mikopo ya wanafunzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, , lakini pili wanafunzi wasio na sifa, kupewa mikopo hii, lakini lingine Ofisi za Kanda zimefunguliwa kwenye suala la mikopo. Kuna Ofisi za Kanda katika Miji Mikubwa kama Mbeya, Arusha, Zanzibar, lakini ofisi hizi pengine kuna mtumishi mmoja tu ambaye hawezi kutimiza majukumu ya kikanda, Zanzibar akuna mtumishi na kuna Ofisi ya Kanda. Lakini wanafunzi wanaopata mikopo kutoka Bodi ya Bara au Bodi ya Muungano ya Mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu wanalazimika kusafiri kutoka Zanzibar kuja Bodi ya Mikopo Dar es salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitengemea sisi ile ofisi ya Kanda iliyopo Zanzibar isaidie kutatua kero za wanafunzi wanaopata mikopo pale Zanzibar. Kwa hiyo, hii ni tatizo nini *result* ya changamoto hizi za wanafunzi, nini *result* yake, matokeo yake wanafunzi wanaandamana hovy hovy, baadaye mnaweka ma-*red block* kila mahali. Mfano leo tu, hatuhitaji hata kutoa historia leo tu wanafunzi wa *natural science* wa Chuo Kikuu cha Dodoma walitaka kuandamana kuja kudai fedha na hawajawahi kuingia darasani toka tarehe Mosi Aprili. Leo wanakuja kudai fedha, kutumia njia za kidemokrasia kwa

sababu maandamano ni haki, mnawanyanyasa, mnaweka magari humo, *tension* barabarani, vitambaa vyekundu wanakuja hapa kuomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la mikopo mnawapelekea baada ya maandamano, kingine ni kuwafukuza wanafunzi. Wanaandamana mnawabandikizia kesi, huyu CHADEMA, huyu nani, huyu CUF jambo ambalo si la msingi kabisa, watu wanadai haki ya msingi kabisa. Lakini changamoto nyingine wanafunzi wanaenda wakijiiza, kwa sababu ya kukosa mikopo hii kwa wakati. Baadae mnaanza kudili watu wanaojiiza sijui huko Dar es Salaam wasiwepo na nini, ninyi hamjatimiza wajibu wenu Serikali ya CCM, tafadhalini timizeni wajibu wenu kwa wanafunzi hawa, tujenge Taifa letu kwa pamoja.

Mheshimwa Mwenyekiti, ushauri wangu, Serikali kupitia Wizara ya Elimu kwanza itimize wajibu wake wa kupeleka fedha kwa wakati, mpeleke fedha ili kuepuka changamoto hizi, lakini pia wanafunzi wanapoandamana kwa kudai haki na ninyi mkijua kwamba fedha hizi hamjawapa kwa wakati muwaache wadai haki zao kwa sababu wanaeleza hisia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni kwamba hili suala la Dkt. Suleiman alilolieleza Baraza la Mitihani. Kuna Baraza la Mitihani (NECTA), mimi nataka kulizungumzia kivingine kabisa, ni kwamba Baraza la Mitihani ndio linalopanga *division* au GPA. Miaka mingi tumekuwa tumekuwa tukitumia *division*, mwaka 2012 kukafeli wanafunzi wengi hasa kutoka Zanzibar ikaundwa tume na Waziri Mkuu iliyoongozwa na Profesa Sifuni Mchome na Wabunge humu akina Mwenyekiti Mbatia walikuwemo, Mkaja na mapendekezo waliyopendekeza kwenda kwenye GPA lakini sasa siku saba tarehe Mosi mlienda Waziri....

Kengele ya kwanza...

**MWENYEKITI:** Ya pili Mheshimiwa Kaiza, tunaendela na Mheshimiwa Zainabu Musa Bakar, baadaye Mheshimiwa Oscar Mukasa atafuatia.

#### TAARIFA

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuweka rekodi vizuri kwenye hiyo Tume iliyoteuliwa na Mheshimwa Waziri Mkuu Pinda tarehe 02/03/2013 siku ya Jumamosi James Mbatia sikushiriki kwenye Tume hiyo.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Zainabu Mussa Bakari.

**MHE. ZAINABU MUSSA BAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, awali nimshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kuniwezesha kuwa na pumzi na kusimama hapa. Pili nikishukuru chama changu kwa kuniwezesha pia kuwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda na mimi nichangie katika Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi. Elimu ni kila kitu katika Taifa hili la Tanzania na Taifa lolote duniani. Elimu ni suala nyeti na ni suala ambalo linaigusa Taifa. Hata katika dini zetu suala hili limetiliwa mkazo, nikirejea katika dini yangu ambayo mimi ni muumini, dini yangu ya kiislamu tumeamrisha kutafuta elimu hata kama ni China na vilevile elimu ni faradhi kwa muislamu wa kike ama wa kiume, na hata katika dini zote nadhani suala hili limetiliwa mkazo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama suala hili limetiliwa mkazo katika dini zote na katika tamaduni zote, ni muhimu pia na Walimu tuwape umuhimu huo huo. Imekuwa ni rahisi sana kwamba walimu hatuwatendei haki katika Taifa hili, Walimu wanapata matatizo mengi kusomesha watoto wetu, wanajitahidi kufundisha watoto wetu kihaki lillah! Leo hii ndiyo tunaodharau Walimu hao, leo hii hatuwasikilizi mahitaji yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi mtu ambaye anakupa kitu muhimu; hivi mtu ambaye anakuthamini, wewe huwezi kumthamini, ni kwa nini? Hiyo siyo haki na hatuwatendei haki kama inavyopaswa. Walimu hao hao leo wanapodai madaai yao Serikali inawawekea kitimoto. Aidha, wanapoandamana wataweza kufukuzwa kazi, ama kitimoto cha aina yoyote cha kuweza kuwadhalilisha hao Walimu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipowathamini Walimu wetu, hivi tutawathamini nani wengine?

**MBUNGE FULANI:** Hakuna!

**MHE. ZAINABU MUSSA BAKARI:** Kwa sababu Walimu hawa ni muhimu katika kila sekta. Wewe usingekuwa kiongozi kama hukupitia kwa Mwalimu, asingekuwa daktari kama hakupitia kwa Mwalimu, asingekuwa Rais kama hakupitia kwa Mwalimu. Sasa inakuwaje tunawakandamiza na kuwadhalilisha? Mwalimu huyu anasomesha miaka 50, lakini leo ukienda hana hata mahali pa kukaa. Hii ni haki? Ni kweli tunawatendea haki? Mwalimu huyu anasomesha miaka 50, hana uwezo hata wa kumiliki baiskeli. Lazima Taifa hili likae, litafakari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyoamini ni kwamba Mwalimu ni mtu wa pili baada ya mzazi na anaweza kutoa radhi zikatufika. Naamini katika mwelekeo huo huo, ni kwamba mambo mengi hatuendelei kwa sababu tumewadharau Walimu. Tutapanga mikakati, mipango ya kila aina lakini hatutaendelea kwa namna hii na style hii tunavyowafanyia Walimu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo hapo hapo!

**MBUNGE FULANI:** Hapo hapo! *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. ZAINABU MUSSA BAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tuliambiwa walimu wanatarajiwa kuajiriwa mnamo mwezi wa Tano, sasa tunaingia mwezi wa Sita, Walimu hawajaajiriwa. Naiuliza Serikali, itawaajiri lini Walimu ambao wamekwisha kwenda kuchukua mafunzo? Walimu ambao wamejitolea, ambao wamesoma pengine hata mikopo wamekosa; angalau wafute jasho lao kwa kupata hiyo ajira, kwa sababu elimu yetu haikuandaliwa kwamba unapomaliza shule ujiajiri mwenyewe, hiyo haipo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, nizungumzie suala la elimu kwa upande wa Zanzibar. Suala la elimu kwa upande wa Zanzibar ni tete na ndiyo maana ikawa wanafunzi wa Kidato cha Nne na Kidato cha Sita wanafeli sana. Hapo mwanzo nilidhani kwamba pengine elimu ya *Form Four* mpaka 'A' level kwa kule Zanzibar labda ni elimu ya juu, kwa sababu suala ambalo linahusiana na Muungano ni suala la elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza, wanafunzi wa *Form Four* wanafanya mitihani inayotungwa Tanzania Bara na siyo Tanzania Zanzibar. Mitaala hiyo inacheleweshwa, ndiyo maana watoto wengi wanafeli. Wakati mwingine mwingine anaulizwa pengine habari za pamba, kule Zanzibar hajaiona, wala hajaijua, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, tunaendelea.

**MHE. ZAINABU MUSSA BAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaendelea na uchangiaji, napenda tutambue uwepo wa wageni kumi wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, ambao ni viongozi wa CCM kutoka Wilaya ya Geita, ambao wanaongozwa na Ndugu Muhoja Mapande, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Geita. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Oscar Mukasa na baadaye Mheshimiwa Deogratias Ngalawa ajiandae.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa ya kuzungumza leo kwa niaba ya wananchi wa Biharamulo, lakini nawashukuru Wabunge wote waliotangulia

kuzungumza kwa michango yao mizuri sana ya kuisimamia Serikali yetu, Wizara hii ya Elimu, Teknolojia na Ufundi. Kwa namna ya pekee pia nakupongeza Waziri na timu yako kwa kazi nzuri, lakini nina haya ya kukuambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako makubwa, watu tuna matumaini na wewe Mheshimiwa Waziri, lakini unaingia kwenye Wizara ambayo yako hata madogo ambayo umekuta haiwezi kuyafanya. Sasa una kazi kubwa mbele hapo! Naanza na mfano mdogo tu halafu nitakuja kwenye hotuba yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2014 kijana aitwae Kuzima Suedi wa Biharamulo, Shule ya Sekondari Kagango, alikuwa miongoni mwa vijana kumi bora wa masomo ya sayansi Kitaifa. Akafurahi sana na sisi tukafurahi sana! Wizara ikamwalika kwenye Wiki ya Elimu mwaka 2015 hapa Dodoma, akaja mzazi, Afisa Elimu, chereko chereko nyingi! Mgeni Rasmi akatoa zawadi kwa watu wachache, akasema waliosalia akiwemo wa Biharamulo, zawadi yao ya *laptop* na *cheque* itawafuata. Mpaka leo ni kuzungushana! Afisa Elimu wa Mkoa, wa Wilaya! Hayo ni madogo tu, nakuja lingine la utangulizi kabla sijaja kwenye hotuba. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii habari ya watoto wetu wa kike wanapopata ujauzito kuondolewa shuleni, nafikiri tusilitazame kwa namna tu ya haki yao ya kusoma, nadhani tulipe picha ya ziada. Hii ni habari ya mfumo dume ambao tunauendeleza kwa kiwango kikubwa sana. Mimi najiuliza jambo moja, linapofanyika lile tendo, ni mmoja tu ambaye masikini matokeo yake yanaonekana hadharani, tumbo linakuwa kubwa. Kungekuwa na utaratibu kila mwanaume anayempa mtu ujauzito naye anavimba nundu tunaona, tungejua na mtu mwingine wa kufukuza; kwamba wa kike anafukuzwa shule, wa kiume kama ni mwanafunzi mwenzake naye anafukuzwa; kama mwanaume ni Mwalimu, ama Mbunge, ama Polisi naye anakamatwa siku hiyo kwa sababu ana nundu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunawaonea hawa kwa sababu sisi ushahidi wa kwamba tumeshiriki kwenye hilo, hauonekani mara moja, mpaka tutafute tafute, tunakaa kubishana jambo ambalo liko wazi. Hebu tuwape haki wanawake! Tutafute namna ya kuwezesha watoto wetu wa kike wasipate ujauzito; hiyo ndiyo kazi ya kwanza, lakini inapotokea bahati mbaya limetokea hilo, tusiwahukumu peke yao. Huo ndiyo ujumbe wangu wa kwanza. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja sasa kwenye mchango. Ukiangalia kitabu cha hotuba pale sura ya kwanza, picha ya kwanza kabisa, umeweka picha ya Mheshimiwa Rais na kuna nukuu ya maneno anayoyasema kuhusu elimu; anamalizia, "Serikali ya Awamu ya Tano, itajielekeza katika kuongeza ubora wa elimu inayotolewa, ni pamoja na kuongeza mkazo katika masomo ya



Sayansi. Hiyo ni nukuu. Tunapozungumza hivi, Biharamulo Wilaya nzima, tuna Walimu 560; Walimu wa Sayansi 30; lakini ukiangalia ukurasa wa 19 wa hotuba hii, umeeleza, “katika udhibiti wa ubora wa elimu kwa mwaka wa fedha huu unaokuja, Wizara imepanga kufanya yafuatayo.” Yametajwa mengi pale, lakini sioni mkakati wa kushughulika na suala la Walimu wa Sayansi. Hakuna hata pale! Sasa tunaongea tu nadharia lakini hatuweki mikakati; hatuwezi kutoka hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dunia ya sasa kama tutaendelea na Walimu 30 wafundishe shule 18 zenye wanafunzi 8,900, Walimu 30 wa Sayansi, hatuwezi kutoka tulipo. Inabaki ni jitihada za Afisa Elimu tu kule Biharamulo masikini anahangaika, hivi tunavyoongea ana Walimu wanane wanaojitolea. Amenituma nikuombe uhakikishe kwenye mgao unaokuja kwa sababu ni walimu na wana *degree* na walishajitolea pale, usiwatoe pale. Usije na ubabe baadaye kwamba sisi tunakupangia uende tunakotaka sisi, wakati wamejitolea mwaka mzima pale kabla wewe hujaweza kulipa. Nitakupa majina uwaweke pale, kwa sababu wameshajitolea na wanaipenda Biharamulo na wana sababu kwa nini walijitolea bila kulipwa wakiwa Biharamulo? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije habari ya mitaala. Mwaka 2014 kama siyo mwaka 2015 mlibadilisha mitaala kwa Darasa la Kwanza na la Pili, mkaondoa masomo sita, mkaleta kusoma kuandika; KKK tatu zile. Hivi tunavyozungumza, watoto walio Darasa la Tatu, Walimu wa Kiingereza hawajui wawafundishe kuanzia wapi, kwa sababu walisoma Kiingereza mpaka mwezi wa Tano mwaka 2015, wakiwa la Pili. Mtaala mpya wa Darasa la Tatu unaochukua hali ya sasa, kwamba Kiingereza kianze Darasa la Kwanza haupo. Kwa hiyo, Walimu wanabahatisha tu; na watakaolingia Darasa la Tatu mwaka 2017 wana habari hiyo hiyo. Hatuwezi kufika kwa mtindo huo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninapozungumza, nina vitabu vitatu; viwili vya sayansi Darasa la Saba; kimoja cha sayansi Darasa la Sita. Nchi hii ukiwa Darasa la Sita ubongo wako una sehemu tatu, ukiwa Darasa la Saba ubongo una sehemu nne. Tutakwenda kweli? Hebu imarisha hivyo vitengo vya ukaguzi, tujue tunawafundisha nini wanafunzi kwa *standard* na *consistence*. Tutapanga mipango mikubwa kabisa, ambayo ukisoma kwenye makaratasi inaingia akilini, lakini uhalisia kule chini ni shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu Wizara, hebu tusikie, Waheshimiwa Wabunge wamesema sana kuhusu Walimu, ni Sekta ya Elimu tu ambayo ukitaka kujenga darasa ni lazima Mtendaji wa Kata amkimbize mwananchi kuchanga, lakini sijawahi kusikia Mtendaji wa Kijiji anamfuata mwananchi kumkamata achange pesa ya umeme wa REA. Tumeweka kwenye mfumo. Sijawahi kusikia Mtendaji wa Kijiji anamfuata mwananchi kumkamata achange mfuko wa barabara ili tujenga lami; hakuna! Hata hivyo anachanga na



tumeweka kwenye mfumo. Ni darasa tu na nyumba ya Mwalimu ndiyo lazima wakimbizwe na Mtendaji wa Kata, hebu tuondoke kwenye ujima, tutafute tozo kwenye kodi ambazo tutakamata Sekta ya Elimu na mundombinu yake, tushughulike nayo kama Taifa, ndiyo tutaondoka kwenye hali hiyo.

Napenda pia kuongelea kidogo *COSTECH*, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia. Hebu tuiwezeshe! Tunataka huo ubunifu waanze kuufanya kuanzia kwenye Shule za Sekondari, wawezeshwe waende kule; wawezeshwe Walimu kutambua vipaji mapema, namna gani tutashughulika navyo, kikiwa kipaji bado kiko Biharamulo, kiko kidato cha pili, kipaji kiko kidato cha tatu, tunakijua kipo na tunapanga mpango wa kukiendeleza na kukikamata kitakapofika Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi tena kwenye hoja ambayo nilitaka kuisahau kuhusiana na vitabu vyetu mashuleni. Kuna kitabu kimoja nimekutana nacho kwenye shule moja huko, kimoja kinasema tuna sayari tisa, kingine tuna sayari kumi. Sasa mimi nikachanganyikiwa, hawa watoto wakitoka hapo unataka huyu huyu ndiye aje kushiriki kwenye dunia ya sayansi na teknolojia? Haiwezekani na hatutafika kwa mwendo huo, nashukuru. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Ni kengele ya kwanza?

**MWENYEKITI:** Ya pili Mheshimiwa!

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Ya kwanza!

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Deogratias Ngalawa na baadaye Mheshimiwa Sebastian Kapufi na Mheshimiwa Mariam Kisangi ajiandae.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru kwanza kwa kupata nafasi ya kuweza angalau kujadili hotuba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Kwanza kabisa napenda kutoa kilio changu cha wana wa Ludewa, kwa sababu Ludewa sasa inaonekana ni eneo ambalo limesahaulika kwenye mambo mengi. Hivi ninavyoongea sasa, Jimbo la Ludewa lina uhaba wa Walimu 496, tuna shule 108; katika shule hizo 108 ni shule saba tu ndizo ambazo zina Walimu wanaoweza kukidhi. Shule nyingine zote 101 zina Walimu wanne kushuka chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shule ambayo ina Walimu wawili na shule zilizo nyingi zina Walimu watatu. Kwa hiyo, cha kwanza napenda tu kutoa masikito yangu kwamba tuna uhaba wa Walimu 496 na bahati mbaya kabisa

katika kipindi hiki mmetupatia Walimu 30. Hata hivyo kuna Walimu 25 ambao wanastaafu Septemba na kupelekea uhaba wa Walimu 521.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kuwasiliana na TAMISEMI, sasa napenda kutoa kilio hiki kwako Mheshimiwa Waziri kwa sababu wewe ndiye msimamizi wa elimu Tanzania. Kwa hiyo, naomba tu mwisho wa siku nikuletee majina kwa watu ambao wanataka kwenda kufundisha Ludewa na ikiwezekana basi mfanye utaratibu mtuletee Walimu. Kwa kweli hali ni ngumu na ndiyo maana nimeamua nije nizungumze katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, hata vyuo vyetu vikuu havipeleki wanafunzi kwenda kufanya *field* kule, kwa sababu ya miundombinu mibovu ya barabara na miundombini mibovu ya mashule yetu, kiasi ambacho kimepelekea hata wanafunzi wenyewe wanaotoka kule kuomba msaada huo. Kwa hiyo, naomba nikuwasilishie hilo na hasa Chuo Kikuu cha Dodoma, kwamba hawawezi kupeleka Ludewa, lakini maeneo mengine yote ya Tanzania wanafunzi wanaweza kwenda kufanya *field*. Hii inapelekea shule zetu za Ludewa kuwa na *pass* ya chini kabisa na vijana wetu wengi kufeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda ku-*declare interest*, mimi ni mmiliki wa shule. Nianze na ada elekezi. Nadhani shule hizi za binafsi ndiyo zinazoleta fundisho kwa Serikali yetu kwamba ni namna gani shule zinapaswa ziwe na ninadhani zimeshaweka *standard* ya kuweza ku-move. Kwa hiyo, sababu ya kuweka ada elekezi, siyo za msingi na wala hazifai. Ninajiuliza swali, tusingekuwa na shule za *private*, watoto tulikuwa tunapeleka Kenya na Uganda. Je, kule Uganda tungeweza kupeleka hizo ada elekezi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *suppose* huku tungekuwa hatuna na kipindi kile kabla ya St. Marys kuanza, watoto tulikuwa tunapeleka Kenya. Kwa hiyo, kosa letu ni kuboresha elimu, kutengeza miundombinu mizuri, mpaka inapelekea kuwa tunaongoza kwa hamsini bora. Hilo ndiyo kosa ambalo Serikali imeliona. Nadhani Serikali ingeshukuru, kwa sababu ninaamini kabisa wanafunzi wengi ambao wanang'ara ndani ya mipaka ya Tanzania na nje ya mipaka ya Tanzania, ni wale ambao wanatoka *private school*, wanatuwakilisha. Kwa hiyo, tungewatengenezea miundombinu mizuri, ikiwezekana hata kuchukua mishahara mlipe nyie Serikali, kwa sababu watoto wanaofundishwa ni watoto wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sababu zile za msingi kupelekea kuweka hizo ada elekezi hamna. Kwa sababu usi-*justify* makosa unayoyafanya, usi-*justify* kutokuweka jitihada zozote ili uweze ku-*capitalize* kwenye shule za binafsi. *Play your part*, fanya shughuli zako, ninaamini ukitengeneza miundombinu mizuri, ukiwa na Walimu wa kutosha, hakuna mtu atakayeenda kwenye shule zenye gharama kubwa. Kwa hiyo, isifike kipindi Serikali inashindwa

kufanya wajibu wake, kwa madai tu iende ika-suppress kwenye hizi shule za binafsi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za binafsi ziachwe ziendele, kwa sababu yale mazingira yaliyowekwa vizuri, wamiliki wa shule wengi wamekopa mikopo, wana madeni yenye riba kubwa. Kwa hiyo, maana yake utakaposema unatoa ada elekezi, tutashindwa kulipa yale madeni na mwisho wa siku sasa wakati huku tayari shule za *private* zimeshakaa vizuri, tunabomoa wakati huku kwetu kwenye *government schools* hatujaparekebisha bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni juu ya ujenzi wa Shule ya VETA Shaurimoyo, katika Jimbo la Ludewa. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri hajaiweka kabisa. Shule hii ya VETA kimsingi ilikuwa inaanzishwa pale kwa ajili ya kupokea miradi mikubwa miwili ya makaa ya mawe Mchuchuma na Chuma cha Liganga, kuwaandaa vijana kwenye shughuli za kiufundi ili kuweza kushiriki katika hiyo miradi inayokuja. Nakumbuka mwaka 2012; kama siyo 2012, ni mwaka 2013, Serikali iliji-commit kwamba itajenga chuo hiki. Naamini sababu zile zile za kukitaka kukijenga hazijatoweka, sababu hizo zipo. Mlipeleka wataalam, ardhi imepimwa, hati mmepata, michoro mnayo, BOQs zote mnazo na mlisema mlisatenga hela kwa ajili ya kujenga hicho Chuo cha VETA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza tena swali hili, Chuo hicho kwanini kimeachwa? Matokeo yake, vile ambavyo wala havikuwepo katika kipindi hicho cha miaka miwili, mitatu iliyopita, leo ndiyo vimewekwa. Sasa watu wa Ludewa wanajiuliza maswali ya msingi, pana tatizo gani? Kwanini kisijengwe na kwanini hakuweka kwenye program yake? Kwenye hili Mheshimiwa Waziri hatutakubali kwa sababu kinachoonekana ni kuibagua Ludewa na Ludewa haitaweza kubaguliwa kwa sababu na yenyewe ipo katika nchi ya Tanzania.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja lakini tunaomba Chuo Ludewa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ngalawa. Tunaendelea na Mheshimiwa Sebastian Kapufi na baadaye Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko pamoja na Mheshimiwa Jesca David Kishoa na Mheshimiwa Maftah Nachuma wajiandae.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kinaitwa *the wind of change* au kwa tafsiri yangu mwenyewe, upepo wa mabadiliko. Huko nyuma waliosoma zamani ilikuwa ukichaguliwa kwenda Shule ya Serikali unaona wewe ndio umefanya vizuri na watu hawakuwa tayari kwenda *private schools*, hilo ni jambo lilikuwa huko nyuma. Wote waliobahatika kwenda Shule

za Serikali, walionekana wamefanya vizuri na wenzetu wachache walioenda shule za *private* walionekana kana kwamba hawakufanya vizuri. Liliendelea hilo kwa muda wote na watu waliziheshimu Shule za Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa muda huu tujiulize, tumekosea wapi? Tujiulize tu swali hilo la msingi, tumekosea wapi? Tukishapata majibu, tutajua. Hata hii habari kwamba kuwe na ada elekezi au zisiwepo, ni suala tu la kujiuliza, tumekosea wapi ikiwa huko nyuma watu walipenda Shule za Serikali? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini katika haya yafutayo: kwa kuuliza wewe ni mjinga kwa dakika chache, kwa kutouliza, wewe unakuwa ni mjinga milele. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri, tujiulize ni wapi tumekosea ili tuweze kuwa werevu kwa muda wa kutosha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye Mkoa wangu wa Katavi, tuna mkakati wa ujenzi wa Chuo Kikuu cha Katavi, naomba sana Halmashauri ya Manispaa ya Katavi kwa jitihada zake yenyewe imeanzisha mkakati huo wa ujenzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Katavi pamoja na mazonge zonge mengi yanayoendelea, naomba Mheshimiwa Waziri watu hawa ambao wamekwishatenga eneo, kwanini na nyie kama Wizara msiwa-support wananchi hawa ambao wameonesha *initiative*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu, nami naomba sana, ikiwa Mheshimiwa Rais Kikwete alitoa zawadi ya Chuo Kikuu cha Dodoma kwa Mkoa huu wa Dodoma na nchi kwa ujumla wake, namwomba na Rais wangu Mheshimiwa Dkt. Magufuli, auangalie Mkoa huu wa Katavi, ni mikoa ya pembezoni kwa ukweli. Nami niseme, uwepo wa Chuo Kikuu ni fursa. Maeneo ambayo yana vyuo, yanaibua mambo mengine! Watu wanaokwenda huko kwa ajili ya kusoma na kufanyaje, wanaibua fursa nyingine katika maeneo hayo. Kwa hiyo, naomba sana nikianzia na hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoke hapo niende kwenye Chuo chetu cha VETA, ni Chuo cha siku nyingi, lakini miundombinu imekuwa ni chakavu. Nakuomba Mheshimiwa Waziri tukiangalie, Chuo kile kimejengwa kwa siku nyingi, kinahitaji tu kuboreshewa miundombinu. Nikitoka hapo niende pia kwenye shule kongwe. Nalisema hili kwa sababu ukurasa wangu wa saba umesema ukarabati wa shule kongwe, umetaja shule saba. Nakuomba Mheshimiwa Waziri, kuna shule ya watoto wa kike ya *Mpanda Girls*. Shule ile haina uzio, ni dada zetu na inapelekea watu wanaanza kuvamia maeneo ya shule. Ufumbuzi pekee ni kuwatengenezea fensi; na nikitoka hapo, ni kweli pamoja na huduma ya maji ili wale dada zetu waendeleo kufanya vizuri. (Makofi)

Mhesimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoka hapo kwenye suala la Chuo Kikuu na Mpanda *Girls*, naomba nizungumzie kidogo suala la maslahi. Mimi naamini katika historia. Historia ni somo ambalo linatufunza wapi tumetoka, wapi tulipo na wapi tunakwenda. Kipindi cha nyuma ilikuwa ukiona mtu amevaa vizuri, anamiliki pikipiki au anamiliki baiskeli, ujue ni Mwalimu. Kipindi cha nyuma! Kwa hiyo, mtu ambaye alikuwa nadhifu, amekaa vizuri, ana maslahi mazuri, ni Mwalimu. Kama historia inatuambia tumetoka wapi? Tuko wapi na tunakwenda wapi? Kwanini tusirudi kwenye *history*, tukaangalia *past* ili ituangalie tuko wapi kwa maana ya sasa hivi na baadaye tunakwenda wapi? Tutapata ufumbuzi. Habari ya maslahi ya Walimu wakaaje, wafanywaje, tujifunze tu, huko nyuma tulikuwa tukifanyaje? (Makofi)

Vilevile Mheshimiwa Waziri, kwa maana ya elimu nilikuwa naomba nizungumzie habari ya maktaba ya Mkoa wa Katavi naomba sana eneo hilo. Kwa upande wa Chuo Kikuu, naomba nikizungumzie Chuo Kikuu Huria. Nimeona kuna mkakati wa makusudi wa kuviboresha Vyuo vya maeneo mengine lakini kwa eneo langu la Katavi niseme tena kuhusu habari ya Chuo Kikuu Huria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hatuna chuo chochote. Chuo pekee ambacho kiko kule kwa sasa hivi, ni Chuo Kikuu Huria. Kwa hiyo, nilikuwa naomba miundombinu hiyo ya Chuo Kikuu Huria tuweza kuiboresha ili watu hawa ambao kwa ukweli watoke pale kwenda katika maeneo mengine kwa ajili ya kufuata huduma za shule, waweze kuipata katika eneo ambalo liko jirani na wao. (Makofi)

Eneo la elimu bure, niseme kitu kimoja, naishukuru Serikali kwa hili. Jamani suala hili ni mchakato, nimewahi kusema huko nyuma. Ukiwa umepika chai, habari kwamba chai ina sukari nyingi, una uwezo wa kuongeza maji; au habari kwamba chai haina sukari, unaweza kutafuta sukari. Kwa hiyo, kwanza tumeanza na elimu bure, lakini kwa kutoka hapo tutaendelea kuboresha kwa kadiri mahitaji yanavyohitajika. La msingi ni kwamba tumeanza. *It is a process*, ni mchakato! Siyo suala la mara moja ukamaliza. Kwa hiyo, naipongeza Serikali, lakini na wazazi tuisahau wajibu wetu wa msingi, kuna maeneo ambayo wazazi wana nafasi yao ya kuendelea kuchangia, tusiachie tu Serikali peke yake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo, naomba suala zima la *study* za kusoma kwa maana ya Kuandika Kuhesabu na Kusoma (KKK) lizingatiwe sana. Hilo litaendelea kutusaidia kuwafanya vijana hawa katika hatua ya awali. Ni aibu leo hii kuzungumza kwamba kuna mwanafunzi amepita shule, halafu hajui kusoma, hajui kuandika, hajui kuhesabu. Ili kukidhi mahitaji ya hilo, eneo la ukaguzi limekaaje jamani? Kwa sababu kama kuna eneo la ukaguzi, tutafikaje kusema huyu hajui kusoma? Au huyu hajui kufanyaje! Maana yake kuna

sehemu tumekosea. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri tuboreshe maeneo hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, nashukuru. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kwa namna ya pekee nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba kwanza nianze kwa kukupa hongera nyingi sana Profesa Ndalichako na timu yako, mnafanya kazi nzuri, hongereni sana. Hiyo ni tafsiri kabisa kwamba akina mama wenye ujuzi, mnaweza, hongereni sana! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara hii, niseme tu kwamba Mheshimiwa Waziri unafahamu kwamba asilimia 68 ya *Civil Service* ya nchi hii ni Walimu. Kwa hiyo, zaidi ya Watumishi wa Serikali hii ni Walimu. 68 percent ndiyo *Civil Service* ya nchi hii. Tafadhali sana! Wewe Mheshimiwa Waziri, Waziri wa TAMISEMI, Waziri wa Utumishi, kaeni pamoja kuhakikisha kwamba Walimu hawa tunawapa kipaumbele cha kwanza. Bila wao hakuna nchi hii. Sisi wote tuko hapa kwa sababu tulisoma, kwa sababu tulifundishwa na Walimu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila shaka kila mmoja anafahamu kwamba Walimu hawa wana changamoto nyingi sana. Shule zetu nyingi hazina nyumba za Walimu, shule nyingi hazina madarasa ya kutosha, Halmashauri zetu zinahangaika kushoto na kulia. Naomba, wakati umefika, Serikali yenyewe itafute fedha popote itakapopata fedha hizo, kujumuika na Halmashauri zetu ili miundombinu ya elimu iweze kuwa rafiki na hakika shule zetu ziweze kuboreka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ambalo napenda kulisema, ni hili jambo la ada elekezi. Mimi huwa sielewi vizuri, labda Mheshimiwa Waziri atanifafanulia. Hivi ada elekezi ambazo mng'ang'ana na hao wenye shule, hizi shule siyo mali ya Serikali! Hizi shule ni mali ya watu binafsi. Mmekaa nao? Mmezungumza nao? Mmlewana? Maana yake haya ni kama mtu mwenye mali yako, halafu anakuja mtu mwingine anasema basi weka ada elekezi. Kila mmoja anajua nchi hii, miaka ya 1980 na 1990, watoto wetu walikuwa wakienda Kenya, Uganda na Malawi kusoma. Sasa wenye mitaji yao wameanzisha shule hizi, tunaanza kuja na ada elekezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu na ushauri wangu kwa Serikali, kaeni na wamiliki wa shule hizi, ni mali zao, mwasikilize, Serikali ifanye *facilitation* tu. Hakuna sababu ya kugombana na hawa watu. Tunataka watoto wetu wakasome tena Kenya? Wakasome Uganda? Ni muhimu sana ada elekezi hizi



mkubaliane na wamiliki wa shule, zile shule ni mali yao na kamwe siyo mali ya Serikali; na tumeshatoka huko ambako mali zilikuwa za Serikali, shule zilikuwa za Serikali; sasa shuke hizi ni za watu binafsi. Naomba sana jambo hili Mheshimiwa Waziri, wewe ni mahiri, wewe mwenyewe ni Mwalimu, mkae mliangalie vizuri mkubaliane na hawa wamiliki wa shule na muafaka upatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika mkizungumza na wamiliki wa shule, wana uelewa, wamewekeza fedha zao nina hakika mtafika mahali kwenye *middle ground* ambapo hata kama ni ada elekezi basi ni rafiki kwa wamiliki wa shule na kwamba pia watafanya biashara pamoja na kwamba elimu kwa kweli kwa kiwango kikubwa ni huduma zaidi kuliko biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda niliseme ni haya mafao na malipo ya Walimu, kwa mfano, Walimu katika Halmashauri ya Mji wa Kasulu, Walimu katika Mkoa wa Kigoma, wamekuwa na malimbikizo mengi sana. Nimepata taarifa kwamba juzi wamelipwa, eti madai yao fedha iliyohakikiwa wameletewa asilimia 13 tu basi. Sasa anayefanya uhakiki ni nani huyo? Hawa Walimu ni kipaumbele. Naomba sana Walimu wa Halmashauri ya Mji wa Kasulu, Walimu wa Kasulu Mjini na Halmashauri wahakikiwe vizuri. Unafanyaje uhakiki unakuja na *ten percent* ya uhakiki! Ni kitu ambacho hakikubaliki. Ingekuwa angalau *40 percent*, *50 percent* unaweza ukaelewa, *ten percent*, *13 percent* ya madai yao yaliyohakikiwa, hilo ni dhahiri kabisa kwamba kuna mahali kuna tatizo na tatizo tusiliruhusu likachafua Serikali ya Awamu ya Tano ambayo imeanza kwa matumaini makubwa kwa Watanzania hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda nilizungumze, sisi Mkoa wa Kigoma, tumeanza kujenga *a grand High School*, Shule ya Sayansi. Maana yake Waheshimiwa Wabunge mnafahamu kwamba Mwanasayansi aliyepata tuzo ya Nobel katika nchi hii, anatoka Mkoa wa Kigoma. Tumeanza kwa juhudi zetu wenyewe, tumejenga *a ground high school*, shule ya sayansi. Imejengwa pale Kasulu, tumejichangisha wenyewe, mkoa mzima tumepata karibu shilingi milioni 600 na tumeanza kujenga shule pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Wizara nayo, wewe Mheshimiwa Mama Ndalichako ni mdau, nawe kama Wizara na Serikali kwa ujumla mwangalie namna nzuri ya kusaidia juhudi za watu wa Kasulu na watu wa Kigoma ili hatimaye ile *grand high school* baadaye tuibadilishe iwe Chuo Kikuu. Kitakuwa Chuo Kikuu cha kwanza cha sayansi. Nina hakika kwa uwezo wa vijana wa Kigoma, kitatoa wanasayansi walio bora na walio mahiri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hiyo imeshaanza na wenzetu wa SUMA JKT wametupa ushirikiano mzuri sana, ndio wanatujengea eneo hili. Nasi Halmashauri ya Mji wa Kasulu tumetoa eneo bila fidia, eneo la ekari 115 nami Mbunge wao nimetumia kila lililokuwa ndani ya uwezo wangu, kuhakikisha



kwamba eneo lile limepimwa na linamilikiwa kihalali sasa na Halmashauri na Mkoa wa Kigoma kwa ajili ya ujenzi wa *Grand High School*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nizungumzie ujenzi wa makitaba. Sisi pale katika Mji wa Kasulu tumejenga maktaba. Kipindi kile nikiwa Mbunge mwaka 2005 tulijenga maktaba kwa kushirikiana na wenzetu wa *Tanzania National Parks*. Tumejenga jingo kubwa, lina gorofa mbili. Jengo lile limegota, nafikiri ni wakati muafaka umefika sasa Wizara na Serikali mwingilie kati mtupe nguvu, mtusaidie ili jengo lile sasa lianze kufanya kazi. Malengo na madhumuni ni kufanya maktaba ile kiwe ni kituo cha elimu katika Mji wa Kasulu na ni mji ambao unakua kwa haraka sana kama miji mingine inavyokua katika nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nizungumzie suala la ukaguzi wa shule. Mheshimiwa Waziri, shule hazikaguliwi. Waheshimiwa Wabunge shule za Sekondri na za Msingi hazikaguliwi. Sasa shule hazikugaliwi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja hii, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Nsanzugwanko, tunaendelea na Mheshimiwa Jesca David Kishoa na baadaye tutaendelea na Mheshimiwa Maftaha Nachuma na mwisho atakuja Mheshimiwa Pascal Yohana.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa nashukuru kwa kupata fursa hii kuchangia kwenye hii Wizara ambayo ina uhusiano mkubwa sana na mkoa ambao nauwakilisha kwa maana ya Mkoa wa Singida. Mkoa wa Singida ni miongoni mikoaa ambayo inafanya vibaya sana katika suala la taaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuendelea, naomba mama yangu, Mheshimiwa Waziri Ndalichako, wakati unakuja kuhitimisha nakuomba uje na majibu ya kwanini Walimu takriban 366 wanaotokea Mkoa wa Singida Wilaya ya Iramba hawajapandishwa madaraja toka mwaka 2013 na wakati katika mkoa huu Wilaya nyingine zote Walimu wao wamepandishwa madaraja, lakini kasoro Wilaya ya Iramba peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote humu ndani tunatambua kwamba dunia ya sasa ni dunia ya ushindani, silaha pekee kwenye dunia ya ushindani ni elimu; lakini cha kusikitisha ni kwamba elimu inayotolewa katika Taifa letu ni elimu duni

kabisa. Ni elimu ambayo haijakidhi vigezo. Nasema hata kwa sababu hapa nina taarifa ya *USAID* ya mwaka huu ambayo inaonyesha kwamba asilimia 70 ya wanafunzi hawajui kusoma Kiswahili, Shule ya Msingi na wakati huo huo asilimia 90 ya wanafunzi hawajui kusoma Kiingereza. Kwa tafsiri nyingine ya watu, hata kuandika barua ya kuomba kazi hawawezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Vyuo Vikuu vilivyopo katika Taifa letu, kuna baadhi ya Vyuo Vikuu kwa sasa vimeamua kupanua magori kuhakikisha kwamba wanaanza kusajili wanafunzi kutoka *Form Four* kwa sababu kuna wanafunzi wa *Form Six* hawajakidhi vigezo kuingia Vyuo Vikuu. Takwimu ya *TCU* ya mwaka 2015 inaonyesha kwamba kuna nafasi 25,000 zimeshindwa kuwa *fulfilled* kwa sababu wanafunzi hawajakidhi vigezo vya kwenda *University*. Hii inasikitisha sana na ni aibu! (Makofi)

Sasa katika kutafakari, nikaangalia, msingi wa haya ni nini? Sababu kubwa, kwanza ni kwa sababu hakuna mkazo kwenye suala la elimu. Hakuna mkazo ambao Serikali imepelekea kwenye suala zima la elimu. Niseme tu, nafikiri hii ni kwa sababu anguko la elimu katika Taifa hili haliwahusu Mawaziri, wala haliwahusu vigogo katika Taifa hili. Ila kwa sababu hiyo hapa we are not talking the same language! Hatuongeti lugha moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna msembo mmoja wa Kiswahili unasema hivi: "kilio na mwenyewe." Katika hali ya kawaida katika *cabinet* hii, msiba wa elimu, hamna *member* hapa kwenye *cabinet* ambayo inamhusu kwa namna yoyote ile. Kwa sababu asilimia kubwa watoto wao wanasoma nje na wengine wanasoma shule za *private*. (Makofi)

Kwa hiyo, ifike mahali tulitazame hili kwa sura nyingine. Mfano mzuri ni *UK*. Uingereza, Waziri kumpeleka mtoto wake kusoma shule ya *private* ni kashfa kubwa sana. Naomba kupitia Bunge hili Tukufu nimwombe Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli atangaze rasmi Mawaziri wote wa Taifa hili, watoto wao wasome shule za *government*. Wasome shule za Serikali! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye suala la madawati, ni aibu! Eti wanafunzi milioni tatu na nusu, wingi wote huo wa wanafunzi, wanakaa chini. Upungufu wa madawati ni karibia 1,174,000. Ukiangalia gharama zinazoweza madawati haya, siyo chini ya shilingi ya bilioni 90 mpaka 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, ni vema wakaona kwamba kuna umuhimu hata suala hilo wakalipeleka kwenye jeshi, jeshi likatutengenezea madawati wakawa wanalipa taratibu; au wakatumia mifuko ya hifadhi kuhakikisha kwamba mifuko ya hifadhi inakopesha wanajeshi halafu Serikali inakuwa inailipa taratibu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la ukaguzi. Unapozungumzia ukaguzi, ukaguzi una uhusiano mkubwa sana na *performance* ya mwanafunzi, kwasababu ukaguzi unapelekea kumtambua Mwalimu bora na ubora wa elimu wanayoitoa. Kwa Taifa letu ni aibu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia *Best Education Statistics* za mwaka 2015, zinaonesha karibia asilimia 81 ya shule zote za Msingi hazijafanyiwa ukaguzi, lakini wakati huo huo asilimia 76 ya Shule za Sekondari hazijafanyiwa ukaguzi. Halafu mwaka 2015 mkatenga fedha shilingi bilioni 22.4 kwa ajili ya kupeleka kwenye ukaguzi, mkachukua shilingi bilioni 20 mkawalipa wakaguzi kama mshahara, halafu shilingi bilioni 2.4 ikatumika kwa ajili ya ukaguzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sawasawa na Mbunge hapa amlipe dereva wake mshahara kila mwezi, halafu asiwe anamwendesha, awe anaendesha mwenyewe. Naona huu ni ubadhirifu wa fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu mmoja anaitwa Aristotle aliwahi kusema hivi: “mizizi ya elimu ni michungu, lakini matunda ya elimu ni matamu.” Mimi nabadilisha kwa Taifa letu, “mizizi ya elimu ni michungu na hata matunda ya elimu ni machungu vile vile.” Tafsiri halisi ya elimu ni ili mtu atoe ujinga awe na uwezo wa kukabiliana na changamoto zinazomzunguka. Kwa Taifa letu, watoto wetu wanakwenda shuleni ili mradi wavae *uniform* wafanane na wengine. Ni masuala ya aibu, ambayo ni lazima tuyafanyie kazi haraka iwezekananyo, maana tunachekwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, naomba Waziri, mama yangu Mheshimiwa Profesa Ndalichako kama itakupendeza, muda wowote nikupatie majina haya ya Walimu wote ambao wana madai yao kwa ajili ya kuweza kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja, ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Maftaha Nachuma na baadaye Mheshimiwa Pascal Yohana na Mheshimiwa Philip Mulugo wajiandae.

**MHE. ABDALLAH N. MAFTAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii nami niweze kuchangia mjadala huu jioni hii ya leo inayohusu Wizara ya Elimu. Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunipa afya njema na leo hii niweze kuchangia Wizara hii ipasavyo. Niseme tu kwamba ninayezungumza hapa pia ni Mwalimu, lakini bahati nzuri nimekuwa kwenye sekta hii ya elimu kama Mkuu wa Shuke kwa miaka mitano, kwa hiyo, nitakachozungumza hapa naomba kitiliwe maanani sana na Waheshimiwa Mawaziri wote wanaonisikiliza; Waziri wa TAMISEMI na Waziri wa Elimu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kauli ya Mwalimu Nyerere mwaka 1968 kwenye kitabu chake cha *Education and Self Reliance*, naomba nimnukuu, alisema hivi: *“an antithesis of education is a kind of learning that enables an individual a learner to attain skills and knowledge and use that skill and knowledge to liberate himself and society in which he or she lives by participating in doing developmental actions.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Mwalimu Nyerere mwaka 1968 alizungumza maneno haya, akiwa na maana ya kwamba, kinyume kabisa na mambo mengine yote, elimu ni jambo la msingi sana; na yule aliyeenda shule, lazima miaka yake yote anayosoma darasani aweze ku-acquire skills, ujuzi na knowledge ile lakini aweze kuitumia ile knowledge kujikomboa mwenyewe lakini kuikomboa jamii inayimzunguka kwa maana ya kwamba kulikomboa Taifa hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza haya kwa masikitiko makubwa sana. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikileta danadana katika suala hili la elimu kwa miaka mingi sana. Kila Waziri anayeingia anakuja na mitaala yake, anabadilisha system ya elimu; kila Waziri anayekuja anakuja kutunga Sera za Elimu. Mwisho wa siku Taifa kama Taifa hatuna sera, hatuna mtaala mmoja; kila siku tunayumba na hatuwezi kufikia malengo haya ambayo Mwalimu Nyerere aliyazungumza ya kwamba lengo la elimu ni kumfanya aliyesoma aweze kujikomboa mwenyewe na kuikomboa jamii yake inayomzunguka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawezi kuikomboa wala kujikomboa mwenyewe kwasababu elimu yenyewe anayoipata kwasababu inakuwa haina dira, haina mwelekeo kwa maana kwamba hapati elimu ile tunasema *quality education*, elimu bora. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalizungumza hili kwasababu leo hii tunavyozungumza kuna Wizara mbili, zote zinashughulikia elimu. Ipo Wizara ya TAMISEMI na ipo Wizara ya Elimu. Cha ajabu kabisa, nimesikia hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wakizungumza wakisema hiki usizungumze kwenye Wizara hii ya leo kwasababu hili lipo ndani ya TAMISEMI, wakati sisi Wabunge tunafahamu ya kuwa wakati Waziri Mkuu alivyowasilisha kwa kiasi kikubwa hatuweza kujadili mambo ya elimu. Kwa hiyo, leo ni siku yetu kama Wabunge tuweze kuwaeleza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili kwasababu nchi hii, mitaala yake na mfumo wake unayumbayumba katika elimu, lazima tuwaeleze. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika hili kwa mtazamo wangu na kwa uelewa wangu na kama Mwalimu mzoefu, siwezi kutofautisha kati ya

Wizara ya Elimu ya Waziri Mheshimiwa Ndalichako na Wizara ya TAMISEMI inayoshughulikia elimu. Wote ni kitu kimoja!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala hili la elimu; ili tuweze kuwa na elimu bora ni lazima tuanze katika ngazi zote za elimu. Leo hatuwezi kuzungumzia suala zima la *vocational training*; elimu ya ufundi ambayo Mheshimiwa Profesa Ndalichako anaishughulikia na elimu ya juu kama hatujaweka misingi imara kuanzia *pre-primary education*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kuwa na wanafunzi wazuri ambao wakifundishwa *vocational skills* katika vyuo mbalimbali vya VETA Tanzania, ambao wataweza kufundishwa elimu ya juu, lazima wawe wamefundishwa vizuri kuanzia chekechea. Kwa hiyo, Serikali lazima ihakikishe kwamba inawekeza Elimu ya Msingi kuanzia *pre-primary school education*. Nazungumza haya kwasababu tumezungumza sana kuhusu elimu ya juu kana kwamba hii elimu ya juu inaanzia elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015 na mwaka 2014 nilikuwa nimefanya utafiti mmoja nikiwa Mwalimu; Mwenyekiti wa Wakuu wa Shule Wilaya ya Lindi, nilipewa *paper* ya ku-present mbele ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa inayohusu matokeo makubwa katika elimu. Katika *conclusion* yangu niliweza kuzungumza baada ya utafiti wangu niliufanya kwamba huwezi kuzungumia matokeo makubwa katika elimu *and then* ukaweka neno sasa hivi, kitu ambacho hakiwezekani kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwasababu elimu kama elimu ni mchakato ambao ni endelevu. Mwanafunzi anatakiwa afundishwe kwa muda wa miaka miwili au miaka mitatu elimu ya awali. Afundishwe vizuri! Afundishwe vizuri elimu ya msingi lakini akifika sekondari afundishwe vizuri, ndiyo mwanafunzi huyu atakuwa na uwezo wa kufundishwa elimu ya ufundi kwa kufundishwa masomo ya *Form Five* na *Six* na masomo ya *degree* yake, ataweza kufanya vizuri na ataweza kuwa mwanafunzi ambaye atajikomboa yeye mwenyewe na kuikomboa jamii yake inayomzunguka, lakini siyo danadana na mzaha tunaoufanya leo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwakuwa hili haliwezi kuepukika kama nilivyoeleza hatuwezi kufanya *separation* kati ya Elimu ya Msingi, Sekondari na Elimu ya Vyuo. Naomba nizungumzie suala zima ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza, kuhusu elimu bure. Wizara kama Wizara imetoa Waraka Na. 6 na hapa Mheshimiwa Waziri amezungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ule waraka kuna maelekezo Waheshimiwa Wabunge naomba myasikilize ambayo yanaeleza, nami hapa waraka wenyewe ninao hapa, huu hapa Waraka Na. 6. Imeelezwa mle ndani

kwamba katika mgawanyo wa pesa zinazopelekwa shuleni inatakiwa zitumike katika muktadha ufuatao: Matumizi ya kwanza ni matumizi ya jumla ya ofisi. Hapa tunamaanisha vitambulisho, shajara, maandalio, ulinzi, umeme, maji na fedha za kujikimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine (b), kuna suala zima la uendeshaji wa taaluma, kuna suala zima la mitihani endelevi, kuna suala zima la madawa baridi ya binadamu, mahitaji ya wasichana na kadhalika na matengenezo madogo madogo. Sasa jambo la kusikitisha, ukija katika utekelezaji wa hiyo sera, nilikuwa nafanya utafiti tu kwenye shule zangu kule Jimbo la Mtwara Mjini, ni jambo la ajabu sana. Shule imepelekewa shilingi 27,000/= halafu inaambiwa ifanye mgawanyo huo wote.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ABDALLAH N. MAFTAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Pascal Yohana, baadaye Mheshimiwa Philip Mulugo ajiandae.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami sasa niweze kuchangia Wizara hii muhimu ambayo kwa kweli na mimi naomba ku-*declare interest* kwamba mimi pia ni Mwalimu kama ambavyo wengine wame-*declare interest*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunajadili bajeti ya Wizara ya Elimu, wanafunzi ambao wako Vyuo vya Elimu ya Juu, tangu wamefungua chuo hawajapata mkopo; na hili ni jambo la kusikitisha sana. Imefika mahali wanafunzi wetu wanacheleweshewa mikopo na mikopo ambayo mwisho wa siku watakuja kuirejesha, lakini wanapokuwa sasa wanadai hizo fedha, tunaenda kuwapiga mabomu, tunawapelekea Polisi jambo ambalo linasikitisha sana. Kiukweli kabisa kama mikopo inakuwa inacheleweshwa, nadhani mtu wa kwanza kupigwa bomu inatakiwa awe Waziri wa Elimu na Watendaji wake lakini siyo wanafunzi wetu. Tunawaonea sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba japokuwa pia wenzangu amegusia sana kwenye suala hili la Bodi ya Mikopo, naomba nami niguse baadhi ya vitu pia. Kuna kitu fulani kinaitwa *Quality Assurance Fee* kwenye elimu ya juu. Mwanafunzi anaambiwa alipie shilingi 20,000/= kwa ajili ya kudhibiti ubora wa elimu. Kimsingi jukumu hili la kudhibiti ubora wa elimu ambalo linafanywa na TCU ni jukumu la Serikali. Hivyo, kumbebesha mwanachuo mzigo, ni suala ambalo kwa kweli haliruhusiwi hata kidogo! Kwasababu TCU ni sehemu ya majukumu, inakuwaje tunakwenda kumbebesha mzigo mwanafunzi masikini? Kwa kweli



hali hii inasikitisha sana na sidhani kama inatakiwa tuendelee kuivumilia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na sifa ambazo amepewa mimi sitaki kumsifia, kwasababu siwezi kumsifia mtu wakati ni majukumu yake. Naomba suala hili ukaliangalie sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie suala lingine, kwenye elimu ya juu. Leo wanafunzi hakuna mawasiliano kati ya Wizara ya Ulinzi pamoja na Wizara ya Elimu. Wametangaza kwamba wanafunzi waliomaliza *Form Six* waende JKT kuanzia tarehe 1 mwezi wa Sita hadi tarehe 6 walipoti JKT. Wakati wowote kuanzia sasa wanafunzi watahitajika kuomba mkopo waliomaliza *Form Six*. Tafsihi yake ni nini? Tafsihi yake ni kwamba wanafunzi wanaoenda JKT wengi wanakosa fursa ya kuomba mkopo. Mwaka 2015 wanafunzi 80 waliokwenda JKT walikosa mkopo Chuo Kikuu cha Dar es salaam peke yake sehemu ya Mlimani. Kwenda JKT imekuwa dhambi leo hii? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala hili Mheshimiwa Waziri aliangalie sana, kuwe na utaratibu maalum; kabla hawajaenda JKT, waombe mkopo mapema ili wanapomaliza pale waende chuo tayari wakiwa wameshaomba mkopo. Kama tatizo ndiyo hilo, mwisho wa siku watu watasema kwamba JKT hatuendi kwasababu tukitoka JKT tutakosa mkopo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine ambalo limekuwa ni tatizo kubwa sana. Hakuna mawasiliano kati ya TCU na Bodi ya Mikopo. Kwanini nasema hakuna mawasiliano? Leo ukisoma kitabu cha TCU kinakuonesha kozi ambazo ukienda kusoma utapata mkopo (*priority course*), lakini wakati huo huo anapoomba mwanafunzi kozi hizo kwenda kusoma Bodi ya Mikopo inasema kwamba hizi kozi siyo za mkopo. Hakuna mawasiliano kati ya Bodi ya Mikopo pamoja na TCU. Alishaongea Mheshimiwa Godbless Lema kwamba hii nchi imekuwa kama *ghetto*, hamna utaratibu, nami nadiriki kusema kwamba nchi hii ni kweli hakuna utaratibu! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme maneno makali, tunaendesha nchi utafikiri ile nchi ya kijuha, kwasababu kama Bodi ya Mikopo ni chombo cha Serikali, TCU ni chombo cha Serikali hawa wanakwambia hii kozi inakopesheka, ukienda kule wanakwambia hii kozi haina mkopo. Maana yake ni nini? Mheshimiwa Waziri, naomba ukaliangalie hili. Kama Taifa tunaibika sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba nizungumze suala lingine. Leo kuna changamoto nyingi sana katika elimu ya juu. Ukienda katika *hostel* za wanafunzi wetu; kwa mfano pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tu sehemu ya Mlimani, wanafunzi ambao *hostel* inaweza ku-accommodate ni wanafunzi



6,500, lakini idadi ya wanafunzi ni 18,000. Wanafunzi wengi wanabebana, wanalala wawili kwenye kitanda kimoja. Hali ambayo ni mbaya sana! Leo hii kama kuna fedha inatakiwa zipelekwe basi zinatakiwa zipelekwe kwenye elimu ya juu za kutosha. Kama Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli alipeleka pesa kwa Mahakimu akasema hakuna pesa, kesho kutwa kapeleka; baada ya siku mbili akapeleka, leo mnaonaje kupeleka pesa elimu ya juu? Pesa zipo. Tatizo la nchi hii siyo pesa, tatizo la nchi hii ni uongozi mbovu ambao nadhani kwa muda mrefu sana tumekuwa tukilia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumze suala lingine kuhusu mfumo wa uandaji wa vitabu vya kufundishia na kujifunzia. Leo kutokana na elimu yetu jinsi ilivyo, kila mtu anapanga la kwake. Akilala Mheshimiwa Waziri anaamka asubuhi anasema, leo tunachanganya *Physics* na *Chemistry*, wanafunzi wanaanza kusoma. Kesho mwingine anarudi anasema hapana ulikosea. Hii hali ni kwasababu ya kukosa uongozi bora. Tatizo ni Uongozi katika nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongezee, leo tunataka elimu yetu iwe bora, kuna tatizo la kutowalipa Walimu wetu wanaoidai Serikali. Nataka nitoe mfano mdogo tu. Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, Walimu wanainaidai Serikali zaidi ya shilingi milioni 800 na kitu, hawajalipwa. Watoto wetu watafaulu vipi kwa namna kama hii ambapo Walimu waliokata tamaa wanaidai Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Momba wanaidai Serikali zaidi ya shilingi milioni 600. Walimu hawajalipwa hizo fedha! Ileje Walimu wanaidai Serikali zaidi ya shilingi milioni 400, hawajalipwa. Unataka watoto wafaulu vipi? Suala hili halihitaji kufunga kwa maombi wala kupiga ramli, tatizo ni Serikali! Walimu wengi wameshakata tamaa. Suala hili lisiposhughulikiwa kwa kweli tutaendelea kulia na vilio vyetu havitaisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongezee, kuna Walimu wamesimamia mtihani a Kidato cha Nne mwaka 2015 hawajalipwa fedha zao, karibu shilingi milioni 118 Halmashauri ya Mbozi; leo ni nani Mbunge hapa, ni nani Waziri hapa ambaye posho yake ya mwaka 2015 hajaichukua? Posho yake ya mwaka 2014 hajaichukua! Mshahara wake wa mwezi uliopita hajachukua? Ni nani Waziri hapa au Mbunge? Tuwaonee huruma Walimu! Walimu hawa waliokata tamaa mwisho wa siku wakianza kuandamana, msije mkaanza kutafuta mchawi ni nani. Mchawi ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Magufuli. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu hawa walipwe fedha hizo na wasipolipwa fedha hizo kwasababu sisi ni Wawakilishi wao, nimechangia hata mara ya kwanza nilizungumzia suala hili; tuataenda kukaa nao, ikiwezekana tuingie barabarani. Muwe tayari kutupiga na mabomu! Sawasawa! Kwasababu

hatuwezi kuvumilia Walimu wetu wanateseka! Hata mimi pia ni Mwalimu, nina uchungu sana! Naomba kama kweli tunawapenda Walimu wetu, tukalipe fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo, bado kuna suala la makazi bora ya Walimu, ni tatizo! Ameongea mwenzangu pale kwamba ametokea mahali, kwa mfano wanasema hii ni TAMISEMI, hii ni wapi; lakini makazi bora kwa Walimu ni tatizo. Kuna shule moja ambayo nilikuwa nafundisha kabla sijawa Mbunge, shule hiyo ina nyumba moja tu ya mwalimu. Walimu wanalala nane kwenye nyumba moja. Unaweka kitanda, unaweka godoro chini, *this is shameful!* Kwa kweli suala hili ni aibu sana, Serikali hii lazima ifike mahali iangalie sana kwenye suala la elimu, ahsante.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Yohana. Tunaendelea na..

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba nisiunge mkono hoja na nimshukuru sana Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kuichapa; tunamuunga mkono, Mungu ibariki UKAWA. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Phillip Mulugo na baadaye Mheshimiwa Rachid Chuachua ajijandae.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru sana kwa kunipa nafasi jioni hii kuchangia na kuweza kushauri mambo mbalimbali kuhusu Wizara ya Elimu. Na-*declare interest* kwamba mimi ni Mwalimu *by profession* lakini vile vile ni mmiliki wa shule binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutalaumu sana, tutaongea sana mambo ya Wizara ya Elimu lakini kidogo kuna mambo ya mkanganyiko wa sheria, sera, kanuni na nyaraka mbalimbali. Mambo yanaweza yasiende tukamlaumu Mheshimiwa Profesa Ndalichako, mambo yanaweza yasiende tukamlaumu Mheshimiwa Simbachawene, mambo yanaweza yasiende kumbe yako Wizara ya Utumishi kwa dada yangu pale; na mambo mengine mengi, lakini mengine yako Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mdogo tu, anayelipa mishahara ya Walimu, ni Wizara ya Fedha; anayepandisha Walimu madaraja katika nafasi mbalimbali ni Utumishi; anayesimamia elimu mashuleni ni TAMISEMI, ndiye anayeangalia kama madawati yapo, kama Walimu wamefika tayari

wanafundisha, nyumba za walimu na kujenga madarasa; na usimamizi wote wa elimu kule Shule za Msingi na Sekondari. Ni TAMISEMI wala siyo Wizara ya Elimu. Anayetengeneza Sera ya Elimu ni Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona wenzangu hapa wanachangia na kila kitu wanapiga madongo kwa Wizara ya Elimu. *Well and good* kwa sababu yote ni Serikali kwa ujumla. Nataka vile vile Serikali mjue hilo kwamba lipo jambo moja na lingine linaweza likasababisha huku kukawa kuzuri ama kukawa kubaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kushauri hilo, naomba niingie kwenye hoja zangu. Kwanza naomba nimpungeze sana Mheshimiwa Waziri, Profesa Ndalichako kwa kuteuliwa kuwa Waziri katika Wizara hii. Namfahamu vizuri sana, tumefanya naye kazi vizuri sana. Ni mama mwenye msimamo, lakini mimi huwa namwita ni mama wa *quality of education*. Namfahamu toka akiwa pale Baraza la Mitihani la Taifa. Huwa hapendi mchezo na hataki mambo holela holela! Nadhani mtakuwa mmeona anavyoendelea hata kutumbua baadhi ya majipu fulani fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima mama huyu tumshauri; na kwa hii miezi sita aliyokaa Wizarani yapo baadhi ya mambo yanaonekana, lakini akikaa miaka mitano, tunaweza tukaanza kuona *impact* ya baadhi ya mambo mazuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri. Suala la kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Elimu Nchini ni suala muhimu sana. Nami kwa sababu ni mzoefu wa mambo haya, Waheshimiwa Wabunge naomba nitoe hili jambo mlione jinsi lilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, kama nilivyosema, anatunga sera, lakini Katibu Mkuu wa Wizara ya TAMISEMI ndiye mwenye Shule za Sekondari na Msingi kama Serikali. Vile vile kuna shule za *private* upande mwingine, hawa watu wa TAMONGSCO na TAPIE, kwa wamiliki wa shule. Sasa inakuwaje tena pale pale kwenye Wizara ya Elimu kwa Mheshimiwa Profesa Ndalichako pana watu wanaitwa Wakaguzi wa shule ambao watakapokwenda kukagua shule, wakakuta kwenye Shule ya Msingi matundu ya vyoo ni machache, ama Walimu darasani hawapo, ama shule haina madawati, ama kuna mlundikano wa wanafunzi, wanaandika ripoti, wanampelekea mwajiri. Unategemea mwajiri atafanya nini? Naomba niseme, mwajiri atafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukipata kitu ambacho kinajitegemea, kama ilivyo EWURA, au kama zilivyo bodi nyingine na mambo mengine ambapo labda tumeanzisha Wakala wa Serikali ama mamlaka ambazo ni *independent*;

zinajitegemea, ni *autonomous, agency*, ili ikague shule zote kwa usawa. Ikienda kwenye *private* wasema bwana shule yako haina ubora, haina *fence*, haina vyoo, haina Walimu wenye vyeti vizuri, haina madirisha fulani, haina vitabu na kadhalika, iandike kwamba shule hii imepata asilimia 70. Ikienda na kwenye shule za Umma iandike vile vile, shule hii haina vyoo, ifanye hivi; imwandikie TAMISEMI arekebishe na itoe siku 60 shule irekebishwe; mambo yatakwenenda vizuri sana, kuliko tunavyofanya sasa. Kwa sababu sasa hivi anayeandika ripoti anampelekea mwajiri wake ambaye akiandika vibaya anaweza hata akamfukuza kazi. (Makofi)

Kwa hiyo, ni suala ambalo kidogo naomba mlifikirie, mimi nina udhoefu nalo. Naomba tuanzishe mamlaka huru ya udhibiti wa shule. Leo tunasema ada elekezi; tukipata hicho kitu kitaangalia kila kitu kwenye shule zetu. Mfano mdogo, unaposajili shule ya *private*, sekondari ama *primary* kuna vigezo vingi sana pale Idara ya Udhibiti ambapo zamani ilikuwa Idara ya ukaguzi. Unakuta mwenye shule anajenga kila kitu, anakamilisha madarasa nane, anaweka miundombinu ya shule, walimu vizuri halafu ndipo Serikali inasajili shule maana ina vigezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda kwenye shule za Umma, shule inaanizishwa hata kama ina madarasa mawili. Tukimpata huyo ambaye atakuwa ana-*regulate*, shule ya Umma haiwezi kunzishwa kwenye madarasa matatu; Haiwezi kuanzishwa haina madawati; haiwezi kuanzishwa hawana vyoo; haiwezi kuanzishwa watoto wakakaa 80 darasani. Kwa sababu yule mtu atakuwa ni *independent*, atatoa ripoti ambayo haina upendeleo. Naomba niishauri Serikali na Mheshimiwa Waziri naomba a-*take care* jambo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba sana nimshauri dada yangu Mheshimiwa Profesa Ndulichako, Wizara hii umepewa utakaa miaka mitano hapo, lakini naomba ufanye mambo mengine tutakayoweza kukukumbuka. Katika nchi hii hatuna Chuo cha Ualimu kinachofundisha Walimu kwenda kufundisha *English Medium*. Nani aseme ni chuo gani kipo hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Serikali imekataza shule za binafsi kuchukua Walimu kutoka nchi ya Rwanda, Uganda, Kenya ama mataifa mengine, tunataka tujiweke sisi kama ni kisiwa, tumepandisha kodi mbalimbali ili shule hizi zibanwe, zianze kuchukua Walimu wa ndani ambao hawana hiyo taaluma. Tunaua elimu sisi wenyewe, kwa nini? Kwa nini tuue elimu sisi wenyewe wakati tunajua hatuna Chuo cha namna hiyo? Vyu vyetu vya elimu vinafundisha *certificate* ya kwenda kufundisha masomo yanayofundishika kwa Kiswahili japo *content* ni ile ile na *syllabus* ni ile ile, wanatafsiri tu mtihani.

Leo ukienda wanapotunga mtihani wa Darasa la Nne kwenye *English Medium* wanachukua maswali kwa Kiswahili halafu wanatafsiri. Kuna ada

tunalipa shule za binafsi kwa sababu unasema eti katafsiri mtihani wa Darasa la Nne. Jamani! Tafadhali, Mheshimiwa Waziri naomba uliangalie hili kwa makini sana. Mimi ni Mwalimu, naliona, ni hatari kubwa! Kwa nini tuweke wigo kwa shule za binafsi zisiajiri Walimu kutoka nchi za nje? Tujue Tanzania hii siyo kisiwa, kuna Mabalozi wapo hapa, kuna wafanyakazi mbalimbali kutoka nchi za nje wapo hapa, wawapeleke wapi watoto wakasome shule? Naomba hili nalo lifanyiwe kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba lingine niishauri Serikali; yapo mambo jamani kwa kweli niseme kama ni kero hivi; ama yupo mtu mmoja Wizarani pale akilala akiamka anasema ngoja leo niandike hivi. Hivi unawezaje ukaandika kwamba shule za *private* hakuna kukaririsha wanafunzi? Mzazi anaamua kumpeleka mtoto kwenye shule ya *private*; kwanza naomba nitoe elimu hii. Serikali inachukua wanafunzi waliofaulu, *the best students*, wanawachagua kuwapeleka Shule za Serikali mwezi Januari. Baada ya hapo, wanaokuwa wamebaki, maana yake ni *slow learners*; hujawachagua wewe kuwapeleka kwenye shule zako za Serikali. Shule za *private* zinaokoa jahazi, zinawachukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwatambue kwamba wale ni *slow learners*. *Slow learner* huyo unamwingiza darasani, wengine ndiyo kama hivyo, hawajui hata kusoma na kuandika; unamwingiza darasani, ni lazima umfundishe pole pole. Inafika mwisho wa mwaka ili afanye mtihani wa *Form Two*, hajui chochote, mzazi anakwambia mimi hapa nalipa ada shilingi milioni mbili kwa mwaka, mtoto wangu bado ana umri mdogo, nataka arudie shule. Serikali inasema aah, aendele. Jamani! Ulishawahi kuona wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwe huru, waachieni wazazi wa nchi hii wawe huru. Unaandika barua kwa Afisa Elimu wa Mkoa, wanasema Serikali imesema hakuna kukaririsha. Si ulimwacha mwenyewe huyu motto, ni *slow learner*, sasa amekwenda kwa watu wengine wamfundishe. Kama wanamfundisha na mtu analipa, anafundishika pole pole huyo! Mwache asome. Ruhusuni shule za binafsi zianze kukaririsha. Hata shule za Serikali vile vile zikaririshe kama zamani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo watu wengine tulisoma, tusingekariri tusingekuwa hapa! Tulirudia shule tukasoma, ndiyo maana kuna *private schools*, ndiyo maana kule kwenye mitihani ya *Form Two* kuna kitu kinaitwa *Qualifying Test*, wanasoma hata Elimu ya Watu Wazima. Nini maana ya kuweka kwamba elimu ni *free*? Jamani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya, lingine, naomba niishauri Serikali. Tunataka kuua Elimu ya Ualimu nchini. Tumevichukua Vyuo vya Ualimu kuvipeleka NACTE. Mungu wangu! Hebu naomba nifafanue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, NACTE maana yake ni *National Council of Technical Education*, yaani Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi. Sasa unamchukua Mwalimu anayesoma *education in general* unampeleka akasomee huko. Hakuna utaalum wa kuwalea walimu kule! Turudishe Walimu kwenye Wizara ya Elimu kama ilivyokuwa zamani.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Philipo! *(Makofi)*

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika zimekwisha? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Zimekwisha! *(Makofi)*

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunashukuru. Tunaendelea na Mheshimiwa Rashid Chuachua.

**MHE. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Maana naona Walimu tuko wengi sana, nami nimefundisha zaidi ya miaka 15, ni muhimu sana kutoacha bajeti hii ipite hivi hivi bila ya kuwasemea Walimu na elimu kwa ujumla. Kwa nini? Kwa sababu, kimsingi elimu ndiyo injini ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la kwanza ni kuzungumzia maslahi na madai ya Walimu. Tulitoa ahadi na tunaendelea kutoa ahadi hiyo kwamba tutawatetea Watumishi wa Umma na hili ni jambo la msingi ambalo ni lazima tulifanye. Tumewaahidi tutawatetea na sisi tutafanya kazi hiyo, ila Serikali nayo itimize wajibu wake katika kuhakikisha inatimiza ahadi inazozitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wana changamoto kubwa. Wapo Walimu ambao wanadai kupandishwa mishahara katika maeneo mbalimbali nchi nzima. Kwa mfano, tu katika Jimbo langu la Masasi Walimu zaidi ya 50 bado wanadai kupandishwa mishahara. Hili ni jambo la msingi na ni lazima Serikali iwajibike kuhakikisha kwamba watu hawa wanapata fursa ya kulipwa mahitaji yao ili waweze kufundisha vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jambo hilo, kimekuwa kilio cha Walimu cha muda mrefu cha kupata posho ya madaraka (*responsibility allowances*). Tunao waraka ambao umetolewa na utumishi, Waraka Na. 3 wa mwaka 2014, unaotoa maelekezo, toka mwaka 2015/2016 maelekezo hayo yalipaswa kutimizwa kwa bajeti iliyopita, kwamba Mwalimu Mkuu wa Shule ya



Msingi alipaswa kulipwa shilingi 200,000/= kila mwezi kama posho ya madaraka; Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari shilingi 250,000/=, Mkaguzi wa Elimu Kata ni shilingi 250,000/= lakini Mkuu wa Chuo cha Ualimu ni shilingi 300,000/= kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maneno mazuri tu, tumwambie Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atupe mkakati ukoje katika kutekeleza mahitaji ya waraka huu unaotaka Walimu walipwe *responsibility allowances*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, ni muhimu tuliweke wazi suala ambalo kimsingi nchi yetu imepita katika mtikisiko wa kutoka kufanya mabadiliko makubwa ya namna ya kutoa vyeti vyetu kwa wanafunzi wetu wa Kidato cha Nne. Hili ni jambo la msingi sana! Sasa hivi tunao vijana wetu ambao tumeshatikisa *standard* ya vyeti vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali, sasa iandae utaratibu na Waziri atuambie utaratibu anaokuja nao, tufute vyeti vyote vyenye *GPA*, badala yake watoto hawa wapewe vyeti ambavyo vina *division*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu tumeamua kufanya mabadiliko, tumetoka tena kwenye *GPA* tunakwenda kwenye *division*, tayari tumeshaathiri watu katika kundi kubwa sana ambao mpaka sasa hivi wanashindwa kutambulika wana *standard* gani ya elimu katika vyeti vyao. Naomba tuliangalie sana hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kidogo kuhusu Elimu Maalum. Kama kuna eneo ambalo limesahaulika katika nchi hii, ni Elimu Maalum. Ninajua tukisema Shule za Sekondari na Shule za Msingi tutasema ziko katika eneo la TAMISEMI, lakini acha tu tuseme, nami ninaishauri Serikali, iangalie uwezekano wa kuchukua shule hizi za Elimu Maalum na kuzipeleka kwenye Wizara badala ya TAMISEMI ili ziweze kupata jicho maalum la kuziangularia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifika katika hizi Shule za Msingi na Shule za Sekondari ambazo zinawasaidia vijana wetu wenye mahitaji maalum, unaweza ukatokwa na machozi. Vijana hawa wanasoma katika mazingira magumu sana. Nadhani hata kama tukienda kwenye *theories of learning* tunajua kabisa miongoni mwa shule ambazo zilitakiwa ziwe na mazingira rafiki na ya kuvutia ni hizi zenye mahitaji maalum. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu kuna shule mbili za msingi; Shule ya Msingi Masasi na Shule ya Msingi Migongo. Watoto hawa wamesahaulika! Naomba Serikali iangalie namna invyoweza kuziboresha shule hili ili na hawa wenye mahitaji maalum wajione ni sehemu ya jamii.



Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na mambo hayo, napenda tu kuelezea jambo la msingi kwamba tunaposhughulikia elimu katika nchi yetu, hatuwezi kuweka mkazo moja kwa moja kwenye *formal education* pekee, yaani kwenye elimu ndani ya mfumo rasmi. Hili nimekuwa nikilisema na leo nalirudia tena. Ninaposoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri sioni inapojitokeza *non formal education*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo takwimu kwamba kama asilimia 50 ya Watanzania ni watoto; na kama asilimia 50 ni watoto, maana yake ni takriban milioni ishirini na kitu. Kama waliopo katika mfumo rasmi wa elimu ni milioni 12 tu, ni wazi kabisa kuna kundi kubwa la watu ambalo haliwezi kufikiwa bila ya kushiriki nje ya mfumo rasmi wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iangalie, hatuwezi kutumia madarasa yetu pekee kutoa elimu ya sekondari. Naiomba Wizara iangalie namna ambavyo inaweza ikazitumia taasisi zake kama vile Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kuhakikisha kwamba watoto wengi ambao wanakosa kuingia katika elimu rasmi, waende nje ya mfumo rasmi wa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo mengi ya kuyaangalia katika hilo. Nimekuwa nikisema, Waziri naye sasa hivi atakuwa na dhamana kubwa ya kuhakikisha tunakuja na mikakati ya kupunguza kiwango cha watu ambao wako nje ya mfumo wa elimu, wasiojua kusoma wala kuandika, wengine ni watu wazima; nao pia tuwaelimishe, tusizingatie tu elimu rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi ya kuzungumza, lakini niseme tu kwamba hali ya elimu tunaendelea kujikokota, tunakwenda, lakini yako mambo ambayo bado ni changamoto. Katika Jimbo la Masasi tuna tatizo kubwa la Walimu wa Shule za Msingi. Tunahitaji Walimu takriban 252; hatuna hata Mwalimu mmoja wa kufundisha Shule ya Awali, katika Walimu wa sayansi kiwango cha sekondari tuna matatizo makubwa. Tunapungukiwa Walimu zaidi ya 60, haya ni matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto tulizonazo, pamoja na juhudi kubwa tunazofanya za kutoa elimu bila malipo, lakini pia tuingeze nguvu katika kutatua changamoto zinazotukabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi, huo ndiyo mchango wangu. Naunga mkono hoja. Naomba Mheshimiwa Waziri aje na majibu ambayo yatatupa imani. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunamalizia na Mheshimiwa Edward Mwalongo kwa muda mdogo uliobaki.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Elimu. Kwanza kabisa, naomba ni-*declare interest* kwamba na mimi ni mmiliki wa shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makubwa niliyonayo hapa ni ushauri. Kwa sababu muda wenyewe ni kidogo sana, nikimbie na mwendo wa ushauri. Kwanza kabisa, namshauri Mheshimiwa Waziri, pale Wizarani liko tatizo la watu kujifanyia kutoa maamuzi. Wanatoa maamuzi hata bila kuangalia maamuzi haya yana madhara gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, sasa hivi tunajadili suala la ada elekezi. Ada elekezi ukijaribu kufanya utafiti, hayuko hata mtu mmoja anayelalamika, lakini watu wa Wizara wameamua tu kuandika elekezi, wanachanganya vichwa vya watu, Watanzania wanababaika na kuona kwamba kuna hoja ya ada elekezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala hili la ada elekezi Mheshimiwa Waziri alitolee ufafanuzi, Watanzania wajue kwamba ada elekezi unataka kumwelekeza nani? Aliyekwambia umpeleke mtoto shule huko ni nani? Kwani shule ya Serikali iko wapi? Shule ya Umma ipo, mtoto apelekwe akasome. Kama ukipeleka shule ya *private* maana yake umehiari mwenyewe. Utakayokutana nayo huko, acha yakukute. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, uko mtazamo pale Wizarani kwamba watu wanaamua tu mambo. Kwa hiyo, naomba usimamie utaratibu. Wewe mama nakufahamu, ni mtaalam, unajua jinsi ya kusimamia mambo. Simamia utaratibu watu wafuate utaratibu wa kuandika na kutoa maelekezo ili kusudi tuonekane kabisa kwamba *private sector* inayotoa elimu ni wadau wa Serikali na Serikali iwe tayari kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni ufaulu hafifu katika shule za Umma. Naomba Serikali ijitahidi kwa sababu leo hii tunaswaga hawa watoto wanaendelea kusoma, lakini tukumbuke, Mheshimiwa Waziri wewe ni mtaalam unafahamu, asubuhi umesema kabisa kwamba unasimama ukijiamini kwamba wewe ni msomi na umesoma katika elimu iliyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hawa watoto tunaowaswaga leo waende wamalize Kidato cha Nne kwa kuongeza idadi tu, tukumbuke kwamba itafika siku hawa watakuwa watawala. Watoto hawa ndio watakaokuwa Mawaziri, Marais na Wabunge. Hebu tujiulize, Taifa hili litakuwaje? Tutaanza kulalamika huduma hospitalini ni mbovu, huduma kila mahali ni mbovu kwa sababu tu watoto ambao tunawaswaga waende ili tujaze madarasa na wamalize *Form Four* watakuwa hawajapata elimu iliyo bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la VETA. Kwenye hotuba nimejaribu kupitia na kuangalia, wamejaribu kulieleza, lakini najiuliza, hivi Waheshimiwa Wabunge, nani Mbunge yumo humu ndani mtoto wake anasoma VETA? Maana tunang'ang'ania ooh, tuanzishe VETA watu wakasome VETA! VETA tulizonazo hazina ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni fundi, nafahamu fika taaluma inayotolewa kule VETA, tunaamini kuna ufundi, lakini hakuna ufundi wowote wa maana unaotolewa. VETA hawana vifaa, hawana *machines*; kama wanazo ni za kizamani mno! Tumejenga Vyuo hatukarabati, sasa leo tunataka watoto waende VETA, wakawe mafundi wa nani? Wafanye kazi ya nani? Naomba sana Serikali iangalie kwamba tunahitaji VETA sawa, lakini ziwe ni VETA zenye ubora. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumaliza VETA, watoto hawa wapewe mitaji ya kuanzia ufundi wao huko mitaani. Vile vile lazima tutambue, unapokuwa na Chuo cha VETA, ni vizuri ukawa na kituo kinachoweza kuwa na mitambo kwa ajili ya kusaidia watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe unamfundisha mtu kushona nguo, halafu unataka akate na mkasi wa mkono, ataendelea saa ngapi? Mafundi wangapi wameendelea mpaka leo? Tuwe tunafanya na utafiti! Kama tunataka watu wawe mafundi wa kushona, tuhakikishe kwamba tuna viwanda vikubwa vya ushonaji ambavyo kazi yake ni kukata nguo wale wachukue wakaunganishe. Sasa wewe unataka mtu akate nguo ile ashone, haiwezekani kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ada elekezi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa kutumia muda mfupi kwa mashauri mazuri, nashukuru ahsante.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kwa vile muda umemalizika, nina tangazo moja tu dogo.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, anawatangazia Wabunge wote wanaotoka Mkoa wa Mjini Magharibi wakutane katika ukumbi wa Pius Msekwa baada ya kuahirisha Bunge.

Waheshimiwa Wabunge sasa naliahirisha Bunge letu mpaka kesho siku ya Ijumaa tarehe 27 Mei saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 2.00 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,  
Tarehe 27 Mei, 2016 Saa Tatu Asubuhi)*